Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2024







Juni 2025
Dodoma

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2024

## YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **viii**
**KIREFU/TAFSIRI YA MANENO** ..... **xiii**
**SURA YA 1** ..... **1**
**HALI YA UCHUMI WA TAIFA** ..... **1**
Ukuaji wa Uchumi ..... 1
Mwenendo wa Mfumuko wa Bei ..... 7
Ukuzaji Rasilimali ..... 9
**SURA YA 2** ..... **35**
**FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA** ..... **35**
Utekelezaji wa Sera ya Fedha ..... 35
Ujazi wa Fedha ..... 35
Mikopo kwa Sekta Binafsi ..... 36
Amana katika Benki za Biashara ..... 37
Mwenendo wa Viwango vya Riba ..... 37
Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania ..... 38
**MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA** ..... **38**
Huduma za Benki ..... 38
Huduma za Mawakala wa Benki ..... 39
Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki ..... 39
Maboresho katika Sekta ya Benki ..... 39
Huduma Ndogo za Fedha ..... 39
Masoko ya Mitaji na Dhamana ..... 40
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ..... 41
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ..... 42
Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ..... 43
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ..... 43
Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa ..... 45
Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania ..... 46
Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ..... 48
Benki ya Biashara Tanzania ..... 48
Soko la Bidhaa Tanzania ..... 49
**SURA YA 3** ..... **56**
**FEDHA ZA SERIKALI** ..... **56**
Utangulizi ..... 56
Mwenendo wa Mapato ..... 57
Mwenendo wa Matumizi ..... 60
Deni la Serikali ..... 61
Tathmini ya Uhimilivu wa Deni ..... 63
Tathmini ya Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa ..... 64
**SURA YA 4** ..... **69**
**SEKTA YA NJE** ..... **69**
Bidhaa Zilizouzwa Nje ..... 69
Bidhaa Asilia ..... 69

Bidhaa Zisizo Asilia ........ 70
Mapato ya Huduma ........ 73
Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi ........ 73
Malipo ya Huduma ........ 74
Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali ........ 74
Mizania ya Malipo na Nchi za Nje ........ 79
Akiba ya Fedha za Kigeni ........ 80
**SURA YA 5 ........ 90**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ........ 90**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA ........ 90**
Ukuaji wa Uchumi ........ 90
Mwenendo wa Biashara Duniani ........ 94
**USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ........ 95**
Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa ........ 95
Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika ........ 96
Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ........ 97
Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 99
**SURA YA 6 ........ 101**
**RASILIMALI WATU ........ 101**
Idadi ya Watu ........ 101
Mgawanyiko wa Watu Kimkoa ........ 101
Mgawanyo wa Watu kwa Umri ........ 103
Nguvu Kazi na Ajira ........ 104
**SURA YA 7 ........ 110**
**KILIMO NA USHIRIKA ........ 110**
**UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO ........ 110**
Mazao ya Chakula ........ 110
Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula ........ 110
Mazao ya Asilia ya Biashara ........ 111
Mazao ya Bustani ........ 111
Mazao ya Mbegu za Mafuta ........ 112
Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo ........ 112
Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao ........ 114
Huduma za Ugani ........ 115
Utafiti katika Uzalishaji wa Mazao ........ 115
Mafunzo ya Kilimo ........ 116
Umwagiliaji ........ 116
**MIFUGO ........ 116**
Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake ........ 116
Biashara ya Mifugo na Mazao yake ........ 118
Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo ........ 119
Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo ........ 119
Mafunzo ya Mifugo ........ 120
Utafiti wa Mifugo ........ 120
Huduma za Ugani katika Mifugo ........ 121
**UVUVI ........ 121**

Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ... 121
Ukuzaji Viumbe Maji ... 121
Uvunaji wa Samaki ... 123
Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi ... 123
Uuzaji na Uagizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi ... 124
Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi ... 125
Mafunzo ya Uvuvi ... 125
**MAENDELEO YA USHIRIKA ... 125**
**SURA YA 8 ... 136**
**MISITU, WANYAMAPORI NA UTALII ... 136**
Misitu na Nyuki ... 136
Upandaji wa Miti ... 136
Mauzo ya Bidhaa za Misitu Nje ya Nchi ... 137
Wanyamapori ... 137
Uwindaji wa Kitalii na Utalii wa Picha ... 139
Utalii ... 139
Malikale ... 142
Makumbusho ya Taifa ... 142
**SURA YA 9 ... 148**
**MADINI ... 148**
Leseni za Shughuli za Madini ... 148
Vibali vya Uuzaji wa Madini ... 148
Dhahabu ... 148
Almasi ... 149
Vito vya Thamani ... 149
Tanzanite ... 149
Makaa ya Mawe ... 149
Madini ya Jasi ... 149
Madini ya ujenzi ... 150
Madini Mengine ... 150
Masoko ya Madini ... 151
**SURA YA 10 ... 154**
**VIWANDA NA BIASHARA ... 154**
Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani ... 154
Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ... 154
Usajili wa Biashara na Viwanda ... 156
Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa ... 156
Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo ... 157
Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia ... 159
Shirika la Maendeleo la Taifa ... 159
Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ... 160
**SURA YA 11 ... 167**
**UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI ... 167**
**UJENZI ... 167**
Mtandao wa Barabara Nchini ... 167
Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari ... 169

Mfuko wa Barabara ... 169
Nyumba na Majengo ya Serikali ... 169
Usajili wa Makandarasi ... 170
Usajili wa Wahandisi ... 170
Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ... 171
Baraza la Taifa la Ujenzi ... 172
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ... 172
**MAENDELEO YA ARDHI ... 173**
Utayarishaji wa Hatimiliki, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Utatuzi wa Migogoro ... 173
Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria ... 173
Uthamini wa Mali na Upimaji wa Mashamba na Viwanja ... 174
Mipango ya Matumizi ya Ardhi ... 175
Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa ... 178
Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ... 178
Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara ... 179
**SURA YA 12 ... 180**
**UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO ... 180**
Usafiri wa Barabara ... 180
Usafiri wa Reli ... 181
Usafiri wa Anga ... 182
Usafiri na Usafirishaji kwa Njia ya Maji ... 184
Shehena za Nchi Jirani ... 188
Uchukuzi Kwenye Maziwa ... 188
Kampuni ya Meli ya China na Tanzania ... 188
Huduma za Hali ya Hewa ... 189
**SURA YA 13 ... 191**
**MAWASILIANO, HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ... 191**
**MAWASILIANO ... 191**
Huduma za Posta ... 191
Huduma za Simu ... 192
Huduma za Intaneti ... 192
Utoaji wa Leseni za Mawasiliano ... 193
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ... 193
Huduma za Mawasiliano ... 194
**HABARI ... 194**
**MAENDELEO YA UTAMADUNI ... 196**
**MAENDELEO YA SANAA ... 197**
**MAENDELEO YA MICHEZO ... 200**
**SURA YA 14 ... 203**
**NISHATI ... 203**
Ufuaji wa Umeme ... 203
Gesi Asilia ... 204
Uagizaji Mafuta ... 205
Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani ... 206
Mwenendo wa Bei za Mafuta ... 207
Gesi Inayotokana na Petroli ... 209

**SURA YA 15** .......... **214**
**MAJI** .......... **214**
Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji .......... 214
Ubora wa Maji .......... 214
Huduma ya Maji Vijijini .......... 215
Huduma ya Maji Mijini .......... 216
Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa .......... 216
Uondoaji wa Majitaka .......... 217
**SURA YA 16** .......... **222**
**ELIMU MAFUNZO NA TEKNOLOJIA** .......... **222**
Elimu ya Awali .......... 222
Elimu ya Msingi .......... 222
Elimu ya Sekondari .......... 223
Elimu katika Vyuo vya Ualimu .......... 224
Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu .......... 225
Elimu ya Ufundi na Mafunzo .......... 225
Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi .......... 225
Sayansi, Teknolojia na Ubunifu .......... 226
Elimu ya Juu .......... 226
Udhibiti wa Mionzi .......... 227
**SURA YA 17** .......... **232**
**AFYA NA MAENDELEO YA JAMII** .......... **232**
**AFYA** .......... **232**
Vituo vya Kutolea Huduma za Afya .......... 232
Hali ya Utoaji Huduma .......... 232
Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba .......... 233
Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto .......... 233
Huduma za Chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja .......... 234
Huduma za Matibabu ya Kibingwa .......... 234
Udhibiti wa Malaria .......... 235
Udhibiti wa Kifua Kikuu .......... 235
Lishe .......... 236
Mafunzo katika Kada za Afya .......... 236
**MAENDELEO YA JAMII** .......... **237**
Ustawi wa Jamii .......... 237
Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii .......... 237
Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto .......... 238
Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto .......... 238
Ukatili wa Kijinsia .......... 239
Huduma za Ustawi kwa Wazee .......... 240
Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .......... 240
**SURA YA 18** .......... **244**
**MASUALA MTAMBUKA** .......... **244**
Mazingira .......... 244
Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia .......... 245
Usalama wa Raia .......... 245

Utambuzi na Usajili wa Watu .......... 247
Usajili wa Jumuiya .......... 247
Usajili, Ufilisi na Udhamini .......... 248
Maendeleo ya Sheria na Mahakama .......... 249
Utawala Bora .......... 250
Jitihada za Kupunguza Umaskini .......... 251
**SURA YA 19 .......... 253**
**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI .......... 253**
Usajili wa Miradi ya Uwekezaji .......... 253
Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta .......... 253
Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa .......... 254
Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje .......... 255
Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje .......... 255
Mazingira ya Biashara na Uwekezaji .......... 258
Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi .......... 259
Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati .......... 261
Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi .......... 261
**SURA YA 20 .......... 264**
**UENDELEZAJI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA .......... 264**
Utangulizi .......... 264
Sera na Mikakati ya Kitaifa Inayohusiana na Nishati Safi ya Kupikia .......... 264
Hali Ilivyo .......... 265
Athari za Matumizi ya Nishati Isiyo Safi ya Kupikia .......... 280
Changamoto Zinazoathiri Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia .......... 281
Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizopo Katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia .......... 283
Hitimisho .......... 284

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Ukurasa**

Jedwali A: TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA.................. xviii

Jedwali B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI.............xix

Jedwali Na. 1: PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI.............................................................................11

Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA ..........................................................................................................12

Jedwali Na. 3: MCHANGO WA PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ................................................13

Jedwali Na. 4: MCHANGO WA PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA.......................................................................................14

Jedwali Na. 5: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA MATUMIZI...........................................................................................15

Jedwali Na. 6: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI.............................................................................16

Jedwali Na. 7: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA 17

Jedwali Na. 8: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ................................................................18

Jedwali Na. 9: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA.......................................................................................20

Jedwali Na. 10: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA AINA YA MATUMIZI.........................................................................................21

Jedwali Na. 11: UKUZAJI RASILIMALI KWA KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI .........................................................................22

Jedwali Na. 12: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MWAKA 2015 KWA AINA YA RASILIMALI ....... 23
Jedwali Na. 13: MCHANGO KATIKA UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI ....... 24
Jedwali Na. 14: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA SEKTA ....... 25
Jedwali Na. 15: FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 26
Jedwali Na. 16: FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 = 100) ....... 27
Jedwali Na. 17: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 28
Jedwali Na. 18: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 29
Jedwali Na. 19: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 30
Jedwali Na. 20: FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 31
Jedwali Na. 21: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 32
Jedwali Na. 22: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Jan - Dec. 2020 =100) ....... 33
Jedwali Na. 23: FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA ( Jan - Dec. 2020 =100) ....... 34
Jedwali Na. 24: MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA ....... 51
Jedwali Na. 25: VIWANGO VYA UKUAJI WA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA 52
Jedwali Na. 26: MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI ....... 53
Jedwali Na. 27: MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA ....... 54

Jedwali Na. 28: VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA ........................................................55
Jedwali Na. 29: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI ..................65
Jedwali Na. 30: MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI ........................................................................................................67
Jedwali Na. 31: THAMANI YA BIASHARA YA BIDHAA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE.............................................................................................81
Jedwali Na. 32: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE .........82
Jedwali Na. 33: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI.........................................................................83
Jedwali Na. 34: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE ........................................................................................................86
Jedwali Na. 35: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI ........................................................................................................87
Jedwali Na. 36: MIZANIA YA MALIPO MWAKA 2018 - 2024 ...........................................88
Jedwali Na. 37: IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA MWAKA 2017 - 2024 ........................................................................................................108
Jedwali Na. 38: UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI .......................................127
Jedwali Na. 39: PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI .................................128
Jedwali Na. 40: ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA .........................................................................................129
Jedwali Na. 41: KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI .............................130
Jedwali Na. 42: ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA....131
Jedwali Na. 43: MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI ...........................................................................................132
Jedwali Na. 44: UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI .............................................133
Jedwali Na. 45: MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI........................134
Jedwali Na. 46: MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI ....................................................135
Jedwali Na. 47: WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA KATIKA MWAKA 2010 - 2024...................................................................................................144
Jedwali Na. 48: MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU NJE YA NCHI MWAKA 2024 .........145
Jedwali Na. 49: MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII NCHINI 2016 - 2024...........146

Jedwali Na. 50: WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO....147
Jedwali Na. 51: UCHIMBAJI WA MADINI - KIASI KILICHOPATIKANA....152
Jedwali Na. 52: MADINI YALIYOPATA KIBALI CHA KUUZWA NJE YA NCHI....153
Jedwali Na. 53: MATUMIZI YA SARUJI NCHINI (Tani)....161
Jedwali Na. 54: UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI....162
Jedwali Na. 55: VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA....163
Jedwali Na. 56: VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI....164
Jedwali Na. 57: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO....165
Jedwali Na. 58: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA....166
Jedwali Na. 59: SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+....190
Jedwali Na. 60: HUDUMA ZA POSTA....201
Jedwali Na. 61: IDADI YA KADI ZA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI....202
Jedwali Na. 62: UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NCHINI NA UPATIKANAJI WA UMEME MWAKA 2024....210
Jedwali Na. 63: MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI (Saa za Gigawati)....212
Jedwali Na. 64: MAUZO YA UMEME KWA MIKOA (GWh)....213
Jedwali Na. 65: UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI....218
Jedwali Na. 66: KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MIKUU YA MIKOA MWAKA 2024....221
Jedwali Na. 67: SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO....228
Jedwali Na. 68: SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO....229
Jedwali Na. 69: IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA....230
Jedwali Na. 70:IDADI YA TAASISI ZA ELIMU....231
Jedwali Na. 71:IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA....241

Jedwali Na. 72: IDADI YA VITANDA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI ....................242
Jedwali Na. 73: KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA MWAKA 2023 - 2024 ....................262

## KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area (Eneo Huru la Biashara Afrika) |
| AGTIF | Agricultural Input Trust Fund (Mfuko wa Pembejeo za Kilimo) |
| ASA | Agricultural Seed Agency (Wakala wa Mbegu za Kilimo) |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania) |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BASA | Bilateral Air Services Agreement (Mikataba ya Usafiri wa Anga Baina ya Tanzania na Nchi Nyingine ) |
| BASATA | Baraza la Sanaa la Taifa |
| BMT | Baraza la Michezo la Taifa |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency (Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni) |
| CAMARTEC | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini) |
| CBE | College of Business Education (Chuo cha Elimu ya Biashara) |
| CMSA | Capital Market and Securities Authority (Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ) |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika) |
| COSOTA | Chama cha Hakimiliki Tanzania |
| DSE | Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar es Salaam) |
| EAC | The East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| FCC | The Fair Competition Commission (Tume ya Ushindani) |
| FCT | Fair Competition Tribunal (Baraza la Ushindani) |
| FETA | Fisheries Education and Training Agency (Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi) |
| IMF | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |
| LATRA | Land Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini) |
| LPG | Liquified Petroleum Gas (Gesi inayotokana na Petroli) |
| M1 | Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu) |
| M2 | Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |

| | |
|---|---|
| M3 | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| MKUMBI | Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara |
| MPRU | Marine Parks and Reserves Tanzania (Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu) |
| MSCL | Marine Services Company Limited (Kampuni ya Huduma za Meli) |
| NAM | Non-Aligned Movement (Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote) |
| NCAA | Ngorongoro Conservation Area Authority (Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro) |
| NDC | The National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa) |
| NEDF | National Entrepreneurship Development Fund (Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali) |
| NFRA | National Food Reserve Agency (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) |
| NHC | National Housing Corporation (Shirika la Nyumba la Taifa) |
| NHIF | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa Wa Bima ya Afya) |
| NIMR | The National Institute for Medical Research (Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu) |
| NSSF | National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| OECD | Organisation for Economic Co-operation and Development (Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo) |
| OPV | Oral Polio Vaccine |
| PPP | Public Private Partnership (Ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi) |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma) |
| RITA | Registration Insolvency and Trusteeship Agency (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) |
| SADC | The Southern African Development Community (Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika) |
| SIDO | Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) |
| SGR | Standard Gauge Railway (Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa) |
| TADB | Tanzania Agricultural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Kilimo |

| | |
|---|---|
| | Tanzania) |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TALIRI | Tanzania Livestock Research Institute (Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania) |
| TANAPA | Tanzania National Parks (Shirika la Hifadhi za Taifa) |
| TANESCO | Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Ugamvi wa Umeme Tanzania) |
| TANIPAC | Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination (Mradi wa Kuzuia Sumu Kuvu) |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency (Wakala wa Barabara Tanzania) |
| TanTrade | Tanzania Trade Development Authority (Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania) |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute (Taaasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania) |
| TARURA | Tanzania Rural and Urban Roads Agency (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) |
| TASAC | Tanzania Shipping Agency Corporation (Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania) |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii) |
| TAWA | Tanzania Wildlife Management Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania) |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TBA | Tanzania Building Agency (Wakala wa Majengo Tanzania) |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation (Shirika la Utangazaji Tanzania) |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards (Shirika la Viwango Tanzania) |
| TCAA | Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania) |
| TCB | Tanzania Commercial Bank (Benki ya Biashara Tanzania) |
| TDCs | Technology Development Centres (Vituo vya Uendelezaji Teknolojia) |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

| | |
|---|---|
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania) |
| TEMESA | Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (Wakala wa Ufundi na Umeme) |
| TIC | Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji Tanzania) |
| TIRA | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamazi wa Bima Tanzania) |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization (Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania) |
| TMA | Tanzania Meteorological Authority (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) |
| TMX | Tanzania Merchantile Exchange (Soko la Bidhaa Tanzania) |
| TNBC | Tanzania National Business Council (Baraza la Taifa la Biashara) |
| TPA | Tanzania Ports Authority (Mamlaka ya Bandari Tanzania) |
| TRA | Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania) |
| TRC | Tanzania Railway Corporation (Shirika la Reli Tanzania) |
| UCSAF | The Universal Communications Service Access Fund (Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote) |
| VETA | Vocational Education and Training Authority (Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi) |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WCF | Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi) |
| WEO | World Economic Outlook |
| WMA | Weight and Measurement Agency (Wakala wa Vipimo) |
| WTO | The World Trade Organization (Shirika la Biashara Duniani) |

## MATUKIO YA KIUCHUMI KATIKA MWAKA 2024

| Na. | TAREHE | MWEZI | TUKIO |
|---|---|---|---|
| 1. | 25 | Februari | Mradi wa umeme wa Julius Nyerere - JNHPP wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 ulianza kazi kwa mara ya kwanza na kuingiza megawati 235 katika Gridi ya Taifa kupitia mtambo namba tisa (9). |
| 2. | 08 | Mei | Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ifikapo mwaka 2033. |
| 3. | 01 | Agosti | Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuzindua rasmi huduma za treni za abiria katika Mradi wa Kimkakati wa Reli kwa Viwango vya Kimataifa - SGR kati ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. |
| 4. | 27 | Novemba | Kufanyika kwa zoezi la uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini Tanzania. |

## Jedwali A: TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA

| Maelezo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu Tanzania Bara (Milioni) | 54.3 | 55.9 | 57.7 | 59.9 | 61.7 | 64.2 | 4.1 |
| Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni)* | 134,540,194 | 145,384,353 | 156,167,137 | 170,820,032 | 186,753,685 | 205,846,493 | 10.2 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2015 (Sh. Milioni) | 123,193,239 | 128,723,538 | 134,951,513 | 141,247,193 | 148,521,017 | 156,635,319 | 5.5 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.) | 2,573,324 | 2,653,790 | 2,708,999 | 2,854,072 | 3,058,847 | 3,204,244 | 4.8 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2015 (Sh.) | 2,269,888 | 2,306,682 | 2,346,983 | 2,370,418 | 2,406,418 | 2,438,214 | 1.3 |
| Kasi ya Upandaji Bei (asilimia) | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 | -18.4 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -3,237.60 | -1,460.00 | -3,247.70 | -6,984.90 | -6,032.30 | -5,157.20 | -14.5 |
| Saruji Iliyotumika (Tani ) | 6,104,108 | 5,887,775 | 6,863,004 | 7,532,173 | 7,950,515 | 7,705,918 | -3.1 |
| Umeme Uliouzwa (GWH)* | 6,642.60 | 6,674.30 | 7,313.20 | 7,729.60 | 8,232.00 | 9,114.7 | 10.7 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 2,604 | 715 | 1,248 | 2,527.80 | 3,373.80 | 3,903.0 | 15.7 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) * | 10,605 | 10,925 | 11,196.80 | 11,420.97 | 11,425.48 | 11,391.19 | -0.3 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) * | 2,338 | 2,473 | 2,671.90 | 2,823.60 | 3,077.36 | 3,314.19 | 7.7 |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 80,164 | 84,162 | 86,131 | 104,687 | 125,500 | 123,769 | -1.4 |
| **Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Mil. US$)** | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | |
| Kahawa | 152.2 | 145 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 292.9 | 28.5 |
| Pamba | 91.8 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | 69.3 | -32.0 |
| Katani | 19.3 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | 23.4 | 14.7 |
| Chai | 45.7 | 32.4 | 32.9 | 30 | 31.1 | 19.4 | -37.6 |
| Tumbaku | 146.5 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.4 | 509.5 | 49.7 |
| Korosho | 353.1 | 359.6 | 159 | 226.9 | 206.4 | 541.7 | 162.5 |
| Karafuu | 9.1 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | 17.1 | -31.9 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | |
| Madini | 2,326.70 | 3369.1 | 3,116.40 | 3,395.30 | 3,551.40 | 4,119.9 | 16.0 |
| Bidhaa za Viwanda | 851.8 | 908.6 | 1,200.00 | 1,419.20 | 1,363.30 | 1,341.3 | -1.6 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 168 | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164 | 180.6 | 10.1 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 202.4 | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 507.1 | 21.5 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) | 242.8 | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 240.8 | 78.1 |
| Bidhaa nyinginezo | 394.3 | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 839.1 | 21.5 |
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha - M3 (Sh. bilioni) | 28,313.10 | 29,920.60 | 34,558.00 | 38,580.00 | 44,002.60 | 48,905.30 | 11.1 |
| Karadha (Sh. bilioni) | 28,103.30 | 26,139.60 | 30,030.50 | 37,557.30 | 43,455.91 | 47,499.00 | 9.3 |
| **Fedha za Serikali** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni) | 21,051,755 | 20,594,735 | 24,395,567 | 26,277,887 | 29,829,895 | 34,610,646 | 12.7 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni) | -14,201,148 | -14,883,723 | -15,817,056 | -20,475,132 | -21,931,209 | -27,398,316 | 25.4 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni) | -9,926,993 | -11,701,584 | -15,080,341 | -15,682,330 | -14,636,421 | -15,353,600 | -11.2 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

## Jedwali B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI

| **Mwaka wa Kalenda** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (mp) | 7.0% | 6.9% | 4.5% | 4.8% | 4.7% | 5.1% | 5.5% |
| Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (mp) | 4.4% | 8.5% | 8.1% | 7.4% | 9.4% | 10.4% | 10.2% |
| Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP) | 32.8% | 34.3% | 38.5% | 40.8% | 39.3% | 37.1% | 37.1% |
| Uwiano wa Akiba kwa Pato la Taifa (Savings/GDP) | 20.5% | 21.0% | 20.9% | 21.1% | 20.9% | 19.7% | 23.8% |
| **MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA** | | | | | | | |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi) | 3.3% | 3.8% | 3.2% | 4.2% | 4.8% | 3.0% | 3.1% |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka) | 3.5% | 3.4% | 3.3% | 3.7% | 4.3% | 3.8% | 3.1% |
| GDP deflator Inflation (bp) | -2.1% | 2.0% | 3.0% | 2.3% | 4.2% | 4.5% | 4.5% |
| GDP deflator Inflation (MP) | -2.4% | 1.5% | 3.4% | 2.5% | 4.5% | 4.0% | 4.5% |
| Riba za Mikopo (mwaka mmoja) | 18.3% | 18.2% | 16.7% | 15.7% | 16.4% | 16.5% | 15.82% |
| Riba za Amana za muda maalum (miezi 12) | 11.7% | 8.8% | 8.8% | 8.3% | 8.3% | 7.1% | 7.85% |
| Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka) | 6.6% | 9.5% | 7.9% | 7.5% | 8.1% | 7.9% | 6.65% |
| Thamani ya Tshs/Dola (wastani wa mwaka) | 2275.40 | 2299.79 | 2305.60 | 2309.20 | 2314.50 | 2395.70 | 2610.50 |
| **UJAZI WA FEDHA** | | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa M3 | 4.5% | 9.6% | 5.7% | 15.5% | 11.6% | 14.1% | 11.1% |
| Kiwango cha ukuaji wa M2 | 3.8% | 11.8% | 8.2% | 17.6% | 12.1% | 11.9% | 9.3% |
| Mikopo Chechefu | 10.7% | 9.8% | 9.8% | 8.5% | 5.8% | 4.3% | 3.3% |
| Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi | 4.9% | 11.1% | 3.1% | 10.0% | 22.5% | 17.1% | 12.4% |
| **UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 8.1% | 7.2% | 8.5% | 9.4% | 9.1% | 10.8% | 11.6% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 15.0% | 14.0% | 15.2% | 12.6% | 13.3% | 19.5% | 20.3% |
| Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje | 13.1% | 14.3% | 13.6% | 11.5% | 13.5% | 14.0% | 18.0% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 16.7% | 17.6% | 16.4% | 16.5% | 18.3% | 19.5% | 20.3% |
| Urari wa malipo ya kawaida | -2.7% | -3.9% | -2.1% | -2.1% | -3.2% | -4.1% | -2.6% |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | 4.6 | 5.9 | 5.3 | 6.2 | 4.7 | 4.5 | 4.4 |
| **UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| **Mwaka wa fedha** | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** |
| Mapato ya ndani | 14.8% | 14.3% | 15.0% | 13.7% | 14.9% | 14.6% | 15.1% |
| Mapato ya kodi | 12.4% | 11.9% | 12.5% | 11.5% | 12.3% | 11.9% | 12.5% |
| Matumizi (Bila rollover) | 16.8% | 17.2% | 17.2% | 17.6% | 19.0% | 19.2% | 18.5% |
| Matumizi ya kawaida | 10.2% | 10.7% | 10.1% | 9.9% | 9.8% | 11.4% | 11.1% |
| Matumizi ya maendeleo | 6.6% | 6.5% | 7.1% | 7.8% | 9.2% | 7.8% | 7.4% |
| Misaada | 0.8% | 0.4% | 0.7% | 0.5% | 0.4% | 0.3% | 0.3% |
| Nakisi (kabla ya misaada) | -2.7% | -3.6% | -2.6% | -4.5% | -4.1% | -4.6% | -3.4% |
| Nakisi (baada ya misaada) | -1.9% | -3.3% | -1.9% | -4.0% | -3.6% | -4.3% | -3.1% |
| Mikopo ya nje | 1.4% | 0.9% | 1.7% | 1.8% | 1.9% | 1.7% | 2.0% |
| Mikopo ya ndani (kutoka benki) | -0.3% | 1.8% | -0.3% | 1.2% | 1.1% | 0.8% | 1.1% |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha



## Sehemu ya Kwanza

# MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA


## SURA YA 1

## HALI YA UCHUMI WA TAIFA

**Ukuaji wa Uchumi**


1. Mwaka 2024, Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi bilioni 156,635.32 ikilinganishwa na shilingi bilioni 148,521.02 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa asilimia 5.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na: utekelezaji endelevu wa miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuanza kwa usafirishaji wa abiria kupitia Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa - SGR kwa kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; hali nzuri ya hewa iliyoimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo; na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi, Mwaka 2020 - 2024 (Asilimia)**





2. Mwaka 2024, shughuli za sanaa na burudani ziliendelea kuongoza kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 17.1, ikifuatiwa na shughuli za ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme asilimia 14.4, shughuli za habari na mawasiliano asilimia 14.3 na shughuli za fedha na bima asilimia 13.8 **(Kielelezo Na. 1.2)**. Aidha, shughuli za kilimo ziliendelea kuongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa wa asilimia 26.3, ikifuatiwa na shughuli za ujenzi asilimia 12.8 na shughuli za uchimbaji madini na mawe asilimia 10.1 **(Kielelezo Na. 1.3)**.

**Kielelezo Na. 1.2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2024 (Asilimia)**





**Kielelezo Na. 1.3: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia)**




3. Shughuli za sanaa na burudani zilikuwa na mchango mdogo katika ukuaji wa Pato la Taifa mwaka 2024 licha ya kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji. Kwa upande mwingine, shughuli za kilimo, ujenzi, fedha na bima, uchimbaji madini na mawe pamoja na biashara na matengenezo ziliendelea kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa. Katika kipindi hicho, shughuli hizo zilichangia zaidi ya asilimia 50 katika ukuaji wa Pato la Taifa. Aidha, mchango wa shughuli mbalimbali za uchumi katika ukuaji wa Pato la Taifa ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.4**.

**Kielelezo Na. 1.4: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia)**




4. Mwaka 2024, Pato ghafi la Taifa (kwa bei za mwaka husika) lilikuwa shilingi bilioni 205,846.49 ikilinganishwa na shilingi bilioni 186,753.69 mwaka 2023. Aidha, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 64,241,822 mwaka 2024 ikilinganishwa na watu 61,718,700 mwaka 2023. Hivyo, Pato la Taifa kwa Mtu lilikuwa wastani wa shilingi 3,204,244 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 3,058,847 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Kiasi hicho ni sawa na dola za Marekani 1,227.4 kwa mtu mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,276.8 kwa mtu mwaka 2023.

5. Mwaka 2024, shughuli za kilimo ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi zilikua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na: juhudi za Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo; kuendelea kutolewa kwa ruzuku ya mbolea; kuimarika kwa huduma za ugani na upatikanaji wa vitendea kazi; matumizi ya teknolojia na pembejeo bora za kilimo; na kuimarika kwa usimamizi wa upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna. Aidha, shughuli za mifugo zilikuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji cha asilimia 5.0, ikifuatiwa na uzalishaji mazao asilimia 4.0, misitu asilimia 3.6 na uvuvi asilimia 2.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0, asilimia 4.2, asilimia 4.3 na asilimia 1.4, mtawalia mwaka 2023.

6. Mwaka 2024, shughuli za kilimo sehemu ya kuuza zilikua kwa asilimia 4.1 na sehemu isiyo ya kuuza ilikua kwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.2 kwa sehemu ya kuuza na asilimia 4.5 sehemu isiyo ya kuuza mwaka 2023. Katika kipindi hicho, sehemu

ya kuuza kwa shughuli za mifugo ilikua kwa asilimia 5.0, kilimo cha mazao asilimia 4.0, misitu asilimia 3.6 na uvuvi asilimia 2.3 kama ilivyokuwa kwa sehemu isiyo ya kuuza.

7. Mwaka 2024, mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 26.3 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 26.8 mwaka 2023. Aidha, shughuli za uzalishaji mazao zilichangia asilimia 16.1 katika Pato la Taifa, mifugo asilimia 6.2, misitu asilimia 2.4 na uvuvi asilimia 1.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 16.3, asilimia 6.3, asilimia 2.6 na asilimia 1.7, mtawalia mwaka 2023.

8. Mwaka 2024, shughuli za uchimbaji madini na mawe zilikua kwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 11.3 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya madini ya dhahabu na makaa ya mawe katika soko la dunia. Aidha, mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 10.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2023.

9. Mwaka 2024, shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.3 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na juhudi za Serikali katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani pamoja na kuweka mazingira wezeshi. Aidha, mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2023.

10. Mwaka 2024, shughuli za ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme zilikua kwa asilimia 14.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.9 mwaka 2023. Ongezeko la kasi ya ukuaji lilitokana na kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere - JNHPP. Aidha, mchango wa shughuli za umeme kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 0.1 mwaka 2023.

11. Mwaka 2024, shughuli za usambazaji maji safi na udhibiti majitaka zilikua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.5 mwaka 2023. Ongezeko la kasi ya ukuaji lilichangiwa na juhudi endelevu za Serikali katika kuboresha miundombinu ya maji safi mijini na vijijini kutokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya usambazaji maji na kudhibiti majitaka. Kwa upande mwingine, shughuli za usambazaji maji safi na udhibiti majitaka sehemu inayouzika na isiyouzika ilikua kwa asilimia 4.1 mwaka 2024. Aidha, mchango wa shughuli za usambazaji maji na udhibiti majitaka katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.5 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

12. Mwaka 2024, shughuli za ujenzi zilikua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.5 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege, reli, ofisi za Serikali, madarasa, vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na nyumba za makazi na biashara. Kwa upande mwingine, shughuli za ujenzi

sehemu inayouzika ilikua kwa asilimia 3.6 na sehemu isiyouzika ilikua kwa asilimia 13.1 mwaka 2024. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 12.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 13.4 mwaka 2023.

13. Mwaka 2024, shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na juhudi za Serikali katika kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini pamoja na kuendelea kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, mchango wa shughuli za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2023.

14. Mwaka 2024, shughuli za huduma za malazi na chakula zilikua kwa asilimia 6.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.3 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususan utalii kufuatia hatua zilizoendelea kuchukuliwa na Serikali, ikiwemo utangazaji na uboreshwaji wa miundombinu ya utalii. Katika kipindi hicho, idadi ya watalii walioingia nchini ilikuwa 2,141,895 ikilinganishwa na watalii 1,808,205 waliongia nchini mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za malazi na chakula katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.2 mwaka 2023.

15. Mwaka 2024, shughuli za uchukuzi na uhifadhi mizigo zilikua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa abiria kufuatia Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa - SGR kuanza kutoa huduma pamoja na kuongezeka kwa shehena za mizigo zilizosafirishwa kutoka bandarini kupitia barabara, reli na anga. Mchango wa shughuli za uchukuzi na uhifadhi mizigo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2023.

16. Mwaka 2024, shughuli za habari na mawasiliano zilikua kwa asilimia 14.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.6 mwaka 2023. Ongezeko la kasi ya ukuaji lilitokana na kuongezeka kwa: maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya mawasiliano; matumizi ya simu za mkononi na mitandao ya kijamii; mikutano ya mitandaoni; na matumizi ya malipo yasiyotumia fedha taslimu kupitia mitandao ya simu. Aidha, mchango wa shughuli za habari na mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2023.

17. Mwaka 2024, shughuli za huduma za fedha na bima zilikua kwa asilimia 13.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 14.6 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa kiwango cha amana na mikopo kwa sekta binafsi, kupungua kwa mikopo chechefu pamoja na kupanuka kwa shughuli za bima. Mchango wa shughuli za huduma za

fedha na bima katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023.

18. Mwaka 2024, shughuli za upangishaji majengo zilikua kwa asilimia 4.3 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na ongezeko la mahitaji ya nyumba za makazi, biashara na ofisi kutokana na ongezeko la idadi ya watu pamoja na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Aidha, shughuli za upangishaji majengo kwa sehemu inayouzika na isiyouzika zilikua kwa asilimia 4.3 mwaka 2024. Vilevile, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.7 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

19. Mwaka 2024, shughuli za utawala wa umma na ulinzi zilikua kwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na juhudi za Serikali kuendeleza kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa shughuli za kiserikali. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023.

20. Mwaka 2024, ukuaji wa shughuli za huduma zinazohusiana na utawala ulikuwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na ongezeko la shughuli za mawakala wa usafiri, kukua kwa sekta ya utalii na ongezeko la huduma za kukodisha vifaa, mashine na mitambo. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.6 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

21. Mwaka 2024, shughuli za utoaji huduma za elimu zilikua kwa asilimia 6.2 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na juhudi za Serikali kwa kushirikiana na wadau kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu, kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari pamoja na ongezeko la ajira kwa walimu. Aidha, shughuli za huduma za elimu zilichangia asilimia 2.2 katika Pato la Taifa mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Kwa upande mwingine, shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi zilikua kwa asilimia 4.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2023. Vilevile, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.7 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

22. Mwaka 2024, shughuli za sanaa na burudani zilikua kwa asilimia 17.1 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi ingawa kasi ya ukuaji ilipungua ikilinganishwa na asilimia 17.7 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuimarika kwa mauzo ya bidhaa za kitamaduni kwa watalii na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara ya tasnia ya burudani. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.4 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

23. Mwaka 2024, ukuaji wa shughuli za kaya binafsi katika kuajiri ulikuwa asilimia 2.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.1 mwaka 2023. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.2 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Kwa

upande mwingine, shughuli za huduma nyingine za kijamii zilikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2023. Mchango wa shughuli za huduma nyingine za kijamii katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 0.9 mwaka 2023.

**Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

24. Mwaka 2024, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0 na kinakidhi vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (asilimia isiyozidi 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (asilimia 3.0 - 7.0). Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kutengemaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani. **Jedwali Na. 1.1** linaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei kwa baadhi ya makundi makuu ya bidhaa na huduma.

**Jedwali Na. 1.1: Fahirisi za Kitaifa za Bei ya Mtumiaji (NCPI) na Viwango vya Mfumuko wa Bei (Kizio 2020 = 100), Mwaka 2020 - 2024**


| Mwaka | | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Uzito** | 28.2 | 1.9 | 10.8 | 15.1 | 7.9 | 2.5 | 14.1 | 5.4 | 1.6 | 2.0 | 6.6 | 2.1 | 2.1 | 100.0 |
| **2020** | **Fahirisi za Bei** | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 |
| **2021** | | 104.3 | 102.2 | 104.6 | 104.1 | 103.2 | 102.7 | 103.3 | 101.8 | 102.7 | 101.1 | 104.9 | 100.3 | 102.8 | 103.7 |
| **2022** | | 111.9 | 103.5 | 107.1 | 107.8 | 106.8 | 104.2 | 109.6 | 102.8 | 104.3 | 101.7 | 107.3 | 100.4 | 105.2 | 108.2 |
| **2023** | | 119.5 | 105.9 | 110.4 | 109.5 | 110.2 | 105.9 | 112.7 | 104.5 | 106.6 | 105.1 | 111.9 | 100.5 | 108.2 | 112.3 |
| **2024** | | 122.0 | 109.0 | 112.6 | 115.2 | 113.3 | 107.9 | 117.4 | 106.0 | 109.7 | 108.4 | 115.7 | 101.7 | 115.4 | 115.7 |
| **2020** | **Mfumuko wa Bei** | 4.1 | -0.1 | 2.2 | 7.6 | 1.8 | 0.8 | 1.4 | 0.4 | 0.1 | 1.3 | 1.5 | 0.0 | 1.0 | 3.3 |
| **2021** | | 4.3 | 2.2 | 4.6 | 4.1 | 3.2 | 2.7 | 3.3 | 1.8 | 2.7 | 1.1 | 4.9 | 0.3 | 2.8 | 3.7 |
| **2022** | | 7.3 | 1.2 | 2.5 | 3.6 | 3.5 | 1.4 | 6.1 | 0.9 | 1.5 | 0.6 | 2.3 | 0.1 | 2.3 | 4.3 |
| **2023** | | 6.8 | 2.4 | 3.0 | 1.6 | 3.2 | 1.7 | 2.8 | 1.7 | 2.2 | 3.4 | 4.3 | 0.1 | 2.9 | 3.8 |
| **2024** | | 2.1 | 3.0 | 2.0 | 5.2 | 2.8 | 1.9 | 4.2 | 1.4 | 2.9 | 3.1 | 3.4 | 1.3 | 6.6 | 3.1 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

25. Mwaka 2024, mfumuko wa bei za msingi (core inflation) ulikuwa wastani wa asilimia 3.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei kwa kundi la chakula na vinywaji baridi uliendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 2.1

mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kufuatia uwepo wa hali nzuri ya hewa na utolewaji wa ruzuku ya mbolea pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu ya umwagiliaji na usafirishaji. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei kwa kundi la nishati, mafuta na ankara za maji uliongezeka na kufikia asilimia 9.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kupanda kwa bei za mkaa na kuni kufuatia juhudi za Serikali katika kuhifadhi mazingira ambazo zilisababisha uhaba wa bidhaa hizo.

**Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi, Mwaka 2012 - 2024**




| | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Msingi | 12.8 | 4.5 | 3.7 | 2.3 | 2.6 | 2.0 | 1.9 | 3.0 | 2.3 | 4.1 | 3.0 | 2.3 | 3.4 |
| Chakula | 22.0 | 8.6 | 7.7 | 8.6 | 7.6 | 9.6 | 3.7 | 4.3 | 5.0 | 4.3 | 7.3 | 6.8 | 2.1 |
| Nishati | 30.9 | 12.8 | 12.1 | -0.9 | 6.3 | 10.5 | 17.2 | 9.0 | 5.0 | 3.1 | 9.1 | 2.3 | 9.3 |
| Mfumuko wa bei | 16.0 | 7.9 | 6.1 | 5.6 | 5.2 | 5.3 | 3.5 | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 |

26. Mwaka 2024, mfumuko wa bei kwa matabaka ya kipato cha chini, kati na juu uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.8, asilimia 7.9 na asilimia 6.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.2, asilimia 4.9 na asilimia 2.5 mtawalia mwaka 2023. Ongezeko la mfumuko wa bei kwa matabaka yote lilitokana na kuongezeka kwa wastani wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika kwa wingi kwa kila tabaka. Baadhi ya bidhaa na huduma zilizokuwa na ongezeko kubwa la wastani wa bei ni pamoja na usafiri, makazi, nishati na burudani. **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei za bidhaa na huduma kulingana na tabaka la walaji.

**Jedwali Na. 1.2: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma kulingana na Tabaka la Kipato (Msingi 2020 = 100), Mwaka 2021 - 2024**

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA CHINI** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2020** | 1.3 | 0.0 | 1.2 | 10.1 | 0.6 | 0.9 | -0.1 | 0.2 | -0.4 | 0.0 | 0.6 | 0.0 | 0.3 | 2.2 |
| **2021** | 0.6 | 7.3 | 3.1 | 2.9 | 3.9 | 1.9 | -7.4 | 1.4 | 3.8 | 10.3 | 5.5 | 0.0 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 7.5 | 0.5 | 3.7 | 3.9 | 6.3 | 2.9 | -2.1 | 1.8 | 13.3 | 2.3 | 3.0 | 0.0 | 3.5 | 4.7 |
| **2023** | 9.8 | 0.7 | 2.4 | 3.4 | 5.3 | 9.1 | -8.4 | 1.0 | 13.8 | 4.4 | 1.9 | 0.0 | 3.5 | 5.2 |
| **2024** | 4.4 | 3.2 | 3.8 | 11.5 | 3.9 | 8.6 | 21.0 | 0.6 | 16.2 | 3.9 | 2.3 | 0.1 | 9.4 | 5.8 |
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA KATI** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2020** | 4.5 | 0.1 | 1.3 | 8.6 | 0.5 | 0.7 | -0.7 | 0.5 | -0.6 | 0.0 | 0.7 | 0.0 | 0.2 | 3.3 |
| **2021** | 1.2 | 4.2 | 0.7 | -1.1 | 4.1 | 4.0 | 2.7 | 1.3 | 0.5 | 5.4 | 10.1 | 0.4 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 9.5 | 0.5 | 2.6 | 5.0 | 4.5 | 1.8 | 7.3 | 0.2 | 16.5 | 1.2 | 3.7 | 0.1 | 3.4 | 5.8 |
| **2023** | 9.9 | 4.0 | 3.0 | 2.5 | 3.8 | 3.5 | 1.2 | 0.0 | 6.4 | 2.8 | 2.9 | -0.1 | 3.5 | 4.9 |
| **2024** | 5.6 | 9.6 | 5.6 | 14.3 | 5.2 | 5.1 | 17.9 | 1.6 | 5.3 | 3.6 | 4.3 | 0.1 | 8.9 | 7.9 |
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA JUU** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2020** | 7.6 | 0.2 | 1.4 | 7.0 | 0.5 | 0.6 | -1.8 | 0.5 | -0.7 | 0.0 | 0.6 | 0.0 | -0.1 | 2.4 |
| **2021** | 3.9 | 11.2 | 3.4 | 0.1 | 8.2 | 3.3 | 1.8 | 1.3 | -1.3 | 3.0 | 7.0 | 0.2 | 1.5 | 3.0 |
| **2022** | 4.8 | 2.3 | 3.1 | 3.4 | 2.5 | 2.0 | 5.9 | 1.1 | 2.3 | 0.8 | 4.0 | 0.0 | 2.3 | 3.8 |
| **2023** | 4.0 | 1.8 | 2.9 | 2.4 | 2.0 | 4.9 | 0.8 | 0.6 | 3.7 | 1.2 | 4.2 | -0.1 | 7.4 | 2.5 |
| **2024** | 5.1 | 5.4 | 5.5 | 8.5 | 3.8 | 4.9 | 5.8 | 4.7 | 9.2 | 6.0 | 5.2 | 0.4 | 26.4 | 6.2 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Ukuzaji Rasilimali

27. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ulifikia shilingi bilioni 66,880.63 ikilinganishwa na shilingi bilioni 60,809.85 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.0. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 76,301.64 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 69,226.05 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ulikuwa asilimia 37.1 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

28. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 77,126.78 kutoka shilingi bilioni 71,482.46 zilizokuwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Aidha, ukuzaji rasilimiali za kudumu kwa bei za mwaka 2015 ulifikia shilingi bilioni 69,140.70 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 63,960.88 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Kwa upande mwingine, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ilipungua kwa shilingi bilioni 3,392.16 mwaka 2024 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 4,175.08 mwaka 2023. Vilevile, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka husika ilipungua kwa

shilingi bilioni 3,432.44 mwaka 2024 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 4,261.13 mwaka 2023.

29. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 23,134.62 kutoka shilingi bilioni 20,944.36 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Aidha, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 53,992.16 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 50,538.10 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Vilevile, sekta ya umma ilichangia asilimia 30.0 ya rasilimali zote za kudumu na sekta binafsi asilimia 70.0 mwaka 2024.

**Jedwali Na. 1: PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **33,916,201** | **36,447,871** | **38,760,377** | **41,851,196** | **44,670,628** | **49,979,019** | **54,052,027** |
| Kilimo cha Mazao | 19,060,478 | 20,066,646 | 21,920,177 | 23,549,769 | 25,580,490 | 30,378,157 | 33,091,582 |
| Mifugo | 9,251,173 | 10,357,287 | 10,622,499 | 11,269,820 | 11,479,664 | 11,678,978 | 12,732,855 |
| Misitu | 3,383,160 | 3,641,955 | 3,720,575 | 4,191,340 | 4,603,883 | 4,804,019 | 4,912,550 |
| Uvuvi | 2,221,390 | 2,381,982 | 2,497,126 | 2,840,267 | 3,006,591 | 3,117,865 | 3,315,039 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **33,410,922** | **37,385,883** | **42,476,524** | **45,334,983** | **52,068,150** | **56,185,595** | **63,460,183** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 6,455,878 | 7,164,222 | 9,867,293 | 11,471,365 | 15436227 | 16,903,691 | 20,843,451 |
| Viwanda | 9,811,013 | 10,512,034 | 11,207,276 | 11,237,325 | 12,170,060 | 13,182,066 | 14,940,873 |
| Umeme | 345,775 | 369,917 | 398,084 | 378,691 | 248,139 | 234,392 | 316,792 |
| Maji safi na Maji taka | 554,536 | 590,324 | 635,959 | 746,403 | 893,174 | 908,275 | 950,587 |
| Ujenzi | 16,243,719 | 18,749,387 | 20,367,912 | 21,501,198 | 23,320,549 | 24,957,172 | 26,408,480 |
| **Huduma** | **46,875,694** | **50,952,480** | **54,021,848** | **57,604,454** | **61,343,645** | **67,784,061** | **74,397,018** |
| Biashara na Matengenezo | 11,067,502 | 12,286,407 | 12,958,573 | 13,789,132 | 14,006,738 | 15,678,782 | 17,662,123 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,381,276 | 9,622,792 | 10,701,520 | 10,860,302 | 11,397,028 | 13,523,735 | 15,383,800 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,653,792 | 1,680,222 | 1,371,161 | 1,601,506 | 1,892,459 | 2,196,214 | 2,327,905 |
| Habari na Mawasiliano | 1,948,180 | 2,052,242 | 2,196,753 | 2,375,155 | 2,605,849 | 2,726,854 | 3,280,596 |
| Fedha na Bima | 4,823,101 | 4,927,613 | 5,013,181 | 5,380,249 | 6,313,664 | 6,391,195 | 6,730,048 |
| Upangishaji Majengo | 3,553,630 | 3,869,528 | 4,348,618 | 4,581,584 | 4,784,774 | 5,086,175 | 5,483,924 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 711,807 | 753,302 | 822,440 | 1,088,002 | 1,175,442 | 1,264,549 | 1,355,768 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,078,145 | 3,340,939 | 3,692,864 | 4,022,127 | 4,297,339 | 4,937,308 | 5,359,593 |
| Utawala na Ulinzi | 5,131,630 | 5,354,893 | 5,530,738 | 5,875,519 | 6,243,146 | 6,581,823 | 6,781,526 |
| Elimu | 3,081,718 | 3,322,028 | 3,440,525 | 3,649,124 | 3,838,330 | 4,130,679 | 4,445,151 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,816,738 | 1,932,964 | 2,060,600 | 2,213,486 | 2,392,940 | 2,601,798 | 2,632,143 |
| Sanaa na Burudani | 374,924 | 427,887 | 416,049 | 513,448 | 623,721 | 749,446 | 896,474 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,037,687 | 1,140,417 | 1,217,190 | 1,358,754 | 1,465,396 | 1,594,457 | 1,732,106 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 215,564 | 241,246 | 251,635 | 296,065 | 306,818 | 321,046 | 325,862 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **114,202,816** | **124,786,234** | **135,258,749** | **144,790,632** | **158,082,423** | **173,948,675** | **191,909,227** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 9,794,956 | 9,753,960 | 10,125,604 | 11,376,505 | 12,737,610 | 12,805,009 | 13,937,266 |
| **Pato la Taifa kwa bei za soko za miaka husika** | **123,997,772** | **134,540,194** | **145,384,353** | **156,167,137** | **170,820,032** | **186,753,685** | **205,846,493** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA

Shilingi Milioni

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A:SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Pato la Taifa - sehemu inayouzika** | **110,217,651** | **119,842,758** | **129,664,277** | **139,270,744** | **152,694,776** | **166,243,573** | **183,424,973** |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **21,296,288** | **22,959,097** | **24,314,330** | **26,295,327** | **27,969,535** | **30,942,993** | **33,427,641** |
| Kilimo cha Mazao | 10,307,806 | 10,851,760 | 11,854,269 | 12,735,397 | 13,833,046 | 16,427,129 | 17,893,272 |
| Mifugo | 6,674,010 | 7,471,864 | 7,663,285 | 8,130,184 | 8,281,247 | 8,424,859 | 9,184,502 |
| Misitu | 2,181,786 | 2,348,644 | 2,399,374 | 2,702,937 | 2,968,865 | 3,097,862 | 3,167,644 |
| Uvuvi | 2,132,686 | 2,286,828 | 2,397,402 | 2,726,809 | 2,886,377 | 2,993,141 | 3,182,223 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **32,392,034** | **36,331,105** | **41,375,431** | **44,176,658** | **50,834,268** | **54,913,777** | **61,881,134** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 6,455,878 | 7,164,222 | 9,867,293 | 11,471,365 | 15,436,227 | 16,903,691 | 20,843,451 |
| Viwanda | 9,811,013 | 10,512,034 | 11,207,276 | 11,237,325 | 12,170,060 | 13,182,066 | 14,940,873 |
| Umeme | 345,775 | 369,917 | 398,084 | 378,691 | 248,139 | 234,392 | 316,792 |
| Maji safi na Maji taka | 387,408 | 412,410 | 448,050 | 525,861 | 629,265 | 639,904 | 669,713 |
| Ujenzi | 15,391,959 | 17,872,522 | 19,454,727 | 20,563,416 | 22,350,577 | 23,953,725 | 25,110,304 |
| **Huduma** | **46,734,373** | **50,798,596** | **53,848,912** | **57,422,253** | **61,153,364** | **67,581,794** | **74,178,933** |
| Biashara na Matengenezo | 11,067,502 | 12,286,407 | 12,958,573 | 13,789,132 | 14,006,738 | 15,678,782 | 17,662,123 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,381,276 | 9,622,792 | 10,701,520 | 10,860,302 | 11,397,028 | 13,523,735 | 15,383,800 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,653,792 | 1,680,222 | 1,371,161 | 1,601,506 | 1,892,459 | 2,196,214 | 2,327,905 |
| Habari na Mawasiliano | 1,948,180 | 2,052,242 | 2,196,753 | 2,375,155 | 2,605,849 | 2,726,854 | 3,280,596 |
| Fedha na Bima | 4,823,101 | 4,927,613 | 5,013,181 | 5,380,249 | 6,313,664 | 6,391,195 | 6,730,048 |
| Upangishaji Majengo | 3,412,309 | 3,715,644 | 4,175,682 | 4,399,384 | 4,594,494 | 4,883,908 | 5,265,840 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 711,807 | 753,302 | 822,440 | 1,088,002 | 1,175,442 | 1,264,549 | 1,355,768 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,078,145 | 3,340,939 | 3,692,864 | 4,022,127 | 4,297,339 | 4,937,308 | 5,359,593 |
| Utawala na Ulinzi | 5,131,630 | 5,354,893 | 5,530,738 | 5,875,519 | 6,243,146 | 6,581,823 | 6,781,526 |
| Elimu | 3,081,718 | 3,322,028 | 3,440,525 | 3,649,124 | 3,838,330 | 4,130,679 | 4,445,151 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,816,738 | 1,932,964 | 2,060,600 | 2,213,486 | 2,392,940 | 2,601,798 | 2,632,143 |
| Sanaa na Burudani | 374,924 | 427,887 | 416,049 | 513,448 | 623,721 | 749,446 | 896,474 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,037,687 | 1,140,417 | 1,217,190 | 1,358,754 | 1,465,396 | 1,594,457 | 1,732,106 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 215,564 | 241,246 | 251,635 | 296,065 | 306,818 | 321,046 | 325,862 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **100,422,695** | **110,088,798** | **119,538,673** | **127,894,238** | **139,957,166** | **153,438,564** | **169,487,707** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 9,794,956 | 9,753,960 | 10,125,604 | 11,376,505 | 12,737,610 | 12,805,009 | 13,937,266 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Pato la Taifa - sehemu isiyouzika** | **13,780,121** | **14,697,436** | **15,720,076** | **16,896,394** | **18,125,257** | **20,510,111** | **22,421,520** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 12,619,912 | 13,488,774 | 14,446,046 | 15,555,869 | 16,701,094 | 19,036,026 | 20,624,386 |
| Mazao | 8,749,506 | 9,211,537 | 10,062,319 | 10,810,523 | 11,743,616 | 13,947,057 | 15,194,462 |
| Mifugo | 2,578,812 | 2,887,197 | 2,961,106 | 3,141,595 | 3,200,334 | 3,256,111 | 3,550,314 |
| Misitu | 1,201,483 | 1,293,414 | 1,321,325 | 1,488,533 | 1,635,169 | 1,706,362 | 1,745,100 |
| Uvuvi | 90,110 | 96,626 | 101,296 | 115,218 | 121,974 | 126,496 | 134,511 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **1,018,888** | **1,054,778** | **1,101,094** | **1,158,324** | **1,233,882** | **1,271,818** | **1,579,049** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 167,128 | 177,914 | 187,909 | 220,543 | 263,910 | 268,372 | 280,874 |
| Ujenzi | 851,760 | 876,864 | 913,184 | 937,781 | 969,972 | 1,003,447 | 1,298,175 |
| **Huduma** | **141,321** | **153,883** | **172,936** | **182,200** | **190,281** | 202,267 | 218,085 |
| Upangishaji Majengo | 141,321 | 153,883 | 172,936 | 182,200 | 190,281 | 202,267 | 218,085 |
| **Pato la Taifa** | **123,997,772** | **134,540,194** | **145,384,353** | **156,167,137** | **170,820,032** | **186,753,685** | **205,846,493** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 3: MCHANGO WA PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***27.4*** | ***27.1*** | ***26.7*** | ***26.8*** | ***26.2*** | ***26.8*** | ***26.3*** |
| Kilimo cha Mazao | 15.4 | 14.9 | 15.1 | 15.1 | 15.0 | 16.3 | 16.1 |
| Mifugo | 7.5 | 7.7 | 7.3 | 7.2 | 6.7 | 6.3 | 6.2 |
| Misitu | 2.7 | 2.7 | 2.6 | 2.7 | 2.7 | 2.6 | 2.4 |
| Uvuvi | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.6 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 5.2 | 5.3 | 6.8 | 7.3 | 9.0 | 9.1 | 10.1 |
| Viwanda | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 7.2 | 7.1 | 7.1 | 7.3 |
| Umeme | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 |
| Maji safi na Maji taka | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| Ujenzi | 13.1 | 13.9 | 14.0 | 13.8 | 13.7 | 13.4 | 12.8 |
| Biashara na Matengenezo | 8.9 | 9.1 | 8.9 | 8.8 | 8.2 | 8.4 | 8.6 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6.8 | 7.2 | 7.4 | 7.0 | 6.7 | 7.2 | 7.5 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1.3 | 1.2 | 0.9 | 1.0 | 1.1 | 1.2 | 1.1 |
| Habari na Mawasiliano | 1.6 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.6 |
| Fedha na Bima | 3.9 | 3.7 | 3.4 | 3.4 | 3.7 | 3.4 | 3.3 |
| Upangishaji Majengo | 2.9 | 2.9 | 3.0 | 2.9 | 2.8 | 2.7 | 2.7 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.7 | 0.7 | 0.7 | 0.7 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.5 | 2.5 | 2.5 | 2.6 | 2.5 | 2.6 | 2.6 |
| Utawala na Ulinzi | 4.1 | 4.0 | 3.8 | 3.8 | 3.7 | 3.5 | 3.3 |
| Elimu | 2.5 | 2.5 | 2.4 | 2.3 | 2.2 | 2.2 | 2.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.3 |
| Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.4 | 0.4 | 0.4 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.9 | 0.9 | 0.9 | 0.8 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **92.1** | **92.8** | **93.0** | **92.7** | **92.5** | **93.1** | **93.2** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 7.9 | 7.2 | 7.0 | 7.3 | 7.5 | 6.9 | 6.8 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 4: MCHANGO WA PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA

Shilingi Milioni

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A:SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Mchango wa Pato la Taifa (GDPmp), sehemu inayouzika** | **88.9** | 89.1 | 89.2 | 89.2 | 89.4 | 89.1 | 89.1 |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***17.2*** | ***17.1*** | ***16.7*** | ***16.8*** | ***16.4*** | ***16.6*** | ***16.2*** |
| Kilimo cha Mazao | *8.3* | *8.1* | *8.2* | *8.2* | *8.1* | *8.8* | *8.7* |
| Mifugo | *5.4* | *5.6* | *5.3* | *5.2* | *4.8* | *4.5* | *4.5* |
| Misitu | *1.8* | *1.7* | *1.7* | *1.7* | *1.7* | *1.7* | *1.5* |
| Uvuvi | *1.7* | *1.7* | *1.6* | *1.7* | *1.7* | *1.6* | *1.5* |
| Uchimbaji Madini na Mawe | *5.2* | *5.3* | *6.8* | *7.3* | *9.0* | *9.1* | *10.1* |
| Viwanda | *7.9* | *7.8* | *7.7* | *7.2* | *7.1* | *7.1* | *7.3* |
| Umeme | *0.3* | *0.3* | *0.3* | *0.2* | *0.1* | *0.1* | *0.2* |
| Maji safi na Maji taka | *0.3* | *0.3* | *0.3* | *0.3* | *0.4* | *0.3* | *0.3* |
| Ujenzi | *12.4* | *13.3* | *13.4* | *13.2* | *13.1* | *12.8* | *12.2* |
| Biashara na Matengenezo | *8.9* | *9.1* | *8.9* | *8.8* | *8.2* | *8.4* | *8.6* |
| Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | *6.8* | *7.2* | *7.4* | *7.0* | *6.7* | *7.2* | *7.5* |
| Malazi na Huduma ya chakula | *1.3* | *1.2* | *0.9* | *1.0* | *1.1* | *1.2* | *1.1* |
| Habari na Mawasiliano | *1.6* | *1.5* | *1.5* | *1.5* | *1.5* | *1.5* | *1.6* |
| Fedha na Bima | *3.9* | *3.7* | *3.4* | *3.4* | *3.7* | *3.4* | *3.3* |
| Upangishaji Majengo | *2.8* | *2.8* | *2.9* | *2.8* | *2.7* | *2.6* | *2.6* |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | *0.6* | *0.6* | *0.6* | *0.7* | *0.7* | *0.7* | *0.7* |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | *2.5* | *2.5* | *2.5* | *2.6* | *2.5* | *2.6* | *2.6* |
| Utawala na Ulinzi | *4.1* | *4.0* | *3.8* | *3.8* | *3.7* | *3.5* | *3.3* |
| Elimu | *2.5* | *2.5* | *2.4* | *2.3* | *2.2* | *2.2* | *2.2* |
| Afya na Huduma za Jamii | *1.5* | *1.4* | *1.4* | *1.4* | *1.4* | *1.4* | *1.3* |
| Sanaa na Burudani | *0.3* | *0.3* | *0.3* | *0.3* | *0.4* | *0.4* | *0.4* |
| Huduma nyingine za Kijamii | *0.8* | *0.8* | *0.8* | *0.9* | *0.9* | *0.9* | *0.8* |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | *0.2* | *0.2* | *0.2* | *0.2* | *0.2* | *0.2* | *0.2* |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **81.0** | **81.8** | **82.2** | **81.9** | **81.9** | **82.2** | **82.3** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 7.9 | 7.2 | 7.0 | 7.3 | 7.5 | 6.9 | 6.8 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Mchango wa Pato la Taifa (GDPmp), sehemu isiyouzika** | **11.1** | **10.9** | **10.8** | **10.8** | **10.6** | **11.0** | **10.9** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 10.2 | 10.0 | 9.9 | 10.0 | 9.8 | 10.2 | 10.0 |
| Mazao | 7.1 | 6.8 | 6.9 | 6.9 | 6.9 | 7.5 | 7.4 |
| Mifugo | 2.1 | 2.1 | 2.0 | 2.0 | 1.9 | 1.7 | 1.7 |
| Misitu | 1.0 | 1.0 | 0.9 | 1.0 | 1.0 | 0.9 | 0.8 |
| Uvuvi | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 |
| Ujenzi | 0.7 | 0.7 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.5 | 0.6 |
| Upangishaji Majengo | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| **Mchango wa Pato la Taifa (GDP)** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 5: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA MATUMIZI

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Matumizi/ Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko za miaka husika** | **123,997,772** | **134,540,194** | **145,384,353** | **156,167,137** | **170,820,032** | **186,753,685** | **205,846,493** |
| **Matumizi ya Mwisho (*Final consumption*)** | **87,527,611** | **92,439,966** | **100,179,732** | **107,062,882** | **115,880,862** | **123,827,382** | **127,869,868** |
| Serikali | 10,468,313 | 10,864,652 | 11,263,617 | 11,862,430 | 12,455,979 | 13,301,054 | 14,298,148 |
| Binafsi | 76,759,564 | 81,252,021 | 88,581,903 | 94,824,443 | 103,000,650 | 110,049,275 | 113,029,048 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 299,734 | 323,293 | 334,212 | 376,009 | 424,233 | 477,052 | 542,672 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **40,639,844** | **46,103,604** | **55,949,293** | **63,708,208** | **67,065,806** | **69,226,052** | **76,301,641** |
| Rasilimali za kudumu | 41,141,962 | 50,010,814 | 60,119,039 | 67,221,823 | 68,247,459 | 71,482,457 | 77,126,778 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 | 1,954,173 | 1,916,891 | 2,004,727 | 2,607,299 |
| Ongezeko la limbikizo | -1,717,221 | -5,180,547 | -6,008,036 | -5,467,787 | -3,098,544 | -4,261,132 | -3,432,436 |
| Mauzo nje | **18,810,172** | **22,101,293** | **19,629,078** | **22,686,817** | **27,609,312** | **33,290,230** | **41,441,353** |
| Bidhaa-fob | 9,720,088 | 12,305,450 | 14,620,151 | 15,523,687 | 16,639,963 | 18,388,713 | 23,700,866 |
| Huduma | 9,090,084 | 9,795,843 | 5,008,927 | 7,163,130 | 10,969,349 | 14,901,517 | 17,740,487 |
| Uagizaji | **23,653,216** | **23,806,198** | **20,992,737** | **26,675,720** | **38,409,637** | **38,287,767** | **43,472,508** |
| Bidhaa-fob | 19,294,815 | 19,713,653 | 17,967,329 | 22,983,447 | 32,730,313 | 32,795,993 | 37,111,751 |
| Huduma | 4,358,401 | 4,092,545 | 3,025,408 | 3,692,272 | 5,679,323 | 5,491,774 | 6,360,757 |
| Makosa na Mapungufu | 673,361 | -2,298,472 | -9,381,013 | -10,615,051 | -1,326,310 | -1,302,212 | 3,706,139 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 6: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***29,504,236*** | ***30,802,622*** | ***32,323,673*** | ***33,588,777*** | ***34,711,277*** | ***36,184,322*** | ***37,677,355*** |
| Kilimo cha Mazao | 15,679,338 | 16,372,351 | 17,196,815 | 17,818,276 | 18,295,700 | 19,064,330 | 19,820,710 |
| Mifugo | 8,276,692 | 8,687,238 | 9,119,559 | 9,574,892 | 10,054,947 | 10,560,054 | 11,092,431 |
| Misitu | 3,339,085 | 3,499,684 | 3,612,827 | 3,739,795 | 3,857,006 | 4,021,644 | 4,166,922 |
| Uvuvi | 2,209,121 | 2,243,349 | 2,394,472 | 2,455,814 | 2,503,624 | 2,538,294 | 2,597,292 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***31,344,128*** | ***34,912,847*** | ***37,251,857*** | ***39,085,652*** | ***41,147,936*** | ***43,234,380*** | ***45,565,454*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 4,659,195 | 5,485,112 | 5,887,452 | 6,442,881 | 7,138,149 | 7,945,921 | 8,605,295 |
| Viwanda | 9,623,501 | 10,184,558 | 10,646,279 | 11,155,762 | 11,624,144 | 12,128,562 | 12,712,638 |
| Umeme | 928,174 | 994,879 | 1,049,610 | 1,154,204 | 1,242,132 | 1,290,960 | 1,477,093 |
| Maji safi na Maji taka | 477,510 | 510,411 | 540,159 | 575,213 | 606,754 | 621,827 | 647,165 |
| Ujenzi | 15,655,747 | 17,737,886 | 19,128,358 | 19,757,591 | 20,536,757 | 21,247,110 | 22,123,264 |
| ***Huduma*** | ***45,453,302*** | ***48,133,895*** | ***50,196,792*** | ***52,618,667*** | ***55,393,899*** | ***58,736,452*** | ***62,613,070*** |
| Biashara na Matengenezo | 10,480,204 | 10,984,480 | 11,216,401 | 11,578,146 | 12,031,598 | 12,542,371 | 13,142,577 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,736,561 | 9,493,191 | 10,293,276 | 10,658,344 | 11,061,950 | 11,510,657 | 11,990,434 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,604,391 | 1,645,950 | 1,419,654 | 1,514,711 | 1,651,099 | 1,788,242 | 1,895,759 |
| Habari na Mawasiliano | 1,989,717 | 2,133,312 | 2,313,032 | 2,524,610 | 2,712,411 | 2,917,297 | 3,334,135 |
| Fedha na Bima | 4,094,972 | 4,281,167 | 4,412,967 | 4,599,677 | 5,024,301 | 5,760,339 | 6,557,881 |
| Upangishaji Majengo | 3,354,518 | 3,505,485 | 3,663,972 | 3,827,460 | 3,997,460 | 4,168,722 | 4,347,172 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 763,332 | 821,636 | 881,833 | 942,013 | 996,609 | 1,051,696 | 1,102,104 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,054,288 | 3,311,753 | 3,569,800 | 3,817,047 | 3,993,799 | 4,191,805 | 4,452,483 |
| Utawala na Ulinzi | 5,064,968 | 5,238,491 | 5,438,146 | 5,713,411 | 6,024,203 | 6,358,312 | 6,674,839 |
| Elimu | 3,046,789 | 3,257,406 | 3,365,355 | 3,537,611 | 3,724,729 | 3,955,485 | 4,202,312 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,746,731 | 1,833,514 | 1,953,479 | 2,065,349 | 2,176,986 | 2,308,205 | 2,540,398 |
| Sanaa na Burudani | 350,027 | 389,225 | 372,120 | 444,488 | 528,722 | 622,264 | 728,773 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 971,690 | 1,037,083 | 1,089,265 | 1,181,814 | 1,249,425 | 1,333,612 | 1,411,680 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 195,113 | 201,203 | 207,492 | 213,987 | 220,607 | 227,445 | 232,523 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **106,301,666** | **113,849,364** | **119,772,323** | **125,293,096** | **131,253,112** | **138,155,154** | **145,855,878** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 8,872,802 | 9,289,875 | 8,951,215 | 9,658,417 | *9,994,080* | *10,365,863* | *10,779,441* |
| **Pato la Taifa (GDP)** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,521,017** | **156,635,319** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 7: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)- sehemu inayouzika** | **110,243,681** | **117,953,902** | **123,282,166** | **129,347,848** | **135,459,199** | **142,543,071** | **150,307,903** |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***25,671,369*** | ***26,821,324*** | ***28,173,634*** | ***29,292,547*** | ***30,264,345*** | ***31,539,362*** | ***32,833,743*** |
| Kilimo cha Mazao | 13,381,343 | 13,996,558 | 14,711,216 | 15,252,963 | 15,658,987 | 16,316,897 | 16,964,164 |
| Mifugo | 7,090,719 | 7,446,156 | 7,832,125 | 8,233,750 | 8,646,525 | 9,080,909 | 9,538,656 |
| Misitu | 3,007,003 | 3,152,322 | 3,253,511 | 3,368,590 | 3,474,151 | 3,622,458 | 3,753,292 |
| Uvuvi | 2,192,305 | 2,226,288 | 2,376,783 | 2,437,243 | 2,484,681 | 2,519,097 | 2,577,632 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***30,352,531*** | ***33,819,773*** | ***36,076,540*** | ***37,899,047*** | ***39,933,072*** | ***42,032,997*** | ***44,218,887*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 4,659,195 | 5,485,112 | 5,887,452 | 6,442,881 | 7,138,149 | 7,945,921 | 8,605,295 |
| Viwanda | 9,623,501 | 10,184,558 | 10,646,279 | 11,155,762 | 11,624,144 | 12,128,562 | 12,712,638 |
| Umeme | 928,174 | 994,879 | 1,049,610 | 1,154,204 | 1,242,132 | 1,290,960 | 1,477,093 |
| Maji safi na Maji taka | 369,545 | 396,149 | 420,891 | 448,945 | 473,562 | 485,327 | 505,102 |
| Ujenzi | 14,772,116 | 16,759,074 | 18,072,308 | 18,697,255 | 19,455,085 | 20,182,229 | 20,918,759 |
| ***Huduma*** | ***45,346,979*** | ***48,022,931*** | ***50,080,777*** | ***52,497,837*** | ***55,267,702*** | ***58,604,849*** | ***62,475,833*** |
| Biashara na Matengenezo | 10,480,204 | 10,984,480 | 11,216,401 | 11,578,146 | 12,031,598 | 12,542,371 | 13,142,577 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,736,561 | 9,493,191 | 10,293,276 | 10,658,344 | 11,061,950 | 11,510,657 | 11,990,434 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,604,391 | 1,645,950 | 1,419,654 | 1,514,711 | 1,651,099 | 1,788,242 | 1,895,759 |
| Habari na Mawasiliano | 1,989,717 | 2,133,312 | 2,313,032 | 2,524,610 | 2,712,411 | 2,917,297 | 3,334,135 |
| Fedha na Bima | 4,094,972 | 4,281,167 | 4,412,967 | 4,599,677 | 5,024,301 | 5,760,339 | 6,557,881 |
| Upangishaji Majengo | 3,248,194 | 3,394,521 | 3,547,957 | 3,706,630 | 3,871,263 | 4,037,119 | 4,209,935 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 763,332 | 821,636 | 881,833 | 942,013 | 996,609 | 1,051,696 | 1,102,104 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,054,288 | 3,311,753 | 3,569,800 | 3,817,047 | 3,993,799 | 4,191,805 | 4,452,483 |
| Utawala na Ulinzi | 5,064,968 | 5,238,491 | 5,438,146 | 5,713,411 | 6,024,203 | 6,358,312 | 6,674,839 |
| Elimu | 3,046,789 | 3,257,406 | 3,365,355 | 3,537,611 | 3,724,729 | 3,955,485 | 4,202,312 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,746,731 | 1,833,514 | 1,953,479 | 2,065,349 | 2,176,986 | 2,308,205 | 2,540,398 |
| Sanaa na Burudani | 350,027 | 389,225 | 372,120 | 444,488 | 528,722 | 622,264 | 728,773 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 971,690 | 1,037,083 | 1,089,265 | 1,181,814 | 1,249,425 | 1,333,612 | 1,411,680 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 195,113 | 201,203 | 207,492 | 213,987 | 220,607 | 227,445 | 232,523 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **101,370,879** | **108,664,027** | **114,330,951** | **119,689,431** | **125,465,119** | **132,177,208** | **139,528,462** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 8,872,802 | 9,289,875 | 8,951,215 | 9,658,417 | 9,994,080 | 10,365,863 | 10,779,441 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp) - sehemu isiyouzika** | **4,930,787** | **5,185,336** | **5,441,372** | **5,603,665** | **5,787,994** | **5,977,946** | **6,327,416** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 3,832,866 | 3,981,298 | 4,150,038 | 4,296,231 | 4,446,932 | 4,644,960 | 4,843,612 |
| Mazao | 2,297,609 | 2,375,410 | 2,485,190 | 2,564,893 | 2,636,294 | 2,746,997 | 2,856,114 |
| Mifugo | 1,185,810 | 1,240,908 | 1,287,262 | 1,340,971 | 1,408,250 | 1,478,965 | 1,553,596 |
| Misitu | 332,233 | 347,517 | 359,470 | 371,362 | 383,014 | 399,356 | 413,801 |
| Uvuvi | 17,215 | 17,464 | 18,116 | 19,004 | 19,375 | 19,643 | 20,100 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **991,597** | **1,093,074** | **1,175,318** | **1,186,604** | **1,214,865** | **1,201,382** | **1,346,567** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 107,966 | 114,262 | 119,268 | 126,268 | 133,192 | 136,501 | 142,063 |
| Ujenzi | 883,632 | 978,812 | 1,056,050 | 1,060,336 | 1,081,673 | 1,064,881 | 1,204,504 |
| **Huduma** | **106,323** | **110,964** | **116,016** | **120,830** | **126,197** | **131,603** | **137,237** |
| Upangishaji Majengo | 106,323 | 110,964 | 116,016 | 120,830 | 126,197 | 131,603 | 137,237 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko za mwaka 2015** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,521,017** | **156,635,319** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu


**Jedwali Na. 8: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | **5.4** | 4.4 | 4.9 | 3.9 | 3.3 | 4.2 | 4.1 |
| Kilimo cha Mazao | 5.2 | 4.4 | 5.0 | 3.6 | 2.7 | 4.2 | 4.0 |
| Mifugo | 4.9 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 4.9 | 4.8 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 | 3.6 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.5 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 | 2.3 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 1.5 | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 | 8.3 |
| Viwanda | 8.3 | 5.8 | 4.5 | 4.8 | 4.2 | 4.3 | 4.8 |
| Umeme | 5.8 | 7.2 | 5.5 | 10.0 | 7.6 | 3.9 | 14.4 |
| Maji safi na Maji taka | 7.4 | 6.9 | 5.8 | 6.5 | 5.5 | 2.5 | 4.1 |
| Ujenzi | 13.8 | 13.3 | 7.8 | 3.3 | 3.9 | 3.5 | 4.1 |
| Biashara na Matengenezo | 6.6 | 4.8 | 2.1 | 3.2 | 3.9 | 4.2 | 4.8 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 11.8 | 8.7 | 8.4 | 3.5 | 3.8 | 4.1 | 4.2 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 5.2 | 2.6 | -13.7 | 6.7 | 9.0 | 8.3 | 6.0 |
| Habari na Mawasiliano | 9.1 | 7.2 | 8.4 | 9.1 | 7.4 | 7.6 | 14.3 |
| Fedha na Bima | -0.5 | 4.5 | 3.1 | 4.2 | 9.2 | 14.6 | 13.8 |
| Upangishaji Majengo | 4.4 | 4.5 | 4.5 | 4.5 | 4.4 | 4.3 | 4.3 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 9.9 | 7.6 | 7.3 | 6.8 | 5.8 | 5.5 | 4.8 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 5.6 | 8.4 | 7.8 | 6.9 | 4.6 | 5.0 | 6.2 |
| Utawala na Ulinzi | 3.2 | 3.4 | 3.8 | 5.1 | 5.4 | 5.5 | 5.0 |
| Elimu | 6.6 | 6.9 | 3.3 | 5.1 | 5.3 | 6.2 | 6.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 8.4 | 5.0 | 6.5 | 5.7 | 5.4 | 6.0 | 10.1 |
| Sanaa na Burudani | 13.7 | 11.2 | -4.4 | 19.4 | 19.0 | 17.7 | 17.1 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 6.5 | 6.7 | 5.0 | 8.5 | 5.7 | 6.7 | 5.9 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 2.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **6.9** | **7.1** | **5.2** | **4.6** | **4.8** | **5.3** | **5.6** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 6.3 | 4.7 | -3.6 | 7.9 | 3.5 | 3.7 | 4.0 |
| **Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za soko za mwaka 2015** | **7.0** | **6.9** | **4.5** | **4.8** | **4.7** | **5.1** | **5.5** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 1.6: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (BEI ZA MWAKA 2015)**



## Jedwali Na. 9: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Ukuaji wa Pato la Taifa - sehemu inayouzika** | **7.1** | **7.0** | **4.5** | **4.9** | **4.7** | **5.1** | **5.5** |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **5.4** | **4.5** | **5.0** | **4.0** | **3.3** | **4.2** | **4.1** |
| Kilimo cha Mazao | 5.6 | 4.6 | 5.1 | 3.7 | 2.7 | 4.2 | 4.0 |
| Mifugo | 4.2 | 5.0 | 5.2 | 5.1 | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 5.2 | 4.8 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 | 3.6 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.6 | 6.8 | 2.5 | 1.9 | 1.4 | 2.3 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 1.5 | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 | 8.3 |
| Viwanda | 8.3 | 5.8 | 4.5 | 4.8 | 4.2 | 4.3 | 4.8 |
| Umeme | 5.8 | 7.2 | 5.5 | 10.0 | 7.6 | 3.9 | 14.4 |
| Maji safi na Maji taka | 5.6 | 7.2 | 6.2 | 6.7 | 5.5 | 2.5 | 4.1 |
| Ujenzi | 13.8 | 13.5 | 7.8 | 3.5 | 4.1 | 3.7 | 3.6 |
| Biashara na Matengenezo | 6.6 | 4.8 | 2.1 | 3.2 | 3.9 | 4.2 | 4.8 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 11.8 | 8.7 | 8.4 | 3.5 | 3.8 | 4.1 | 4.2 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 5.2 | 2.6 | -13.7 | 6.7 | 9.0 | 8.3 | 6.0 |
| Habari na Mawasiliano | 9.1 | 7.2 | 8.4 | 9.1 | 7.4 | 7.6 | 14.3 |
| Fedha na Bima | -0.5 | 4.5 | 3.1 | 4.2 | 9.2 | 14.6 | 13.8 |
| Upangishaji Majengo | 4.3 | 4.5 | 4.5 | 4.5 | 4.4 | 4.3 | 4.3 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 9.9 | 7.6 | 7.3 | 6.8 | 5.8 | 5.5 | 4.8 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 5.6 | 8.4 | 7.8 | 6.9 | 4.6 | 5.0 | 6.2 |
| Utawala na Ulinzi | 3.2 | 3.4 | 3.8 | 5.1 | 5.4 | 5.5 | 5.0 |
| Elimu | 6.6 | 6.9 | 3.3 | 5.1 | 5.3 | 6.2 | 6.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 8.4 | 5.0 | 6.5 | 5.7 | 5.4 | 6.0 | 10.1 |
| Sanaa na Burudani | 13.7 | 11.2 | -4.4 | 19.4 | 19.0 | 17.7 | 17.1 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 6.5 | 6.7 | 5.0 | 8.5 | 5.7 | 6.7 | 5.9 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 2.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **7.1** | **7.2** | **5.2** | **4.7** | **4.8** | **5.3** | **5.6** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 6.3 | 4.7 | -3.6 | 7.9 | 3.5 | 3.7 | 4.0 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Ukuaji wa Pato la Taifa - sehemu isiyouzika** | 6.5 | 5.2 | 4.9 | 3.0 | 3.3 | 3.3 | 5.8 |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 5.0 | 3.9 | 4.2 | 3.5 | 3.5 | 4.5 | 4.3 |
| Mazao | 3.1 | 3.4 | 4.6 | 3.2 | 2.8 | 4.2 | 4.0 |
| Mifugo | 9.8 | 4.6 | 3.7 | 4.2 | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 1.7 | 4.6 | 3.4 | 3.3 | 3.1 | 4.3 | 3.6 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.4 | 3.7 | 4.9 | 2.0 | 1.4 | 2.3 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 14.1 | 5.8 | 4.4 | 5.9 | 5.5 | 2.5 | 4.1 |
| Ujenzi | 12.5 | 10.8 | 7.9 | 0.4 | 2.0 | -1.6 | 13.1 |
| Upangishaji Majengo | 9.9 | 4.4 | 4.6 | 4.1 | 4.4 | 4.3 | 4.3 |
| **Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za soko za mwaka 2015** | **7.0** | **6.9** | **4.5** | **4.8** | **4.7** | **5.1** | **5.5** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 10: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2015 KWA AINA YA MATUMIZI

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Matumizi | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Gharama zake (GDPbp)** | **106,301,666** | **113,849,364** | **119,772,323** | **125,293,096** | **131,253,112** | **138,155,154** | **145,855,878** |
| **Kodi za uzalishaji** | **8,872,802** | **9,289,875** | **8,951,215** | **9,658,417** | **9,994,080** | **10,365,863** | **10,779,441** |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,521,017** | **156,635,319** |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko za mwaka 2015** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,521,017** | **156,635,319** |
| **Matumizi ya Mwisho(Final consumption)** | **77,496,083** | **79,584,578** | **83,532,038** | **87,480,181** | **89,503,360** | **92,394,403** | **98,591,315** |
| Serikali | 9,965,992 | 10,196,780 | 10,457,021 | 10,804,144 | 11,149,850 | 11,831,714 | 13,621,838 |
| Binafsi | 67,252,169 | 69,096,209 | 72,777,412 | 76,351,978 | 77,997,028 | 80,174,169 | 84,543,762 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 277,922 | 291,589 | 297,605 | 324,059 | 356,482 | 388,521 | 425,715 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **45,155,626** | **48,650,734** | **51,210,017** | **54,636,423** | **61,112,749** | **60,809,850** | **66,880,629** |
| Rasilimali za kudumu | 46,824,212 | 53,293,526 | 56,436,601 | 58,860,660 | 63,270,605 | 63,960,884 | 69,140,700 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 776,123 | 925,034 | 1,096,591 | 1,161,299 | 1,043,459 | 1,024,048 | 1,132,087 |
| Ongezeko la limbikizo | -2,444,709 | -5,567,827 | -6,323,175 | -5,385,536 | -3,201,316 | -4,175,082 | -3,392,158 |
| Mauzo nje | **15,273,479** | **18,015,712** | **14,958,602** | **17,301,312** | **20,307,688** | **22,944,215** | **26,161,351** |
| Bidhaa-fob | 7,559,698 | 9,941,744 | 10,400,109 | 11,030,299 | 11,055,648 | 11,309,498 | 13,385,376 |
| Huduma | 7,713,780 | 8,073,968 | 4,558,493 | 6,271,013 | 9,252,039 | 11,634,717 | 12,775,975 |
| Uagizaji | **22,569,279** | **21,717,641** | **19,867,913** | **24,412,030** | **32,068,975** | **30,563,534** | **33,520,861** |
| Bidhaa-fob | 19,092,549 | 18,560,540 | 17,441,130 | 21,500,877 | 27,899,126 | 26,637,365 | 29,193,722 |
| Huduma | 3,476,730 | 3,157,101 | 2,426,783 | 2,911,153 | 4,169,849 | 3,926,170 | 4,327,139 |
| Makosa na Mapungufu | -181,441 | -1,394,144 | -1,109,207 | -54,373 | 2,392,371 | 2,936,083 | -1,477,115 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 11: UKUZAJI RASILIMALI KWA KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Rasilimali/ Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 34,044,435 | 42,221,028 | 49,747,719 | 55,339,606 | 56,289,401 | 57,488,804 | 61,422,001 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,439,945 | 1,626,468 | 2,104,131 | 2,525,856 | 2,566,601 | 2,523,075 | 3,374,687 |
| Mitambo na Vifaa | 2,776,908 | 2,951,572 | 4,057,780 | 4,577,241 | 4,591,367 | 6,452,530 | 6,948,222 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 1,378,753 | 1,501,925 | 2,014,715 | 2,322,447 | 2,279,644 | 2,294,783 | 2,478,163 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 417,015 | 476,835 | 609,366 | 729,533 | 726,652 | 683,694 | 717,001 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,084,906 | 1,232,987 | 1,585,327 | 1,727,139 | 1,793,793 | 2,039,571 | 2,186,702 |
| Rasilimali za kudumu | 41,141,962 | 50,010,814 | 60,119,039 | 67,221,823 | 68,247,459 | 71,482,457 | 77,126,778 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 | 1,954,173 | 1,916,891 | 2,004,727 | 2,607,299 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -1,717,221 | -5,180,547 | -6,008,036 | -5,467,787 | -3,098,544 | -4,261,132 | -3,432,436 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **40,639,844** | **46,103,604** | **55,949,293** | **63,708,208** | **67,065,806** | **69,226,052** | **76,301,641** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 12: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MWAKA 2015 KWA AINA YA RASILIMALI

**Shilingi Milioni**

| **Aina ya Rasilimali/ Mwaka** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023r** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 38,590,978 | 44,798,699 | 46,631,376 | 48,634,282 | 52,329,858 | 51,643,709 | 54,162,029 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,876,483 | 2,108,988 | 2,148,677 | 2,143,604 | 2,365,663 | 3,085,376 | 5,336,422 |
| Mitambo na Vifaa | 3,223,695 | 3,048,264 | 3,789,868 | 4,050,012 | 4,245,799 | 5,191,264 | 5,325,054 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 1,531,393 | 1,549,217 | 1,843,357 | 1,925,453 | 2,103,267 | 1,795,030 | 1,923,105 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 434,150 | 468,173 | 524,605 | 548,111 | 586,026 | 550,319 | 577,128 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,167,515 | 1,320,184 | 1,498,719 | 1,559,197 | 1,639,992 | 1,695,187 | 1,816,962 |
| Rasilimali za kudumu | 46,824,212 | 53,293,526 | 56,436,601 | 58,860,660 | 63,270,605 | 63,960,884 | 69,140,700 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 776,123 | 925,034 | 1,096,591 | 1,161,299 | 1,043,459 | 1,024,048 | 1,132,087 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | (2,444,709) | (5,567,827) | (6,323,175) | (5,385,536) | (3,201,316) | (4,175,082) | (3,392,158) |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **45,155,626** | **48,650,734** | **51,210,017** | **54,636,423** | **61,112,749** | **60,809,850** | **66,880,629** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 13: MCHANGO KATIKA UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI**

**Asilimia**

| **Aina** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023r** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 83.8 | 91.6 | 88.9 | 86.9 | 83.9 | 83.0 | 80.5 |
| Vifaa vya Usafiri | 3.5 | 3.5 | 3.8 | 4.0 | 3.8 | 3.6 | 4.4 |
| Mitambo na Vifaa | 6.8 | 6.4 | 7.3 | 7.2 | 6.8 | 9.3 | 9.1 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 3.4 | 3.3 | 3.6 | 3.6 | 3.4 | 3.3 | 3.2 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 1.0 | 1.0 | 1.1 | 1.1 | 1.1 | 1.0 | 0.9 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 2.7 | 2.7 | 2.8 | 2.7 | 2.7 | 2.9 | 2.9 |
| Rasilimali za kudumu | 101.2 | 108.5 | 107.5 | 105.5 | 101.8 | 103.3 | 101.1 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 3.0 | 2.8 | 3.3 | 3.1 | 2.9 | 2.9 | 3.4 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -4.2 | -11.2 | -10.7 | -8.6 | -4.6 | -6.2 | -4.5 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 14: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA SEKTA

**Shilingi Milioni**

| **Sekta** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023r** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A. Rasilimali za kudumu | 41,141,962 | 50,010,814 | 60,119,039 | 67,221,823 | 68,247,459 | 71,482,457 | 77,126,778 |
| Serikali: | 10,716,619 | 12,602,717 | 15,570,831 | 16,939,888 | 16,738,193 | 17,155,790 | 18,913,260 |
| Mashirika: | 903,317 | 1,050,226 | 1,442,857 | 1,645,300 | 1,744,776 | 1,858,544 | 2,027,813 |
| Taasisi: | 862,257 | 1,200,259 | 1,563,095 | 1,749,614 | 1,748,131 | 1,930,026 | 2,193,548 |
| Sekta binafsi | 28,659,770 | 35,157,613 | 41,542,256 | 46,887,021 | 48,016,360 | 50,538,097 | 53,992,156 |
| B: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 | 1,954,173 | 1,916,891 | 2,004,727 | 2,607,299 |
| C. Ongezeko la Limbikizo | -1,717,221 | -5,180,547 | -6,008,036 | -5,467,787 | -3,098,544 | -4,261,132 | 3,432,436 |
| **Jumla la Ukuzaji Rasilimali (A+B+C)** | **40,639,844** | **46,103,604** | **55,949,293** | **63,708,208** | **67,065,806** | **69,226,052** | **76,301,641** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 15: FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)**

| MWAKA | BIDHAA ZOTE | | ***VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI | |
|---|---|---|---|---|
| | FAHIRISI | BADILIKO (ASILIMIA) | FAHIRISI | BADILIKO (ASILIMIA) |
| 2016 | 90.9 | | 87.52 | |
| 2017 | 92.6 | 1.9 | 90.53 | 3.4 |
| 2018 | 94.4 | 2.0 | 94.59 | 4.5 |
| 2019 | 98.0 | 3.8 | 98.93 | 4.6 |
| **2020 | 100.00 | 2.1 | 100.00 | 1.1 |
| 2021 | 102.37 | 2.4 | 100.58 | 0.6 |
| 2022 | 107.16 | 4.7 | 108.16 | 7.5 |
| 2023 | 112.77 | 5.2 | 118.78 | 9.8 |
| 2024 | 119.30 | 5.8 | 123.98 | 4.4 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI

## Jedwali Na. 16: FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 = 100)

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 87.52 | 96.37 | 90.95 | 81.16 | 92.80 | 94.57 | 109.22 | 98.54 | 95.16 | 91.47 | 96.60 | 91.76 | 95.45 | 90.94 |
| 2017 | 90.53 | 99.20 | 92.14 | 81.89 | 95.71 | 96.03 | 109.11 | 98.91 | 96.76 | 95.02 | 97.12 | 94.10 | 96.08 | 92.63 |
| 2018 | 94.59 | 99.20 | 95.03 | 86.58 | 97.53 | 96.10 | 95.51 | 98.82 | 97.84 | 100.22 | 97.23 | 96.17 | 97.49 | 94.44 |
| 2019 | 98.93 | 99.98 | 98.79 | 91.42 | 99.42 | 99.13 | 100.23 | 99.79 | 100.13 | 100.12 | 99.36 | 100.00 | 99.66 | 97.99 |
| 2020** | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 |
| 2021 | 100.58 | 107.27 | 103.06 | 102.93 | 103.91 | 101.93 | 92.55 | 101.39 | 103.83 | 110.34 | 105.46 | 100.00 | 100.71 | 102.37 |
| 2022 | 108.16 | 107.86 | 106.86 | 106.97 | 110.42 | 104.89 | 90.61 | 103.25 | 117.66 | 112.84 | 108.58 | 100.00 | 104.23 | 107.16 |
| 2023 | 118.78 | 108.60 | 109.45 | 110.63 | 116.24 | 114.46 | 82.97 | 104.32 | 133.86 | 117.78 | 110.68 | 99.97 | 107.88 | 112.77 |
| 2024 | 123.98 | 112.13 | 113.60 | 123.32 | 120.74 | 124.33 | 100.38 | 104.97 | 155.60 | 122.42 | 113.21 | 100.04 | 117.99 | 119.30 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 17: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)**

| Mwaka | Miezi/ Robo-Mwaka | | | | | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Wastani | |
| 2016 | 87.19 | 89.15 | 88.69 | 88.67 | 88.43 | |
| 2017 | 89.26 | 91.18 | 91.12 | 91.43 | 90.75 | 2.6 |
| 2018 | 90.35 | 92.69 | 92.89 | 93.83 | 92.44 | 1.9 |
| 2019 | 95.62 | 96.95 | 96.51 | 97.36 | 96.61 | 4.5 |
| **2020 | 99.69 | 99.96 | 100.42 | 99.92 | 100.00 | 3.5 |
| 2021 | 101.71 | 102.57 | 101.87 | 103.45 | 102.40 | 2.4 |
| 2022 | 105.12 | 108.89 | 109.48 | 110.01 | 108.38 | 5.8 |
| 2023 | 112.37 | 113.39 | 113.78 | 115.33 | 113.72 | 4.9 |
| 2024 | 120.76 | 124.14 | 123.00 | 122.80 | 122.68 | 7.9 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

## Jedwali Na. 18: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)

| | ***Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesin a Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2018 Robo ya kwanza | 87.41 | 99.43 | 93.46 | 82.62 | 96.44 | 94.88 | 94.15 | 98.17 | 97.69 | 100.03 | 96.12 | 100.00 | 95.48 | 90.35 |
| Robo ya pili | 92.18 | 99.43 | 94.58 | 84.42 | 97.15 | 95.01 | 94.50 | 98.07 | 98.37 | 100.03 | 96.12 | 100.00 | 96.96 | 92.69 |
| Robo ya tatu | 91.69 | 99.43 | 96.00 | 85.55 | 97.52 | 95.08 | 94.95 | 98.02 | 98.17 | 100.03 | 96.66 | 100.00 | 97.39 | 92.89 |
| Robo ya nne | 91.00 | 99.57 | 97.63 | 89.50 | 98.39 | 95.20 | 98.33 | 98.07 | 98.72 | 100.03 | 97.90 | 100.00 | 98.28 | 93.83 |
| 2019 Robo ya kwanza | 93.66 | 99.85 | 98.02 | 90.52 | 99.33 | 98.34 | 100.45 | 99.40 | 99.92 | 100.03 | 99.34 | 100.00 | 99.95 | 95.62 |
| Robo ya pili | 96.72 | 99.85 | 98.57 | 90.39 | 99.55 | 99.59 | 101.06 | 99.87 | 100.12 | 100.03 | 99.47 | 100.00 | 100.03 | 96.95 |
| Robo ya tatu | 95.12 | 99.85 | 99.20 | 91.58 | 99.39 | 99.60 | 101.06 | 99.15 | 101.01 | 100.03 | 99.45 | 100.00 | 99.44 | 96.51 |
| Robo ya nne | 97.19 | 99.85 | 99.17 | 92.21 | 99.71 | 99.69 | 100.61 | 99.30 | 99.70 | 100.03 | 99.04 | 100.00 | 99.67 | 97.36 |
| **2020 Robo ya kwanza | 101.46 | 99.85 | 99.85 | 96.53 | 99.93 | 99.71 | 100.93 | 99.54 | 99.97 | 100.00 | 99.05 | 100.00 | 99.25 | 99.87 |
| Robo ya pili | 99.72 | 99.85 | 99.96 | 101.49 | 99.99 | 100.04 | 99.31 | 100.15 | 99.99 | 100.00 | 99.05 | 100.00 | 99.88 | 99.99 |
| Robo ya tatu | 99.38 | 99.85 | 99.95 | 102.39 | 100.04 | 100.12 | 99.53 | 100.15 | 100.02 | 100.00 | 100.95 | 100.00 | 100.30 | 100.26 |
| Robo ya nne | 99.44 | 100.44 | 100.24 | 99.59 | 100.03 | 100.12 | 100.23 | 100.15 | 100.02 | 100.00 | 100.95 | 100.00 | 100.57 | 99.89 |
| 2021 Robo ya kwanza | 100.68 | 104.06 | 100.68 | 99.92 | 102.79 | 103.70 | 100.91 | 101.36 | 100.06 | 104.76 | 107.20 | 100.00 | 100.21 | 101.71 |
| Robo ya pili | 102.03 | 104.31 | 99.99 | 97.98 | 104.06 | 103.97 | 102.50 | 101.24 | 100.64 | 105.60 | 110.88 | 100.57 | 100.75 | 102.57 |
| Robo ya tatu | 99.63 | 103.90 | 100.16 | 97.71 | 104.07 | 103.97 | 103.47 | 101.25 | 100.57 | 105.53 | 110.88 | 100.57 | 100.69 | 101.87 |
| Robo ya nne | 102.36 | 104.56 | 101.79 | 99.97 | 105.36 | 104.32 | 103.99 | 101.54 | 100.55 | 105.54 | 111.53 | 100.57 | 100.99 | 103.45 |
| 2022 Robo ya kwanza | 104.28 | 104.70 | 102.85 | 103.83 | 107.30 | 104.48 | 104.25 | 101.62 | 115.16 | 105.54 | 112.88 | 100.57 | 102.20 | 105.12 |
| Robo ya pili | 111.70 | 104.70 | 102.92 | 105.35 | 107.68 | 105.19 | 111.04 | 101.59 | 116.25 | 106.11 | 114.50 | 100.55 | 104.65 | 108.89 |
| Robo ya tatu | 112.07 | 104.98 | 103.70 | 102.76 | 108.73 | 106.41 | 116.39 | 101.55 | 118.18 | 107.27 | 114.05 | 100.50 | 104.76 | 109.48 |
| Robo ya nne | 115.03 | 104.70 | 103.78 | 103.51 | 111.09 | 107.18 | 109.37 | 101.56 | 118.64 | 107.38 | 115.53 | 100.46 | 104.89 | 110.01 |
| 2023 Robo ya kwanza | 121.13 | 104.70 | 104.57 | 103.76 | 111.53 | 107.83 | 109.30 | 101.54 | 120.57 | 109.58 | 116.90 | 100.49 | 105.45 | 112.37 |
| Robo ya pili | 123.48 | 104.70 | 104.99 | 105.94 | 111.20 | 107.82 | 108.40 | 101.42 | 123.91 | 109.58 | 117.24 | 100.45 | 105.68 | 113.39 |
| Robo ya tatu | 120.59 | 112.05 | 106.94 | 106.05 | 113.29 | 111.18 | 113.17 | 101.55 | 126.12 | 109.58 | 117.83 | 100.41 | 110.01 | 113.78 |
| Robo ya nne | 121.68 | 114.61 | 109.24 | 109.89 | 115.50 | 111.20 | 115.27 | 101.69 | 127.72 | 109.58 | 118.07 | 100.52 | 110.03 | 115.33 |
| 2024 Robo ya kwanza | 127.91 | 117.08 | 111.54 | 115.23 | 117.49 | 114.84 | 127.60 | 103.23 | 129.17 | 111.59 | 122.17 | 100.58 | 115.08 | 120.76 |
| Robo ya pili | 131.42 | 119.97 | 112.36 | 123.99 | 118.04 | 115.23 | 133.69 | 103.17 | 130.84 | 113.37 | 122.45 | 100.60 | 117.31 | 124.14 |
| Robo ya tatu | 127.13 | 120.31 | 112.72 | 124.73 | 118.97 | 115.30 | 133.48 | 103.18 | 132.08 | 114.66 | 122.75 | 100.60 | 117.82 | 123.00 |
| Robo ya nne | 127.69 | 120.64 | 113.16 | 122.70 | 120.41 | 115.18 | 131.27 | 103.32 | 132.48 | 114.63 | 122.66 | 100.60 | 119.16 | 122.80 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI

## Jedwali Na. 19: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)

| | ***Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2018 Robo ya kwanza | 87.9 | 100.0 | 94.8 | 84.5 | 96.7 | 95.5 | 96.4 | 97.9 | 98.9 | 94.3 | 94.8 | 100.0 | 98.3 | 92.6 |
| Robo ya pili | 88.9 | 100.0 | 95.8 | 86.4 | 97.6 | 95.5 | 98.7 | 98.0 | 99.5 | 100.0 | 95.0 | 100.0 | 99.7 | 94.1 |
| Robo ya tatu | 89.8 | 99.6 | 97.0 | 87.1 | 97.9 | 95.5 | 99.8 | 98.0 | 99.8 | 100.0 | 95.6 | 100.0 | 100.6 | 94.9 |
| Robo ya nne | 89.5 | 99.7 | 97.6 | 88.7 | 98.2 | 95.4 | 101.4 | 98.0 | 99.3 | 100.0 | 97.7 | 100.0 | 100.8 | 95.6 |
| 2019 Robo ya kwanza | 90.9 | 99.8 | 97.9 | 89.1 | 99.3 | 98.4 | 101.5 | 99.4 | 99.8 | 100.0 | 99.6 | 100.0 | 100.8 | 96.4 |
| Robo ya pili | 93.6 | 99.8 | 98.5 | 94.5 | 99.6 | 99.8 | 102.3 | 99.9 | 100.4 | 100.0 | 99.7 | 100.0 | 100.8 | 98.1 |
| Robo ya tatu | 92.9 | 99.8 | 99.0 | 95.3 | 99.5 | 99.7 | 102.0 | 99.1 | 101.0 | 100.0 | 98.9 | 100.0 | 100.4 | 97.9 |
| Robo ya nne | 94.3 | 99.8 | 99.2 | 95.9 | 99.7 | 99.7 | 101.6 | 99.3 | 99.2 | 100.0 | 99.3 | 100.0 | 99.0 | 98.2 |
| **2020 Robo ya kwanza | 99.6 | 99.8 | 99.9 | 97.9 | 99.9 | 99.7 | 101.8 | 99.5 | 100.0 | 100.0 | 99.4 | 100.0 | 98.7 | 100.0 |
| Robo ya pili | 99.1 | 99.8 | 100.0 | 100.8 | 100.0 | 100.1 | 99.4 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 99.4 | 100.0 | 100.2 | 99.7 |
| Robo ya tatu | 100.0 | 99.8 | 100.0 | 101.4 | 100.1 | 100.1 | 99.4 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 100.5 | 100.1 |
| Robo ya nne | 101.3 | 100.7 | 100.2 | 99.8 | 100.1 | 100.1 | 99.5 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 100.6 | 100.3 |
| 2021 Robo ya kwanza | 102.8 | 104.6 | 102.6 | 100.3 | 107.1 | 102.9 | 100.6 | 101.3 | 98.6 | 102.4 | 105.4 | 100.0 | 100.7 | 102.2 |
| Robo ya pili | 104.7 | 113.5 | 103.1 | 99.7 | 108.1 | 103.3 | 101.7 | 101.0 | 98.6 | 103.6 | 107.4 | 100.2 | 101.6 | 103.1 |
| Robo ya tatu | 102.7 | 113.2 | 103.1 | 99.6 | 108.1 | 103.3 | 102.3 | 101.0 | 98.6 | 103.0 | 107.3 | 100.2 | 101.5 | 102.8 |
| Robo ya nne | 105.5 | 113.7 | 104.8 | 101.0 | 109.3 | 103.7 | 102.7 | 102.0 | 99.0 | 103.0 | 108.1 | 100.2 | 102.1 | 104.0 |
| 2022 Robo ya kwanza | 108.0 | 113.9 | 106.0 | 103.0 | 110.2 | 103.9 | 103.1 | 102.4 | 99.7 | 103.0 | 109.7 | 100.2 | 102.7 | 105.3 |
| Robo ya pili | 111.2 | 113.9 | 106.1 | 103.9 | 110.4 | 104.3 | 108.4 | 102.4 | 99.7 | 103.5 | 111.7 | 100.2 | 103.3 | 107.4 |
| Robo ya tatu | 107.9 | 113.9 | 107.0 | 103.0 | 110.7 | 105.6 | 113.1 | 102.3 | 101.9 | 104.3 | 111.3 | 100.1 | 103.6 | 107.8 |
| Robo ya nne | 108.5 | 113.5 | 107.6 | 104.1 | 112.0 | 107.7 | 106.9 | 102.5 | 102.5 | 104.4 | 112.5 | 100.0 | 105.7 | 107.1 |
| 2023 Robo ya kwanza | 112.9 | 113.6 | 108.2 | 104.6 | 112.3 | 109.2 | 107.2 | 102.8 | 102.5 | 105.0 | 115.1 | 100.1 | 106.2 | 108.5 |
| Robo ya pili | 114.0 | 113.6 | 108.4 | 105.4 | 112.1 | 109.3 | 106.6 | 102.8 | 102.3 | 105.0 | 115.7 | 100.0 | 107.4 | 108.8 |
| Robo ya tatu | 112.4 | 117.0 | 110.1 | 105.7 | 113.3 | 111.9 | 110.4 | 103.5 | 105.6 | 105.0 | 116.4 | 100.0 | 115.5 | 110.0 |
| Robo ya nne | 114.0 | 118.9 | 112.5 | 108.3 | 114.4 | 111.9 | 110.8 | 103.0 | 108.2 | 105.0 | 116.8 | 100.2 | 117.0 | 111.3 |
| 2024 Robo ya kwanza | 118.5 | 121.4 | 114.9 | 112.9 | 116.0 | 115.5 | 113.9 | 106.7 | 111.1 | 108.6 | 121.3 | 100.3 | 137.3 | 115.1 |
| Robo ya pili | 121.3 | 122.7 | 115.9 | 116.5 | 117.0 | 116.1 | 115.5 | 108.0 | 113.5 | 111.3 | 122.0 | 100.4 | 141.5 | 117.1 |
| Robo ya tatu | 117.5 | 122.5 | 116.6 | 115.2 | 117.6 | 116.1 | 115.6 | 108.1 | 115.4 | 112.7 | 122.3 | 100.4 | 142.0 | 116.5 |
| Robo ya nne | 119.3 | 121.7 | 116.1 | 115.5 | 118.8 | 116.0 | 115.3 | 108.6 | 117.2 | 112.8 | 122.3 | 100.4 | 143.1 | 116.9 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI

**Jedwali Na. 20: FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)**

| Mwaka | Miezi/ Robo-Mwaka | | | | Wastani | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | | |
| 2016 | 85.46 | 86.73 | 86.65 | 86.98 | 86.45 | |
| 2017 | 87.99 | 89.47 | 90.83 | 92.16 | 90.11 | 4.2 |
| 2018 | 92.65 | 94.11 | 94.87 | 95.59 | 94.31 | 4.7 |
| 2019 | 96.37 | 98.13 | 97.92 | 98.21 | 97.66 | 3.6 |
| **2020 | 99.96 | 99.70 | 100.08 | 100.26 | 100.00 | 2.4 |
| 2021 | 102.17 | 103.08 | 102.81 | 104.03 | 103.02 | 3.0 |
| 2022 | 105.30 | 107.39 | 107.81 | 107.14 | 106.91 | 3.8 |
| 2023 | 108.47 | 108.78 | 110.02 | 111.25 | 109.63 | 2.5 |
| 2024 | 115.15 | 117.11 | 116.45 | 116.90 | 116.40 | 6.2 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

## Jedwali Na. 21: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Jan - Dec. 2020 =100)

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2020 Robo ya kwanza | 98.80 | 99.48 | 99.52 | 98.10 | 99.44 | 99.41 | 101.06 | 99.12 | 100.52 | 99.87 | 99.51 | 99.97 | 99.61 | 99.16 |
| Robo ya pili | 101.16 | 99.92 | 100.06 | 100.58 | 100.05 | 99.85 | 101.33 | 99.98 | 100.57 | 100.04 | 99.67 | 99.97 | 100.20 | 100.72 |
| Robo ya tatu | 100.11 | 100.28 | 100.08 | 100.57 | 100.26 | 100.31 | 98.69 | 100.22 | 100.07 | 100.04 | 100.35 | 100.03 | 100.24 | 100.04 |
| Robo ya nne | 99.92 | 100.33 | 100.34 | 100.76 | 100.25 | 100.43 | 98.93 | 100.68 | 98.85 | 100.05 | 100.47 | 100.03 | 99.95 | 100.08 |
| 2021 Robo ya kwanza | 102.31 | 101.37 | 103.65 | 103.09 | 102.60 | 102.04 | 101.86 | 101.25 | 102.49 | 100.92 | 103.50 | 100.20 | 102.25 | 102.46 |
| Robo ya pili | 106.03 | 102.28 | 104.50 | 104.18 | 102.98 | 102.51 | 103.09 | 101.82 | 102.87 | 101.24 | 105.13 | 100.28 | 102.62 | 104.16 |
| Robo ya tatu | 104.33 | 102.49 | 104.76 | 104.50 | 103.33 | 103.06 | 103.88 | 102.03 | 102.96 | 101.17 | 105.31 | 100.31 | 103.03 | 103.94 |
| Robo ya nne | 104.34 | 102.79 | 105.30 | 104.69 | 103.88 | 103.35 | 104.51 | 102.26 | 102.56 | 101.16 | 105.59 | 100.34 | 103.26 | 104.20 |
| 2022 Robo ya kwanza | 108.75 | 103.23 | 106.51 | 106.56 | 105.60 | 103.55 | 105.61 | 102.42 | 103.98 | 101.41 | 106.54 | 100.44 | 104.59 | 106.29 |
| Robo ya pili | 112.39 | 103.49 | 106.83 | 108.63 | 106.31 | 103.92 | 109.96 | 102.46 | 104.01 | 101.60 | 107.19 | 100.49 | 105.16 | 108.41 |
| Robo ya tatu | 112.17 | 103.46 | 107.30 | 108.26 | 107.17 | 104.39 | 112.42 | 102.69 | 104.45 | 101.87 | 107.27 | 100.54 | 105.31 | 108.80 |
| Robo ya nne | 114.18 | 103.65 | 107.86 | 107.88 | 107.96 | 104.88 | 110.52 | 103.50 | 104.68 | 101.90 | 108.28 | 100.14 | 105.75 | 109.30 |
| 2023 Robo ya kwanza | 119.35 | 103.76 | 109.16 | 108.19 | 108.67 | 105.39 | 111.89 | 104.06 | 105.28 | 104.65 | 109.62 | 100.28 | 106.46 | 111.40 |
| Robo ya pili | 121.89 | 104.86 | 110.25 | 109.44 | 109.33 | 105.56 | 111.84 | 104.33 | 105.94 | 105.10 | 111.90 | 100.09 | 107.22 | 112.69 |
| Robo ya tatu | 118.66 | 107.31 | 110.81 | 109.66 | 111.01 | 106.34 | 113.18 | 104.73 | 107.02 | 105.32 | 112.85 | 100.74 | 109.44 | 112.42 |
| Robo ya nne | 118.16 | 107.66 | 111.26 | 110.72 | 111.77 | 106.38 | 113.95 | 104.88 | 108.07 | 105.48 | 113.21 | 100.74 | 109.85 | 112.73 |
| 2024 Robo ya kwanza | 121.24 | 108.11 | 112.06 | 113.48 | 112.43 | 107.49 | 115.83 | 105.74 | 109.08 | 107.52 | 114.62 | 101.41 | 114.11 | 114.75 |
| Robo ya pili | 123.46 | 108.56 | 112.45 | 115.68 | 113.01 | 107.68 | 117.54 | 106.16 | 109.49 | 108.42 | 115.45 | 101.72 | 115.40 | 116.18 |
| Robo ya tatu | 121.18 | 109.52 | 112.87 | 116.21 | 113.68 | 108.14 | 118.16 | 106.03 | 109.93 | 108.79 | 116.25 | 101.86 | 115.72 | 115.90 |
| Robo ya nne | 122.24 | 109.92 | 113.03 | 115.29 | 114.11 | 108.35 | 118.12 | 106.12 | 110.33 | 108.80 | 116.30 | 101.94 | 116.44 | 116.15 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI

**Jedwali Na. 22: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Jan - Dec. 2020 =100)**

| Mwaka | Robo ya Mwaka | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Wastani wa Fahirisi | |
| **2020 | 99.16 | 100.72 | 100.04 | 100.08 | 100.00 | |
| 2021 | 102.46 | 104.16 | 103.94 | 104.20 | 103.69 | 3.7 |
| 2022 | 106.29 | 108.41 | 108.80 | 109.30 | 108.20 | 4.3 |
| 2023 | 111.40 | 112.69 | 112.42 | 112.73 | 112.31 | 3.8 |
| 2024 | 114.75 | 116.18 | 115.90 | 116.15 | 115.75 | 3.1 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan -Dec. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 23: FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA ( Jan - Dec. 2020 =100)**

| Mwaka | FAHIRISI | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA | BADILIKO (Asilimia) | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KIPATO CHA | | | | KIPATO CHA | | | |
| | CHINI | KATI | JUU | | CHINI | KATI | JUU | |
| **2020 | 100.0 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | | | | |
| 2021 | 102.37 | 102.4 | 103.02 | 103.69 | 2.4 | 2.4 | 3.0 | 3.7 |
| 2022 | 107.16 | 108.38 | 106.91 | 108.2 | 4.7 | 5.8 | 3.8 | 4.3 |
| 2023 | 112.77 | 113.72 | 109.63 | 112.31 | 5.2 | 4.9 | 2.5 | 3.8 |
| 2024 | 119.3 | 122.68 | 116.4 | 115.75 | 5.8 | 7.9 | 6.2 | 3.1 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

## SURA YA 2

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA


**Utekelezaji wa Sera ya Fedha**

30. Mwaka 2024, Benki Kuu ya Tanzania ilianza rasmi kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ili kudhibiti mfumuko wa bei na kuongeza ufanisi kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Kwa muktadha huo, riba ya Benki Kuu ilipangwa kuwa asilimia 5.5 kwa robo ya mwaka iliyoishia Machi 2024 na kupandishwa hadi asilimia 6.0 katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024. Riba hii haikubadilika kwa robo mbili za mwisho za mwaka 2024. Aidha, riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki za biashara ilikuwa wastani wa asilimia 7.67 mwaka 2024 ambayo ilikuwa ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 wa riba ya Benki Kuu. Hii iliashiria uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi.

**Ujazi wa Fedha**

31. Mwaka 2024, kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha ilikuwa ya kuridhisha sambamba na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2024, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 11.1 na kufikia shilingi bilioni 48,905.3 kutoka shilingi bilioni 44,002.6 kipindi kama hicho mwaka 2023. Mwenendo huo ulichangiwa zaidi na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 9.3 na kufikia shilingi bilioni 37,140.1 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024 kutoka na shilingi bilioni 34,001.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 11.2 na kufikia shilingi bilioni 22,905.8 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024 kutoka shilingi bilioni 20,601.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha, Mwaka 2020 - 2024**



**Mikopo kwa Sekta Binafsi**


32. Mwaka 2024, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 36,097.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 32,102.0 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa asilimia 12.4. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi lilichangiwa na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara pamoja na utekelezaji thabiti wa sera za fedha na bajeti. Aidha, mikopo katika sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 41.0 mwaka 2024 ikifuatiwa na shughuli za uzalishaji viwandani (asilimia 16.3), shughuli binafsi (asilimia 14.7) na uchukuzi na mawasiliano (asilimia 13.2). Ukuaji wa mikopo katika sekta ya kilimo ulichangiwa na ongezeko la mahitaji ya mikopo kwa ajili ya ununuzi wa mazao, hususan korosho na nafaka. Vilevile, mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli binafsi (ujenzi, biashara ndogo na za kati, matumizi binafsi na shughuli nyingine kama vile elimu) iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi (asilimia 38.9), ikifuatiwa na mikopo kwa shughuli za kilimo, biashara (asilimia 13.1), pamoja na uzalishaji viwandani (asilimia 10.1).

**Jedwali Na. 2.1: Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi Mwaka, 2020 - 2024 (Shilingi Bilioni)**

| **Shughuli** | **Kipindi Kilichoishia Desemba (Shilingi Bilioni)** | | | | | **Ukuaji (Asilimia)** | | **Mchango (Asilimia)** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2023** | **2024** | **2023** | **2024** |
| Kilimo | 1,725.6 | 1,592.5 | 2,327.4 | 3,340.8 | 4,712.1 | 43.5 | 41.0 | 10.4 | 13.1 |
| Uchimbaji madini na maw | 429.4 | 474.0 | 575.9 | 785.4 | 500.3 | 36.4 | -36.3 | 2.4 | 1.4 |
| Uzalishaji viwandani | 1,878.4 | 2,111.1 | 2,709.5 | 3,132.0 | 3,643.1 | 15.6 | 16.3 | 9.8 | 10.1 |
| Ujenzi | 1,072.3 | 998.4 | 1,200.6 | 1,483.1 | 1,655.1 | 23.5 | 11.6 | 4.6 | 4.6 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 1,142.4 | 1,053.9 | 1,207.0 | 1,420.3 | 1,607.9 | 17.7 | 13.2 | 4.4 | 4.5 |
| Biashara | 3,054.9 | 3,657.3 | 4,556.4 | 4,473.4 | 4,723.9 | -1.8 | 5.6 | 13.9 | 13.1 |
| Mahoteli na migahawa | 549.5 | 542.7 | 511.3 | 534.0 | 548.4 | 4.4 | 2.7 | 1.7 | 1.5 |
| Umeme | 114.7 | 143.9 | 130.3 | 291.3 | 268.5 | 123.6 | -7.8 | 0.9 | 0.7 |
| Shughuli binafsi | 6,793.9 | 8,047.7 | 10,365.7 | 12,238.0 | 14,032.9 | 18.1 | 14.7 | 38.1 | 38.9 |
| Shughuli nyinginezo | 3,547.2 | 3,722.5 | 3,788.3 | 4,403.8 | 4,405.1 | 16.2 | 0.0 | 13.7 | 12.2 |
| **Jumla** | **20,308.3** | **22,344.1** | **27,372.5** | **32,102.0** | **36,097.4** | **17.3** | **12.4** | **100** | **100** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 2.2: Mchango wa Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara katika baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia)**




**Amana katika Benki za Biashara**

33. Mwaka 2024, amana za benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 13.8 na kufikia shilingi bilioni 41,525.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 36,501.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na ongezeko la huduma za mawakala wa benki na matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kutoa huduma za fedha. Aidha, amana za sekta binafsi ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 40,025.8 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 35,345.0 mwaka 2023. Vilevile, uwiano wa amana za fedha za kigeni kwa amana zote ulifikia asilimia 27.4 mwaka 2024 kutoka asilimia 25.6 mwaka 2023.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

34. Mwaka 2024, viwango vya riba katika masoko ya fedha viliongezeka kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kudhibiti mfumuko wa bei. Wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya benki uliongezeka hadi asilimia 7.50 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.37 mwaka 2023. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi iliongezeka na kufikia asilimia 10.67 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.32 mwaka 2023. Kuongezeka kwa riba baina ya benki na riba za dhamana za Serikali kulipunguza fedha katika mzunguko na hivyo kusaidia kudhibiti kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma.

35. Mwaka 2024, wastani wa riba za jumla za mikopo ulipungua hadi asilimia 15.47 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 15.75 mwaka 2023. Aidha, viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja vilipungua hadi wastani wa asilimia 15.82 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.53 mwaka 2023. Vilevile, wastani wa riba za

amana za muda maalumu uliongezeka hadi asilimia 7.85 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.07 mwaka 2023. Wastani wa riba za amana za mwaka mmoja uliongezeka na kufikia asilimia 9.17 mwaka 2024 kutoka asilimia 8.65 mwaka 2023. Hivyo, tofauti ya viwango vya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo za mwaka mmoja ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.65 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.88 mwaka 2023. Kupungua kwa tofauti ya viwango vya riba za amana na riba za mikopo kunaashiria kupungua kwa vihatarishi katika utoaji wa mikopo kulikochangiwa na jitihada za Serikali za kuongeza urasimishaji wa taarifa kupitia utoaji wa vitambulisho vya Taifa pamoja na anuani za makazi.

**Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

36. Katika robo tatu za kwanza za mwaka 2024, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilishuka kutokana na upungufu wa ukwasi wa dola za Marekani nchini. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi uliofanywa na mataifa yaliyoendelea, ikiwemo Marekani kwa lengo la kukabiliana na mfumuko wa bei pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta ya nishati katika soko la dunia. Hata hivyo, katika robo ya nne, ukwasi wa fedha za kigeni uliongezeka kwa kiasi kikubwa na kusababisha kuimarika kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani. Kuimarika kwa thamani ya shilingi kulitokana na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani, hususan kushuka kwa viwango vya riba katika nchi zilizoendelea na kupungua kwa bei za mafuta ghafi. Kwa ujumla, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,610.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,395.7 mwaka 2023. Aidha, thamani ya shilingi ilipungua kwa asilimia 9.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023.

## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

**Huduma za Benki**

37. Hadi Desemba 2024, idadi ya benki nchini ilipungua na kufikia 42 kutoka benki 44 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hii ilitokana na kuhamishwa kwa mali na madeni ya Canara Bank Tanzania Limited kwenda Exim Bank Tanzania Limited, pamoja na kuungana kwa Tandahimba Community Bank Ltd na Kilimanjaro Cooperative Bank Limited ambazo ziliunda benki mpya ya biashara inayoitwa Benki ya Ushirika Tanzania. Aidha, matawi ya benki yaliongezeka na kufikia 1,027 mwaka 2024 kutoka matawi 1,011 mwaka 2023. Hadi Desemba 2024, amana za wateja zilifikia shilingi bilioni 42,943.0 kutoka shilingi bilioni 37,980.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Kwa upande mwingine, mikopo kwa wateja ilifikia shilingi bilioni 37,682.8 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 33,194.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 13.5.

**Huduma za Mawakala wa Benki**

38. Mwaka 2024, benki 30 zilitoa huduma za benki kwa njia ya uwakala ikilinganishwa na benki 31 mwaka 2023. Idadi ya mawakala wa benki iliongezeka kwa asilimia 37.0 na kufikia mawakala 145,430 mwaka 2024 kutoka mawakala 106,176 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilichangiwa na hatua ya Benki Kuu ya Tanzania kulegeza masharti ya kufanya biashara ya uwakala.

**Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki**

39. Mwaka 2024, uwiano wa mtaji halisi na mtaji mkuu kwa mali hatarishi ulikuwa asilimia 19.3 na asilimia 19.9 ikilinganishwa na asilimia 17.7 na asilimia 18.4 mtawalia mwaka 2023. Aidha, uwiano wa ukwasi dhidi ya amana za muda mfupi katika benki uliongezeka hadi asilimia 29.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 28.7 mwaka 2023.

40. Mwaka 2024, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023. Hii ilitokana na hatua mbalimbali zilizoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania, ikiwemo: kuzielekeza benki kutumia taarifa za wakopaji kutoka kwa kampuni za kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu za utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Aidha, idadi ya taasisi zilizotumia kanzidata ya wakopaji iliongezeka na kufikia 188 mwaka 2024 ikilinganishwa na taasisi 181 mwaka 2023. Vilevile, idadi ya wakopaji waliosajiliwa kwenye kanzidata ya wakopaji iliongezeka na kufikia 11,209,343 mwaka 2024 ikilinganishwa na wakopaji 8,134,863 mwaka 2023.

**Maboresho katika Sekta ya Benki**

41. Mwaka 2024, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia benki na taasisi za fedha ili kuhakikisha sekta hii inaendelea kuwa thabiti, imara na himilivu. Katika kipindi hicho, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa jumla ya kanuni tatu ambazo ni Kanuni za ufilisi wa lazima; kanuni za majaribio ya teknolojia ya fedha katika mazingira yaliyodhibitiwa; pamoja na kanuni za kuchukua hatua stahiki kwa benki na taasisi za fedha zenye upungufu wa mtaji. Aidha, katika kipindi hicho, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa jumla ya miongozo sita, ikiwemo miongozo ya mitaala ya watoa elimu ya fedha, miongozo ya ada na gharama za benki na taasisi za fedha, pamoja na miongozo ya ada na gharama za watoa huduma ndogo za fedha.

**Huduma Ndogo za Fedha**

42. Hadi Desemba 2024, Benki Kuu ilikuwa imepokea jumla ya maombi ya leseni 2,963 kutoka kwa watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili ikilinganishwa na maombi 2,221 yaliyokuwa yamepokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kati ya maombi hayo, leseni 2,342 zilitolewa baada ya kukidhi vigezo na masharti ikilinganishwa na leseni 1,579 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, hadi Desemba 2024, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilikuwa imepokea jumla ya maombi ya leseni 1,258 za watoa

huduma ndogo za fedha wa daraja la tatu ikilinganishwa na maombi 1,215 yaliyokuwa yamepokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kati ya maombi hayo, leseni 964 zilitolewa baada ya kukidhi vigezo na masharti ikilinganishwa na leseni 884 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Vilevile, hadi Desemba 2024, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipokea maombi 60,997 ya watoa huduma ndogo za fedha daraja la nne ikilinganishwa na maombi 49,026 yaliyopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kati ya maombi hayo, vikundi 58,926 vilisajiliwa baada ya kukidhi vigezo na masharti ikilinganishwa na vikundi 48,284 vilivyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

**Masoko ya Mitaji na Dhamana**

43. Mwaka 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - CMSA ilitoa leseni 231 ikilinganishwa na leseni 184 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 25.5. Leseni zilizotolewa zilikuwa katika makundi yafuatayo: Soko la Hisa (1); Soko la Bidhaa (1); Hifadhi Kuu ya Dhamana (1); kampuni za utendaji katika Soko la Hisa (21); Watendaji katika Soko la Bidhaa (5); Watendaji katika Soko la Hatifungani (8); Washauri Wateule (4); Washauri wa Uwekezaji (25); Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (20); Mameneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (18); Watunza Dhamana (9); na Wawakilishi wa Taasisi zinazotoa huduma katika masoko ya mitaji (118). Hadi Desemba 2024, mtaji wa soko la hisa kwa kampuni za ndani uliongezeka kwa asilimia 7.4 na kufikia shilingi trilioni 12.24 ikilinganishwa na shilingi trilioni 11.40 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, mtaji wa jumla wa soko la hisa uliongezeka kwa asilimia 22.3 na kufikia shilingi trilioni 17.87 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi trilioni 14.61 mwaka 2023. Kuongezeka kwa mtaji kulitokana na kuimarika kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa, ikiwemo CRDB Bank Plc, NMB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited (NICO), Swissport Tanzania Plc, Twiga Cement Plc, Afriprise, Tanzania Breweries Plc na Tanzania Cigarette Plc.

44. Mwaka 2024, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani iliongezeka kwa asilimia 7.3 na kufikia alama 4,618.78 ikilinganishwa na alama 4,304.40 mwaka 2023. Ongezeko hilo linaashiria ufanisi wa soko, hususan kuongezeka kwa bei ya hisa za kampuni zinazotoa huduma katika sekta za viwanda na fedha zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Kwa upande mwingine, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote za ndani na nje iliongezeka kwa asilimia 22.2 na kufikia alama 2,139.73 mwaka 2024 ikilinganishwa na alama 1,750.63 mwaka 2023.

45. Mwaka 2024, mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 1.5 na kufikia shilingi bilioni 228.64 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 225.22 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine. Aidha,

mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yalipungua kwa asilimia 14.5 na kufikia shilingi trilioni 3.36 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.93 mwaka 2023. Hii ilitokana na wawekezaji kupendelea kuendelea na umiliki wa hatifungani zao hadi kipindi zitakapoiva kutokana na faida na manufaa ya uwekezaji kwenye bidhaa hizi. Kwa upande mwingine, mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 6.40 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.07 mwaka 2023.

46. Hadi Desemba 2024, thamani ya uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja iliongezeka kwa asilimia 41.6 na kufikia shilingi bilioni 2,608.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,841.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ongezeko hili lilitokana na mwitikio wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji.

**Jedwali Na. 2.2: Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja, Mwaka 2023 - 2024**

| Meneja wa Mifuko | Jina la Mfuko | 31 Desemba 2023 | | 31 Desemba 2024 | | Ongezeko la thamani | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Shilingi) | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Shilingi) | Ongezeko la Thamani ya Mfuko (Asilimia) | Ongezeko la Bei ya Kipande (Asilimia) |
| UTT AMIS Plc | Mfuko wa Umoja | 339,983,591,268.08 | 983.84 | 371,502,175,945.93 | 1101.13 | 9.3 | 11.9 |
| | Mfuko wa Wekeza Maisha | 12,063,090,559.95 | 866.08 | 19,141,116,469.00 | 970.94 | 58.7 | 12.1 |
| | Mfuko wa Watoto | 14,560,377,763.80 | 634.52 | 24,012,875,156.00 | 715.79 | 64.9 | 12.8 |
| | Mfuko wa Jikimu | 22,994,371,528.45 | 170.51 | 32,326,675,609.90 | 183.95 | 40.6 | 7.9 |
| | Mfuko wa Ukwasi | 890,749,211,777.39 | 383 | 1,359,669,789,869.22 | 434 | 52.6 | 13.3 |
| | Mfuko wa Hatifungani | 542,099,396,791.84 | 116.6 | 768,247,503,090.03 | 119.61 | 41.7 | 2.6 |
| Watumishi Housing Investments | Mfuko wa Faida | 19,242,094,320.45 | 110.24 | 33,491,896,212.64 | 123.17 | 74.1 | 11.7 |
| **Thamani ya Jumla** | | **1,841,692,134,009.95** | | **2,608,392,032,352.71** | | **41.6** | |

**Chanzo:** Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja na Watumishi Housing Investments

## Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

47. Mwaka 2023/24, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF ulisajili wanachama wapya 42,811 ikilinganishwa na wanachama 47,851 waliosajiliwa mwaka 2022/23. Aidha, wanachama wachangiaji wa Mfuko walifikia 767,234 mwaka 2023/24 ikilinganyishwa na wanachama 729,346 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Katika kipindi hicho, idadi ya wastaafu walionufaika na Mfuko ilipungua na kufikia wastaafu 36,371 kutoka wastaafu 55,152 mwaka 2022/23. Kwa upande mwingine, Mfuko ulikusanya shilingi trilioni 1.84 kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.68 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ajira na kupanda kwa madaraja ya watumishi. Aidha, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi bilioni 1,484.78 mwaka 2023/24

ikilinganishwa na mafao ya shilingi bilioni 1,563.55 yaliyolipwa mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 5.0. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wastaafu na thamani ya madai yaliyowasilishwa kwenye Mfuko.

48. Mwaka 2023/24, thamani ya uwekezaji wa Mfuko ilifikia shilingi trilioni 8.67 kutoka shilingi trilioni 7.90 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 9.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa michango na uwekezaji wa mitaji iliyoiva. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yalipungua kwa asilimia 20.0 na kufikia shilingi bilioni 548.28 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 685.44 mwaka 2022/23. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa thamani ya hisa zilizowekezwa kwenye kampuni mbalimbali na kuendelea kushuka kwa thamani ya majengo ya Mfuko. Vilevile, thamani ya rasilimali halisi za Mfuko iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 9,239.28 mwaka 2023/24 kutoka shilingi bilioni 8,393.77 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 10.1. Hii ilichangiwa na kupungua kwa gharama za uendeshaji.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii**

49. Mwaka 2023/24, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF uliandikisha wanachama wapya 291,266 ikilinganishwa na wanachama wapya 243,895 walioandikishwa mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 19.4. Katika kipindi hicho, wanachama wachangiaji wa Mfuko walifikia 1,358,882 kutoka wanachama 1,189,222 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Ongezeko hilo lilichangiwa na ukuaji wa shughuli za sekta binafsi pamoja na ushirikiano baina ya Mfuko na taasisi nyingine za Serikali. Aidha, idadi ya wastaafu katika Mfuko ilifikia 31,914 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wastaafu 28,820 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 10.7.

50. Mwaka 2023/24, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka kwa asilimia 19.8 na kufikia shilingi bilioni 884.82 ikilinganishwa na shilingi bilioni 738.61 mwaka 2022/23. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maombi ya fao la kupoteza ajira pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wastaafu. Kwa upande mwingine, mapato halisi yatokanayo na uwekezaji wa Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 19.3 na kufikia shilingi bilioni 433.47 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 380.39 mwaka 2022/23. Ongezeko hilo lilichangiwa na uwekezaji uliofanywa na Mfuko katika hatifungani za Serikali. Aidha, thamani ya vitega uchumi vya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 10.4 na kufikia shilingi bilioni 7,434.27 kutoka shilingi bilioni 6,730.18 mwaka 2022/23. Hii ilitokana na ongezeko la michango ya wanachama pamoja na uwekezaji uliofanywa na Mfuko katika hatifungani za Serikali.

51. Mwaka 2023/24, Mfuko ulikusanya michango ya shilingi bilioni 1,969.61 kutoka kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,712.61 zilizokusanywa mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Hii ilichangiwa na ukuaji wa shughuli za sekta binafsi, maboresho ya mifumo ya ukaguzi na matumizi ya TEHAMA katika usajili na uchangiaji.

Kwa upande mwingine, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 15.53 na kufikia shilingi bilioni 8,308.18 mwaka 2023/24 kutoka shilingi bilioni 7,191.33 mwaka 2022/23. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa thamani ya uwekezaji wa Mfuko na kuongezeka kwa michango ya wanachama.

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

52. Mwaka 2023/24, idadi ya waajiri waliosajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ilifikia 34,996 kutoka waajiri 30,860 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Aidha, idadi ya waajiri wanaochangia iliongezeka na kufikia waajiri 29,238 mwaka 2023/24 kutoka waajiri 25,137 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 16.3. Vilevile, idadi ya wafanyakazi wanaochangiwa iliongezeka kwa asilimia 12.99 na kufikia wafanyakazi 1,817,054 mwaka 2023/24 kutoka wafanyakazi 1,608,111 mwaka 2022/23. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji uliofanyika kuhusu umuhimu wa kujiunga na kuchangia katika Mfuko, kufanya kaguzi za mara kwa mara pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa waajiri wanaokiuka matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi. Kwa upande mwingine, michango kutoka kwa waajiri iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 91.68 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 86.48 mwaka 2022/23. Ongezeko hilo lilitokana na kaguzi za mara kwa mara zilizofanyika, maboresho ya mifumo ya uwasilishaji wa michango na kuimarika kwa mahusiano kati ya waajiri na Mfuko.

53. Mwaka 2023/24, mapato ya uwekezaji wa Mfuko yalipungua kwa asilimia 13.6 na kufikia shilingi bilioni 87.88 ikilinganishwa na shilingi bilioni 102.40 mwaka 2022/23. Hii ilitokana na kupungua kwa uwekezaji katika hatifungani za Serikali zenye faida kubwa zaidi. Aidha, mapato yaliyotokana na shughuli nyingine za kiuchumi yalikuwa shilingi milioni 138.48 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi milioni 85.97 mwaka 2022/23.

54. Mwaka 2023/24, Mfuko ulilipa madai ya shilingi bilioni 26.78 kama gharama za matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki wakiwa kazini ikilinganishwa na shilingi bilioni 23.58 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asimilia 13.6. Hii ilitokana na ongezeko la madai yaliyopokelewa na kuchakatwa kutoka kwa wanufaika mbalimbali pamoja na juhudi za Mfuko kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma. Kwa upande mwingine, thamani halisi ya mali za Mfuko iliongezeka kwa asilimia 13.3 na kufikia shilingi bilioni 683.13 mwaka 2023/24 kutoka shilingi bilioni 602.77 mwaka 2022/23. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato pamoja na kuimarishwa kwa usimamizi wa matumizi.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

55. Hadi Desemba 2024, idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya - NHIF ilipungua kwa asilimia 3.5 na kufikia wanachama 1,196,205 kutoka wanachama 1,246,046 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kupungua kwa idadi ya wanachama wachangiaji kulisababishwa na kukosekana kwa uhiari wa sekta binafsi na

sekta isiyo rasmi kujiunga na Mfuko (kuwa na bima ya afya) pamoja na jamii kuwa na uelewa mdogo wa dhana ya bima ya afya. Aidha, idadi ya wanufaika iliongezeka na kufikia wanufaika 5,028,735 mwaka 2024 kutoka wanufaika 4,987,292 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya wanachama wa vifurushi pamoja na usajili wa kampuni mpya zilizosajiliwa na Mfuko.

**Jedwali Na. 2.3: Wanachama Wachangiaji na Wanufaika wa Mfuko, Mwaka 2019/20 - 2023/24**

| Mwaka | Idadi ya Wanachama | Idadi ya Wanufaika | Ongezeko la Wanachama (Asilimia) | Ongezeko la Wanufaika (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 1,055,555 | 4,403,581 | - | - |
| 2020/21 | 1,212,519 | 4,550,207 | 14.9 | 3.3 |
| 2021/22 | 1,353,535 | 4,821,233 | 11.6 | 6.0 |
| 2022/23 | 1,246,046 | 4,987,292 | -7.9 | 3.4 |
| 2023/24 | 1,196,205 | 5,028,735 | -3.9 | 0.8 |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

56. Mwaka 2023/24, thamani ya madai yaliyowasilishwa na watoa huduma ilikuwa ni shilingi bilioni 667.83. Kati ya hizo, shilingi bilioni 605.60 zililipwa, sawa na asilimia 90.7 ya madai. Kutolipwa kwa baadhi ya madai yaliyowasilishwa kulitokana na: watoa huduma kutozingatia miongozo ya tiba; matumizi ya majina ya kibiashara katika uandishi wa dawa badala ya majina ya asili; utoaji wa dawa nyingi zinazofanana na zenye uwezo wa kutibu ugonjwa mmoja; na vitendo vya udanganyifu kwa baadhi ya watoa huduma. Kwa upande mwingine, malipo ya shilingi bilioni 605.60 mwaka 2023/24 ni pungufu kwa asilimia 19.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 752.14 zilizolipwa mwaka 2022/23. Upungufu huo ulisababishwa na kuimarishwa kwa matumizi ya TEHAMA katika uchakataji wa madai; mapitio ya vitita vya mafao vinavyotolewa na Mfuko; na kuwepo kwa watumishi wa mfuko katika vituo vya kutolea huduma kuhakiki wanachama.

57. Mwaka 2023/24, rasilimali halisi za Mfuko zilipungua na kufikia shilingi bilioni 866.5 kutoka shilingi bilioni 987.0 mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 12.2. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na uwekezaji. Katika kipindi hicho, Mfuko ulikusanya mapato ya shilingi bilioni 758.12 ikilinganishwa na shilingi bilioni 697.12 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Hii ilitokana na Mfuko kuendelea kusajili wanachama kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi pamoja na jitihada za ufuatiliaji na ukusanyaji wa michango kutoka kwa wanachama.

**Jedwali Na. 2.4: Mapato ya Mfuko, Mwaka 2019/20- 2023/24**

| Vyanzo vya Mapato | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | Ongezeko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Michango | 467,772.19 | 489,479.55 | 552,580.23 | 633,627.12 | 700,106.80 | 10.5 |
| Uwekezaji | 80,757.62 | 77,110.90 | 69,446.95 | 59,259.39 | 51,002.04 | (13.9) |
| Vyanzo vingine | 1,903.36 | 3,161.57 | 2,468.62 | 4,230.23 | 7,010.45 | 65.7 |
| **Jumla** | **550,433.17** | **569,752.02** | **624,495.80** | **697,116.73** | **758,119.28** | **8.8** |

**Chanzo:** Mfuko wa Bima ya Afya

58. Mwaka 2023/24, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na Mfuko viliongezeka na kufikia vituo 10,201 kutoka vituo 9,467 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Kati ya hivyo, vituo 7,447 (asilimia 73.0) vilikuwa vya Serikali; vituo 1,938 (asilimia 19.0) vya binafsi na vituo 816 (asilimia 8.0) vya mashirika ya dini. Ongezeko la vituo lilitokana na matumizi ya mfumo wa kidigitali katika kusajili vituo vipya.

**Jedwali Na. 2.5: Vituo vilivyosajiliwa na Mfuko, Mwaka 2019/20 - 2023/24**

| Ngazi ya Kituo | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zahanati | 6,485 | 6,252 | 6,582 | 6,896 | 7,365 | 6.8 |
| Vituo vya Afya | 853 | 832 | 912 | 999 | 1,162 | 16.3 |
| Hospitali | 346 | 381 | 417 | 449 | 493 | 9.8 |
| Maduka ya Dawa | 597 | 560 | 685 | 625 | 602 | (3.7) |
| ADDO | 461 | 179 | 207 | 129 | 129 | 0.0 |
| Polikliniki | - | - | - | 242 | 323 | 33.5 |
| Kliniki Maalumu | 211 | 265 | 360 | 113 | 113 | 0.0 |
| Vituo vya Uchunguzi | 16 | 13 | 14 | 12 | 13 | 8.3 |
| Vituo vya Uokozi | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | (50.0) |
| **Jumla** | **8,969** | **8,482** | **9,178** | **9,467** | **10,201** | **7.8** |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa**

59. Mwaka 2023/24, wanachama 510,040 walijiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa ikilinganishwa na wanachama 636,690 waliojiunga mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 19.9. Idadi hiyo inafanya jumla ya wanachama wa Mfuko kufikia 5,008,996 mwaka 2023/24. Kupungua kwa idadi ya wanachama walioandikishwa mwaka 2023/24 kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo dhana ya kusubiri kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote miongoni mwa wananchi sambamba na uhiari wa kujiunga na Mfuko. Katika kipindi hicho, vituo 7,334 vilitoa huduma kwa wanachama wa Mfuko ikilinganishwa na vituo 6,755 mwaka 2022/23. Kati ya hivyo, vituo vya umma vilikuwa 7,312, vituo vya mashirika ya dini 20 na vituo binafsi viwili (2). Aidha, vituo vya Serikali vilijumuisha zahanati 6,163, vituo vya afya 932, hospitali za halmashauri 182, hospitali za wilaya 6 na hospitali za rufaa za mikoa 29.

60. Mwaka 2023/24, shilingi milioni 3,587.7 zilikusanywa kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi milioni 3,755.8 zilizokusanywa mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 4.5. Hii ilitokana na idadi ndogo ya wanachama waliojiunga na Mfuko mwaka 2023/24. Kwa upande mwingine, shilingi milioni 2,224.4 zililipwa kwa watoa huduma mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi milioni 3,959.4 zilizolipwa mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 43.8. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato ya Mfuko kutokana na idadi ndogo ya wanachama waliojiunga mwaka 2023/24 kwa kuwa gharama za huduma zina ukomo unaoendana na fedha zilizopo katika Mfuko.

**Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania**

61. Mwaka 2024, watoa huduma za bima waliosajiliwa na Mamlaka ya Usimamazi wa Shughuli za Bima Tanzania - TIRA waliongezeka na kufikia 2,208 kutoka watoa huduma 1,549 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 42.5. Ongezeko hilo lilichangiwa na urahisishaji wa usajili wa makundi mapya, matumizi ya mifumo ya kidigitali na kuongezeka kwa aina za huduma zinazotolewa. Katika kipindi hicho, idadi ya kampuni za bima zilizosajiliwa ilikuwa 35 kama ilivyokuwa mwaka 2023.

62. Mwaka 2024, mauzo ya bima yaliongezeka kwa asilimia 14.3 na kufikia shilingi bilioni 1,418.1 kutoka shilingi bilioni 1,240.2 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa aina za huduma zinazotolewa, matumizi ya TEHAMA na utoaji wa elimu kwa umma. Aidha, mauzo ya bima za kawaida yaliongezeka kwa asilimia 12.7 hadi shilingi bilioni 1,099.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 974.0 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilichangiwa na ukuaji wa bima za vyombo vya moto, afya na moto. Vilevile, mauzo ya bima za maisha yalikuwa shilingi bilioni 290.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 264.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Kwa upande mwingine, mauzo ya bima ya biashara za nje yaliongezeka kwa asilimia 4.8 na kufikia shilingi bilioni 28.6 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 27.3 mwaka 2023.

63. Mwaka 2024, thamani ya mali za kampuni za bima ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 2,339.9 kutoka shilingi bilioni 2,151.8 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya ada za bima, uwekezaji katika hatifungani za Serikali pamoja na uwekezaji mwingine. Aidha, madeni ya kampuni za bima yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,492.6 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 1,454.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na malipo ya madai yaliyosubiri uthibitisho. Vilevile, thamani halisi ya kampuni za bima iliongezeka asilimia 21.5 na kufikia shilingi bilioni 847.3 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 697.4 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuimarika kwa mitaji ya kampuni, faida kutoka kwenye uwekezaji, na uwiano bora wa mali ikilinganisha na madeni.

**Jedwali Na. 2.6: Ada za Bima Zilizoandikishwa Mwaka, 2023 - 2024 (Shilingi bilioni)**

| Aina ya Bima | 2023 | 2024 | Mchango 2023 (Asilimia) | Mchango 2024 (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Bima ya vyombo vya moto | 338.0 | 384.8 | 35.6 | 35.0 |
| Bima ya moto | 183.9 | 189.9 | 19.4 | 17.3 |
| Bima ya afya | 161.0 | 162.0 | 16.9 | 14.7 |
| Bima ya ndege | 50.3 | 55.4 | 5.3 | 5.0 |
| Bima ya uhandisi | 40.4 | 72.2 | 4.3 | 6.6 |
| Bima baharini | 40.1 | 55.1 | 4.2 | 5.0 |
| Bima nyingine | 17.1 | 51.4 | 1.8 | 4.7 |
| Bima ya ajali | 22.6 | 48.6 | 2.4 | 4.4 |
| Bima ya dhima | 23.7 | 36.3 | 2.5 | 3.3 |
| Bima ya wizi | 18.1 | 14.6 | 1.9 | 1.3 |
| Bima ya dhamana | 40.7 | 10.2 | 4.3 | 0.9 |
| Bima ya nishati | 0.0 | 8.1 | 0.0 | 0.7 |
| Bima ya usafirishaji | 6.5 | 5.1 | 0.7 | 0.5 |
| Bima ya kilimo | 6.7 | 4.4 | 0.7 | 0.4 |
| Bima za safari | 1.2 | 0.7 | 0.1 | 0.1 |
| **Jumla Bima za Kawaida** | **950.3** | **1,099.0** | **100.0** | **100.0** |
| Bima za maisha za binafsi | 44.0 | 40.3 | 16.7 | 13.9 |
| Bima maisha za vikundi | 218.7 | 249.5 | 83.3 | 85.9 |
| Bima nyingine | 0.0 | 0.7 | 0.0 | 0.2 |
| **Jumla bima za Maisha** | **262.7** | **290.5** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

64. Mwaka 2024, mali za uwekezaji katika sekta ya bima ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,440.1 kutoka shilingi bilioni 1,278.3 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.7. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la uwekezaji kwenye hatifungani za Serikali. Aidha, uwekezaji wa hatifungani za Serikali uliongezeka kwa asilimia 15.3 na kufikia shilingi bilioni 430.0 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 373.1 mwaka 2023. Uwekezaji mwingine uliongezeka kwa asilimia 35.5 na kufikia shilingi bilioni 16.4 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 12.1 mwaka 2023. Vilevile, uwekezaji katika majengo na ardhi uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 163.5 na hisa za kampuni zilizoorodheshwa zilifikia shilingi bilioni 128.0.

65. Mwaka 2024, idadi ya wakata bima na wanufaika iliongezeka na kufikia milioni 25.9 kutoka milioni 23.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa bima, matumizi ya mifumo ya kidigitali, pamoja na kuongezeka kwa aina za bima na watoa huduma waliosajiliwa. Aidha, madai yaliyopokelewa yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 732.0 mwaka 2024 kutoka

shilingi bilioni 680.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Katika kipindi hicho, madai yaliyolipwa yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 592.0 kutoka shilingi bilioni 466.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 26.9. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho ya mifumo ya ulipaji, matumizi ya TEHAMA na uimarishaji wa tathmini ya madai.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

66. Mwaka 2024, mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB uliongezeka kwa asilimia 61.0 na kufikia shilingi bilioni 507.33 kutoka shilingi bilioni 315.14 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na mkopo wa shilingi bilioni 174 uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika - AfDB ili kuiwezesha Benki kufikia wakulima, wavuvi na wafugaji wengi nchini. Hadi Desemba 2024, amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 52.4 na kufikia shilingi bilioni 924.76 kutoka shilingi bilioni 606.94 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hii ilitokana na hatua ya Serikali kuiongezea TADB mtaji wa shilingi bilioni 174 kupitia mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na kupatikana kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa - AFD. Aidha, Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 286.38 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 161.13 iliyotolewa mwaka 2023. Vilevile, Benki kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo ilitoa dhamana kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 130.79 mwaka 2024 ikilinganishwa na dhamana kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 77.28 mwaka 2023. Ongezeko la dhamana ya mikopo iliyotolewa lilichangiwa na kuongezeka kwa mtaji wa Mfuko kutokana na ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa.

67. Mwaka 2024, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilipata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 24.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18.78 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 31.0. Hii ilitokana na juhudi za Benki kuongeza ukopeshaji, kufuatilia urejeshwaji wa mikopo na kupunguza gharama za uendeshaji. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua hadi asilimia 2.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 3.8 mwaka 2023. Kiwango hiki ni chini ya ukomo wa asilimia 5.0 uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania.

**Benki ya Biashara Tanzania**

68. Mwaka 2024, amana katika Benki ya Biashara Tanzania - TCB zilifikia shilingi bilioni 1,286.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,120.7 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 14.8. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho yaliyofanyika katika huduma za fedha na uanzishwaji wa huduma mpya. Katika kipindi hicho, idadi ya wateja ilikuwa 914,159 ikilinganishwa na wateja 831,199 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.0.

69. Hadi Desemba 2024, thamani ya mikopo iliyotolewa na Benki ilifikia shilingi bilioni 1,150.8 kutoka shilingi bilioni 911.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na

ongezeko la asilimia 26.3. Hii ilichangiwa na maboresho katika utaratibu wa ukusanyaji wa mikopo. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kilikuwa asilimia 3.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023. Kiwango hiki ni chini ya ukomo wa asilimia 5.0 uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania.

70. Mwaka 2024, uwekezaji wa benki katika dhamana za Serikali uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 209.5 kutoka shilingi bilioni 147.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 42.0. Aidha, benki ilipata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 31.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 46.3 mwaka 2023. Ongezeko la faida lilitokana na kuongezeka kwa mikopo na huduma zilizotolewa na benki. Kwa upande mwingine, thamani ya mali za benki iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,741.8 mwaka 2024 kutoka shilingi bilioni 1,389.3 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 25.4.

**Soko la Bidhaa Tanzania**

71. Mwaka 2024, tani 716,186.52 za mazao na madini ya vito zenye thamani ya shilingi bilioni 2,624.58 ziliuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania - TMX ikilinganishwa na tani 33,662.02 za mazao zenye thamani ya shilingi bilioni 99.78 zilizouzwa mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bidhaa mpya zilizouzwa kupitia soko la bidhaa ikiwemo korosho, dengu, kahawa, maharage ya soya na madini ya vito; idadi ya wanunuzi pamoja na bei ya baadhi ya bidhaa. Kwa upande mwingine, ushuru wa halmashauri wa shilingi bilioni 53.87 ulikusanywa kutokana na mauzo kupitia Soko la Bidhaa mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.73 zilizokusanywa mwaka 2023.

**Jedwali Na. 2.7: Bidhaa Zilizouzwa Kupitia TMX, Mwaka 2023 - 2024**

| Na. | Bidhaa | 2023 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiasi (Kg) | Thamani (Shilingi) | Kiasi (Kg) | Thamani (Shilingi) |
| 1 | Kahawa ya Maganda - Robusta | 29,634,372 | 81,494,341,784 | 32,454,166 | 176,993,441,103 |
| 2 | Kahawa ya Maganda -Arabica | 859,122 | 2,699,297,226 | 906,434 | 4,264,691,197 |
| 3 | Kakao | 1,116,220 | 9,442,580,980 | 9,096,727 | 195,574,954,107 |
| 4 | Ufuta | 1,030,803 | 3,968,974,905 | 145,886,612 | 535,678,706,743 |
| 5 | Mbaazi | 928,589 | 1,977,554,497 | 100,082,095 | 198,473,280,306 |
| 6 | Chai | 92,912 | 198,659,299 | 629,642 | 1,139,974,294 |
| 7 | Korosho | - | - | 402,956,008 | 1,451,347,767,933 |
| 8 | Kahawa Safi (FAQ) - Robusta | - | - | 1,214,694 | 14,305,400,683 |
| 9 | Kahawa Safi (FAQ) - Arabica | - | - | 142,994 | 1,382,430,488 |
| 10 | Dengu | - | - | 21,508,219 | 42,258,331,596 |
| 11 | Maharage ya Soya | - | - | 1,204,201 | 1,812,095,040 |
| 12 | Choroko | - | - | 104,557 | 126,378,786 |
| 13 | Tanzanite | - | - | 120.109 | 1,108,782,508 |
| 14 | Spinel | - | - | 55.59 | 110,705,982 |
| 15 | Sapphire | - | - | 0.555 | 224,910 |
| 16 | Kornerupine | - | - | 0.005 | 235,620 |
| | **Jumla** | **33,662,018** | **99,781,408,691** | **716,186,524** | **2,624,577,401,296** |

**Chanzo:** Soko la Bidhaa Tanzania

- Hazikuuzwa kupitia TMX

## Jedwali Na. 24: MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

| | Kipindi Kinachoishia Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | | | Badiliko 2023 - 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Kiasi | Asilimia |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **6,992.9** | **7,466.4** | **7,169.3** | **8,407.3** | **9,736.3** | **10,099.8** | **12,024.8** | **1,925.0** | **19.1** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **11,723.7** | **13,325.1** | **14,321.7** | **17,625.5** | **18,948.2** | **20,600.2** | **22,905.8** | **2,305.6** | **11.2** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 7,316.7 | 7,955.1 | 8,711.0 | 9,462.8 | 11,430.7 | 13,400.1 | 14,234.2 | 834.1 | 6.2 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **19,040.4** | **21,280.3** | **23,032.6** | **27,088.8** | **30,378.9** | **34,001.7** | **37,140.1** | **3,138.4** | **9.2** |
| Amana za fedha za kigeni | 6,783.1 | 7,032.9 | 6,887.9 | 7,469.7 | 8,201.1 | 10,000.8 | 11,765.3 | 1,764.5 | 17.6 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **25,823.5** | **28,313.1** | **29,920.6** | **34,558.0** | **38,580.0** | **44,002.6** | **48,905.3** | **4,902.7** | **11.1** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **10,629.8** | **12,034.5** | **10,722.5** | **13,966.0** | **9,437.5** | **11,302.4** | **13,583.9** | **2,281.5** | **20.2** |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni Benki Kuu | 10,692.3 | 12,063.1 | 10,308.8 | 13,219.1 | 10,732.8 | 12,079.3 | 11,863.3 | -216.0 | -1.8 |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye mabenki | -62.5 | -28.5 | 413.8 | 746.8 | -1,295.3 | -776.9 | 1,720.6 | 2,497.5 | -321.5 |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **15,193.7** | **16,278.6** | **19,198.0** | **20,592.1** | **29,142.5** | **32,700.2** | **35,671.8** | **2,971.6** | **9.1** |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 4,481.6 | 3,893.9 | 5,831.3 | 7,686.4 | 10,184.8 | 11,353.9 | 11,401.6 | 47.7 | 0.4 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 17,726.8 | 19,695.4 | 20,308.3 | 22,344.1 | 27,372.5 | 32,102.0 | 36,097.4 | 3,995.4 | 12.4 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -7,014.7 | -7,310.7 | -6,941.6 | -9,438.4 | -8,414.8 | -10,711.3 | -12,177.5 | -1,466.2 | 13.7 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 25: VIWANGO VYA UKUAJI WA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

| | Kipindi kinachoishia Desemba (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **0.6** | **6.8** | **-4** | **17.3** | 15.8 | **3.7** | 19.1 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **5.1** | **13.7** | **7.5** | **23.1** | **7.5** | **8.7** | 11.2 |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 1.7 | 8.7 | 9.5 | 8.6 | 20.8 | 17.2 | 6.2 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **3.8** | **11.8** | **8.2** | **17.6** | **12.1** | **11.9** | 9.2 |
| Amana za fedha za kigeni | 6.6 | 3.7 | -2.1 | 8.4 | 9.8 | 21.9 | 17.6 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **4.5** | **9.6** | **5.7** | **15.5** | **11.6** | **14.1** | **11.1** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **-8.3** | **13.2** | **-10.9** | **30.2** | **-32.4** | **19.8** | **-1.8** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **15.8** | **7.1** | **17.9** | **7.3** | **41.5** | **12.2** | **9.1** |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 36.8 | -13.1 | 49.8 | 31.8 | 32.5 | 11.5 | 8.1 |
| Mikopo kwa sekta Binafsi | 4.9 | 11.1 | 3.1 | 10 | 22.5 | 17.1 | 12.4 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | -15.9 | 11.7 | 49.9 | - | 13.9 | 41.7 | 8.1 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -0.5 | 4.2 | -5 | 36 | -10.8 | 27.3 | 10.0 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 26: MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI**

| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shiling/Dola (Mwisho wa mwaka) | 2,291.3 | 2,300.0 | 2,309.8 | 2,307.4 | 2,320.2 | 2,516.0 | 2,420.8 |
| Badiliko la thamani ya shilingi (Asilimia) | 2.2 | 0.4 | 0.4 | -0.1 | 0.6 | 8.4 | -3.8 |
| Shilingi/Dola (Wastani wa mwaka) | 2,275.4 | 2,299.8 | 2,305.6 | 2,309.2 | 2,314.5 | 2,395.7 | 2,610.5 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (Asilimia) | 1.5 | 1.1 | 0.25 | 0.2 | 0.2 | 3.5 | 8.97 |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 27: MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA**

| | Kipindi kilichoishia Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | | | Badiliko (Asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2023** | **2024** |
| Amana za Sekta Binafsi | | | | | | | | | |
| Amana za Hundi (Zinazohamishika) | 7,031.7 | 7,866.5 | 8,121.4 | 9,894.0 | 11,909.1 | 12,976.1 | 14,695.1 | 9.0 | 13.2 |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 7,154.7 | 7,750.4 | 8,519.4 | 9,350.8 | 11,240.7 | 13,037.2 | 13,999.0 | 16.0 | 7.4 |
| Amana za fedha za kigeni | 6,376.3 | 6,160.6 | 6,427.1 | 7,146.0 | 7,575.1 | 9,331.7 | 11,358.6 | 23.2 | 21.7 |
| **Jumla** | **20,562.8** | **21,777.5** | **23,067.9** | **26,390.7** | **30,724.9** | **35,345.0** | **40,052.8** | **15.0** | **13.3** |
| Amana za Serikali | 358.5 | 981.3 | 652.9 | 422.5 | 704.4 | 1156.0 | 1473.0 | 64.1 | 27.4 |
| **Jumla ya Amana zote** | **20,921.3** | **22,758.9** | **23,720.7** | **26,813.2** | **31,429.4** | **36,501.1** | **41,525.7** | **16.1** | **13.8** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 28: VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA**

| Aina ya Riba | Wastani wa Mwaka (Asilimia) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
| Riba ya Benki kuu (Discount rate) | 16.00 | 7.00 | 7.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 8.38 |
| Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla | 6.00 | 2.21 | 5.13 | 4.50 | 4.44 | 4.53 | 5.37 | 7.50 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | 11.10 | 6.43 | 7.71 | 4.42 | 4.78 | 4.64 | 7.32 | 10.67 |
| Siku 35 | 5.54 | 2.51 | 3.47 | 2.37 | 2.60 | 2.25 | 4.20 | 5.99 |
| Siku 91 | 5.49 | 2.89 | 4.17 | 2.37 | 2.74 | 2.80 | 5.36 | 6.94 |
| Siku 182 | 10.01 | 4.13 | 5.07 | 2.88 | 3.20 | 3.47 | 6.37 | 8.00 |
| Siku 364 | 11.79 | 7.08 | 8.04 | 2.32 | 4.85 | 4.79 | 7.69 | 10.72 |
| **Riba za Hatifungani** | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 14.52 | 9.42 | 11.45 | 8.14 | 7.67 | 6.56 | 9.75 | 11.64 |
| Miaka mitano | 15.78 | 11.64 | 12.56 | 11.24 | 9.19 | 9.04 | 9.89 | 10.67 |
| Miaka saba | 16.31 | 12.62 | 13.09 | 11.48 | 10.09 | 9.58 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 16.79 | 14.39 | 15.04 | 12.51 | 11.59 | 10.63 | 11.35 | 12.63 |
| Miaka kumi na tano | 17.54 | 14.69 | 15.52 | 14.05 | 13.59 | 11.7 | 11.95 | 14.73 |
| Miaka ishirini | - | 17.7 | 17.35 | 15.79 | 16.06 | 12.22 | 12.96 | 15.30 |
| Miaka ishirini na tano | | | | | 16.09 | 12.76 | 13.46 | 15.55 |
| **Riba za Amana** | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 3.03 | 2.52 | 2.44 | 2.34 | 1.95 | 1.69 | 1.86 | 2.80 |
| Amana za muda maalum kwa ujumla | 10.04 | 8.24 | 7.25 | 6.7 | 6.85 | 7.11 | 7.07 | 7.85 |
| Mwaka mmoja | 11.66 | 8.78 | 8.8 | 8.28 | 8.32 | 8.53 | 8.65 | 9.17 |
| **Riba za Mikopo** | | | | | | | | |
| Mikopo kwa ujumla | 17.77 | 17.43 | 16.97 | 16.66 | 16.59 | 16.18 | 15.76 | 15.47 |
| Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja | 18.3 | 18.25 | 16.69 | 15.73 | 16.43 | 16.79 | 16.53 | 15.82 |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## SURA YA 3

## FEDHA ZA SERIKALI

**Utangulizi**

72. Mwaka 2024/25, Serikali iliendelea kuchukua hatua za kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo. Hatua hizo zilichukuliwa kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kibajeti na kuendelea kugharamia utekelezaji wa vipaumbele mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, (2021/22 - 2025/26) pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

73. Baadhi ya maeneo mahsusi yaliyopewa kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo: kuendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na ya kimkakati; kuimarisha sekta za uzalishaji; kuimarisha rasilimali watu hususan katika sekta za huduma za jamii; kuongeza matumizi ya TEHAMA; na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji wa sekta binafsi. Aidha, maeneo mengine yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na: kugharamia mishahara ya watumishi wa umma; deni la Serikali; uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; na maandalizi ya Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika ya mwaka 2027 yanayojumuisha ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo.

74. Shabaha za uchumi jumla katika bajeti ya mwaka 2024/25 zilikuwa: kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa hadi asilimia 5.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023; kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 - 5.0 katika muda wa kati; mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/24; mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 12.6 mwaka 2023/24; kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.4 ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Mwenendo wa baadhi ya malengo unaonesha kuwa: Pato la Taifa lilikua kwa zaidi ya lengo lililokusudiwa na kufikia asilimia 5.5 mwaka 2024; mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya lengo husika na ulikuwa asilimia 3.1 mwaka 2024 na akiba ya fedha za kigeni hadi Machi 2025 ilikuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.6 ambayo ni zaidi ya lengo. Mwenendo wa malengo ya kibajeti utapatikana mara baada ya mwaka wa fedha kukamilika.

75. Mwaka 2024/25, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha bajeti ya Serikali ya shilingi bilioni 49,345.7 mwezi Juni 2024. Hata hivyo, kutokana na kupokelewa kwa jumla ya shilingi 945.7 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika - AfDB na Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa, Serikali iliwasilisha mapendekezo ya bajeti ya nyongeza ambayo iliidhinishwa na Bunge. Hivyo, bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 imeongezeka kutoka shilingi bilioni 49,345.7 hadi shilingi bilioni 50,291.4. Kutokana na ongezeko hilo, lengo la nakisi ya bajeti liliongezeka kutoka asilimia 2.9 ya Pato la Taifa hadi asilimia 3.4.

76. Bajeti ya mwaka 2024/25 inajumuisha: mapato ya ndani jumla ya shilingi bilioni 34,610.6; misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 794.4; mikopo kutoka nje shilingi bilioni 8,268.6, ambapo mikopo yenye masharti ya kibiashara ni shilingi bilioni 2,986.6; na Mikopo ya kibiashara kutoka ndani shilingi bilioni 6,617.8. Kwa upande wa matumizi, shilingi bilioni 33,863.8 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 16,427.6 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, utekelezaji wa bajeti ya Serikali ulionesha mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na usimamizi madhubuti wa matumizi ya fedha za umma.

**Mwenendo wa Mapato**

**Mapato ya Ndani**


77. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 25,669.8, sawa na asilimia 100.2 ya lengo la kipindi hicho na ukuaji wa asilimia 16.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Katika kipindi hicho, mapato ya kodi, ambayo yalichangia asilimia 82.7 ya makusanyo ya ndani yalifikia shilingi bilioni 21,223.3, sawa na ufanisi wa asilimia 101.4 na ukuaji wa asilimia 15.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi ulitokana na kuongezeka kwa uhiari wa ulipaji kodi kupitia uboreshaji wa huduma kwa walipakodi na uboreshwaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini pamoja na kuanza kwa matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Forodha - TANCIS ulioboreshwa ambao umeimarisha usimamizi wa vyanzo vyote vya mapato ya forodha.

**Jedwali Na. 3.1: Mapato ya Ndani, Mwaka 2023/24 - 2024/25 (Shilingi Bilioni)**

| | 2023/24 | 2024/25 | | Ufanisi | Ukuaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Makadirio | Halisi | (Asilimia) | (Asilimia) |
| **Mapato ya Ndani** | **22,026.0** | **25,609.7** | **25,669.8** | **100.2** | **16.5** |
| **Mapato Yanayokusanywa na TRA** | **19,428.0** | **21,973.4** | **22,291.7** | **101.4** | **14.7** |
| Kodi | 18,376.8 | 20,924.3 | 21,223.3 | 101.4 | 15.5 |
| Yasiyo ya Kodi | 1,051.1 | 1,049.1 | 1,068.4 | 101.8 | 1.6 |
| **Mapato Yasiyo ya Kodi** | **2,598.1** | **3,636.3** | **3,378.1** | **92.9** | **30.0** |
| Wizara na Idara Zinazojitegemea | 1,344.0 | 1,924.6 | 1,678.9 | 87.2 | 24.9 |
| Ofisi ya Msajili wa Hazina | 405.9 | 704.8 | 658.3 | 93.4 | 62.2 |
| Halmashauri | 848.1 | 1,007.0 | 1,040.9 | 103.4 | 22.7 |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

**Kielelezo Na. 3.1: Mapato ya Kodi, Julai 2024 - Machi 2025**




## Misaada na Mikopo Nafuu


78. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, misaada iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 999.6 sawa na asilimia 212.0 ya makadirio ya kipindi hicho. Aidha, mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 4,168.1, sawa na asilimia 101.6 ya lengo la kipindi hicho. Ufanisi wa misaada na mikopo nafuu ulichangiwa na utekelezaji unaoridhisha wa miradi ya maendeleo pamoja na uwasilishwaji wa taarifa za utekelezaji kwa Washirika wa Maendeleo kwa wakati.

**Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Fedha za Nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Julai 2024 - Machi 2025**


Mwenendo wa Misaada na Mikopo Nafuu




Mwenendo kwa Aina ya Matumizi



Mchango wa Misaada na Mikopo




Mchango kwa Aina za Matumizi




**Mikopo Yenye Masharti ya Kibiashara ya Ndani na Nje**

79. Mwaka 2024/25, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 6,617.8 kutoka vyanzo vya ndani. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Serikali ilikopa shilingi bilioni 5,072.8 kutoka soko la ndani, sawa na asilimia 76.7 ya lengo la mwaka 2024/25. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,203.6 zilitumika kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 1,869.2 zilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa upande mwingine, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Serikali ilikopa shilingi bilioni 2,413.7 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi

mbalimbali ya maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 80.8 ya shilingi bilioni 2,986.6 ambazo Serikali ilipanga kukopa mwaka 2024/25.

**Mwenendo wa Matumizi**

80. Mwaka 2024/25, Serikali iliendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kuboresha uendeshaji wa shughuli zake na kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria mbalimbali ikiwemo: Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma ya Mwaka 2024. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali katika kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwemo, kuzichukulia hatua taasisi za Serikali zinazokiuka taratibu za ununuzi wa umma ikiwemo kufanya ununuzi bila kupata ridhaa za bodi za zabuni.

81. Mwaka 2024/25, Serikali ilikadiria kutumia shilingi bilioni 50,291.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 33,863.7 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 16,427.6 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 32.9 ya bajeti yote. Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida ilijumuisha shilingi bilioni 13,121.5 kwa ajili ya kulipa deni la Serikali, shilingi bilioni 11,980.9 mishahara na shilingi bilioni 8,646.3 matumizi mengineyo. Vilevile, bajeti ya matumizi ya maendeleo ilijumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 12,901.8 na fedha za nje shilingi bilioni 3,640.9.

82. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, ridhaa ya matumizi iliyotolewa kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni 34,470.9, sawa na asilimia 91.4 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 24,442.1 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 10,028.8 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kiasi kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilijumuisha shilingi bilioni 8,329.0 za kugharamia malipo ya deni la Serikali inayojumuisha malipo ya riba kwa deni la ndani na nje shilingi bilioni 3,502.4 na malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje shilingi bilioni 4,826.6. Vilevile, matumizi ya kawaida yalijumuisha shilingi bilioni 8,355.4 za kugharamia malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali, sawa na asilimia 98.0 ya lengo la shilingi bilioni 8,525.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4,367.3 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu na shilingi bilioni 3,988.1 zililipwa kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.


83. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 10,028.8 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilitolewa, sawa na asilimia 80.8 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 9,828.7 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 200.1 fedha za nje. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 3,783.4 kilipelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi (D-fund) ambazo zinasubiri kuhasibiwa. Kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa

fedha za maendeleo kulisababishwa na kutohasibiwa kwa wakati kwa fedha zinazopelekwa moja kwa moja na Washirika wa Maendeleo kwenye utekelezaji wa miradi.

**Deni la Serikali**

84. Hadi Machi 2025, Deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 104,931.1 kutoka shilingi bilioni 91,708.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 34,255.4 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 70,675.7. Ongezeko la deni lilitokana na Serikali kuendelea kupokea mikopo mipya na ya zamani kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

**Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Deni la Serikali, Machi 2018 - 2025 (Shilingi Bilioni)**




| | Machi-2018 | Machi-2019 | Machi-2020 | Machi-2021 | Machi-2022 | Machi-2023 | Machi-2024 | Machi-2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Ndani | 14,158.6 | 13,133.1 | 14,730.7 | 16,116.5 | 21,778.0 | 26,851.7 | 30,753.8 | 34,255.4 |
| Deni la Nje | 35,729.9 | 37,639.2 | 40,245.4 | 43,736.1 | 47,483.2 | 50,158.7 | 60,954.5 | 70,675.7 |
| Deni la Serikali | 49,728.03 | 50,772.27 | 54,976.15 | 59,852.62 | 69,261.20 | 77,010.4 | 91,708.3 | 104,931.1 |

**Deni la Nje**

85. Hadi Machi 2025, deni la Serikali la nje lilifikia dola za Marekani milioni 26,670.32 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 23,720.86 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo ya zamani na mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, mashirika ya fedha ya kimataifa yaliendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia 67.8 ya deni lote la nje ikilinganishwa na asilimia 63.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Benki za biashara zilichangia asilimia 26.9 na Washirika wa Maendeleo walichangia asilimia 5.3 ya deni lote la nje.

**Jedwali Na. 3.2: Deni la Nje kwa Wakopeshaji Mwaka, 2023 - 2025 (Dola za Marekani Milioni)**


| Taasisi | Machi 2023 | Mchango (Asilimia) | Machi 2024 | Mchango (Asilimia) | Machi 2025 | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya Fedha ya Kimataifa | 13,456.60 | 62 | 15,972.60 | 67.3 | 18,071.70 | 67.8 |
| Washirika wa Maendeleo | 2,267.00 | 10.5 | 1,379.10 | 5.8 | 1,426.20 | 5.3 |
| Benki za kibiashara | 5,976.60 | 27.5 | 6,369.20 | 26.9 | 7,172.50 | 26.9 |
| **Jumla** | **21,700.20** | **100** | **23,720.80** | **100** | **26,670.30** | **100** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

**Deni la Ndani**

86. Hadi Machi 2025, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 34,255.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 30,753.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.4. Katika kipindi hicho, mikopo ya hatifungani iliendelea kuwa sehemu kubwa ya deni la ndani ikiwa na asilimia 66.5 ya deni lote la ndani. Aidha, dhamana za Serikali za muda mfupi zilikuwa asilimia 5.5 na hati fungani maalum asilimia 13.0.

**Kielelezo Na. 3.4: Mwenendo wa Deni la Ndani, Mwaka 2020 - 2025 (Shilingi Bilioni)**




87. Hadi Machi 2025, benki za biashara ziliendelea kuongoza kwa kuhodhi asilimia 37.1 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimia 42.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, mifuko ya hifadhi ya jamii ilihodhi asilimia 33.9 ikifuatiwa na watu binafsi asilimia 14.6 na kampuni za bima asilimia 6.9. Kumekuwepo na hamasa na ongezeko la ushiriki wa watu binafsi katika dhamana za serikali kutoka asilimia 8.0 Machi 2023 hadi asilimia 14.6 Machi 2025 kufuatia kuendelea kutolewa kwa elimu kwa umma.

**Jedwali Na. 3.3: Deni la Ndani kwa Wakopeshaji, Mwaka 2023 - 2025 (Shilingi bilioni)**

| Taasisi | Machi 2023 | Mchango Asilimia | Machi 2024 | Mchango Asilimia | Machi 2025 | Mchango Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za Biashara | 7,204.82 | 34.8 | 10,169.95 | 42.0 | 9,948.42 | 37.1 |
| Taasisi za Fedha | 211.72 | 1.0 | 686.44 | 2.8 | 1,178.54 | 4.4 |
| Mifuko ya Jamii | 7,961.12 | 38.5 | 8,211.84 | 33.9 | 9,091.49 | 33.9 |
| Kampuni za Bima | 1,494.73 | 7.2 | 1,844.75 | 7.6 | 1,845.50 | 6.9 |
| Taasisi za Kigeni | 1,006.93 | 4.9 | - | - | 132.25 | 0.5 |
| Mashirika Madogo | 1,162.49 | 5.6 | 593.79 | 2.4 | 700.63 | 2.6 |
| Watu binafsi | 1,660.20 | 8.0 | 2,733.60 | 11.3 | 3,918.89 | 14.6 |
| **Jumla** | **20,702.01** | **100.00** | **24,240.37** | **100.0** | **26,815.73** | **100.0** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Tathmini ya Uhimilivu wa Deni**

88. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Oktoba, 2024 ilionesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Tathmini hiyo hufanyika kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa; uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje; na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

89. Kwa mujibu wa Tathmini hiyo, viashiria vya deni vilionesha kuwa mwaka 2024/25: thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 24.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 123.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 13.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 17.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Kwa upande wa viashiria vya deni lote (deni la nje na ndani), thamani ya sasa ya deni kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.3 ikilinganisha na ukomo wa asilimia 55.

**Jedwali Na.3.4: Mwenendo wa Viashiria vya Deni la Serikali**

| **Viashiria vya Deni la Nje** | **2024/25** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2034/35** | **Ukomo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni (PV)/pato la taifa | 24.1 | 24 | 23 | 21.4 | 20.3 | 19.6 | 16.6 | 40 |
| Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje | 123.8 | 124.5 | 119.5 | 111.9 | 106.4 | 100.3 | 85.2 | 180 |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje | 13.9 | 12.8 | 12.3 | 12.8 | 12.6 | 12.4 | 9 | 15 |
| Ulipaji wa deni /Mapato ya ndani | 17.2 | 15.5 | 14.8 | 15.2 | 14.8 | 15 | 10.9 | 18 |
| **Viashiria vya Deni la Nje na Ndani** | **2024/25** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2034/35** | **Ukomo** |
| Deni (PV)/ Pato la Taifa | 40.3 | 39.5 | 38.1 | 36.8 | 36.5 | 36.4 | 35.9 | 55 |
| Deni (PV)/ Mapato ya ndani | 251.1 | 241.3 | 232.1 | 224.4 | 222.3 | 221.7 | 219 | - |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 50.9 | 40.8 | 37.1 | 35.9 | 36.1 | 39.9 | 37 | - |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Tathmini ya Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa**

90. Machi 2025, Kampuni ya Moody's Investors Services ilifanya mapitio ya pili ya uchumi wa Tanzania ili kubaini uwezo wa nchi kukopesheka. Katika mapitio hayo, Tanzania iliendelea kubaki katika daraja la B1 ikiwa ni mtazamo thabiti (Stable Outlook) kama ilivyokua Machi 2024. Daraja la B1 linaashiria kuendelea kuimarika kwa uchumi wa nchi na uwezo wa nchi kuhimili misukosuko ya kiuchumi kutoka nje. Kwa upande mwingine, Kampuni ya Fitch Ratings ilifanya mapitio kama hayo Desemba 2024 na kuipa Tanzania alama ya B+ ikiwa na mtazamo thabiti (Stable Outlook) kama ilivyokuwa Juni 2024. Matokeo hayo ni muhimu katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje pamoja na kuongeza upatikanaji wa fedha katika masoko ya fedha ya kimataifa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya Serikali na sekta binafsi.


## Jedwali Na. 29: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

**Shilingi Milioni**

| | 2021/22 Halisi | 2022/23 Halisi | 2023/24 Halisi | 2024/25 Bajeti | 2024/25 Matarajio hadi Machi | 2024/25 Matarajio hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri) | **24,395,566.1** | **26,277,887.1** | **29,829,894.6** | **34,610,646.4** | **25,669,814.8** | **34,610,646.4** |
| MAPATO YA NDANI | 23,506,098.2 | 25,256,847.8 | 28,683,341.7 | 33,254,305.8 | 24,628,954.7 | 33,254,305.8 |
| 1. Mapato yatokanayo na Kodi | 20,931,261.6 | 21,411,398.9 | 24,760,798.4 | 28,118,753.1 | 21,223,302.4 | 28,118,753.1 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 4,367,465.7 | 4,583,909.9 | 5,351,281.6 | 6,107,513.3 | 4,510,966.2 | 6,107,513.3 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 6,297,722.6 | 7,066,881.5 | 7,594,384.7 | 8,691,184.1 | 6,941,316.6 | 8,691,184.1 |
| Bidhaa toka nje | 3,344,798.5 | 3,639,577.6 | 3,748,862.6 | 4,329,465.8 | 3,402,251.3 | 4,329,465.8 |
| Bidhaa za ndani | 2,952,924.1 | 3,427,304.0 | 3,845,522.2 | 4,361,718.2 | 3,539,065.3 | 4,361,718.2 |
| Kodi ya Mapato | 7,549,185.9 | 7,760,301.5 | 9,159,412.6 | 10,160,099.0 | 7,746,281.2 | 10,160,099.0 |
| Kodi nyingine | 3,712,545.6 | 3,073,133.2 | 3,718,162.4 | 4,194,150.2 | 3,307,454.0 | 4,194,150.2 |
| Marejesho (Refunds Accounts) | (995,658.2) | (1,072,827.2) | (1,062,443.0) | (1,034,193.5) | (1,282,715.7) | (1,034,193.5) |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 2,574,836.6 | 3,845,448.9 | 3,922,543.3 | 5,135,552.7 | 3,405,652.4 | 5,135,552.7 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | 889,467.9 | 1,021,039.3 | 1,146,552.9 | 1,356,340.7 | 1,040,860.0 | 1,356,340.7 |
| B. JUMLA YA MATUMIZI | **31,815,747.3** | **34,445,838.0** | **36,567,630.8** | **42,751,915.7** | **31,841,598.8** | **42,751,915.7** |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 15,998,691.7 | 20,475,131.8 | 21,931,209.5 | 27,398,315.8 | 19,765,077.8 | 27,398,315.8 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 15,817,055.6 | 13,970,706.2 | 14,636,421.3 | 15,353,599.8 | 12,076,521.0 | 15,353,599.8 |
| Fedha za ndani | 12,386,668.7 | 12,259,082.3 | 11,182,316.4 | 11,712,761.6 | 9,944,972.7 | 11,712,761.6 |
| Fedha za nje | 3,430,387.0 | 1,711,623.9 | 3,454,104.9 | 3,640,838.2 | 2,131,548.4 | 3,640,838.2 |
| C. NAKISI/SALIO (A-B) | **(7,420,181.2)** | **(8,167,950.9)** | **(6,737,736.2)** | **(8,141,269.2)** | **(6,171,784.1)** | **(8,141,269.2)** |
| D. KUZIBA NAKISI | **7,420,181.2** | **8,167,950.9** | **6,737,736.2** | **8,141,269.2** | **6,171,784.1** | **8,141,269.2** |
| 1. Fedha kutoka nje | 3,818,767.9 | 3,681,040.7 | 4,671,036.5 | 5,545,852.3 | 3,511,403.9 | 5,545,852.3 |
| Ruzuku | 622,525.4 | 506,327.7 | 634,687.6 | 794,390.3 | 693,445.5 | 794,390.3 |
| Basket support | 85,966.8 | 90,052.5 | 40,312.1 | 66,483.0 | 32,678.0 | 66,483.0 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 1,298,502.6 | 1,851,237.4 | 2,013,708.2 | 2,326,471.4 | 1,611,053.1 | 2,326,471.4 |
| Mikopo ya miradi | 2,818,336.6 | 1,115,243.7 | 2,892,901.4 | 2,888,989.0 | 1,405,424.9 | 2,888,989.0 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | 1,809,493.7 | 3,011,725.4 | 2,101,240.6 | 2,986,638.2 | 1,729,837.9 | 2,986,638.2 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign) | (2,816,057.3) | (2,893,546.0) | (3,011,813.4) | (3,517,119.6) | (1,961,035.6) | (3,517,119.6) |
| 2. Fedha za Ndani | 2,850,002.5 | 4,597,523.4 | 2,175,319.3 | 2,595,417.0 | 3,096,418.8 | 2,595,417.0 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | 1,003,509.3 | 2,171,460.3 | 2,445,972.9 | 294,625.8 | 2,466,361.9 | 294,625.8 |
| Mikopo ya mabenki | 1,846,493.2 | 2,426,063.1 | (270,653.6) | 2,300,791.1 | 630,056.8 | 2,300,791.1 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | 3,044,431.8 | 3,513,913.7 | 3,257,143.9 | 4,022,373.0 | 3,250,216.6 | 4,022,373.0 |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | 753,597.9 | (97,656.8) | (99,896.3) | - | (436,038.6) | - |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | (3,044,431.8) | (3,513,913.7) | (3,257,143.9) | (4,022,373.0) | (3,250,216.6) | (4,022,373.0) |
| Expenditure float | (2,187.1) | (12,956.4) | (8,723.3) | - | - | - |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Kielelezo Na. 3.4: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI (Shilingi Milioni)**



# Jedwali Na. 30: MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

**Shilingi Milioni**

| Fungu | Maelezo | Halisi 2023/2024 | | | Bajeti iliyoidhinishwa 2024/2025 | | | Makadirio 2025/2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **701** | **Huduma za Kawaida** | **10,684,676** | **1,374,733** | **12,059,409** | **14,393,556** | **1,944,419** | **16,337,976** | **17,078,733** | **2,593,807** | **19,672,540** |
| 70111 | Utawala na Shughuli za Bunge (CS) | 2,927,868 | 892,334 | 3,820,201 | 4,063,650 | 1,322,851 | 5,386,502 | 5,012,826 | 1,709,025 | 6,721,851 |
| 70112 | Fedha na Masuala ya Kodi (CS) | 3,154,409 | 438,807 | 3,593,216 | 4,444,509 | 553,996 | 4,998,505 | 5,198,385 | 766,348 | 5,964,733 |
| 70113 | Mambo ya Nje (CS) | 178,785 | 18,401 | 197,185 | 226,798 | 11,633 | 238,432 | 290,263 | 45,540 | 335,803 |
| 70121 | Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje (CS) | 2,402 | 0 | 2,402 | 2,882 | 0 | 2,882 | 3,210 | 0 | 3,210 |
| 70122 | Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa(CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70131 | Huduma za Umma (CS) | 14,206 | 0 | 14,206 | 16,560 | 3,265 | 19,825 | 19,108 | 1,823 | 20,931 |
| 70132 | Huduma za Mipango na Takwimu (CS) | 36,084 | 22,150 | 58,234 | 48,612 | 52,379 | 100,991 | 51,960 | 69,894 | 121,854 |
| 70133 | Huduma nyingine za Kawaida (CS) | 4,320 | 3,043 | 7,363 | 5,758 | 296 | 6,054 | 6,665 | 1,177 | 7,842 |
| 70140 | Utafiti wa Msingi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70150 | Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma (CS) | 987 | 0 | 987 | 2,813 | 0 | 2,813 | 2,601 | 0 | 2,601 |
| 70160 | Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70170 | Deni la Taifa (CS) | 4,365,614 | 0 | 4,365,614 | 5,581,973 | 0 | 5,581,973 | 6,493,715 | 0 | 6,493,715 |
| 70180 | Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **702** | **Ulinzi** | **2,754,559** | **1,837,971** | **4,592,530** | **2,985,220** | **314,918** | **3,300,138** | **3,303,106** | **315,298** | **3,618,403** |
| 70210 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi (CS) | 2,752,548 | 77,240 | 2,829,788 | 2,984,250 | 140,811 | 3,125,061 | 3,302,069 | 116,043 | 3,418,112 |
| 70220 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70230 | Misaada ya Nje ya Ulinzi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70240 | Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi (CS) | 2,011 | 1,760,731 | 1,762,742 | 970 | 174,107 | 175,077 | 1,037 | 199,254 | 200,291 |
| 70250 | Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **703** | **Usalama wa Raia** | **1,588,285** | **124,683** | **1,712,968** | **1,765,643** | **385,803** | **2,151,447** | **2,161,462** | **568,960** | **2,730,422** |
| 70310 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi (CS) | 851,042 | 59,000 | 910,042 | 912,360 | 224,375 | 1,136,735 | 1,054,660 | 203,355 | 1,258,015 |
| 70320 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia (CS) | 49,599 | 11,983 | 61,582 | 56,661 | 6,527 | 63,188 | 62,714 | 15,139 | 77,853 |
| 70330 | Mahakama (CS) | 273,406 | 17,413 | 290,819 | 349,609 | 107,447 | 457,056 | 522,814 | 163,829 | 686,644 |
| 70340 | Magereza (CS) | 271,000 | 2,349 | 273,349 | 285,876 | 7,336 | 293,213 | 310,043 | 6,357 | 316,400 |
| 70350 | Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70360 | Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu (CS) | 143,238 | 33,939 | 177,177 | 161,137 | 40,119 | 201,255 | 211,230 | 180,279 | 391,509 |
| **704** | **Shughuli za Kiuchumi** | **1,238,961** | **7,164,274** | **8,403,235** | **1,258,539** | **8,511,635** | **9,770,174** | **1,389,859** | **9,829,883** | **11,219,742** |
| 70411 | Shughuli za Kiuchumi na Biashara (CS) | 110,429 | 76,025 | 186,454 | 155,248 | 88,549 | 243,798 | 197,568 | 93,288 | 290,857 |
| 70412 | Masuala ya Kazi (CS) | 10,710 | 7,889 | 18,598 | 19,949 | 10,513 | 30,461 | 23,690 | 9,892 | 33,582 |
| 70421 | Kilimo (CS) | 256,260 | 472,415 | 728,675 | 345,004 | 1,260,641 | 1,605,646 | 361,780 | 1,218,960 | 1,580,740 |
| 70422 | Misitu (CS) | 49,792 | 35 | 49,827 | 63,278 | 5,673 | 68,950 | 63,532 | 34,442 | 97,973 |
| 70423 | Uvuvi na Uwindaji (CS) | 24,916 | 80,458 | 105,374 | 27,515 | 83,839 | 111,354 | 21,663 | 76,753 | 98,416 |
| 70431 | Makaa ya Mawe na Nishati nyingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70432 | Petroli na Gesi Asilia (CS) | 18,790 | 310,028 | 328,819 | 20,600 | 67,388 | 87,988 | 8,149 | 169,332 | 177,481 |
| 70433 | Nishati ya Nyukilia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70434 | Nishati nyingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70435 | Umeme (CS) | 2,636 | 1,841,931 | 1,844,567 | 56,274 | 1,726,459 | 1,782,733 | 56,147 | 1,995,181 | 2,051,329 |
| 70436 | Nishati isiyo ya umeme (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70441 | Uchimbaji Madini yasiyo Nishati (CS) | 66,465 | 85,322 | 151,787 | 90,082 | 140,661 | 230,743 | 99,117 | 124,605 | 223,722 |
| 70442 | Uzalishaji Viwandani (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70443 | Ujenzi (CS) | 18,344 | 23,457 | 41,801 | 22,802 | 54,475 | 77,278 | 27,157 | 54,475 | 81,632 |
| 70451 | Usafiri wa Barabara (CS) | 176,774 | 3,963,194 | 4,139,968 | 212,354 | 4,805,978 | 5,018,332 | 237,491 | 5,346,569 | 5,584,060 |
| 70452 | Usafiri wa Majini (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70453 | Usafiri wa Reli (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70454 | Usafiri wa Anga (CS) | 196 | 53,381 | 53,578 | 310 | 109,718 | 110,028 | 278 | 343,870 | 344,147 |
| 70455 | Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70460 | Mawasiliano (CS) | 66,575 | 95,504 | 162,079 | 58,751 | 83,965 | 142,715 | 98,761 | 266,758 | 365,519 |
| 70471 | Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Jedwali Na. 30 Linaendelea**

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 70472 | Hoteli na Migahawa (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70473 | Utalii (CS) | 431,111 | 149,701 | 580,811 | 134,667 | 54,761 | 189,428 | 141,588 | 43,758 | 185,346 |
| 70474 | Miradi ya Maendeleo (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70481 | Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi (CS) | 129 | 0 | 129 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70482 | Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na Uwindaji (CS) | 5,834 | 4,933 | 10,767 | 51,705 | 19,014 | 70,720 | 52,938 | 52,000 | 104,938 |
| 70483 | Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70484 | Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70485 | Utafiti na Maendeleo ya Usafiri (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70486 | Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70487 | Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70490 | Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **705** | **Hifadhi ya Mazingira** | **42,587** | **1,016** | **43,603** | **69,587** | **68,479** | **138,066** | **74,099** | **58,725** | **132,825** |
| 70510 | Hifadhi ya Taka (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70520 | Hifadhi ya Maji Taka (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70530 | Kupunguza Uharibifu wa Mazingira (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70540 | Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70550 | Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira (CS) | 845 | 0 | 845 | 1,124 | 0 | 1,124 | 1,145 | 0 | 1,145 |
| 70560 | Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu (CS) | 41,741 | 1,016 | 42,758 | 68,463 | 68,479 | 136,942 | 72,954 | 58,725 | 131,680 |
| **706** | **Nyumba na Huduma za Jamii** | **166,613** | **748,690** | **915,303** | **216,616** | **885,071** | **1,101,688** | **236,434** | **1,139,484** | **1,375,918** |
| 70610 | Maendeleo ya Nyumba (CS) | 41,465 | 3,119 | 44,584 | 44,816 | 14,333 | 59,149 | 46,582 | 75,695 | 122,277 |
| 70620 | Maendeleo ya Jamii (CS) | 68,521 | 315,253 | 383,774 | 102,435 | 304,581 | 407,016 | 115,094 | 112,093 | 227,187 |
| 70630 | Usambazaji Maji (CS) | 56,626 | 430,319 | 486,945 | 69,366 | 566,157 | 635,523 | 74,758 | 951,696 | 1,026,454 |
| 70640 | Taa za Barabarani (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70650 | Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70660 | Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **707** | **Afya** | **1,194,710** | **622,178** | **1,816,888** | **1,383,306** | **1,022,852** | **2,406,158** | **1,416,202** | **1,304,628** | **2,720,830** |
| 70711 | Madawa (IS) | 740 | 227,184 | 227,923 | 1,321 | 205,088 | 206,410 | 1,382 | 300,000 | 301,382 |
| 70712 | Bidhaa nyingine za madawa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70713 | Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70721 | Huduma za Tiba za Jumla (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70722 | Huduma Maalumu za Tibas (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70723 | Huduma za Meno (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70724 | Huduma za Wakunga Wasaidizi (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70731 | Huduma za Hospitali (IS) | 31,661 | 9,493 | 41,154 | 28,371 | 25,620 | 53,991 | 26,841 | 16,992 | 43,833 |
| 70732 | Huduma Maalumu za Hospitali (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70733 | Huduma za Vifaa vya Kujifungulia (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70734 | Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi (IS) | 642 | 0 | 642 | 822 | 0 | 822 | 930 | 0 | 930 |
| 70740 | Huduma za Afya kwa Umma (IS) | 716,862 | 296,348 | 1,013,209 | 783,265 | 471,643 | 1,254,908 | 826,783 | 535,153 | 1,361,935 |
| 70750 | Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70760 | Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu (CS) | 444,807 | 89,153 | 533,960 | 569,527 | 320,500 | 890,027 | 560,266 | 452,484 | 1,012,750 |
| **708** | **Burudani, Utamaduni na Dini** | **32,261** | **10,767** | **43,028** | **29,082** | **258,226** | **287,308** | **34,771** | **426,821** | **461,592** |
| 70810 | Huduma za Burudani na Michezo (IS) | 1,138 | 262 | 1,400 | 2,522 | 35 | 2,557 | 2,971 | 130 | 3,101 |
| 70820 | Huduma za Utamaduni (IS) | 31,123 | 10,505 | 41,628 | 26,541 | 258,191 | 284,732 | 31,710 | 426,691 | 458,401 |
| 70830 | Huduma za Utangazaji na Uchapishaji (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70840 | Dini na Huduma nyingine za Kijamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70850 | Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70860 | Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 18 | 0 | 18 | 89 | 0 | 89 |
| **709** | **Elimu** | **3,740,258** | **1,915,485** | **5,655,744** | **3,715,076** | **2,460,629** | **6,175,705** | **3,896,463** | **3,117,686** | **7,014,149** |
| 70911 | Elimu ya Awali (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70912 | Elimu ya Msingi (IS) | 2,022,280 | 412,148 | 2,434,428 | 1,968,682 | 739,427 | 2,708,109 | 2,059,578 | 870,998 | 2,930,577 |
| 70921 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV) (IS) | 1,182,306 | 548,772 | 1,731,078 | 1,121,962 | 501,378 | 1,623,340 | 1,163,690 | 664,769 | 1,828,458 |
| 70922 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI) (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70930 | Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu (IS) | 390,396 | 834,917 | 1,225,314 | 427,280 | 1,072,675 | 1,499,955 | 465,053 | 1,404,608 | 1,869,661 |
| 70941 | Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu (IS) | 24,613 | 27,688 | 52,301 | 41,365 | 32,123 | 73,488 | 44,954 | 40,483 | 85,437 |
| 70942 | Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu (IS) | 14,157 | 2,000 | 16,157 | 21,782 | 2,000 | 23,782 | 20,962 | 1,200 | 22,162 |
| 70950 | Elimu isiyopambanuliwa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70960 | Huduma za Ziada kwa Elimu (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70970 | Utafiti na Maendeleo ya Elimu (CS) | 49,791 | 8,486 | 58,277 | 59,330 | 13,043 | 72,373 | 65,096 | 23,523 | 88,619 |
| 70980 | Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu (CS) | 56,714 | 81,474 | 138,188 | 74,676 | 99,982 | 174,658 | 77,132 | 112,105 | 189,236 |
| **710** | **Kinga ya Jamii** | **24,259** | **24,661** | **48,920** | **30,205** | **107,332** | **137,538** | **33,391** | **107,652** | **141,042** |
| 71011 | Ugonjwa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71012 | Ulemavu (IS) | 1,165 | 1,536 | 2,701 | 1,898 | 1,689 | 3,588 | 1,726 | 1,000 | 2,726 |
| 71020 | Wazee (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71030 | Waathirika (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71040 | Familia na Watoto (IS) | 2,024 | 2,447 | 4,471 | 2,866 | 5,178 | 8,044 | 2,995 | 4,420 | 7,415 |
| 71050 | Ukosefu wa Ajira (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71060 | Nyumba (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71070 | Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu (IS) | 10,956 | 400 | 11,356 | 12,902 | 1,415 | 14,317 | 13,643 | 3,000 | 16,643 |
| 71080 | Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71090 | Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 10,114 | 20,278 | 30,392 | 12,538 | 99,051 | 111,589 | 15,027 | 99,232 | 114,259 |
| **7** | **Jumla** | **21,467,168** | **13,824,459** | **35,291,627** | **25,846,831** | **15,959,364** | **41,806,195** | **29,624,520** | **19,462,944** | **49,087,464** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
CS: Collective Services IS: Individual Services

## SURA YA 4

## SEKTA YA NJE

**Bidhaa Zilizouzwa Nje**

91. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 9,121.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,696.6 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia, hususan korosho, tumbaku na kahawa pamoja na bidhaa zisizo asilia ikiwemo dhahabu, mazao ya mbogamboga na maua na mbegu za mafuta. Aidha, mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 79.2 ya mauzo yote nje ya nchi, ikifuatiwa na bidhaa asilia zilizochangia asilimia 16.2 na bidhaa zisizorekodiwa asilimia 4.6.

**Bidhaa Asilia**

92. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 1,473.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 953.3 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 54.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya korosho, tumbaku na kahawa kufuatia kuongezeka kwa bei katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa korosho na kahawa ndani ya nchi. Mchango wa thamani ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi uliongezeka na kufikia asilimia 16.2 mwaka 2024 kutoka asilimia 12.4 mwaka 2023.

**Korosho**

93. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya korosho nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 541.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 206.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 162.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje kwa asilimia 95.0 na kufikia tani 428,300 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 219,600 zilizouzwa mwaka 2023. Aidha, wastani wa bei ya korosho uliongezeka kwa asilimia 34.6 na kufikia dola za Marekani 1,264.7 kwa tani mwaka 2024 kutoka wastani wa dola za Marekani 939.9 kwa tani mwaka 2023.

**Kahawa**

94. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya kahawa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 292.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 227.9 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 28.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wastani wa bei ya kahawa kwa asilimia 32.0 na kufikia dola za Marekani 3,564.3 kwa tani mwaka 2024 kutoka dola za Marekani 2,700.8 kwa tani mwaka 2023. Hata hivyo, tani 82,200 za kahawa ziliuzwa nje mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 84,400 zilizouzwa nje mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 2.6.

**Pamba**

95. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya pamba nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 69.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 101.9 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 32.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya pamba katika soko la ndani sambamba na kupungua kwa bei ya pamba katika soko la dunia kwa asilimia 9.9 na kufikia wastani wa dola za Marekani 1,318.0 kwa tani mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,463.4 kwa tani mwaka 2023. Aidha, kiasi cha pamba kilichouzwa nje kilipungua kwa asilimia 24.5 hadi tani 52,600 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 69,600 zilizouzwa mwaka 2023.

**Katani**

96. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya katani nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 23.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 20.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kwa asilimia 69.4 na kufikia tani 21,200 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 12,500 zilizouzwa mwaka 2023. Hata hivyo, wastani wa bei ya katani ulipungua hadi dola za Marekani 1,102.3 kwa tani mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,628.9 kwa tani mwaka 2023.

**Chai**

97. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya chai nje ilikuwa dola za Marekani milioni 19.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 31.1 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 37.6. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha chai kilichouzwa nje kwa asilimia 29.0 hadi tani 15,700 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 22,200 zilizouzwa mwaka 2023. Aidha, bei ya chai ilipungua kwa asilimia 12.0 na kufikia dola za Marekani 1,234.9 kwa tani mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,403.6 kwa tani mwaka 2023.

**Tumbaku**

98. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya tumbaku nje ilikuwa dola za Marekani milioni 509.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 340.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 49.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya tumbaku kwa asilimia 32.3 na kufikia tani 108,500 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 82,000 mwaka 2023. Aidha, wastani wa bei ya tumbaku uliongezeka kwa asilimia 13.1 na kufikia dola za Marekani 4,695.9 kwa tani mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 4,150.8 kwa tani mwaka 2023.

**Bidhaa Zisizo Asilia**

99. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 7,228.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,321.6 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya madini na bidhaa nyingine ikiwemo mazao ya mbogamboga na maua pamoja na mbegu za mafuta.

**Madini**

100. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 4,119.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,551.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.0. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu na madini mengine. Katika kipindi hicho, mauzo ya madini yalichangia asilimia 57.0 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia. Aidha, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 11.8 na kufikia dola za Marekani milioni 3,419.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,058.9 mwaka 2023. Vilevile, thamani ya mauzo ya dhahabu ilichangia asilimia 83.0 katika mauzo ya madini.

**Bidhaa za Viwandani**

101. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani ilikuwa dola za Marekani milioni 1,341.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,363.3 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 1.6. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa nyingine za viwandani nje ya nchi, hususan mbolea na saruji ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani yalikuwa yakiongezeka. Katika kipindi hicho, mauzo ya bidhaa za viwandani yalichangia asilimia 18.6 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia.

**Samaki na Mazao ya Samaki**

102. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya samaki na mazao ya samaki nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 180.6 ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 164.0 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji pamoja na bei ya samaki na mazao ya samaki katika soko la dunia. Hata hivyo, kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa nje kilipungua na kufikia tani 29,000 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 41,000 mwaka 2023.

**Mbogamboga na Maua**

103. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 507.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 417.2 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 21.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa bidhaa hizi katika masoko ya nje.

**Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje**

104. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 839.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 690.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 21.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya nafaka na kufikia dola za Marekani milioni 300.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 173.0 mwaka 2023. Bidhaa zinazojumuishwa katika kundi la bidhaa nyinginezo ni pamoja na mbegu za mafuta, nafaka (hususan mahindi na mchele), kakao, ngozi, maharage na bidhaa za mbao. Aidha, sehemu kubwa ya bidhaa hizo ziliuzwa nchi jirani.

### Jedwali Na. 4.1: Bidhaa Zilizouzwa Nje, Mwaka 2020 - 2024

| **Bidhaa** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia (US$ milioni)** | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 145.2 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 292.9 | 28.5 |
| Kiasi ('000 tani) | 64.0 | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 82.2 | -2.6 |
| Bei (US$ kwa tani) | 2,268.9 | 2,284.4 | 2,919.6 | 2,700.8 | 3,564.3 | 32.0 |
| **Pamba** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | 69.3 | -32.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 52.6 | -24.5 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,206.4 | 1,665.0 | 2,113.2 | 1,463.4 | 1,318.0 | -9.9 |
| **Katani** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | 23.4 | 14.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | 21.2 | 69.4 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,566.2 | 1,600.0 | 1,629.1 | 1,628.9 | 1,102.3 | -32.3 |
| **Chai** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 32.4 | 32.9 | 30.0 | 31.1 | 19.4 | -37.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 15.7 | -29.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,345.5 | 1,356.5 | 1,420.3 | 1,403.6 | 1,234.9 | -12.0 |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.4 | 509.5 | 49.7 |
| Kiasi ('000 tani) | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 108.5 | 32.3 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,494.2 | 3,381.5 | 3,624.1 | 4,150.8 | 4,695.9 | 13.1 |
| **Korosho** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 359.6 | 159.0 | 226.9 | 206.4 | 541.7 | 162.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | 428.3 | 95.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,120.6 | 1,030.3 | 970.0 | 939.9 | 1,264.7 | 34.6 |
| **Karafuu** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | 17.1 | -32.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | 2.8 | -39.4 |
| Bei (US$ kwa tani) | 4,770.0 | 7,347.6 | 7,104.0 | 5,356.9 | 6,011.1 | 12.2 |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **808.1** | **627.9** | **766.5** | **953.3** | **1,473.3** | **54.5** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)** | | | | | | |
| **Madini** | **3,375.0** | **3,116.4** | **3,395.3** | **3,551.4** | **4,119.9** | **16.0** |
| Dhahabu | 2,957.5 | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,419.6 | 11.8 |
| Almasi | 20.2 | 8.5 | 62.7 | 23.6 | 53.2 | 125.5 |
| Madini mengine | 397.2 | 370.8 | 497.4 | 469.0 | 647.1 | 38.0 |
| **Bidhaa za Viwandani** | **902.7** | **1,200.0** | **1,419.2** | **1,363.3** | **1,341.3** | **-1.6** |
| Nyuzi za Pamba | 6.9 | 3.6 | 1.9 | 0.5 | 1.2 | 150.0 |
| Kahawa iliyozalishwa | 5.2 | 16.3 | 21.8 | 4.5 | 11.1 | 144.2 |
| Tumbaku iliyozalishwa | 18.3 | 32.0 | 34.5 | 37.9 | 36.0 | -5.1 |
| Mazao ya Katani | 23.2 | 33.6 | 35.4 | 31.4 | 22.9 | -27.1 |
| Bidhaa nyingine za Viwandani | 849.1 | 1,114.5 | 1,325.6 | 1,289.0 | 1,270.2 | -1.5 |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **139.6** | **164.3** | **168.2** | **164.0** | **180.6** | **10.1** |
| **Mazao ya Mboga na Maua** | **274.1** | **378.6** | **289.6** | **417.2** | **507.1** | **21.6** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **87.7** | **90.2** | **131.2** | **135.2** | **240.8** | **78.0** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **474.2** | **813.5** | **654.9** | **690.5** | **839.1** | **21.5** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **5,253.3** | **5,763.0** | **6,058.4** | **6,321.6** | **7,228.8** | **14.3** |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 310.4 | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 419.6 | -0.5 |
| ***Jumla Kuu (Bidhaa Zote) - f.o.b** | **6,371.7** | **6,756.2** | **7,223.8** | **7,696.6** | **9,121.6** | **18.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
*Inajumuisha biashara zisizo rekodiwa (unrecorded trade)

**Mapato ya Huduma**

105. Mwaka 2024, mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 6,899.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,231.7 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za utalii pamoja na huduma za usafirishaji. Aidha, mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yaliongezeka kwa asilimia 15.7 na kufikia dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,373.8 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuimarika kwa shughuli za utalii nchini ambapo idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia 18.5 na kufikia watalii 2,141,895 mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii 1,808,205 mwaka 2023. Vilevile, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yalikuwa dola za Marekani milioni 2,356.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,333.4 mwaka 2023. Kuendelea kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji kulichangiwa na kuimarika kwa huduma za bandari, viwanja vya ndege pamoja na usafirishaji wa abiria na mizigo kwenda nje ya nchi kupitia Shirika la Ndege Tanzania - ATCL. Mapato ya huduma yalichangia asilimia 43.1 ya thamani ya mauzo yote ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

**Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi**

106. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 4.0 na kufikia dola za Marekani milioni 14,278.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 13,728.9 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji.

**Bidhaa za Kukuza Mitaji**

107. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini ilikuwa dola za Marekani milioni 6,034.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,592.9 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama ya vyombo vya usafiri, majengo na ujenzi.

**Bidhaa za Kati**

108. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa za kati zilizoingizwa nchini ilikuwa dola za Marekani milioni 4,392.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,466.3 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 1.6. Hii ilitokana na kupungua kwa gharama ya uagizaji wa mafuta ya petroli na mbolea pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, thamani ya uagizaji mafuta ya petroli ilipungua kwa asilimia 4.4 na kufikia dola za Marekani milioni 2,837.2 ambayo ni sawa na asilimia 19.9 ya thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje.

**Bidhaa za Matumizi ya Kawaida**

109. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 3,849.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni

3,667.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za vyakula, hususan sukari za viwandani na vyakula vya kusindika.

**Malipo ya Huduma**

110. Mwaka 2024, malipo ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 2,608.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,395.9 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za huduma za usafirishaji, pamoja na kuongezeka kwa malipo ya huduma za usafiri nje ya nchi na huduma nyinginezo.

**Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje ya Nchi, Mwaka 2020 - 2024 (Dola za Marekani Milioni)**


| Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa za Kukuza Mitaji** | **3,138.8** | **3,836.0** | **5,167.5** | **5,592.9** | **6,034.3** | **7.9** |
| Vifaa vya Usafirishaji | 738.1 | 970.4 | 1,420.4 | 1,571.4 | 1,892.0 | 20.4 |
| Majengo na Ujenzi | 925.5 | 1,159.0 | 1,455.1 | 1,486.4 | 1,670.0 | 12.4 |
| Mitambo | 1,475.3 | 1,706.6 | 2,291.9 | 2,535.2 | 2,472.4 | -2.5 |
| **Bidhaa za Kati** | **2,229.8** | **3,250.5** | **5,102.1** | **4,466.3** | **4,392.7** | **-1.6** |
| Uagizaji Mafuta | 1,282.7 | 2,084.4 | 3,532.6 | 2,967.0 | 2,837.2 | -4.4 |
| Mbolea | 187.7 | 189.4 | 500.9 | 414.0 | 345.4 | -16.6 |
| Malighafi za Viwanda | 759.4 | 976.7 | 1,068.6 | 1,085.2 | 1,210.1 | 11.5 |
| **Bidhaa za Matumizi ya Kawaida** | **2,460.9** | **2,914.7** | **3,936.9** | **3,667.5** | **3,849.7** | **5.0** |
| Bidhaa za Vyakula | 420.4 | 500.9 | 735.5 | 885.5 | 958.3 | 8.2 |
| Bidhaa Nyingine | 2,040.5 | 2,413.8 | 3,201.4 | 2,782.0 | 2,891.4 | 3.9 |
| **Jumla (f.o.b)** | **7,831.7** | **10,003.4** | **14,208.7** | **13,728.9** | **14,278.9** | **4.0** |
| **Jumla (c.i.f)** | **8,468.4** | **10,849.9** | **15,654.5** | **15,117.5** | **15,684.5** | **3.8** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali**

111. Mwaka 2024, mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ikiwemo jumuiya za kikanda na kimataifa yaliendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa misukosuko katika uchumi wa dunia kufuatia vita inayoendelea nchini Ukraine na Mashariki ya Kati. Katika kipindi hicho, asilimia 26.3 ya mauzo yote ya bidhaa za Tanzania ziliuzwa katika nchi ya Afrika Kusini, ikifuatiwa na India (asilimia 18.8) pamoja na Umoja wa Falme za Kiarabu (asilimia 7.2). Aidha, mazao ya nafaka (mahindi na mchele) na mbogamboga yaliuzwa nchi ya Kenya na mbegu za mafuta, tumbaku, kahawa na korosho ziliuzwa katika nchi za China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu. Vilevile, asilimia 99.9 ya dhahabu yote iliyouzwa mwaka 2024 iliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, India, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uswisi, ambapo asilimia 65.1 ya dhahabu hiyo iliuzwa Afrika Kusini.

**Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania kwenda Nje ya Nchi Mwaka 2024 kwa Nchi Zilizochangia Zaidi ya Asilimia 3.0**




112. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ilikuwa dola za Marekani milioni 1,160.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,180.8 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 1.7. Hii ilichangiwa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Burundi na Sudani ya Kusini. Aidha, bidhaa zilizouzwa zaidi katika soko la EAC zilikuwa mchele, mahindi, chuma na mbolea.

113. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ilikuwa dola za Marekani milioni 2,968.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,727.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 71.8. Hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu kwenda nchi ya Afrika ya Kusini.

114. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika soko la Bara la Ulaya ilikuwa dola za Marekani milioni 989.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,126.3 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 12.1. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo kwenda Uswisi, hususani mauzo ya dhahabu.

115. Mwaka 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 3,638.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,370.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya korosho nchini India na nchi nyinginezo.

**Jedwali Na. 4.3: Thamani ya Mauzo ya Bidhaa katika Nchi Mbalimbali, Mwaka 2020 - 2024 (Dola za Marekani Milioni)**


| JUMUIYA/ NCHI | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 1,475.9 | 874.0 | 936.4 | 1,100.4 | 962.7 | -12.5 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 27.1 | 32.3 | 26.6 | 25.9 | 26.9 | 3.9 |
| **JUMLA- BARA LA ULAYA** | **1,502.9** | **906.3** | **963.0** | **1,126.3** | **989.6** | **-12.1** |
| **AFRIKA** | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 1161.6 | 916.7 | 929.6 | 1123.5 | 2292.7 | 104.1 |
| Zambia | 54.1 | 68.6 | 80.0 | 98.6 | 162.6 | 64.9 |
| Swaziland | 0.1 | 0.1 | 0.3 | 0.4 | 0.1 | -65.9 |
| Zimbabwe | 21.1 | 14.8 | 15.5 | 38.9 | 34.6 | -10.9 |
| Msumbiji | 21.0 | 15.5 | 35.2 | 17.7 | 37.0 | 109.1 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 144.2 | 207.2 | 280.5 | 312.8 | 313.3 | 0.2 |
| Nchi nyingine za SADC | 51.4 | 80.4 | 100.7 | 135.7 | 127.9 | -5.7 |
| **JUMLA-SADC** | **1,458.3** | **1,303.4** | **1,441.8** | **1,727.5** | **2,968.3** | **71.8** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | |
| Burundi | 177.7 | 163.3 | 212.8 | 172.3 | 61.5 | -64.3 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 144.2 | 207.2 | 280.5 | 312.8 | 313.3 | 0.2 |
| Kenya | 230.2 | 397.2 | 381.7 | 176.5 | 320.9 | 81.8 |
| Rwanda | 205.3 | 277.8 | 262.5 | 188.2 | 163.8 | -13.0 |
| Uganda | 191.2 | 314.0 | 264.2 | 311.7 | 291.0 | -6.6 |
| Sudani ya Kusini | 3.4 | 8.9 | 13.1 | 19.2 | 10.1 | -47.7 |
| JUMLA-EAC | 952.0 | 1,368.5 | 1,414.9 | 1,180.8 | 1,160.5 | -1.7 |
| Nchi nyingine za Afrika | 30.5 | 49.5 | 67.6 | 71.1 | 130.6 | 83.7 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **2,296.6** | **2,514.2** | **2,643.7** | **2,666.6** | **3,946.1** | **48.0** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | |
| Marekani | 47.0 | 39.1 | 74.6 | 97.8 | 101.5 | 3.7 |
| Canada | 3.2 | 3.7 | 6.1 | 4.1 | 13.8 | 232.6 |
| Nchi nyingine za bara la Amerika | 2.7 | 1.8 | 2.7 | 4.4 | 6.0 | 35.4 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **52.8** | **44.5** | **83.4** | **106.4** | **121.2** | **14.0** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | |
| China | 238.9 | 273.1 | 293.7 | 427.9 | 443.0 | 3.5 |
| India | 528.7 | 1,008.7 | 1,178.6 | 1,554.0 | 1,637.0 | 5.3 |
| Japani | 55.8 | 67.5 | 89.0 | 67.9 | 99.8 | 46.9 |
| Umoja wa falme za kiarabu | 754.9 | 1,051.8 | 763.0 | 686.4 | 625.2 | -8.9 |
| Honkong | 128.3 | 61.3 | 177.0 | 45.9 | 42.5 | -7.5 |
| Singapuri | 43.7 | 139.2 | 183.0 | 142.0 | 15.9 | -88.8 |
| Nchi nyingine za Asia | 453.8 | 319.6 | 445.2 | 446.3 | 775.0 | 73.7 |
| **JUMLA-ASIA** | **2,204.1** | **2,921.2** | **3,129.4** | **3,370.5** | **3,638.3** | **7.9** |
| Nchi nyinginezo | 4.9 | 4.7 | 5.2 | 5.2 | 6.8 | 29.0 |
| **JUMLA KUU** | **6,061.3** | **6,390.9** | **6,824.8** | **7,274.9** | **8,702.0** | **19.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
*Haijumuishi biashara zisizo rekodiwa (unrecorded trade)

116. Mwaka 2024, Tanzania iliagiza kwa wingi bidhaa kutoka nchi za China (asilimia 30.5), India (asilimia 13.6), Umoja wa Falme za Kiarabu (asilimia 10.6), Japani (asilimia 3.8), Afrika Kusini (asilimia 3.4) na Marekani (asilimia 2.9). Aidha, bidhaa zilizoagizwa

kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni pamoja na: mitambo, matrekta na bidhaa za kielektroniki kutoka China; mafuta ya petroli na mbolea kutoka Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu; na magari na chuma kutoka Japan, India na Afrika Kusini.

**Kielelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Uagizaji wa Bidhaa Nchini Mwaka 2024 kwa Nchi Zenye Mchango wa Zaidi ya Asilimia 2**




117. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka EAC ilikuwa dola za Marekani milioni 527.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 523.6 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, bidhaa zilizoagizwa kutoka SADC zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 786.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 786.1 mwaka 2023. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi za EAC ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 633.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 657.2 mwaka 2023. Vilevile, urari wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi za SADC ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,182.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 941.4 mwaka 2023.

118. Mwaka 2024, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 11,301.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 10,987.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mtaji pamoja na bidhaa za kati hususan mafuta. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya na Uswisi iliongezeka kwa asilimia 19.7 na kufikia dola za Marekani milioni 1,526.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,275.7 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji na bidhaa za kati kutoka katika Jumuiya hiyo.

**Jedwali Na. 4.4: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani, Mwaka 2020 - 2024 (Dola za Marekani Milioni)**

| JUMUIYA/ NCHI | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 1,147.3 | 1,001.9 | 1,659.1 | 1,275.5 | 1,526.7 | 19.7 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 347.6 | 368.3 | 326.3 | 623.9 | 498.1 | -20.2 |
| **JUMLA - BARA LA ULAYA** | **1,494.9** | **1,370.2** | **1,985.4** | **1,899.4** | **2,024.8** | **6.6** |
| **AFRIKA** | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 344.7 | 432.1 | 548.9 | 555.5 | 531.4 | -4.3 |
| Zambia | 49.4 | 70.5 | 91.0 | 113.1 | 149.9 | 32.6 |
| Swaziland | 26.4 | 39.6 | 43.7 | 37.8 | 42.9 | 13.7 |
| Zimbabwe | 4.7 | 9.9 | 8.1 | 9.8 | 13.0 | 33.1 |
| Msumbiji | 2.3 | 4.6 | 22.6 | 3.4 | 3.7 | 9.5 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 2.1 | 2.6 | 3.1 | 2.9 | 6.8 | 132.4 |
| Nchi nyingine za SADC | 38.6 | 57.4 | 61.8 | 63.7 | 38.6 | -39.3 |
| **JUMLA-SADC** | **468.2** | **616.6** | **779.2** | **786.1** | **786.4** | **0.0** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | |
| Burundi | 0.3 | 0.6 | 2.6 | 3.1 | 1.0 | -67.5 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 2.1 | 2.6 | 3.1 | 2.9 | 6.8 | 132.4 |
| Kenya | 253.5 | 413.0 | 426.6 | 408.9 | 400.4 | -2.1 |
| Rwanda | 2.1 | 2.2 | 3.1 | 1.4 | 3.2 | 133.9 |
| Uganda | 77.4 | 109.6 | 142.6 | 107.3 | 115.8 | 7.9 |
| Sudani ya Kusini | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 422.1 |
| **JUMLA-EAC** | **335.3** | **528.0** | **578.0** | **523.6** | **527.3** | **0.7** |
| Nchi nyingine za Afrika | 62.8 | 70.0 | 251.4 | 204.2 | 111.0 | -45.6 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **864.2** | **1,212.1** | **1,605.6** | **1,511.0** | **1,417.9** | **-6.2** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | |
| Marekani | 239.8 | 260.4 | 335.1 | 378.3 | 456.2 | 20.6 |
| Canada | 30.9 | 45.4 | 56.9 | 81.8 | 71.5 | -12.6 |
| Nchi nyingine za bara la Amerika | 60.6 | 79.2 | 176.1 | 113.9 | 332.4 | 191.8 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **331.2** | **385.0** | **568.2** | **574.0** | **860.1** | **49.8** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | |
| China | 2,116.8 | 2,700.0 | 3,946.3 | 4,158.7 | 4,780.1 | 14.9 |
| India | 1,091.2 | 1,209.1 | 1,960.6 | 1,949.0 | 2,130.6 | 9.3 |
| Japani | 345.6 | 465.5 | 521.6 | 649.5 | 593.2 | -8.7 |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 821.2 | 1,378.6 | 2,492.3 | 1,417.9 | 1,663.7 | 17.3 |
| Honkong | 47.8 | 53.1 | 83.9 | 77.7 | 68.3 | -12.2 |
| Singapuri | 31.6 | 82.2 | 107.9 | 156.5 | 58.5 | -62.7 |
| Nchi nyingine za Asia | 1,275.6 | 1,901.9 | 2,203.3 | 2,578.1 | 2,006.6 | -22.2 |
| **JUMLA-ASIA** | **5,729.8** | **7,790.4** | **11,315.9** | **10,987.4** | **11,301.0** | **2.9** |
| Nchi nyinginezo | 48.2 | 92.1 | 179.4 | 145.7 | 80.8 | -44.5 |
| **JUMLA KUU (c.i.f)** | **8,468.4** | **10,849.9** | **15,654.5** | **15,117.5** | **15,684.5** | **3.8** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Mizania ya Malipo na Nchi za Nje**

**Urari wa Malipo Yote**

119. Mwaka 2024, urari wa malipo yote ya nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 80.5 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 41.9 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa ziada ya urari wa mapato yatokanayo na huduma.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

120. Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 5,157.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 6,032.3 mwaka 2023. Kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa mwaka 2024 kulitokana na ongezeko kubwa la mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

121. Mwaka 2024, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 4,290.5 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 3,835.9 mwaka 2023, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 11.9. Hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutokana na kuimarika kwa sekta hiyo pamoja na kuongezeka kwa mapato ya huduma za usafirishaji.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

122. Urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 866.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,196.5 mwaka 2023. Ufanisi huo wa kupungua kwa nakisi ulitokana na kuimarika kwa urari wa biashara ya huduma.

**Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi**

123. Urari wa mapato ya vitega uchumi ambao unajumuisha kiasi cha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,742 mwaka 2024 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,496.6 mwaka 2023, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 16.4. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa malipo ya riba ya mikopo na uwekezaji wa moja kwa moja.

**Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida**

124. Mwaka 2024, urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 576.7 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 732.5 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 21.3.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

125. Mwaka 2024, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,032 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,960.6 mwaka 2023.

Upungufu wa nakisi ulitokana na kuongezeka kwa mapato ya huduma, mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi na kupungua kwa gharama za uagizaji wa bidhaa.

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

126. Urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 318.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 223.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 42.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa misaada kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Urari wa Rasilimali Fedha**

127. Mwaka 2024, urari wa malipo katika rasilimali fedha unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,383.1 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 3,629.9 mwaka 2023. Kupungua kwa ziada kulitokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa nje ya nchi (hususan benki za biashara).

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

128. Hadi Desemba 2024, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,546.9 kutoka dola za Marekani milioni 5,440.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kiasi hicho kilitosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4, ambayo ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0.

**Jedwali Na. 31: THAMANI YA BIASHARA YA BIDHAA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE**

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Bidhaa | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 10,064,249 | 11,378,808 | 13,882,712 | 14,384,874 | 15,637,519 | 17,299,166 | 22,679,088 |
| Bidhaa Halisi | 8,307,170 | 10,824,002 | 13,673,643 | 14,178,681 | 15,337,701 | 16,979,274 | 22,052,229 |
| Zilizouzwa Tena | 422,733 | 554,806 | 209,069 | 206,192 | 299,818 | 319,891 | 626,859 |
| Zilizoagizwa | 18,789,124 | 20,939,079 | 19,631,818 | 24,862,261 | 36,239,349 | 36,294,408 | 37,111,751 |
| Urari | -8,724,875 | -9,560,271 | -5,749,106 | -10,477,387 | -20,601,830 | -18,995,242 | -14,432,663 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali Na. 32: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE

| Kiasi (000'Tani) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Kahawa | 78.1 | 64.0 | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 82.2 | -2.6 |
| Pamba | 82.3 | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 52.6 | -24.5 |
| Katani | 13.8 | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | 21.2 | 69.4 |
| Chai | 31.7 | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 15.7 | -29.0 |
| Tumbaku | 46.3 | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 108.5 | 32.2 |
| Korosho | 296.8 | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | 428.3 | 95.0 |
| Karafuu | 1.8 | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | 2.8 | -39.4 |
| Almasi (Carat) | 590,000.0 | 154,331.1 | 47,430.0 | 306,319.9 | 201,923.0 | 369,311.2 | 82.9 |
| Dhahabu( gms) | 66,078,000 | 66,871,114.9 | 59,392,496.2 | 64,091,782.5 | 79,706,632.9 | 56,357,186.9 | -29.3 |
| 1 Carat = 200 milligrams | | | | | | | |
| **Thamani (Shilingi Milioni)** | | | | | | | |
| **Bidhaa** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Kahawa | 349,423 | 331,453 | 354,768 | 369,434 | 542,637 | 759,504 | 40.0 |
| Pamba | 212,310 | 199,823 | 185,917 | 237,123 | 245,860 | 180,338 | -26.7 |
| Katani | 53,829 | 40,071 | 46,126 | 55,781 | 48,071 | 60,747 | 26.4 |
| Chai | 104,044 | 73,987 | 75,173 | 68,778 | 73,261 | 50,066 | -31.7 |
| Tumbaku | 389,502 | 339,428 | 291,367 | 409,480 | 824,917 | 1,328,985 | 61.1 |
| Korosho | 821,945 | 824,634 | 363,012 | 520,400 | 507,084 | 1,401,112 | 176.3 |
| Karafuu | 20,807.4 | 38,915.6 | 118,412.6 | 96,607.8 | 60,967.4 | 43,408.1 | -28.8 |
| Almasi (Carat) | 184,967 | 46,080 | 19,443 | 143,782 | 57,050 | 138,593 | 142.9 |
| Dhahabu( gms) | 5,043,077 | 6,752,407 | 6,257,279 | 6,499,100 | 7,270,054 | 8,851,091 | 21.7 |


**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali Na. 33: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI


| | Kiasi (000" Tani) | | | | | Badiliko (Asilimia) | Thamani (Dola za Marekani Milioni) | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2023/24** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2023/24** |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 64 | 68 | 55.2 | 84.4 | 82.2 | -2.6 | 145.2 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 292.9 | 28.5 |
| Pamba | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 52.6 | -24.4 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | 69.3 | -32.0 |
| Katani | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | 21.2 | 69.6 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | 23.4 | 14.5 |
| Chai | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 15.7 | -29.1 | 32.4 | 32.9 | 30.0 | 31.1 | 19.4 | -37.5 |
| Tumbaku | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 108.5 | 32.3 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.5 | 509.5 | 49.6 |
| Korosho | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | 428.3 | 95.0 | 359.6 | 159.0 | 226.9 | 206.4 | 541.7 | 162.4 |
| Karafuu | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | 2.8 | -39.6 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | 17.1 | -32.0 |
| **Jumla** | | | | | | | **808.1** | **627.9** | **766.5** | **953.3** | **1,473.3** | **54.5** |
| **Bidhaa zisizo asilia** | | | | | | | | | | | | |
| Madini | | | | | | | 3,375.0 | 3,116.4 | 3,395.3 | 3,551.4 | 4,119.9 | 16.0 |
| Bidhaa za Viwanda | | | | | | | 902.7 | 1,200.00 | 1,419.20 | 1,363.34 | 1,341.3 | -1.6 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164 | 180.6 | 10.1 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 507.1 | 21.5 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 240.8 | 78.1 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 839.1 | 21.5 |
| **Jumla** | | | | | | | **5,253.30** | **5,763.00** | **6,058.40** | **6,321.60** | **7,228.8** | **14.4** |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | 310.4 | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 419.6 | -0.5 |
| **Jumla Kuu** | | | | | | | **6,371.70** | **6,756.20** | **7,223.80** | **7,696.60** | **9,121.6** | **18.5** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.5: THAMANI YA BIDHAA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI MWAKA 2017 - 2023**



**Kielelezo Na. 4.6: MCHANGO WA BIDHAA KATIKA MAUZO NJE YA NCHI MWAKA 2024**



**Jedwali Na. 34: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

| Bidhaa | (Shilingi/Tani*) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
| kahawa | 5,818,259 | 4,585,610 | 5,178,939 | 5,217,177 | 6,692,686 | 6,429,800 | 9,243,000 | 43.8 |
| Pamba | 3,099,625 | 2,690,875 | 2,753,527 | 3,806,866 | 4,846,836 | 3,530,423 | 3,428,467 | -2.9 |
| Katani | 3,910,417 | 3,901,618 | 3,575,866 | 3,657,568 | 3,734,604 | 3,841,269 | 2,865,989 | -25.4 |
| Chai | 3,841,673 | 3,292,541 | 3,070,579 | 3,101,340 | 3,254,080 | 3,302,729 | 3,180,280 | -3.7 |
| Tumbaku | 8,444,280 | 9,143,243 | 7,975,654 | 7,727,540 | 8,312,638 | 10,053,861 | 12,248,961 | 21.8 |
| Korosho | 3,733,995 | 2,759,651 | 2,570,147 | 2,351,759 | 2,224,266 | 2,309,110 | 3,271,367 | 41.7 |
| Karafuu | 6,840,000 | 16,005,679 | 10,868,651 | 16,801,625 | 16,293,998 | 12,996,777 | 15,278,639 | 17.6 |
| Almasi (Shilingi/ carat) | 205,594 | 313,503 | 298,578 | 409,930 | 469,384 | 282,534 | 369,311 | 30.7 |
| Dhahabu (Shilingi/gramu) | 56,522 | 62,185 | 100,976 | 105,355 | 101,403 | 91,210 | 157,053 | 72.2 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania
*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

**Jedwali Na. 35: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI**

USD/Tani*

| Bidhaa | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 3,019.2 | 2,633.0 | 1,996.5 | 2,268.9 | 2,284.4 | 2,919.6 | 2,700.8 | 3,564.3 | 32.0 |
| Pamba | 1,450.3 | 1,461.1 | 1,162.2 | 1,206.4 | 1,665.0 | 2,113.2 | 1,463.4 | 1,318.0 | -9.9 |
| Katani | 1,686.7 | 1,535.6 | 1,581.7 | 1,566.2 | 1,600.0 | 1,629.1 | 1,628.9 | 1,102.3 | -32.3 |
| Chai | 1,783.6 | 1,727.4 | 1,444.2 | 1,345.5 | 1,356.5 | 1,420.3 | 1,403.6 | 1,234.9 | -12.0 |
| Tumbaku | 4,055.6 | 3,648.6 | 3,440.9 | 3,494.2 | 3,381.5 | 3,624.1 | 4,150.8 | 4,695.9 | 13.1 |
| Korosho | 1,607.5 | 1,580.6 | 1,194.6 | 1,120.6 | 1,030.3 | 970.0 | 939.9 | 1,264.7 | 34.6 |
| Karafuu | 7,865.1 | 4,384.6 | 5,047.8 | 4,770.0 | 7,347.6 | 7,104.0 | 5,356.9 | 6,011.1 | 12.2 |
| Almasi (kwa carat) | 227.5 | 200.1 | 137.8 | 131.0 | 179.6 | 204.7 | 116.7 | 143.9 | 23.3 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 28.1 | 25.1 | 27.3 | 44.0 | 46.0 | 44.2 | 38.4 | 60.7 | 58.1 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania
*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu


## Jedwali Na. 36: MIZANIA YA MALIPO MWAKA 2018 - 2024

**Dola za Marekani Milioni**

| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024p |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa** | **-4,227.0** | **-3,237.6** | **-1,460.0** | **-3,247.1** | **-6,984.9** | **-6,032.3** | **-5,157.2** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 4,292.7 | 5,377.6 | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 8,519.7 | 8,615.2 | 7,831.7 | 10,003.4 | 14,208.7 | 13,728.9 | 14,278.9 |
| **Urari wa Huduma** | **2,088.9** | **2,492.5** | **864.7** | **1,510.7** | **2,296.6** | **3,835.9** | **4,290.5** |
| Mapato | 4014.7 | 4281.0 | 2183.8 | 3117.7 | 4762.0 | 6231.7 | 6899.4 |
| Malipo | 1925.7 | 1788.4 | 1319.0 | 1607.0 | 2465.4 | 2395.9 | 2608.9 |
| **Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi** | **-639.2** | **-1,013.7** | **-1,264.5** | **-1,191.6** | **-1,393.2** | **-1,496.6** | **-1,742.0** |
| Yaliyoingia | 155.9 | 212.4 | 111.2 | 102.5 | 183.9 | 301.2 | 356.4 |
| Yaliyotoka | 795.2 | 1226.2 | 1375.7 | 1294.2 | 1577.1 | 1797.7 | 2098.4 |
| **Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida** | **468.5** | **418.5** | **401.2** | **553.7** | **599.3** | **732.5** | **576.7** |
| Iliyoingia | 535.8 | 474.9 | 453.9 | 640.1 | 716.5 | 1280.9 | 1177.4 |
| Serikalini | 170.3 | 103.5 | 141.2 | 104.7 | 76.4 | 131.0 | 139.2 |
| Sekta nyingine | 365.5 | 371.4 | 312.7 | 535.4 | 640.2 | 1150.0 | 1038.3 |
| Iliyotoka | 67.3 | 56.4 | 52.7 | 86.4 | 117.2 | 548.4 | 600.7 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-2,308.7** | **-1,340.2** | **-1,458.5** | **-2,374.3** | **-5,482.2** | **-2,960.6** | **-2,032.0** |
| **Urari wa Uhamisho wa Mitaji** | **464.1** | **481.2** | **344.3** | **412.1** | **274.0** | **223.4** | **318.7** |
| Iliyoingia | 464.1 | 481.2 | 344.3 | 412.1 | 274.0 | 223.4 | 318.7 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **Urari katika uwekezaji** | **1,616.7** | **2,518.8** | **910.0** | **4,037.1** | **3,634.7** | **3,629.9** | **1,383.1** |
| Uwekezaji katika miradi | -971.6 | 1217.2 | 943.8 | 1190.5 | 1437.6 | 1648.9 | 1717.6 |
| Uwekezaji katika hisa | -8.2 | 37.8 | -3.6 | -7.9 | 24.6 | 13.9 | -26.1 |
| Uwekezaji aina nyingine | 653.3 | 1263.7 | -30.1 | 2854.5 | 2172.5 | 1967.1 | -308.4 |
| Makosa na Masahihisho | -556.1 | -1072.7 | -560.7 | -222.8 | 585.0 | -850.8 | 410.8 |
| **Urari wa Malipo yote** | **-784.0** | **587.0** | **-764.9** | **1852.1** | **-988.4** | **41.9** | **80.5** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.7: MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE MWAKA 2018 - 2024**



## SURA YA 5

## HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

### HALI YA UCHUMI WA DUNIA

**Ukuaji wa Uchumi**

129. Kulingana na taarifa ya mwenendo wa uchumi wa dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF toleo la Aprili 2025, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo: athari za utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea; migogoro ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati; gharama kubwa za mikopo katika masoko ya fedha zilizoathiri zaidi nchi zinazoendelea; na athari za mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na changamoto hizo, uchumi wa dunia uliendelea kuwa himilivu mwaka 2024 kufuatia kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia pamoja na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi nyingi kama ilivyotarajiwa.

130. Mwaka 2024, kasi ya ukuaji wa Pato la nchi zilizoendelea iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 1.8 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2023. Kuongezeka kwa ukuaji kulichangiwa zaidi na kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia na hivyo kuwezesha kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi hizo. Aidha, uchumi wa Marekani uliimarika zaidi kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya ndani ambapo matumizi binafsi yalikua kwa asilimia 2.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.4 kwa miaka 2000 - 2019. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi ilishuka na kufikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2023. Vilevile, kasi ya ukuaji wa Pato la nchi za Asia zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi ikijumuisha China na India ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.1 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuendelea kuwepo kwa athari za kushuka kwa shughuli za upangishaji majengo nchini China kufuatia athari za UVIKO-19 tangu mwaka 2021 uliosababisha kupungua kwa imani ya walaji kwenye sekta hiyo na hivyo kupunguza mahitaji ya ndani

131. Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.6 mwaka 2023. Kuongezeka kwa ukuaji kulichangiwa na kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia, kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kufuatia ongezeko la uwekezaji katika sekta ya umma, kuimarika kwa mauzo ya bidhaa nje na utekelezaji mzuri wa sera za kupunguza mfumuko wa bei.

**Jedwali Na. 5.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia, Mwaka 2020 - 2024**

| **Kundi/Mwaka** | **Ukuaji Halisi (Asilimia)** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
| Dunia | -2.7 | 6.6 | 3.6 | 3.5 | 3.3 |
| Nchi Zilizoendelea | -4.0 | 6.0 | 2.9 | 1.7 | 1.8 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | -1.7 | 7.0 | 4.1 | 4.7 | 4.3 |
| Nchi za Asia Zinazoibukia na Zinazoendelea | -0.5 | 7.8 | 4.7 | 6.1 | 5.3 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | -1.5 | 4.7 | 4.1 | 3.6 | 4.0 |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF-WEO), Aprili 2025

132. Mwaka 2024, ukuaji wa Pato la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulifikia wastani wa asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2023. Aidha, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ulishuka na kufikia wastani wa asilimia 1.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwaka 2023. Kupungua kwa ukuaji wa uchumi katika nchi za SADC na EAC kulichangiwa na migogoro ya kisiasa inayoendelea katika baadhi ya nchi ikiwemo DRC na Sudani; na mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri sekta ya kilimo na miundombinu.

**Jedwali Na. 5.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za SADC na EAC, Mwaka 2020 - 2024**

| **Nchi/Mwaka** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ukuaji wa Nchi za SADC** | | | | | |
| Angola | -4.0 | 2.1 | 4.2 | 1.0 | 4.5 |
| Botswana | -8.7 | 11.9 | 5.5 | 3.2 | -3.0 |
| Comoros | -0.2 | 2.0 | 2.6 | 3.0 | 3.3 |
| Tanzania | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |
| DRC | 1.7 | 1.7 | 9.2 | 8.5 | 6.5 |
| Eswatin | -1.6 | 10.7 | 0.5 | 5.0 | 3.7 |
| Lesotho | -5.3 | 1.9 | 2.0 | 2.0 | 2.6 |
| Madagascar | -7.1 | 4.7 | 4.2 | 4.2 | 4.2 |
| Malawi | 1.0 | 4.6 | 0.9 | 1.9 | 1.8 |
| Mauritius | -14.5 | 3.4 | 8.7 | 5.0 | 4.7 |
| Msumbiji | -1.2 | 2.4 | 4.4 | 5.4 | 1.9 |
| Namibia | -8.1 | 3.6 | 5.4 | 4.4 | 3.7 |
| Seychelles | -11.7 | 0.6 | 12.7 | 2.3 | 3.0 |
| Afrika Kusini | -6.2 | 5.0 | 1.9 | 0.7 | 0.6 |
| Zambia | -2.8 | 6.2 | 5.2 | 5.4 | 4.0 |
| Zimbabwe | -7.8 | 8.5 | 6.1 | 5.3 | 2.0 |
| **Wastani** | **-4.5** | **4.6** | **4.9** | **3.9** | **3.1** |
| **Ukuaji wa Nchi za EAC** | | | | | |
| Burundi | 0.3 | 3.1 | 1.8 | 2.7 | 3.5 |
| Kenya | -0.3 | 7.6 | 4.9 | 5.6 | 4.5 |
| Rwanda | -3.4 | 10.9 | 8.2 | 8.3 | 8.9 |
| Somalia | -2.8 | 3.5 | 2.7 | 4.2 | 4.0 |
| Sudan Kusini | -6.5 | 5.3 | -5.2 | 2.5 | -27.6 |
| Tanzania | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |
| Uganda | -1.1 | 5.5 | 6.2 | 4.9 | 6.3 |
| DRC | 1.7 | 1.7 | 9.2 | 8.5 | 6.5 |
| **Wastani** | **-1.0** | **5.3** | **4.1** | **5.2** | **1.5** |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF-WEO), Aprili 2025

### Mwenendo wa Bei

133. Mwaka 2024, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2023. Kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma duniani kulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kupunguza ongezeko la ukwasi, kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta na mbolea, pamoja na kupungua kwa vikwazo katika mnyororo wa ugavi. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulifikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka

2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi za Ulaya zinazoibukia na zinazoendelea ulikuwa wa wastani wa asilimia 16.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.1 mwaka 2023. Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi za Asia zinazoibukia na zinazoendelea ulikuwa wa wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2023.

134. Mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa wastani wa asilimia 18.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.6 mwaka 2023. Ongezeko la mfumuko wa bei lilichangiwa na athari za kushuka kwa thamani ya fedha pamoja na kushuka kwa uzalishaji katika shughuli za kilimo kwa baadhi ya nchi. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 54.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 50.3 mwaka 2023. Hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mfumuko wa bei kwa nchi za Zimbabwe, Malawi na Angola. Vilevile, mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa wastani wa asilimia 23.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 15.5 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 5.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za SADC na EAC, Mwaka 2019 - 2023**

| **Nchi** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mfumuko wa Bei wa Nchi za SADC (Asilimia)** | | | | | |
| Angola | 22.3 | 25.8 | 21.4 | 13.6 | 28.2 |
| Botswana | 1.9 | 6.7 | 12.2 | 5.1 | 2.8 |
| Comoros | 0.8 | 0.0 | 12.4 | 8.5 | 5.0 |
| Tanzania | 3.3 | 3.7 | 4.4 | 3.8 | 3.1* |
| DRC | 11.4 | 9.0 | 9.3 | 19.9 | 17.7 |
| Eswatin | 3.9 | 3.7 | 4.8 | 4.9 | 4.0 |
| Lesotho | 5.0 | 6.0 | 8.3 | 6.3 | 6.1 |
| Madagascar | 4.2 | 5.8 | 8.2 | 9.9 | 7.6 |
| Malawi | 8.6 | 9.3 | 20.8 | 28.8 | 32.2 |
| Mauritius | 2.5 | 4.0 | 10.8 | 7.0 | 3.6 |
| Msumbiji | 0.9 | 6.6 | 10.4 | 7.0 | 3.2 |
| Namibia | 2.2 | 3.6 | 6.1 | 5.9 | 4.2 |
| Seychelles | 1.0 | 10.0 | 2.6 | -0.9 | 0.2 |
| Afrika Kusini | 3.3 | 4.6 | 6.9 | 5.9 | 4.4 |
| Zambia | 15.7 | 22.0 | 11.0 | 10.9 | 15.0 |
| Zimbabwe | 557.2 | 98.5 | 193.4 | 667.4 | 736.1 |
| **Wastani** | **40.3** | **13.7** | **21.4** | **50.3** | **54.6** |
| **Mfumuko wa Bei wa Nchi za EAC (Asilimia)** | | | | | |
| Tanzania | 3.3 | 3.7 | 4.4 | 3.8 | 3.1* |
| Uganda | 2.8 | 2.2 | 7.2 | 5.4 | 3.3 |
| Kenya | 5.3 | 6.1 | 7.6 | 7.7 | 4.5 |
| Rwanda | 7.7 | 0.8 | 13.9 | 14.0 | 4.8 |
| Burundi | 7.5 | 8.4 | 18.9 | 27.1 | 20.2 |
| Sudani ya Kusini | 24.0 | 30.2 | -3.2 | 39.7 | 128.4 |
| Somalia | 4.1 | 4.6 | 6.8 | 6.2 | 5.5 |
| DRC | 11.4 | 9.0 | 9.3 | 19.9 | 17.7 |
| **Wastani** | **8.3** | **8.1** | **9.7** | **15.5** | **23.4** |

**Chanzo**: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2025
*Makadirio ya IMF yalikuwa asilimia 3.2 lakini takwimu rasmi kutoka NBS ni asilimia 3.1

**Mwenendo wa Biashara Duniani**

135. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Biashara Duniani ya Shirika la Biashara Duniani - WTO toleo la Aprili 2025, ukuaji wa shughuli za biashara ya bidhaa duniani uliongezeka na kufikia asilimia 2.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.0 mwaka 2023. Hii ilitokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa za viwandani, kupungua kwa mfumuko wa bei katika soko la dunia na baadhi ya nchi zilizoendelea kuanza kupunguza riba mwishoni mwa mwaka 2024 na hivyo kuchochea uwekezaji katika biashara.

136. Mwaka 2024, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Ulaya ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.9 mwaka 2023 na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Bara la Ulaya ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 5.0 mwaka 2023. Ukuaji hasi wa uagizaji na uuzaji wa bidhaa katika Bara la Ulaya ulichangiwa na kushuka wa biashara ndani ya bara la Ulaya (intra EU-trade). Aidha, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Asia ulikua kwa asilimia 8.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.2 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uuzaji wa bidhaa kwenda bara la Ulaya kutoka China. Uagizaji wa bidhaa nje ya Bara hilo uliongezeka na kufikia ukuaji wa asilimia 4.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.7 mwaka 2023. Vilevile, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji wa asilimia 1.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.7 mwaka 2023 na uagizaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji wa asilimia 1.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.6 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 5.4: Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa Duniani, 2021 - 2024**

| **Kundi/Mwaka** | **Ukuaji Halisi (Asilimia)** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
| **Dunia** | 9.6 | 3.0 | -1.0 | 2.9 |
| **Uuzaji wa bidhaa nje** | | | | |
| Bara la Ulaya | 8.1 | 3.7 | -2.9 | -1.7 |
| Bara la Asia | 13.1 | 0.4 | 0.2 | 8.0 |
| Afrika | 4.2 | -2.4 | 5.7 | 1.3 |
| **Uagizaji wa bidhaa kutoka nje** | | | | |
| Bara la Ulaya | 8.8 | 6.0 | -5.0 | -2.2 |
| Bara la Asia | 10.5 | -0.7 | -0.7 | 4.4 |
| Bara la Afrika | 7.4 | 8.8 | 2.6 | 1.8 |

**Chanzo:** Shirika la Biashara Duniani (WTO), Aprili 2025

## USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

### Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa

137. Mwaka 2024, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Kimataifa kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika uliofanyika Paris, Ufaransa. Mkutano huo ulilenga masuala mbalimbali ikiwemo: kulifanya suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia kuwa la kipaumbele katika ajenda ya kimataifa; kuainisha hatua madhubuti za kisera za kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kutoa fursa kwa washiriki kutoa ahadi za kifedha ili kufikia azma ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kupitia mkutano huo ahadi ya kiasi cha dola za Marekani bilioni 2.2 ilitolewa kwa ajili ya kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia barani Afrika. Fedha hizo ni sehemu ya kiasi cha dola za Marekani bilioni 4 zinazohitajika kila mwaka kuanzia mwaka 2024 hadi 2030 ili kufikia lengo la matumizi ya nishati safi ya kupikia.

138. Mwaka 2024, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani uliofanyika Davos, Uswisi. Mkutano huo ulitoa fursa kwa viongozi wa kitaifa, wataalamu wa Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia, wanataaluma na watafiti kujadili mada mbalimbali kuhusu changamoto za maendeleo pamoja na utatuzi wake. Tanzania ilishiriki katika majadiliano kuhusu namna ya kutengeneza fursa katika nchi za Afrika, hususan kwenye sekta ya kilimo ambapo iliainisha mikakati, mipango na miradi inayotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau kwa lengo la kuinua sekta hiyo na mchango wake katika ukuaji wa uchumi. Aidha, Serikali ya Tanzania na taasisi ya *Global Plastic Action Partnership (GPAP)* ya Uswisi zilikubaliana kutekeleza mradi wa kudhibiti taka za plastiki jijini Dodoma pamoja na kuanzisha mpango wa kupunguza uzalishaji wa taka zenye athari zaidi kwenye maeneo ya bahari.

139. Mwaka 2024, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote - NAM uliofanyika Kampala, Uganda. Katika Mkutano huo, nchi wanachama zilipitisha Azimio la Kampala linalojumuisha masuala mbalimbali kuhusu misimamo ya nchi za NAM ikiwemo kupinga aina zote za ukandamizaji unaofanywa na nchi moja dhidi ya nchi nyingine katika misingi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, Azimio hilo linahimiza kuendeleza ushirikiano miongoni mwa nchi zinazoendelea (*south-south cooperation*) na ushirikiano baina ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea (*north-south cooperation*). Vilevile, Azimio linahimiza kuendelea kudai mageuzi katika mifumo ya kimataifa ya kifedha (*international financing architecture*) na mifumo ya kibiashara (*world trading systems*) ili kupunguza pengo la kiuchumi na kuongeza mchango wa nchi zinazoendelea katika uchumi wa dunia na mnyororo wa uongezaji thamani.

140. Mwaka 2024, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Pili wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya Indonesia na Afrika (*Indonesia - Africa Forum II*) uliofanyika Jakarta, Indonesia. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano baina ya Indonesia na nchi za Afrika katika sekta za nishati, afya, madini na kilimo. Pembezoni mwa Mkutano huo (side meeting), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania - TMDA na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Indonesia - BPOM zilisaini hati ya makubaliano ya ushirikiano katika udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha, Tanzania na Indonesia zilibadilishana hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania - TPDC na Shirika la Petroli la Indonesia - *PT Petramina* iliyosainiwa mwaka 2023. Utekelezaji wa hati hiyo utaiwezesha TPDC kupata uzoefu kutoka Indonesia ambao ni wabobezi katika uchimbaji na utafutaji wa mafuta ya petroli na gesi asilia.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika**

141. Mwaka 2024, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika - AU uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia. Pamoja na masuala

mengine, Mkutano huo ulipitisha Mpango wa Pili wa Miaka wa Miaka 10 wa Utekelezaji wa Ajenda ya 2063 ya Maendeleo ya Afrika (2024 - 2033). Aidha, Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Ajenda ya 2063 ilionesha kuwa Tanzania ilifanya vizuri katika maeneo mengi ikiwemo elimu, afya, nishati ya umeme na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

142. Mwaka 2024, Tanzania iliendelea kushiriki katika majadiliano kuhusu itifaki na makubaliano mengine ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika - AfCFTA kwa lengo la kuongeza wigo wa ushirikiano wa kibiashara na nchi nyingine za Afrika. Katika kipindi hicho, Jamhuri ya Liberia iliridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa AfCFTA na hivyo kufanya nchi wanachama wa AfCFTA kufikia 48 kati ya nchi wanachama 54 wa AU. Aidha, Itifaki ya Wanawake na Vijana katika Biashara Barani Afrika chini ya mkataba wa AfCFTA ilipitishwa katika Mkutano wa 37 wa AU. Itifaki hiyo inalenga kutatua changamoto zinazoyakabili makundi hayo na kuimarisha ushindani katika soko.

143. Mwaka 2024, nchi wanachama wa AfCFTA ziliridhia Itifaki ya Biashara ya Kidigitali inayolenga kurahisisha uwianishaji wa mifumo na sera za biashara ya kidigitali, kupunguza gharama ya ufanyaji biashara ndani ya Afrika na kuchochea ukuaji wa biashara na uwekezaji biashara baina ya nchi wanachama. Katika jitihada za kupunguza gharama za ufanyaji biashara, nchi wanachama wa AfCFTA zilianza kutumia mfumo wa malipo unaojulikana kama *Pan-African Payments and Settlement System (PAPSS)*.

**Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

144. Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 44 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC uliofanyika Agosti 2024 jijini Harare, Jamhuri ya Zimbabwe. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulimteua Mheshimiwa Dkt. Emmerson Dambudzo Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe kuwa Mwenyekiti Mpya wa SADC. Aidha, Mkutano huo ulimteua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC. Katika hatua nyingine, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika jijini Harare, Jamhuri ya Zimbabwe Novemba 2024. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulipokea na kujadili taarifa ya hali ya amani na usalama katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo iliyoonesha kuzorota kwa hali ya kibinadamu na usalama katika nchi hiyo. Wakuu wa Nchi za SADC walitoa msimamo wa kuendelea kuisaidia Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika kutatua mgogoro uliopo. Aidha, Mkutano huo ulitoa maelekezo ya kuongeza mwaka mmoja kwa Misheni ya Ulinzi wa Amani ya SADC - SAMIDRC kukabiliana na vitendo vinavyovuruga utulivu mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kurejesha amani, utulivu na usalama katika eneo hilo.

145. Mwaka 2024, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Mawaziri wa Afya kutathmini hali ya afya kikanda katika masuala yanayohusu milipuko ya magonjwa ya dharura, kifua kikuu, malaria, lishe, VVU na UKIMWI uliofanyika jijini Luanda, Jamhuri ya Angola. Mkutano huo uliidhinisha Ripoti ya Malaria ya SADC ya mwaka 2023 kwa kuhimiza Nchi Wanachama kuimarisha afua za kukabiliana na ugonjwa wa malaria, hususan udhibiti jumuishi wa mbu, kuimarisha ufuatiliaji wa kitaifa wa ugonjwa wa malaria na wadudu waenezao malaria pamoja na Nchi Wanachama kushirikiana katika ubadilishanaji wa taarifa za malaria. Vilevile, Mkutano huo ulihimiza Nchi Wanachama kuweka kipaumbele cha kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za ndani kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kukidhi mahitaji ya udhibiti yatakayowezesha kutokomeza ugonjwa wa malaria.

146. Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji na Jopo la Tathmini ya Uchumi Jumla uliofanyika kwa njia ya mtandao Agosti 2024. Katika Mkutano huo pamoja na mambo mengine, mawaziri walijadili hatua zilizofikiwa na nchi wanachama katika kutekeleza Mfumo wa Utengamano wa Uchumi Jumla wa SADC pamoja na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Jopo la Tathmini ya Uchumi Jumla. Aidha, Mkutano huo ulipokea na kujadili Taarifa za Tathmini za Kiuchumi za Nchi za Botswana, Namibia na Tanzania na kushauri kufanyika kwa maboresho ya kimuundo na sera kwa nchi zilizofanyiwa Tathmini. Tathmini ya kiuchumi ya nchi ya Botswana ilifanywa na Angola wakati Zambia iliifanyia tathmini nchi ya Namibia na tathmini ya nchi ya Tanzania ilifanywa na Zimbabwe.

147. Kwa ujumla tathmini hiyo ilionesha kuwa kwa mwaka 2024 katika nchi 15 wanachama wa SADC, nchi mbili tu (Eswatini na Lesotho) ziliweza kufikia vigezo vyote vitatu vya msingi, na hakuna nchi iliyoweza kufikia vigezo vyote vya upili. Kwa upande wa Tanzania iliweza kufikia vigezo viwili kati ya vitatu vya msingi ambavyo ni kuwa ndani ya lengo la SADC la mfumuko wa bei wa kati ya asilimia 3-7 ambapo Tanzania ilikuwa na mfumuko wa bei wa asilimia 3.1 mwaka 2024 na kigezo cha pili ni ukomo wa uwiano wa deni la Taifa kwa Pato la Taifa usiozidi asilimia 60 ambapo Tanzania ilifikia uwiano wa deni kwa Pato la Taifa wa asilimia 49.7 mwaka 2024. Kigezo ambacho Tanzania ilishindwa kukifikia ni kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ambapo Tanzania ilivuka kigezo hiki kidogo kwa kuwa na nakisi ya asilimia 3.1 mwaka 2023/24.

**Jedwali Na. 5.5: Mwenendo wa Viashiria vya Msingi kwa Nchi Wanachama wa SADC**[1]

| Nchi | 2023 | | | 2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mfumuko wa Bei (3-7%) | Nakisi ya bajeti (3% ya Pato la Taifa) | Deni la Serikali (60% ya Pato la Taifa) | Mfumuko wa Bei (3-7%) | Nakisi ya bajeti (3% ya Pato la Taifa) | Deni la Serikali (60% ya Pato la Taifa) |
| Angola | 13.6 | -2.8 | 89.4 | 28.2 | -1.2 | 70.4 |
| Botswana | 5.2 | -4.2 | 22.7 | 2.8 | -9.0 | 33.3 |
| DRC | 19.8 | -5.3 | 13.3 | 17.9 | -2.7 | 16.0 |
| Eswatini | 5.0 | -0.1 | 39.2 | 4.0 | -2.1 | 40.7 |
| Lesotho | 6.4 | 7.1 | 55.6 | 6.1 | 10.6 | 53.5 |
| Madagascar | 9.9 | -4.2 | 37.2 | 7.6 | -4.3 | 37.4 |
| Malawi | 28.7 | -8.3 | 84.8 | 32.3 | -10.2 | 86.4 |
| Mauritius | 7.0 | -4.9 | 74.1 | 3.6 | -5.7 | 73.3 |
| Msumbiji | 7.1 | -2.0 | 72.6 | 3.2 | -7.7 | 74.2 |
| Namibia | 5.9 | -2.4 | 65.1 | 4.2 | -3.9 | 66.0 |
| Seychelles | -1.0 | 1.7 | 58.2 | 0.3 | 3.4 | 61.5 |
| Afrika ya Kusini | 6.0 | -4.6 | 70.5 | 3.2 | -5.0 | 76.2 |
| Tanzania | 3.8 | -4.2 | 48.9 | 3.1 | -3.1 | 49.7 |
| Zambia | 10.9 | -6.9 | 104.8 | 15.0 | -3.6 | 96.4 |
| Zimbabwe* | 29.4 | -6.4 | 96.6 | 8.3 | 0.6 | 60.6 |
| **Wastani** | **10.5** | **-3.2** | **62.2** | **9.3** | **-2.9** | **59.7** |

**Chanzo:** Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

*Ukokotoaji wa Mfumoko wa bei umefanyika kwa kutumia sarafu ya nchi husika

**Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

148. Mwaka 2024, Tanzania iliendelea kushiriki katika utekelezaji wa hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa ushiriki wa nchi unakuwa na manufaa kwa mujibu wa malengo ya kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi za EAC uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo

[1] Nchi ya Comoro haijajumuishwa katika tathmini kwa kuwa siyo mwanachama rasmi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

uliridhia marekebisho ya Ibara ya 132(4) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa mfumo mpya wa uchangiaji wa bajeti ya EAC. Mfumo huo unalenga kupunguza changamoto ya baadhi ya nchi wanachama kutolipa michango kwa wakati.

149. Mwaka 2024, nchi za EAC ziliendelea kushirikiana katika kuimarisha sekta ya kilimo ambapo orodha ya visumbufu vya mazao ya ndizi, mihogo, viazi na mtama iliandaliwa ambayo ni kundi la kwanza katika mazao ya ziada ya kipaumbele. Orodha hiyo itasaidia nchi wanachama kuongeza juhudi za kudhibiti visumbufu hivyo kwa pamoja na kupunguza vikwazo vya kibiashara vinavyotokana na hatua za kudhibiti magonjwa na usalama wa mazao (phytosanitary measures) katika Jumuiya.

150. Mwaka 2024, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilipitisha Kanuni za Afrika Mashariki za Kusimamia Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (EAC Special Economic Zone Regulations). Kanuni hizo zitawezesha bidhaa zinazozalishwa katika maeneo hayo kwa kutumia malighafi za ndani na kukidhi matakwa ya kanuni za Jumuiya za uasili wa bidhaa kuingizwa sokoni bila kutozwa ushuru. Aidha, bidhaa zitakazozalishwa katika maeneo maalumu ya kiuchumi kwa kutumia malighafi kutoka nje na kukidhi matakwa ya kanuni za Jumuiya za uasili wa bidhaa, zitaruhusiwa kuuzwa katika soko la Jumuiya baada ya kukamilisha taratibu zote za kikodi. Kupitishwa kwa kanuni hizo kunatoa fursa kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuongeza uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa nchini, hususan bidhaa ambazo zimekuwa zikiagizwa kwa wingi nje ya nchi.

# SURA YA 6

## RASILIMALI WATU

**Idadi ya Watu**

151. Mwaka 2024, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 66,278,276 ikilinganishwa na watu 63,670,531 mwaka 2023. Aidha, Tanzania Bara ilikuwa na watu 64,241,822, sawa na asilimia 96.9 ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 2,036,454, sawa na asilimia 3.1. Aidha, wanawake walikadiriwa kuwa 33,799,398, sawa na asilimia 51 ya watu wote na wanaume walikuwa 32,478,878 (asilimia 49). Makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2024 ni maoteo ya mwenendo wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

**Mgawanyiko wa Watu Kimkoa**

152. Mwaka 2024, mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wapatao 5,739,734, sawa na asilimia 8.9 ya watu wote Tanzania Bara ikifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 3,992,565 (asilimia 6.2). Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilichangiwa na upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi zilizowavutia watu kuhamia kutoka mikoa mingine na urahisi wa upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii. Hata hivyo, mkoa wa Njombe ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 939,503, sawa na asilimia 1.5 ya watu wote Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wapatao 962,135, sawa na asilimia 47.2 ya watu wote Tanzania Zanzibar. Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 209,534, sawa na asilimia 10.3 ya watu wote Tanzania Zanzibar.

153. Mwaka 2024, msongamano wa watu Tanzania ulikuwa wastani wa watu 75 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 72 mwaka 2023. Msongamano wa watu Tanzania Bara ulikuwa wastani wa watu 73 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 70 mwaka 2023. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 4,120 kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokuwa na wastani wa watu 422 kwa kila kilometa ya mraba. Aidha, mkoa wa Lindi uliendelea kuwa na msongamano mdogo zaidi wa wastani wa watu 19 kwa kila kilometa ya mraba ukifuatiwa na mkoa wa Katavi uliokuwa na wastani wa watu 27 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, msongamano wa watu ulikuwa wastani wa watu 828 kwa kila kilometa ya mraba mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa watu 793 mwaka 2023. Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 4,183 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na mkoa wa Kusini Pemba uliokuwa na wastani wa watu 884 kwa kila kilometa ya mraba. Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo zaidi wa wastani wa watu 245 kwa kila kilometa ya mraba.

154. Mwaka 2024, wastani wa idadi ya watu kwa kaya kwa Tanzania na Tanzania Bara ulibaki kuwa watu 4.3 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Mkoa wa Simiyu uliongoza kwa kuwa na wastani wa watu 6.7 kwa kaya na mkoa wa Mtwara ulikuwa na wastani mdogo zaidi wa watu 3.3 kwa kaya. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, wastani wa idadi ya watu kwa kaya ulikuwa watu 5.0 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Mkoa wa Kusini Pemba uliongoza kwa kuwa na wastani mkubwa wa idadi ya watu kwa kaya wa watu 5.7 na mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani mdogo zaidi wa watu 4.2 kwa kaya kama ilivyokuwa mwaka 2023.

**Jedwali 6.1: Mgawanyo wa Idadi ya Watu Kimkoa Mwaka 2024**

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Uwiano Kijinsia | Msongamano wa Watu | Idadi ya Kaya | Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Wanaume | Wanawake | | | | |
| **Tanzania** | **66,278,276** | **32,478,878** | **33,799,398** | **96** | **75** | **15,327,734** | **4.3** |
| **Tanzania Bara** | **64,241,822** | **31,485,439** | **32,756,383** | **96** | **73** | **14,918,125** | **4.3** |
| Dodoma | 3,300,186 | 1,626,561 | 1,673,625 | 97 | 80 | 810,517 | 4.1 |
| Arusha | 2,524,141 | 1,217,221 | 1,306,920 | 93 | 67 | 659,014 | 3.8 |
| Kilimanjaro | 1,976,588 | 967,935 | 1,008,653 | 96 | 149 | 528,507 | 3.7 |
| Tanga | 2,790,841 | 1,370,451 | 1,420,390 | 96 | 105 | 678,093 | 4.1 |
| Morogoro | 3,405,761 | 1,690,175 | 1,715,586 | 99 | 48 | 884,050 | 3.9 |
| Pwani | 2,144,928 | 1,063,719 | 1,081,209 | 98 | 66 | 575,088 | 3.7 |
| Dar es Salaam | 5,739,734 | 2,784,936 | 2,954,798 | 94 | 4120 | 1,652,566 | 3.5 |
| Lindi | 1,262,641 | 617,465 | 645,176 | 96 | 19 | 367,188 | 3.4 |
| Mtwara | 1,738,231 | 829,810 | 908,421 | 91 | 104 | 524,244 | 3.3 |
| Ruvuma | 1,982,240 | 972,141 | 1,010,099 | 96 | 31 | 500,518 | 4.0 |
| Iringa | 1,260,104 | 611,090 | 649,014 | 94 | 35 | 340,072 | 3.7 |
| Mbeya | 2,495,901 | 1,207,485 | 1,288,416 | 94 | 66 | 671,006 | 3.7 |
| Singida | 2,166,130 | 1,080,503 | 1,085,627 | 100 | 44 | 427,016 | 5.1 |
| Tabora | 3,657,677 | 1,804,150 | 1,853,527 | 97 | 48 | 645,610 | 5.7 |
| Rukwa | 1,680,335 | 817,901 | 862,434 | 95 | 74 | 359,976 | 4.7 |
| Kigoma | 2,669,703 | 1,296,670 | 1,373,033 | 94 | 72 | 517,643 | 5.2 |
| Shinyanga | 2,410,306 | 1,193,201 | 1,217,105 | 98 | 128 | 455,298 | 5.3 |
| Kagera | 3,226,032 | 1,584,665 | 1,641,367 | 97 | 128 | 758,038 | 4.3 |
| Mwanza | 3,992,565 | 1,958,571 | 2,033,994 | 96 | 422 | 811,092 | 4.9 |
| Mara | 2,565,172 | 1,243,346 | 1,321,826 | 94 | 118 | 509,228 | 5.0 |
| Manyara | 2,035,641 | 1,032,000 | 1,003,641 | 103 | 46 | 433,984 | 4.7 |
| Njombe | 939,503 | 446,784 | 492,719 | 91 | 44 | 260,230 | 3.6 |
| Katavi | 1,253,158 | 622,697 | 630,461 | 99 | 27 | 234,751 | 5.3 |
| Simiyu | 2,338,396 | 1,142,345 | 1,196,051 | 96 | 93 | 347,360 | 6.7 |
| Geita | 3,241,053 | 1,604,982 | 1,636,071 | 98 | 162 | 611,660 | 5.3 |
| Songwe | 1,444,855 | 698,635 | 746,220 | 94 | 64 | 355,376 | 4.1 |
| **Tanzania Zanzibar** | **2,036,454** | **993,439** | **1,043,015** | **95** | **828** | **409,609** | **5.0** |
| Kaskazini Unguja | 275,531 | 135,990 | 139,541 | 97 | 586 | 58,696 | 4.7 |
| Kusini Unguja | 209,534 | 105,510 | 104,024 | 101 | 245 | 50,289 | 4.2 |
| Mjini Magharibi | 962,135 | 464,313 | 497,822 | 93 | 4183 | 196,138 | 4.9 |
| Kaskazini Pemba | 295,724 | 144,299 | 151,425 | 95 | 515 | 52,794 | 5.6 |
| Kusini Pemba | 293,530 | 143,327 | 150,203 | 95 | 884 | 51,692 | 5.7 |

**Mgawanyo wa Watu kwa Umri**


155. Mwaka 2024, watoto wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa 10,331,575, sawa na asilimia 16.1 ya watu wote Tanzania Bara. Idadi ya watu wenye umri wa miaka 5 hadi 14 walikuwa 17,528,354, sawa na asilimia 27.3. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 35 ilikuwa 21,880,166, sawa na asilimia 34.1 ya watu wote. Idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ambayo ndiyo nguvukazi ilikuwa 34,046,617, sawa na asilimia 53.0. Vilevile, idadi ya watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi ilikuwa 2,335,276, sawa na asilimia 3.6. Watu wenye umri tegemezi ambao ni umri chini ya miaka 15 na umri wa miaka 65 na zaidi walikuwa 30,195,205, sawa na asilimia 47.0 ya watu wote.

**Jedwali Na. 6.2: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsi Mwaka 2024**


| Umri | Wanawake | Wanaume | Jumla | Uwiano (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 0-4 | 5,122,670 | 5,208,905 | 10,331,576 | 16.1 |
| 5-014 | 8,699,718 | 8,828,636 | 17,528,355 | 27.3 |
| 15-35 | 11,391,698 | 10,488,468 | 21,880,165 | 34.1 |
| 35-64 | 6,273,259 | 5,893,192 | 12,166,451 | 18.9 |
| 65+ | 1,276,005 | 1,059,271 | 2,335,275 | 3.6 |
| **Jumla** | **32,763,350** | **31,478,472** | **64,241,822** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 6.1: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri Mwaka 2024**



**Kielelezo 6.2: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsi Mwaka 2024**




**Nguvu Kazi na Ajira**

156. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi kwa Vijana kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira. Katika kipindi hicho, vijana 10,699 walipata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ikilinganishwa na vijana 10,220 waliopata mafunzo mwaka 2023. Kati ya hao: vijana 6,300 walipata mafunzo ya uanagenzi; vijana 3,085 walipata mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi; na vijana 1,314 wanaofanya biashara au kujihusisha katika sekta ndogo ya utalii na ukarimu walipata mafunzo ya kukuza ujuzi.

157. Mwaka 2024, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania - TaESA ilisajili watafutakazi 18,916 kupitia Mfumo wa Kidijitali wa Huduma za Ajira ikilinganishwa na watafutakazi 17,107 waliosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.6. Kati ya hao, wanawake walikuwa 9,536 (asilimia 50.4) na wanaume 9,380. Katika kipindi hicho, watafutakazi 11,542 (wanaume 6,033 na wanawake 5,509) walipata mafunzo ya kushindania fursa za ajira ikilinganishwa na watafutakazi 10,847 waliopata mafunzo mwaka 2023. Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha watafutakazi kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kukuza maadili ya kazi.

158. Mwaka 2024, vijana 1,253 (wanaume 718 na wanawake 535) waliunganishwa na fursa za ajira ikilinganishwa na vijana 311 waliounganishwa na fursa za ajira mwaka 2023. Katika kipindi hicho, wahitimu 3,085 (wanaume 1,835 na wanawake 1,250) wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo waliunganishwa na waajiri kwa ajili ya kufanya mafunzo ya uzoefu wa kazi ikilinganishwa na wahitimu 2,895 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Aidha, watanzania 3,591 (wanaume 660 na wanawake 2,931) waliunganishwa

na fursa za ajira nje ya nchi mwaka 2024, ikilinganishwa na watanzania 2,529 waliofaidika na fursa hizo mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 42.0.

159. Utafiti wa Ajira na Mapato katika sekta rasmi wa mwaka 2022/23 ulionesha kuwa ajira katika sekta rasmi zilifikia 3,635,755 kutoka ajira 3,450,053 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 5.4. Kati ya hizo, ajira 1,095,726 zilikuwa za sekta ya umma, sawa na asilimia 30.1 na ajira 2,540,029 (asilimia 69.9) zilikuwa za sekta binafsi. Matokeo ya Utafiti huo yalibainisha kuwa ajira za masharti ya muda mrefu zilifikia 3,313,909 mwaka 2022/23 kutoka ajira 3,002,620 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Kwa upande mwingine, ajira za muda mfupi zilipungua kwa asilimia 28.1 hadi ajira 321,846 mwaka 2022/23 kutoka ajira 447,433 mwaka 2019/20.

**Jedwali Na: 6.2 Mchanganuo wa Ajira Rasmi**

| Aina za Ajira | 2019/20 | | | | 2022/23 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umma | Binafsi | Jumla | Mchango (Asilimia) | Umma | Binafsi | Jumla | Mchango (Asilimia) |
| Ajira za Masharti ya Muda Mrefu | 896,793 | 2,105,827 | 3,002,620 | 87.0 | 1,082,917 | 2,230,992 | 3,313,909 | 91.1 |
| Ajira za Muda Mfupi | 25,035 | 422,397 | 447,433 | 13.0 | 12,810 | 309,036 | 321,846 | 8.9 |
| **Jumla** | **921,828** | **2,528,224** | **3,450,053** | **100.0** | **1,095,726** | **2,540,029** | **3,635,755** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

160. Matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa wanawake walioajiriwa walikuwa asilimia 38.3 na wanaume asilimia 61.7. Aidha, asilimia 67.1 ya vijana wenye umri wa miaka 15-35 waliajiriwa kwa masharti ya muda mrefu mwaka 2022/23 ikilinganishwa na asilimia 45.9 walioajiriwa mwaka 2019/20. Aidha, kiwango cha ajira za muda mrefu kwa watu wenye umri wa miaka 36 na zaidi kilikuwa asilimia 32.9 mwaka 2022/23 ikilinganishwa asilimia 54.1 mwaka 2019/20. Mchango wa sekta binafsi ulikuwa asilimia 67.3 ya ajira za kudumu na sekta ya umma asilimia 32.7. Vilevile, sekta ya umma ilichangia asilimia 4.0 ya ajira za muda mfupi ikilinganishwa na sekta binafsi asilimia 96.0.

161. Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti huo, idadi ya waajiriwa wenye ulemavu ilikuwa 14,699, sawa na asilimia 0.4 ya waajiriwa katika sekta rasmi. Kati ya hao, wanawake walikuwa 6,304 (asilimia 42.9) na wanaume 8,395 (asilimia 57.1). Sekta ya umma ilikuwa na waajiriwa wengi wenye ulemavu (asilimia 51.6) ikilinganishwa na sekta binafsi (asilimia 48.4).

162. Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuchangia asilimia 33.2 ya waajiriwa wote mwaka 2022/23 ikilinganishwa na asilimia 29.6 mwaka 2019/20. Mikoa ya Songwe na Katavi iliajiri watu wachache zaidi ambapo kila mkoa ulitoa ajira kwa kiwango kisichozidi

asilimia moja ya waajiriwa wote. Aidha, sekta ya uzalishaji viwandani ilikuwa na mchango mkubwa kwenye ajira wa asilimia 15.0 ikifuatiwa na sekta ya elimu iliyochangia asilimia 14.7 na utawala asilimia 12.5. Shughuli za upangishaji majengo zilikuwa na mchango mdogo zaidi wa ajira wa asilimia 0.2 ya ajira zote.

**Jedwali Na. 6.3: Mchanganuo wa Ajira Kisekta (Asilimia)**

| Sekta | Binafsi | | Umma | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2022/23 | 2019/20 | 2022/23 | 2019/20 | 2022/23 |
| Kilimo, misitu na uvuvi | 10.6 | 5.3 | 2.3 | 2.8 | 8.4 | 4.6 |
| Uchimbaji madini na mawe | 2 | 2.7 | 0.3 | 0.6 | 1.6 | 2.1 |
| Uzalishaji viwandani | 23.5 | 21.2 | 0.3 | 0.5 | 17.3 | 15.0 |
| Umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) | 0.7 | 0.5 | 2.7 | 1.7 | 1.2 | 0.9 |
| Usambazaji maji, majitaka, udhibiti wa taka na shughuli za kutibu maji | 0.3 | 0.2 | 1.3 | 1.3 | 0.6 | 0.5 |
| Ujenzi | 4.1 | 3.4 | 0.3 | 1.1 | 3.1 | 2.7 |
| Biashara na Matengenezo | 10.9 | 14 | 0.1 | 3.1 | 8.0 | 10.7 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 3 | 2.9 | 1.7 | 1.3 | 2.7 | 2.4 |
| Malazi na huduma ya chakula | 10.6 | 11.1 | 0.2 | 0.1 | 7.8 | 7.8 |
| Habari na Mawasilinao | 2.3 | 2.4 | 0.9 | 0.7 | 1.9 | 1.9 |
| Fedha na Bima | 2.1 | 2.6 | 1.2 | 1.3 | 1.8 | 2.2 |
| Upangishaji Majengo | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.2 |
| Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 1.2 | 1.1 | 1.8 | 2.3 | 1.3 | 1.4 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 4.7 | 6.3 | 1.0 | 2.7 | 3.7 | 5.2 |
| Utawala na Ulinzi | 0.9 | 0.6 | 43.2 | 40.0 | 12.2 | 12.5 |
| Elimu | 9.6 | 7.8 | 32.7 | 30.6 | 15.8 | 14.7 |
| Afya na Huduma za Jamii | 5.6 | 5.1 | 8.5 | 9 | 6.4 | 6.3 |
| Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.6 | 0.3 | 0.1 | 0.3 | 0.4 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 7.4 | 11.9 | 0.8 | 0.8 | 5.6 | 8.5 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 6.4: Mchanganuo wa Ajira Kimkoa (Asilimia)**

| Mkoa | Binafsi | | Umma | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2022/23 | 2019/20 | 2022/23 | 2019/20 | 2022/23 |
| Dodoma | 1.3 | 1.7 | 1.7 | 1.7 | 3.0 | 3.3 |
| Arusha | 4.8 | 4.4 | 0.9 | 0.8 | 5.6 | 5.2 |
| Kilimanjaro | 3.4 | 3.0 | 0.7 | 1.1 | 4.0 | 4.1 |
| Tanga | 4.6 | 2.8 | 1.6 | 1.6 | 6.2 | 4.4 |
| Morogoro | 6.4 | 5.4 | 2.7 | 2.6 | 9.1 | 8.0 |
| Pwani | 1.2 | 1.3 | 1.0 | 1.1 | 2.3 | 2.4 |
| Dar es Salaam | 27.2 | 30.6 | 2.4 | 2.6 | 29.6 | 33.2 |
| Lindi | 0.4 | 0.3 | 1.1 | 1.1 | 1.5 | 1.5 |
| Mtwara | 0.8 | 0.9 | 0.6 | 0.6 | 1.4 | 1.6 |
| Ruvuma | 1.3 | 1.1 | 0.7 | 0.7 | 2.0 | 1.8 |
| Iringa | 1.8 | 1.2 | 0.7 | 0.9 | 2.5 | 2.1 |
| Mbeya | 3.7 | 3.2 | 1.5 | 1.5 | 5.2 | 4.7 |
| Singida | 1.1 | 0.9 | 0.9 | 1.0 | 2.0 | 1.8 |
| Tabora | 0.7 | 0.7 | 0.7 | 0.9 | 2.0 | 1.5 |
| Rukwa | 0.8 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 1.4 | 1.2 |
| Kigoma | 1.2 | 1.0 | 0.8 | 0.9 | 2.0 | 1.9 |
| Shinyanga | 1.9 | 1.2 | 1.1 | 1.6 | 3.0 | 2.8 |
| Kagera | 1.7 | 1.1 | 0.9 | 1.4 | 2.6 | 2.4 |
| Mwanza | 4.0 | 3.1 | 1.4 | 1.4 | 5.4 | 4.5 |
| Mara | 1.2 | 1.2 | 1.3 | 1.3 | 2.4 | 2.4 |
| Manyara | 1.1 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 1.9 | 1.5 |
| Njombe | 0.9 | 0.5 | 0.5 | 0.8 | 1.4 | 1.3 |
| Katavi | 0.2 | 0.2 | 0.3 | 0.4 | 0.5 | 0.6 |
| Simiyu | 0.4 | 0.5 | 0.7 | 0.6 | 1.1 | 1.1 |
| Geita | 06.09 | 0.6 | 0.6 | 0.8 | 1.5 | 1.4 |
| Songwe | 0.6 | 0.3 | 0.2 | 0.5 | 0.9 | 0.8 |
| **Jumla** | **2,528,224** | **2,540,029** | **921,828** | **1,095,726** | **3,450,053** | **3,635,755** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

163. Matokeo ya Utafiti huo yalionesha kuwa ajira mpya zilikuwa 70,558 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na ajira 40,471 mwaka 2019/20. Kati ya hizo, ajira kwa wanawake zilikuwa 26,969 na wanaume 43,689. Kwa majibu wa Utafiti, sekta ya umma ilichangia ajira mpya 30,029 na sekta binafsi ajira 40,530. Kati ya ajira mpya zilizotolewa, kada za wahudumu na wafanyakazi wa madukani ilitoa ajira 34,189 ikifuatiwa na wanasheria, watawala, mameneja na wanataaluma ambao kwa pamoja walitoa ajira 34,053.

## Jedwali Na. 37: IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA MWAKA 2017 - 2024

| Mkoa | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 2,419,941 | 2,492,989 | 2,568,514 | 2,647,410 | 2,729,668 | 3,085,625 | 3,177,174 | 3,300,186 |
| Arusha | 1,948,219 | 1,999,907 | 2,051,852 | 2,104,074 | 2,156,511 | 2,356,255 | 2,419,445 | 2,524,141 |
| Kilimanjaro | 1,823,151 | 1,864,329 | 1,906,978 | 1,951,252 | 1,996,952 | 1,861,934 | 1,936,220 | 1,976,588 |
| Tanga | 2,284,712 | 2,337,053 | 2,391,791 | 2,449,235 | 2,509,439 | 2,615,597 | 2,697,944 | 2,790,841 |
| Morogoro | 2,531,268 | 2,596,287 | 2,662,468 | 2,730,058 | 2,799,260 | 3,197,104 | 3,298,632 | 3,405,761 |
| Pwani | 1,236,481 | 1,265,504 | 1,295,267 | 1,325,852 | 1,357,271 | 2,024,947 | 2,076,480 | 2,144,928 |
| Dar es Salaam | 5,017,294 | 5,147,070 | 5,275,315 | 5,401,814 | 5,526,638 | 5,383,728 | 5,604,582 | 5,739,734 |
| Lindi | 963,465 | 983,738 | 1,004,439 | 1,025,800 | 1,047,783 | 1,194,028 | 1,241,992 | 1,262,641 |
| Mtwara | 1,397,723 | 1,424,083 | 1,451,078 | 1,478,874 | 1,507,426 | 1,634,947 | 1,710,148 | 1,738,231 |
| Ruvuma | 1,543,869 | 1,579,811 | 1,616,991 | 1,655,443 | 1,695,057 | 1,848,794 | 1,927,924 | 1,982,240 |
| Iringa | 1,068,695 | 1,095,172 | 1,122,131 | 1,149,481 | 1,177,327 | 1,192,728 | 1,233,733 | 1,260,104 |
| Mbeya | 2,006,072 | 2,070,412 | 2,136,614 | 2,204,543 | 2,274,236 | 2,343,754 | 2,416,550 | 2,495,901 |
| Singida | 1,569,304 | 1,612,854 | 1,658,086 | 1,705,182 | 1,754,370 | 2,008,058 | 2,068,494 | 2,166,130 |
| Tabora | 2,769,093 | 2,870,522 | 2,974,427 | 3,081,263 | 3,191,194 | 3,391,679 | 3,468,780 | 3,657,677 |
| Rukwa | 1,160,568 | 1,195,550 | 1,231,959 | 1,270,049 | 1,310,007 | 1,540,519 | 1,579,858 | 1,680,335 |
| Kigoma | 2,528,708 | 2,616,200 | 2,706,831 | 2,800,919 | 2,898,568 | 2,470,967 | 2,533,738 | 2,669,703 |
| Shinyanga | 1,816,316 | 1,874,709 | 1,933,768 | 1,993,589 | 2,054,229 | 2,241,299 | 2,298,016 | 2,410,306 |
| Kagera | 2,919,942 | 3,022,037 | 3,127,908 | 3,238,347 | 3,353,241 | 2,989,299 | 3,093,648 | 3,226,032 |
| Mwanza | 3,393,620 | 3,532,378 | 3,676,300 | 3,826,573 | 3,983,793 | 3,699,872 | 3,809,881 | 3,992,565 |
| Mara | 2,123,683 | 2,209,143 | 2,298,317 | 2,391,845 | 2,490,155 | 2,372,015 | 2,444,607 | 2,565,172 |
| Manyara | 1,692,667 | 1,750,864 | 1,810,929 | 1,873,105 | 1,937,450 | 1,892,502 | 1,938,948 | 2,035,641 |
| Njombe | 786,347 | 803,299 | 820,355 | 837,557 | 854,932 | 889,946 | 925,816 | 939,503 |
| Katavi | 706,472 | 738,237 | 771,287 | 805,887 | 842,200 | 1,152,958 | 1,178,923 | 1,253,158 |
| Simiyu | 1,998,224 | 2,094,798 | 2,196,449 | 2,304,228 | 2,418,495 | 2,140,497 | 2,198,807 | 2,338,396 |
| Geita | 2,148,409 | 2,239,949 | 2,335,134 | 2,434,800 | 2,539,114 | 2,977,608 | 3,053,478 | 3,241,053 |
| Songwe | 1,166,094 | 1,202,419 | 1,239,970 | 1,278,850 | 1,319,064 | 1,344,687 | 1,384,882 | 1,444,855 |
| **Tanzania Bara** | **51,020,337** | **52,619,314** | **54,265,158** | **55,966,030** | **57,724,380** | **59,851,347** | **61,718,700** | **64,241,822** |
| Kaskazini Unguja | 216,697 | 222,066 | 227,317 | 232,480 | 237,505 | 257290 | 263,634 | 275,531 |
| Kusini Unguja | 131,162 | 133,767 | 136,235 | 138,589 | 140,821 | 195873 | 203,646 | 209,534 |
| Mjini Magharibi | 683,833 | 700,791 | 717,468 | 733,914 | 750,033 | 893169 | 927,681 | 962,135 |
| Kaskazini Pemba | 260,884 | 271,594 | 282,716 | 294,267 | 306,173 | 272091 | 278,042 | 295,724 |
| Kusini Pemba | 241,715 | 251,631 | 261,853 | 272,348 | 283,076 | 271350 | 278,828 | 293,530 |
| **Zanzibar** | **1,534,291** | **1,579,849** | **1,625,589** | **1,671,598** | **1,717,608** | **1,889,773** | **1,951,831** | **2,036,454** |
| **Tanzania** | **52,554,628** | **54,199,163** | **55,890,747** | **57,637,628** | **59,441,988** | **61,741,120** | **63,670,531** | **66,278,276** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu



Sehemu ya Pili

# MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

# SURA YA 7

# KILIMO NA USHIRIKA

## UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO

### Mazao ya Chakula

164. Mwaka 2024, uzalishaji wa mazao makuu ya chakula ulikuwa tani 22,803,316 ikilinganishwa na tani 20,402,014 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Kati ya hizo, tani 14,587,177 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 8,216,139 mazao yasiyo ya nafaka. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo mengi ya uzalishaji, kuimarika kwa huduma za ugani na upatikanaji wa vitendea kazi, matumizi ya teknolojia na pembejeo bora za kilimo na kuimarika kwa usimamizi wa mazao kabla na baada ya kuvuna. Aidha, mahitaji ya chakula yalikuwa tani 17,753,989 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 16,390,404 mwaka 2023. Kwa kuzingatia mahitaji na uzalishaji wa mazao ya chakula, nchi ilikuwa na ziada ya chakula tani 5,049,327. Hivyo, kulingana na mahitaji ya chakula, nchi ilikuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula wa asilimia 128.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 124.5 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 7.1: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Chakula, Mwaka 2020 - 2024 (Tani '000')**

| Zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mazao ya Nafaka** | | | | | | |
| Mahindi | 6,711 | 7,039 | 6,417 | 8,011 | 10,084 | 25.9 |
| Mchele | 3,038 | 2,687 | 1,708 | 2,332 | 3,046 | 30.6 |
| Ngano | 77 | 70 | 62 | 87 | 119 | 36.8 |
| Mtama/Uwele/ Ulezi | 1,043 | 1,077 | 1,046 | 1,019 | 1,339 | 31.4 |
| **Mazao yasiyo Nafaka** | | | | | | |
| Muhogo | 2,427 | 2,486 | 2,411 | 2,575 | 2,317 | -10.0 |
| Maharage/ Mikunde | 1,895 | 2,235 | 2,499 | 2,803 | 2,495 | -11.0 |
| Ndizi | 1,358 | 1,442 | 1,290 | 1,224 | 1,152 | -5.9 |
| Viazi (Vitamu na Mviringo) | 1,646 | 1,626 | 1,715 | 2,351 | 2,252 | -4.2 |
| **Jumla** | **18,195** | **18,665** | **17,148** | **20,402** | **22,803** | **11.8** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

### Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula

165. Mwaka 2024, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA ulikabidhiwa ghala 12 zilizojengwa kupitia Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania - TANIPAC. Ghala hizo ziliongeza uwezo wa kuhifadhi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na kufikia tani 360,000 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 341,000 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Kwa upande mwingine, Serikali ilikamilisha ujenzi wa ghala 28 zenye uwezo

wa kuhifadhi tani 1,000 za nafaka kila moja katika halmashauri nne (4) za Mkoa wa Ruvuma.

**Mazao ya Asilia ya Biashara**

166. Mwaka 2024, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ulikuwa tani 1,487,364 ikilinganishwa na tani 1,218,136[2] mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 22.1. Ongezeko hilo lilitokana na wakulima kuendelea kufuata kanuni bora za kilimo cha mazao ya biashara.

**Jedwali Na. 7.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Asilia ya Biashara, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 348,958 | 122,836 | 144,792 | 174,486 | 282,510 | 61.9 |
| Kahawa | 60,651 | 73,027 | 66,837 | 62,917 | 77,417 | 23.0 |
| Chai | 28,715 | 27,510 | 24,825 | 26,451 | 22,337 | -15.6 |
| Pareto | 2,510 | 2,412 | 2,694 | 3,815 | 2,866 | -24.9 |
| Tumbaku | 37,546 | 58,508 | 70,699 | 122,858 | 117,464 | -4.4 |
| Korosho | 232,681 | 210,786 | 240,158 | 310,787 | 528,262 | 70.0 |
| Mkonge | 36,379 | 36,170 | 44,151 | 56,773 | 61,216 | 7.8 |
| Sukari | 311,358 | 367,718 | 379,280 | 460,049 | 395,293 | -14.1 |
| **Jumla** | **1,058,798** | **898,967** | **973,436** | **1,218,136** | **1,487,364** | **22.1** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Mazao ya Bustani**

167. Mwaka 2024, uzalishaji wa mazao ya bustani unaojumuisha maua, matunda, viungo na mboga ulikuwa tani 7,513,501.7 ikilinganishwa na tani 8,438,273.98 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 11.0. Upungufu huo ulitokana na uwepo wa mvua nyingi na visumbufu vilivyosababisha upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna.

[2] Takwimu ya imebadilika kutokana na mapitio ya takwimu za mazao ya pamba, pareto, chai, korosho na mkonge

**Jedwali Na. 7.3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matunda | 5,582,117 | 5,199,312 | 5,407,284 | 6,530,302 | 6,212,065 | -4.9 |
| Mboga | 1,852,676 | 2,011,684 | 2,212,852 | 1,777,878 | 1,232,526 | -30.7 |
| Maua | 1,710 | 1,338 | 1,351 | 577 | 534 | -7.4 |
| Viungo | 123,507 | 92,389 | 101,628 | 129,517 | 68,377 | -47.2 |
| **Jumla** | **7,560,010** | **7,304,723** | **7,723,115** | **8,438,274** | **7,513,502** | **-11.0** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Mazao ya Mbegu za Mafuta**

168. Mwaka 2024, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta yanayojumuisha alizeti, karanga, ufuta, chikichi, soya na nazi ulikuwa tani 2,230,135.2 ikilinganishwa na tani 2,156,682.6 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Ongezeko hilo lilichangiwa na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa mpango wa ruzuku na hali nzuri ya hewa.

**Jedwali Na. 7.4: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 649,437 | 478,900 | 425,653 | 1,132,298 | 1,217,026 | 7.5 |
| Karanga | 631,465 | 895,219 | 936,799 | 586,216 | 620,603 | 5.9 |
| Ufuta | 228,920 | 236,162 | 79,170 | 266,994 | 240,010 | -10.1 |
| Chikichi | 42,387 | 58,791 | 60,790 | 62,125 | 51,834 | -16.6 |
| Soya | 31,460 | 44,106 | 5,152 | 13,584 | 48,532 | 257.3 |
| Nazi | 77,939 | 192,239 | 201,539 | 95,465 | 52,131 | -45.4 |
| **Jumla** | 1,661,608 | 1,905,417 | 1,709,103 | 2,156,683 | 2,230,135 | 3.4 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

169. Mwaka 2024, upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka kwa asilimia 22.5 na kufikia tani 72,031.89 ikilinganishwa na tani 58,807.61 mwaka 2023. Kati ya hizo, tani 56,114 zilizalishwa nchini ikilinganishwa na tani 42,096.68 zilizozalishwa nchini mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 33.3. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mbegu pamoja na upatikanaji wa ithibati ya *International Seed Testing Association* (ISTA) inayowezesha kampuni kuzalisha mbegu kwa wingi baada ya Serikali kujiunga na skimu za mbegu za Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo - OECD. Aidha, tani 15,917.43 za mbegu ziliingizwa kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na tani 16,710.93 zilizoingizwa kutoka nje mwaka 2023. Kwa mbegu zilizozalishwa nchini, tani 4,498.07 zilizalishwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo - ASA na tani 51,615.93 zilizalishwa na sekta binafsi. Aidha, ASA na sekta binafsi kwa pamoja

walizalisha na kusambaza kwa wakulima mbegu bora za alizeti tani 1,504.62, karanga tani 72.89, ufuta tani 23.48 na miche ya chikichi 111,123.

170. Mwaka 2023/24, upatikanaji wa mbolea uliongezeka kwa asilimia 17.2 na kufikia tani 1,213,780 kutoka tani 1,035,745 mwaka 2022/23. Aidha, uzalishaji wa ndani ulikuwa tani 158,628 ikilinganishwa na tani 84,696 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 87.3. Aidha, uagizaji wa mbolea ulikuwa tani 728,758 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na tani 824,085 mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 11.6. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani, hususan katika viwanda vya Itracom na Minjingu na uwepo wa bakaa ya mbolea ya mwaka 2022/23. Vilevile, matumizi ya mbolea nchini yaliongezeka kwa asilimia 44.8 na kufikia tani 840,714 mwaka 2023/24 kutoka tani 580,628 mwaka 2022/23. Ongezeko la matumizi ya mbolea lilitokana na Serikali kuendelea kutoa mbolea ya ruzuku.

**Jedwali Na. 7.5: Upatikanaji wa Mbolea Nchini, Mwaka 2019/20 - 2023/24 (Tani)**

| **Mwaka** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio ya Mahitaji | 586,604 | 718,051 | 698,260 | 667,730 | 848,884 | 27.1 |
| **Upatikanaji** | | | | | | |
| Bakaa | 168,397 | 219,206 | 117,900 | 126,964 | 326,344 | 157 |
| Uzalishaji Ndani ya Nchi | 33,873 | 42,695 | 62,724 | 84,696 | 158,678 | 87.4 |
| Kiasi kilichoingizwa Ndani ya Nchi | 524,972 | 504,122 | 407,994 | 824,085 | 728,758 | -11.6 |
| **Jumla ya Upatikanaji** | **727,242** | **766,023** | **588,618** | **1,035,745** | **1,213,780** | **17.2** |
| Kiasi kilichouzwa Nje ya Nchi | 145,367 | 171,254 | 98,055 | 128,774 | 112,612 | -12.6 |
| Matumizi ya Ndani ya Nchi | 457,855 | 476,870 | 363,599 | 580,628 | 840,714 | 44.8 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

171. Mwaka 2023/24, wastani wa bei ya mbolea ya kukuzia - UREA katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 391 kwa tani ikilinganishwa na dola za Marekani 688 kwa tani mwaka 2022/2023, sawa na upungufu wa asilimia 43.2. Aidha, wastani wa bei ya mbolea ya kupandia - DAP katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 590 kwa tani mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 800 kwa tani mwaka 2022/2023, sawa na upungufu wa asilimia 26.3. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa athari ya vita inayoendelea kati ya Ukraine na Urusi hali iliyopelekea kuimarika kwa mazingira ya uzalishaji wa mbolea kwa nchi zinazotegemea malighafi ya kutengeneza mbolea kutoka Urusi kuanza kuagiza malighafi hizo na pia kuimarika kwa uzalishaji wa mbolea kwa nchi za Urusi na Ukrane.

172. Mwaka 2024, mikopo 19 yenye thamani ya shilingi milioni 208.36 ilitolewa na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo - AGITF ikilinganishwa na mikopo 42 yenye thamani ya shilingi milioni 1,371.40 iliyotolewa mwaka 2023. Mikopo iliyotolewa ilijumuisha:

uendeshaji wa shamba (milioni 114.29); miundombinu ya umwagiliaji (milioni 61.08); na mashine za kuongeza thamani (milioni 33.0). Aidha, shilingi milioni 1,849.65 zilirejeshwa, sawa na asilimia 35.2 ya lengo la marejesho ya shilingi milioni 5,247.86 mwaka 2024 ikilinganishwa na marejesho ya shilingi milioni 1,625.30 (asilimia 22.9) ya lengo la shilingi milioni 7,082.43 mwaka 2023.

**Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao**

173. Mwaka 2024, bei ya mahindi ilipungua kwa asilimia 34.6 na kufikia wastani wa shilingi 68,800 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 105,200 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2023. Aidha, bei ya mchele ilipungua kwa asilimia 20.3 na kufikia wastani wa shilingi 219,600 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 275,440 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2023. Kupungua kwa bei ya mahindi na mchele kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo. Vilevile, bei ya maharage ilishuka kwa asilimia 5.7 na kufikia wastani wa shilingi 261,150 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 276,930 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 7.6: Wastani wa Bei za Jumla za Mazao Makuu ya Chakula, Mwaka 2020 - 2024 (Shilingi/Gunia la Kilogramu 100)**

| Zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 63,200 | 47,800 | 83,200 | 105,200 | 68,800 | -34.6 |
| Mchele | 159,500 | 142,800 | 216,800 | 275,440 | 219,600 | -20.3 |
| Mtama | 107,600 | 99,200 | 123,600 | 139,910 | 140,500 | 0.4 |
| Ulezi | 129,500 | 151,800 | 169,500 | 141,000 | 180,400 | 27.9 |
| Ngano | 123,400 | 124,900 | 182,100 | 191,930 | 194,900 | 1.5 |
| Maharage | 197,400 | 176,100 | 215,100 | 276,930 | 261,150 | -5.7 |
| Viazi mviringo | 75,600 | 68,000 | 82,000 | 97,710 | 99,300 | 1.6 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

174. Mwaka 2024, wastani wa bei ya kahawa aina ya robusta katika soko la ndani ulikuwa shilingi 5,060 kwa kilogramu ikilinganishwa na shilingi 2,965 kwa kilogramu mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 70.7. Aidha, wastani wa bei ya korosho uliongezeka kwa asilimia 85.3 na kufikia shilingi 3,188 kwa kilogramu mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,720 kwa kilogramu mwaka 2023. Kuimarika kwa bei ya korosho kulitokana na minada iliyofanyika kwa njia ya kidigitali kupitia Soko la Bidhaa Tanzania - TMX.

**Jedwali Na. 7.7: Wastani wa Bei za Jumla za Mazao ya Asili ya Biashara, Mwaka 2020 - 2024 (Shilingi/Gunia la Kilogramu 100)**

| Zao | Aina/ Daraja | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | Arabika | 4,500 | 6,500 | 8,428 | 5,978 | 7,500 | 25.5 |
| | Robusta | 1,300 | 1,400 | 2,646 | 2,965 | 5,060 | 70.7 |
| Pamba | Pamba mbegu | 900 | 1,400 | 1,800 | 1,150 | 1,350 | 17.4 |
| Korosho | *Standard grade* | 2,229 | 2,150 | 1,860 | 1,720 | 3,188 | 85.3 |
| | *Under grade* | 1,642 | 1,595 | 1,331 | 1,200 | 2,076 | 73.0 |
| Tumbaku* | Mvuke (VFC) | 1.55 | 1.79 | 1.79 | 2.34 | 2.3 | -1.7 |
| | Moshi (DFC) | 1.25 | 1.51 | 1.51 | 1.69 | 1.91 | 13.0 |
| Chai* | Majani mabichi | 314 | 314 | 366 | 366 | 366 | 0.0 |
| | Majani makavu | 1.49 | 1.62 | 1.55 | 1.24 | 1.46 | 17.7 |
| Mkonge | Singa | 3,300 | 3,500 | 3,626 | 3,483 | 3,566 | 2.4 |
| Pareto | Maua makavu | 2,500 | 3,200 | 3,200 | 3,500 | 3,700 | 5.7 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo
* Dola za Marekani/Kilogramu

**Huduma za Ugani**

175. Mwaka 2024, Serikali kupitia Mfumo wa Ruzuku ya Mbolea na Kituo cha Huduma kwa Wateja iliendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya kilimo kwa wakulima. Katika kipindi hicho, wakulima waliosajiliwa kwenye Mfumo wa Ruzuku ya Mbolea walikuwa 530,384 ikilinganishwa na wakulima 986,060 waliosajiliwa mwaka 2023. Aidha, maswali/hoja za wakulima/wadau wengine wa kilimo zilizoulizwa kupitia Kituo cha Huduma kwa Wateja zilikuwa 5,879 mwaka 2024 ikilinganishwa na maswali/hoja 116,865 mwaka 2023. Kwa upande mwingine, pikipiki 555 na vishikwambi 5,426 vilinunuliwa na kusambazwa kwa maafisa ugani mwaka 2024 ikilinganishwa na pikipiki 5,889 na vishikwambi 805 mwaka 2023.

**Utafiti katika Uzalishaji wa Mazao**

176. Mwaka 2024, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - TARI iligundua aina mpya 16 za mbegu bora za mazao mbalimbali ikilinganishwa na aina tano (5) za mbegu bora zilizogunduliwa mwaka 2023. Mbegu hizo zilikuwa karanga aina mbili (2), korosho aina nane (8) na maharage aina sita (6).

177. Mwaka 2024, TARI ilizalisha tani 846.57 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta ikilinganishwa na tani 1,131.36 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 25.2. Kati ya mbegu zilizozalishwa, tani 16.85 zilikuwa mbegu mama, tani 206.93 mbegu za awali, tani 563.59 mbegu za msingi na tani 59.2 mbegu zilizothibitishwa. Upungufu wa uzalishaji wa mbegu ulitokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mvua nyingi zilizoathiri uzalishaji wa mbegu. Vilevile, miche 10,766,506 ilizalishwa mwaka 2024 ikilinganishwa na miche 6,316,095 iliyozalishwa mwaka 2023,

sawa na ongezeko la asilimia 70.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya miche ya miti ya matunda.

**Mafunzo ya Kilimo**

178. Mwaka 2024, wanafunzi 2,580 walidahiliwa katika vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 3,372 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 23.5. Upungufu huo ulitokana na Serikali kufanya mabadiliko katika mfumo wa utoaji mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo vilivyo chini ya Wizara ya Kilimo kwa kujielekeza katika uhaulishaji wa teknolojia za kilimo kwa wakulima. Aidha, wakufunzi 12 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya shahada ya uzamili na shahada ya kwanza mwaka 2024 ikilinganishwa na wakufunzi tisa (9) waliopatiwa mafunzo hayo mwaka 2023.

**Umwagiliaji**

179. Mwaka 2024, eneo la umwagiliaji lilikuwa hekta 727,280.6, kama ilivyokuwa mwaka 2023 kutokana na kutokamilika kwa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji. Katika kipindi hicho, vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji viliongezeka kwa asilimia 19.8 na kufikia 756 kutoka vyama 631 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa uhamasishaji na utoaji wa mafunzo kuhusu umuhimu wa kujisajili katika vyama vya umwagiliaji.

**MIFUGO**

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

180. Mwaka 2024, idadi ya ng'ombe nchini ilikadiriwa kuwa milioni 39.2 ikilinganishwa na ng'ombe milioni 37.9 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Aidha, idadi ya mbuzi ilikadiriwa kuwa milioni 28.6 ikilinganishwa na mbuzi milioni 27.6 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko la mifugo lilichangiwa na Serikali na wadau wa mifugo kuendelea na ujenzi na uhamasishaji wa matumizi ya majosho, utoaji wa ruzuku kwenye dawa za kuogeshea mifugo na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa chanjo.

**Jedwali Na. 7.8: Idadi ya Mifugo, Mwaka 2020 - 2024 (Milioni)**

| Aina ya Mifugo | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ng'ombe | 33,928,391 | 35,256,637 | 36,584,883 | 37,913,129 | 39,241,375 | 3.5 |
| Mbuzi | 24,568,396 | 25,574,446 | 26,580,497 | 27,586,547 | 28,592,597 | 3.6 |
| Kondoo | 8,516,990 | 8,802,462 | 9,087,935 | 9,373,407 | 9,658,880 | 3.0 |
| Nguruwe | 3,208,495 | 3,439,362 | 3,670,229 | 3,901,096 | 4,131,962 | 5.9 |
| Kuku | 87,659,580 | 92,799,956 | 97,940,332 | 103,080,708 | 108,221,085 | 5.0 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

181. Mwaka 2024, tani 1,054,114 za nyama zilizalishwa ikilinganishwa na tani 963,857 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Aidha, mayai milioni 7,105.9 yalizalishwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mayai milioni 6,409.2 yaliyozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Vilevile, uzalishaji wa maziwa uliongezeka na kufikia lita milioni 4,009.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na lita milioni 3,971.8 zilizozalishwa mwaka 2023. Kwa upande mwingine, lita milioni 81.90 za maziwa zilisindikwa ikilinganishwa na lita milioni 77.9 zilizosindikwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na utoaji wa elimu na uhamasishaji wa ufugaji wa kibiashara; kuimarika kwa upatikanaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na nyama; na kuongezeka kwa ulaji wa mazao ya mifugo. Kwa upande mwingine, vituo vya kukusanyia maziwa viliongezeka na kufikia vituo 258 mwaka 2024 kutoka vituo 246 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 7.9: Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo, Mwaka 2020 - 2024**

| Aina ya Zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji Maziwa (Lita '000')** | | | | | |
| Ng'ombe wa asili | 2,170,461 | 2,345,650 | 2,400,000 | 2,637,863 | 2,605,008 |
| Ng'ombe wa kisasa | 930,923 | 1,102,422 | 1,200,000 | 1,299,246 | 1,404,977 |
| Mbuzi wa maziwa | - | - | - | 34,694 | - |
| **Jumla** | **3,101,384** | **3,448,072** | **3,600,000** | **3,971,803** | **4,009,985** |
| **Uzalishaji Nyama (Tani)** | | | | | |
| Ng'ombe | 508,355 | 526,351 | 544,984 | 612,809 | 666,227 |
| Mbuzi na kondoo | 102,137 | 107,791 | 113,782 | 162,693 | 181,662 |
| Nguruwe | 41,468 | 44,420 | 47,583 | 55,912 | 58,775 |
| Kuku | 86,206 | 91,404 | 96,916 | 132,442 | 147,450 |
| **Jumla** | **738,166** | **769,967** | **803,264** | **963,857** | **1,054,114** |
| **Uzalishaji Mayai ('000')** | | | | | |
| Mayai | **4,510,345** | **4,979,772** | **5,500,000** | **6,409,224** | **7,105,908** |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

182. Mwaka 2024, tani 55,410 za vipande vya ngozi zilizalishwa ikilinganishwa na tani 53,508 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa kwa wafugaji kuhusu ufugaji wa kisasa na wa kibiashara pamoja na elimu iliyotolewa kwa wachunaji na wapanga madaraja ya ngozi.

**Jedwali Na. 7.10: Uzalishaji wa Ngozi, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Mwaka | Ng'ozi za Ng'ombe | Ng'ozi za Mbuzi na Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2020 | 14,510 | 24,648 | 39,158 |
| 2021 | 20,340 | 30,773 | 51,113 |
| 2022 | 21,180 | 32,076 | 53,256 |
| 2023 | 21,168 | 32,340 | 53,508 |
| 2024 | 22,080 | 33,330 | 55,410 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

183. Mwaka 2024, ng'ombe 1,809,310, mbuzi 1,861,005 na kondoo 465,251 wenye thamani ya shilingi bilioni 1,680.07 waliuzwa katika minada mbalimbali nchini ikilinganishwa na ng'ombe 2,957,724, mbuzi 2,554,266 na kondoo 273,982 wenye thamani ya shilingi bilioni 3,478.4 waliouzwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa thamani wa asilimia 51.7. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya ng'ombe na mbuzi waliouzwa katika minada kulikosababishwa na baadhi ya wafugaji kutouza mifugo kufuatia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo kuuza ziada ya mazao badala ya mifugo.

184. Mwaka 2024, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilikuwa ng'ombe 48,080, mbuzi na kondoo 210,643 wenye thamani ya shilingi bilioni 70.7 ikilinganishwa na ng'ombe 20,536, mbuzi na kondoo 37,157 wenye thamani ya shilingi bilioni 44.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 59.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mifugo hai nje ya nchi.

**Jedwali Na. 7.11: Biashara ya Mifugo na Mazao ya Mifugo, Mwaka 2020 - 2024**

| **Soko la Ndani** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ng'ombe** | **Kondoo** | **Mbuzi** | **Punda** | **Jumla** | **Thamani (Shilingi Bilioni)** |
| 2020 | 1,023,200 | 205,161 | 987,867 | * | 2,216,228 | 865 |
| 2021 | 1,843,904 | 360,745 | 2,081,233 | 191,656 | 4,477,538 | 1,531 |
| 2022 | 2,194,937 | 201,610 | 1,879,623 | * | 4,276,170 | 1,741 |
| 2023 | 2,957,724 | 273,982 | 2,554,266 | * | 5,785,972 | 3,478 |
| 2024 | 1,809,310 | 465,251 | 1,861,005 | * | 4,135,566 | 1,680 |

| **Soko la Nje** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ng'ombe** | **Kondoo na Mbuzi** | **Jumla** | **Thamani (Shilingi Bilioni)** |
| 2020 | 3,574 | 49,184 | 52,758 | 1.9 |
| 2021 | 24,014 | 106,099 | 130,113 | 46.6 |
| 2022 | 23,356 | 39,952 | 63,307 | 62.4 |
| 2023 | 20,536 | 37,157 | 57,693 | 44.4 |
| 2024 | 48,080 | 210,643 | 258,723 | 70.7 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi
*Haikuuzwa

185. Mwaka 2024, mauzo ya nyama nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 6.5 na kufikia tani 13,745.38 zenye thamani ya shilingi bilioni 126.67 ikilinganishwa na tani 14,701.2 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 220.52 mwaka 2023. Kati ya mauzo hayo, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 1,024.33, nyama ya mbuzi tani 9,421.27, nyama ya kondoo tani 3,195.09, nyama ya kuku tani 32.35, nyama ya nguruwe tani 10.94 na nyama nyingine tani 61.4. Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya nyama nje ya nchi.

186. Mwaka 2024, tani 6,688.9 za vipande vya ngozi zenye thamani ya shilingi bilioni 8.06 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 4,933 zenye thamani ya shilingi bilioni 6.11 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 31.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa ubora wa mifugo, kuongezeka kwa mahitaji ya ngozi ghafi nje ya nchi, na kufutwa kwa tozo ya kibali cha kusafirisha ngozi nje ya nchi.

**Jedwali Na. 7.12: Uuzaji wa Ngozi Nje ya Nchi, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi na Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2020 | 3,020 | 161 | 3,181 |
| 2021 | 7,251 | 120 | 7,371 |
| 2022 | 6,691 | 781 | 7,472 |
| 2023 | 4,511 | 422 | 4,933 |
| 2024 | 5,970 | 719 | 6,689 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo**

187. Mwaka 2024, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ilizalisha na kusambaza dozi 76,221,600 za chanjo katika halmashauri zote nchini ikilinganishwa na dozi 67,458,590 zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Kati ya chanjo hizo, dozi 72,931,450 zilikuwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo, dozi 487,000 kimeta, dozi 149,450 chambavu, dozi 1,905,500 mapafu ya ng'ombe, dozi 6,550 kutupa mimba, dozi 368,850 mapafu ya mbuzi na dozi 372,800 ugonjwa wa kimeta na chambavu. Ongezeko hilo lilitokana na ununuzi wa mashine na vifaa vya kisasa vya kuzalisha chanjo pamoja na utoaji wa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kuchanja mifugo.

**Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo**

188. Mwaka 2024, mashamba ya Serikali yalizalisha kilogramu 36,964 za mbegu bora za malisho ikilinganishwa na kilogramu 22,691.65 zilizozalishwa mwaka 2023. Aidha, mashamba ya Serikali yalizalisha marobota 135,991 ya hei mwaka 2024 ikilinganishwa na marobota 130,132 yaliyozalishwa mwaka 2023. Ongezeko la uzalishaji wa malisho katika mashamba ya Serikali lilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa mashine, zana na vifaa vya shamba. Kwa upande mwingine, mashamba binafsi yalizalisha marobota 142,332 ya hei mwaka 2024 ikilinganishwa na marobota 118,077 yaliyozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji kwa wadau kuwekeza katika uzalishaji wa malisho.

189. Mwaka 2024, viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo viliongezeka kwa asilimia 13.1 na kufikia viwanda 250 kutoka viwanda 221 vilivyokuwepo mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi kulikowezesha kusajiliwa kwa viwanda vipya 29 vya kuzalisha vyakula vya mifugo.

Viwanda hivyo vilisajiliwa katika mikoa ya Arusha (viwanda 5), Dar es Salaam (12), Pwani (7), Morogoro (2), Mwanza (1), Katavi (1) na Dodoma (1). Kufuatia ongezeko la viwanda, tani 1,880,000 za vyakula vya mifugo zilizalishwa na sekta binafsi mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 1,580,000 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.0. Katika kipindi hicho, Serikali ilikagua na kusajili maeneo 279 ya kuzalisha vyakula vya mifugo, maeneo 437 ya kuuzia vyakula vya mifugo na maeneo 87 ya kuhifadhi rasilimali za vyakula vya mifugo ikilinganishwa na maeneo 221, maeneo 364 na maeneo 73 mtawalia, mwaka 2023. Ongezeko la maeneo yaliyosajiliwa na kukaguliwa lilitokana na juhudi za Serikali kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa vyakula vya mifugo pamoja na utoaji wa mafunzo kuhusu mfumo wa utoaji wa vibali vya kielektroniki - MIMIS kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo.

**Mafunzo ya Mifugo**

190. Mwaka 2024, Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo ulidahili wanafunzi 4,936 katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 4,452 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika kipindi hicho, Wakala ulitoa mafunzo kwa wafugaji 4,236 kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mifugo na malisho ikilinganishwa na wafugaji 3,254 waliopatiwa mafunzo mwaka 2023.

**Utafiti wa Mifugo**

191. Mwaka 2024, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania - TALIRI ilifanya tafiti 57 ikilinganishwa na tafiti 87 zilizofanyika mwaka 2023. Tafiti hizo zilihusu uboreshaji wa mbari za mifugo, uendelezaji wa malisho, uzalishaji wa mbegu bora za malisho na ushiriki wa wanawake na vijana katika shughuli za ufugaji. Tafiti hizo ziliwezesha uzalishaji na usambazaji wa ng'ombe chotara wa nyama na maziwa 191 na mbuzi chotara 116 katika wilaya za Bahi, Mpwapwa, Mkuranga, Morogoro na Muheza pamoja na Jiji la Tanga na Mbeya ikilinganishwa na ng'ombe chotara 191 na mbuzi chotara 77 waliozalishwa mwaka 2023. Aidha, kondoo 56 walizalishwa na kusambazwa katika wilaya za Siha na Longido.

192. Mwaka 2024, TALIRI ilizalisha na kusambaza kilogramu 5,589 za mbegu bora za malisho za nyasi (punje na vipando) ikilinganishwa na kilogramu 5,298 za mbegu zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshaji wa mitambo na ununuzi wa vifaa shamba. Mbegu hizo zilisambazwa katika mikoa ya Dodoma, Rukwa, Mbeya, Kilimanjaro, Shinyanga, Tanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Morogoro, Manyara na Arusha.

**Huduma za Ugani katika Mifugo**

193. Mwaka 2024, Serikali ilitoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani 1,058 ikilinganishwa na maafisa ugani 515 mwaka 2023. Aidha, katika kuboresha huduma za ugani, Serikali ilisajili maafisa ugani 3,517 na wafugaji 2,879 katika mfumo wa M-Kilimo mwaka 2024 ikilinganishwa na maafisa ugani 3,201 na wafugaji 752 waliosajiliwa mwaka 2023. Vilevile, Serikali iliendelea kuboresha mazingira ya maafisa ugani kwa kuwapatia pikipiki 252 mwaka 2024 ikilinganishwa na pikipiki 948 walizopatiwa mwaka 2023.

**UVUVI**

**Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi**

194. Mwaka 2024, Serikali kupitia ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi iliwezesha kukamatwa kwa vifaa na zana mbalimbali zinazotumika katika uvuvi haramu **(Jedwali Na. 7.13)**. Aidha, samaki wachanga kilogramu 8,142; kaa wachanga kilogramu 278; na jongoo bahari kilogramu 224 walikamatwa na kuteketezwa kwa idhini ya mahakama. Vilevile, watuhumiwa 990 wa uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira walikamatwa na kulipa faini ya shilingi milioni 372.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na watuhumiwa 1,070 waliokamatwa na kulipa faini ya shilingi milioni 560.5 mwaka 2023.

**Jedwali Na.7.13: Idadi ya Vifaa na Zana Zilizokamatwa katika Uvuvi Haramu, Mwaka 2022 - 2024**

| Na. | Aina ya Zana | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Nyavu za Makila | 2,988 | 176 | 460 |
| 2 | Kokoro | 2,268 | 416 | 386 |
| 3 | Nyavu za timba | 11,264 | 3,842 | 2,138 |
| 4 | Nyavu za dagaa | 443 | 10 | 12 |
| 5 | Vyandarua | 42 | 0 | 42 |
| 6 | Pikipiki | 0 | 4 | 0 |
| 7 | Magari | 0 | 1 | 0 |
| 8 | Kamba za kokoro (mita) | 290,133 | 362,509 | 307,350 |
| 9 | Nyavu za gonga | 1 | 0 | 0 |
| 10 | Boti | 60 | 17 | 30 |
| 11 | Mitumbwi | 380 | 432 | 301 |
| 12 | Injini za boti | 70 | 80 | 66 |
| 13 | Kasia | 2 | 2 | 53 |
| 14 | Kipe | 1 | 0 | 0 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Ukuzaji Viumbe Maji**

195. Mwaka 2024, wakuzaji viumbe maji walikuwa 35,986 ikilinganishwa na wakuzaji viumbe maji 34,057 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Ongezeko hilo lilitokana na elimu ya ugani iliyotolewa kuhusu ukuzaji wa viumbe maji pamoja na mikopo

iliyotolewa na Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Aidha, mabwawa ya kufugia samaki yalikuwa 34,417 mwaka 2024 ikilinganishwa na mabwawa 32,878 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Vilevile, vizimba vya kuzalishia samaki katika maziwa na malambo viliongezeka kwa asilimia 22.4 na kufikia vizimba 1,215 mwaka 2024 ikilinganishwa na vizimba 993 mwaka 2023. Kati ya hivyo, vizimba 1,133 viko katika Ziwa Victoria, vizimba vitatu (3) katika Ziwa Tanganyika na vizimba 79 katika malambo mbalimbali.

196. Mwaka 2024, vifaranga 66,684,806 vya samaki vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga 35,967,180 vilivyozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 85.4. Kati ya hivyo, Serikali ilizalisha vifaranga 16,122,027 na vituo vya sekta binafsi vilizalisha vifaranga 50,562,779. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na uhamasishaji wa matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara. Aidha, tani 7,911.4 za chakula cha samaki zilitumika nchini mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 4,337.9 zilizotumika mwaka 2023. Kati ya hizo, tani 3,455.4 zilizalishwa nchini na tani 4,456.0 ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Ongezeko la matumizi ya chakula cha samaki lilitokana na uwekezaji unaoendelea kufanyika, hususan kwa njia ya vizimba na mabwawa. Vilevile, wananchi 11,723 walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wananchi 8,788 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 7.14: Wakuzaji Viumbe Maji, Mabwawa, Vizimba na Vifaranga Mwaka, 2020 - 2024**

| Mwaka | Idadi ya Wakuzaji Viumbe Maji | Idadi ya Mabwawa ya Samaki | Idadi ya Vizimba | Idadi ya Vifaranga |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2020 | 28,009 | 27,979 | 431 | 21,676,187 |
| 2021 | 30,064 | 30,032 | 473 | 27,120,320 |
| 2022 | 31,998 | 31,407 | 780 | 29,295,638 |
| 2023 | 34,057 | 32,878 | 993 | 35,967,180 |
| 2024 | 35,986 | 34,417 | 1,215 | 66,684,806 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

197. Mwaka 2024, uzalishaji wa samaki (sato na kambale) ulikuwa tani 34,828.50 zenye thamani ya shilingi bilioni 261 ikilinganishwa na tani 29,106.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 235 mwaka 2023, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 19.7. Aidha, uzalishaji wa mwani ulikuwa tani 8,637.75 zenye thamani ya shilingi bilioni 9.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 4,379.1 zenye thamani ya shilingi bilioni 4.6 mwaka 2023. Ongezeko la uzalishaji viumbe maji lilitokana na upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu, matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara.

**Jedwali Na. 7.15: Mwenendo wa Ukuzaji Viumbe Maji, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Samaki (Sato na Kambale) (Tani) | Samaki Maji Chumvi Mwatiko (Tani) | Mwani (Tani) | Kambamiti (Tani) | Kambakoche (Tani) | Kaa (Kg) | Majongo Bahari (Kg) | Lulu (Vipande) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | 18,716.6 | - | 1,410.0 | 73.6 | - | - | - | 164 |
| 2021 | 20,258.0 | - | 2,438.0 | 97 | - | 410 | 115 | 360 |
| 2022 | 25,286.5 | 6 | 3,514.8 | 74.85 | 30 | 1,144 | 370 | 164 |
| 2023 | 29,106.6 | - | 4,379.1 | - | 30 | 600 | 860 | 550 |
| 2024 | 34,828.5 | - | 8,637.8 | 5.2 | 30 | 2,500 | 1,500 | 250 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uvunaji wa Samaki**

198. Mwaka 2024, tani 522,788.33 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 4,352.7 zilivunwa ikilinganishwa na tani 479,976.62 zenye thamani ya bilioni 3,359.8 zilizovunwa mwaka 2023. Kati ya hizo, tani 458,799.57 zilivunwa katika maji baridi na tani 63,988.76 zilivunwa katika maji chumvi. Kupungua kwa uvunaji wa samaki katika maji chumvi kulitokana na ukosefu wa vyombo vya kisasa vya uvuvi na mabadiliko ya tabianchi yaliyochangia wavuvi kushindwa kufika maeneo yenye samaki wengi.

**Jedwali Na. 7.16: Uvunaji wa Samaki, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Mwaka | Maji baridi | Maji chumvi | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2020 | 409,828.30 | 63,763.90 | 473,592.20 |
| 2021 | 414,104.80 | 62,914.00 | 477,018.80 |
| 2022 | 404,639.10 | 66,873.40 | 471,512.50 |
| 2023 | 415,879.60 | 64,097.00 | 479,977.60 |
| 2024 | 458,799.57 | 63,988.76 | 522,788.33 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

199. Mwaka 2024, Serikali ilifanya kaguzi 7,652 ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ikilinganishwa na kaguzi 7,023 zilizofanyika mwaka 2023. Kaguzi hizo zilifanyika katika viwanda 41 vikubwa na vya kati vya kuchakata samaki, mialo 130, masoko sita (6), maghala 98 na vyombo 2,641 vya kusafirisha mazao ya uvuvi. Aidha, vibali 18,232 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa ndani kwa ajili ya uuzaji wa tani 24,372.7 za mazao ya uvuvi katika masoko ya ndani mwaka 2024 ikilinganishwa na vibali 4,901 vilivyotolewa kwa uuzaji wa tani 39,452 mwaka 2023. Ongezeko la idadi ya vibali lilitokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali za kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara anakuwa na kibali chake, badala ya kibali kimoja kutumika na zaidi ya mfanyabiashara mmoja. Vilevile, vyeti vya afya 8,711 vilitolewa kwa wafanyabiashara kwa ajili ya uuzaji wa tani 39,791.97 za

mazao ya uvuvi nje ya nchi mwaka 2024 ikilinganishwa na vyeti 9,672 vilivyotolewa kwa uuzaji wa tani 42,592.03 mwaka 2023.

200. Mwaka 2024, Maabara ya Taifa ya Uvuvi ilifanya uchunguzi wa kimaabara wa vimelea na kemikali katika sampuli 2,938 ikilinganishwa na sampuli 2,725 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uchakataji wa samaki viwandani kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati wanaojihusisha na usafirishaji wa samaki na mazao ya uvuvi katika soko la ndani na nje. Uchunguzi huo ulilenga kulinda afya za walaji wa samaki na mazao ya uvuvi katika soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, kati ya sampuli zilizofanyiwa uchunguzi, sampuli 2,901 sawa na asilimia 98.7 zilikidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kimataifa ikilinganishwa na asilimia 93.4 ya sampuli mwaka 2023. Sampuli hizo zilijumuisha samaki na mazao ya uvuvi, maji na vyakula kutoka katika viwanda vya kuchakata samaki na wafanyabiashara wadogo.

**Uuzaji na Uagizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi**

201. Mwaka 2024, samaki hai wa mapambo 173,377 na tani 59,746.41 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 677.55 zilipata vibali vya kuuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na samaki hai wa mapambo 166,024 na tani 42,371.41 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 509.91 zilizopata vibali vya kuuzwa nje mwaka 2023. Ongezeko la thamani ya samaki na mazao ya uvuvi yaliyopata vibali vya kuuzwa nje lilitokana na kuimarika kwa biashara ya mazao ya uvuvi nje ya nchi pamoja na kuongezeka kwa viwanda na wafanyabiashara wenye leseni za uuzaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi. Katika kipindi hicho, mapato ya mrabaha yaliyotokana na mauzo ya mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 19.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 16.2 mwaka 2023. Aidha, mazao ya uvuvi yaliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi yalijumuisha tani 424.49 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 176.84 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 433.55 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 145.25 zilizopata vibali mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 21.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwanda vya kuchakata mabondo pamoja na bei ya mabondo katika masoko ya kimataifa. Mauzo ya mabondo yaliwezesha mapato ya shilingi bilioni 3.74 kama mrabaha mwaka 2024 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 3.41 mwaka 2023.

202. Mwaka 2024, tani 6.48 za samaki zenye thamani ya shilingi milioni 99.91 ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 9.50 zenye thamani ya shilingi milioni 269.8 mwaka 2023. Kupungua kwa uingizaji wa samaki kulitokana na kuongezeka kwa uvunaji wa ndani uliokidhi sehemu kubwa ya mahitaji ya samaki nchini. Aidha, mapato ya mrabaha yaliyotokana na uagizaji wa samaki yalikuwa shilingi milioni 26.63 mwaka 2024 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 45.46 mwaka 2023.

**Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi**

203. Mwaka 2024, Serikali iliendelea na juhudi za kuwezesha uongezaji thamani ya bidhaa za uvuvi na kipato cha wavuvi. Kutokana na hilo, masoko ya samaki yalifikia saba (7) ikilinganishwa na masoko matatu (3) mwaka 2023. Aidha, mialo ya samaki 31 kati ya mialo 130 iliyopo iliboreshwa na kuidhinishwa na EU kwa ajili ya kupokea mazao ya uvuvi na kuuza katika soko la Ulaya.

204. Hadi Desemba 2024, kulikuwa na viwanda vikubwa vya samaki 25 na viwanda vidogo 32 ikilinganishwa na viwanda vikubwa 21 na viwanda vidogo 29 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji wa uwekezaji katika sekta ya uvuvi uliofanywa na Serikali. Katika kipindi hicho, kulikuwa na viwanda vitano vya kati vya kutengeneza nyavu, viwanda vitatu vya kutengeneza boti, viwanda 18 vya mabondo na maghala 98 ya kuhifadhia mazao ya uvuvi.

205. Mwaka 2024, Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu - MPRU iliendelea kusimamia shughuli za uhifadhi wa bahari na maeneo tengefu ili kutunza na kulinda ikolojia ya viumbe vya bahari na kuendelea kuvutia utalii na uwekezaji wa hoteli za kiikolojia. Aidha, wageni 49,108 walitembelea maeneo ya hifadhi za bahari mwaka 2024 ikilinganishwa na wageni 42,696 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Vilevile, mapato ya shilingi milioni 2,727.5 yalikusanywa kutoka kwa wageni waliotembelea maeneo ya hifadhi za bahari mwaka 2024 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 2,013.6 yaliyokusanywa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 35.5. Ongezeko la wageni na mapato lilitokana na uhamasishaji wa utalii wa ndani pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa shughuli za uhifadhi wa rasilimali za bahari.

**Mafunzo ya Uvuvi**

206. Mwaka 2024, Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi - FETA ilidahili wanafunzi 1,116 ikilinganishwa na wanafunzi 1,222 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 8.7. Katika kipindi hicho, wavuvi na wakuzaji viumbe maji 10,892 walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi, upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa na ukuzaji viumbe maji ikilinganishwa na wavuvi na wakuzaji viumbe maji 15,799 waliopatiwa mafunzo mwaka 2023. Aidha, wadau wa uvuvi 93,733 walipatiwa elimu kupitia maonesho ya Nanenane, Sabasaba, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Mvuvi Duniani ikilinganishwa na wadau 80,617 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.3.

## MAENDELEO YA USHIRIKA

207. Mwaka 2024, vyama vya ushirika viliongezeka kwa asilimia 6.4 na kufikia 7,820 kutoka vyama 7,349 mwaka 2023. Kati ya hivyo, Vyama vya Masoko ya Mazao vilikuwa 4,533, Vyama vya Akiba na Mikopo 2,135, vyama vya aina nyingine 1,103 na Vyama

Vikuu vilikuwa 49. Aidha, wanachama wa vyama vya ushirika walifikia 8,405,413 mwaka 2024 kutoka wanachama 8,400,304 mwaka 2023. Ongezeko la vyama vya ushirika na wanachama lilitokana na uhamasishaji wa wadau kuhusu umuhimu wa ushirika kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Vilevile, viwanda vya kuchakata mazao vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vilifikia 329 mwaka 2024 kutoka viwanda 328 mwaka 2023.

208. Mwaka 2024, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilitoa mafunzo kwa wanachama 416,349, viongozi wa bodi za vyama vya ushirika 201,274 na watendaji wa vyama vya ushirika 22,312. Mafunzo hayo yalihusu uzingatiaji wa miongozo mbalimbali ya ushirika, haki na wajibu kwa mwanachama, uongozi bora pamoja na uandishi wa vitabu vya hesabu.

209. Mwaka 2024, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO lilikagua hesabu za vyama vya ushirika 4,760 ikilinganishwa na vyama 3,911 vilivyokaguliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 21.7. Kati ya hivyo, vyama 631, sawa na asilimia 13.3 vilipata hati inayoridhisha, vyama 2,871 (asilimia 60.3) vilipata hati yenye mashaka, vyama 995 (asilimia 20.9) vilipata hati chafu na vyama 263 (asilimia 5.5) vilipata hati isiyo na maoni.

## Jedwali Na. 38: UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | Jumla | Bei[2] | Iliyozalishwa | iliyotumika[3] | Kilo kwa kila mtu[4] |
| | Umma | Binafsi | (000 Tani) | (Sh./Tani) | Tani | Jumla | |
| | (000 Tani) | (000 Tani) | | | | Tani | |
| 2005/06 | 1,545 | 956 | 2,501 | 22,383 | 263,317 | 343,292 | 12.0 |
| 2006/07 | 1,430 | 611 | 2,041 | 29,000 | 192,095 | 366,708 | 12.0 |
| 2007/08 | 1,967 | 799 | 2,766 | 32,767 | 265,434 | 382,518 | 13.0 |
| 2008/09 | 2,056 | 693 | 2,749 | 32,771 | 279,850 | 396,113 | 13.4 |
| 2009/10 | 1,972 | 598 | 2,570 | 42,046 | 263,461 | 398,070 | 13.7 |
| 2010/11 | 2,357 | 661 | 3,018 | 43,865 | 304,135 | 410,259 | 12.0 |
| 2011/12 | 2,036 | 680 | 2,716 | 48,833 | 262,879 | 439,307 | 12.0 |
| 2012/13 | 2,242 | 711 | 2,953 | 52,167 | 296,698 | 468,000 | 12.0 |
| 2013/14 | 2,198 | 602 | 2,800 | 50,500 | 294,300 | 434,782 | 12.0 |
| 2014/15 | 2,466 | 697 | 3,163 | 51,333 | 304,007 | 511,680 | 12.0 |
| 2015/16 | 2,270 | 569 | 2,839 | 59,707 | 293,075 | 525,784 | 12.0 |
| 2016/17 | 2,504 | 557 | 3,061 | 72,667 | 324,930 | 456,000 | 12.8 |
| 2017/18 | 2,550 | 626 | 3,175 | 72,667 | 303,752 | 515,004 | 13.5 |
| 2018/19 | 2,792 | 797 | 3,589 | 72,667 | 359,219 | 524,772 | 13.5 |
| 2019/20 | 2,659 | 728 | 3,387 | 77,333 | 311,358 | 372,787 | 12.8 |
| 2020/21 | 2,985 | 1,092 | 4,014 | 79,000 | 367,718 | - | 12.0 |
| 2021/22 | 2,697 | 1,060 | 3,757 | 77,500 | 379,281 | 379,281 | 12.0 |
| 2022/23r | 3,396 | 1,046 | 4,442 | 78,375 | 460,049 | 460,049 | 12.0 |
| 2023/24 | 3,377 | 865 | 4,242 | 75,000 | 395,293 | 783,487 | 12.0 |
| **Badiliko 2022/23 - 2023/24 (Asilimia)** | **-0.6** | **-17.3** | **-4.5** | **-4.3** | **-14.1** | **70.3** | **0.0** |

**Chanzo:** Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

\- sukari yote iliyozalishwa imetumika Tanzania Bara

## Jedwali Na. 39: PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

| Msimu [1] | Pamba yenye mbegu | | Pamba iliyoondolewa mbegu | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mauzo nchini | |
| | Uzalishaji (Tani) | Bei ya wastani (Shilingi/kg) | Kiasi (Tani) | Kiasi (tani) 2 | Bei ya wastani (Shilingi/tani) |
| 2005/06 | 376,591 | 220 | 126,228 | .. | .. |
| 2006/07 | 130,585 | 350 | 43,770 | .. | .. |
| 2007/08 | 200,662 | 450 | 70,773 | 37,488 | .. |
| 2008/09 | 368,697 | 480 | 123,582 | 66,554 | .. |
| 2009/10 | 267,644 | 480 | 54,851 | .. | .. |
| 2010/11 | 163,518 | 900 | 54,809 | .. | .. |
| 2011/12 | 225,938 | 1,000 | 75,731 | .. | .. |
| 2012/13 | 351,156 | 660 | 117,702 | .. | .. |
| 2013/14 | 245,815 | 700 | 82,394 | .. | .. |
| 2014/15 | 202,312 | 750 | 67,812 | | |
| 2015/16 | 149,765 | 800 | 50,199 | 525,784 | |
| 2016/17 | 132,934 | 1,000 | 42,203 | - | - |
| 2017/18 | 222,790 | 1,100 | 80,575 | 39,244 | 3,667 |
| 2018/19 | 348,901 | 1,200 | 129,408 | 51,942 | 3,123 |
| 2019/20 | 348,958 | 1,200 | 128,660 | 25,162 | 3,781 |
| 2020/21 | 122,836 | 900 | 46,923 | 9,479 | 2,924 |
| 2021/22 | 144,792 | 1,800 | 67,178 | 14,779 | 2,761 |
| 2022/23r | 174,486 | 1,150 | 108,633 | 11,950 | 1,952 |
| 2023/24 | 282,510 | 1,400 | 108,766 | 13,052 | 2,557 |
| **Badiliko (Asilimia) 2022/23 - 2023/24** | **61.9** | **21.7** | **0.1** | **9.2** | **31.0** |

**Chanzo:** Bodi ya Mauzo ya Pamba

[1]Msimu ni kati ya Juni na Mei

Takwimu hazikupatikana

Pamba ya Tanzania hainunuliwi wala kuuzwa katika madaraja kwa sasa

**Jedwali Na. 40: ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA**

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (Hekta) | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (Tani) | | | | | | Bei kwa Mkulima | Mauzo Nchini[2] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kiumilikaji: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | (Shs/Kilo) | (Tani) |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | | |
| 2005/06 | 11,310 | 10,977 | 22,287 | 91,337 | 31,881 | 123,218 | 29,046 | 94,172 | 123,218 | 93 | 3,881 |
| 2006/07 | 11,271 | 11,956 | 23,227 | 109,632 | 49,024 | 158,656 | 39,673 | 118,983 | 158,656 | 100 | 4,737 |
| 2007/08 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 97,310 | 51,160 | 148,470 | 33,456 | 115,015 | 148,471 | 111 | 4,253 |
| 2008/09 | 11,271 | 11,449 | 22,722 | 100,644 | 41,167 | 141,811 | 31,677 | 110,134 | 141,811 | 118 | 4,464 |
| 2009/10 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 106,021 | 44,716 | 150,737 | 33,309 | 117,428 | 150,737 | 124 | 5,084 |
| 2010/11 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 95,511 | 47,616 | 143,127 | 112,368 | 30,759 | 143,127 | 152 | 6,065 |
| 2011/12 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 88,582 | 52,359 | 140,941 | 27,009 | 113,932 | 140,941 | 200 | 4,839 |
| 2012/13 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 113,628 | 54,872 | 168,500 | 30,997 | 137,503 | 168,500 | 206 | 5,498 |
| 2013/14 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 101,489 | 47,001 | 148,490 | 27,935 | 120,555 | 148,490 | 225 | 5,672 |
| 2014/15 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 100,018 | 52,467 | 152,485 | 23,283 | 129,202 | 152,485 | 176 | 6,302 |
| 2015/16 | 11,272 | 11,449 | 22,721 | 96,759 | 44,605 | 141,364 | 25,413 | 115,915 | 141,328 | 230 | 10,257 |
| 2016/17 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 78,929 | 41,495 | 120,424 | 20,592 | 99,832 | 120,424 | 285 | 4,648 |
| 2017/18 | 11,322 | 11,705 | 23,028 | 97,428 | 55,620 | 153,048 | 31,599 | 121,449 | 153,048 | 299 | 5,434 |
| 2018/19 | 11,322 | 11,705 | 23,027 | 104,203 | 61,081 | 165,284 | 36,506 | 128,778 | 165,284 | 312 | 3,926 |
| 2019/20 | 12,445 | 11,030 | 23,475 | 76,028 | 53,188 | 129,216 | 22,930 | 106,286 | 129,216 | 312 | 27,128 |
| 2020/21 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 72,138 | 51,655 | 123,793 | 25,178 | 98,614 | 123,792 | 312 | 28,875 |
| 2021/22 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 73,030 | 54,203 | 127,233 | 25,872 | 101,361 | 127,233 | 314 | 4,312 |
| 2022/23r | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 58,729 | 45,209 | 103,938 | 16,735 | 87,203 | 103,938 | 366 | 3,414 |
| 2023/24 | 11,272 | 11,500 | 22,772 | 55,526 | 44,991 | 100,517 | 15,260 | 85,257 | 100,517 | 366 | 2,672 |
| **Badiliko 2022/23-2023/24 (Asilimia)** | **-9.4** | **1.2** | **-4.3** | **-5.5** | **-0.5** | **-3.3** | **-8.8** | **-2.2** | **-3.3** | **0.0** | **-21.7** |

**Chanzo:** Bodi ya Chai Tanzania

1Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

## Jedwali Na. 41: KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (Tani) | | | | Bei (Shilingi/Kilogramu) | | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Arabica | | Robusta | Jumla | Arabica | | Robusta | Kiasi | Thamani |
| | Laini | Ngumu | | | Laini | Ngumu | Maganda | (Tani) | (Shs '000) |
| 2005/06 | 24,116 | 1,362 | 8,856 | 34,334 | 1,200.0 | 420.0 | 270.0 | 33,300.0 | 793,042.5 |
| 2006/07 | 33,345 | 2,417 | 19,076 | 54,838 | 2,840.0 | 1,796.0 | 1,616.0 | 548.4 | 129,867.5 |
| 2007/08 | 26,330 | 1,588 | 15,606 | 43,524 | 2,995.0 | 1,875.0 | 1,734.0 | 43,523.0 | 89,099.3 |
| 2008/09 | 37,207 | 1,727 | 29,643 | 68,577 | 2,887.0 | 2,172.0 | 1,836.0 | 68,577.0 | 165,615.6 |
| 2009/10 | 22,217 | 915 | 11,467 | 34,599 | 3,988.0 | 2,475.0 | 1,563.0 | 34,599.0 | 108,741.1 |
| 2010/11 | 30,309 | 2,013 | 24,348 | 56,670 | 4,500.0 | 1,300.0 | 1,200.0 | 56,670.0 | 264,143.6 |
| 2011/12 | 20,775 | 941 | 11,590 | 33,306 | 8,144.4 | 5,436.4 | 3,276.9 | 33,306.0 | 212,292.6 |
| 2012/13 | 33,204 | 1,655 | 36,150 | 71,009 | 4,850.0 | 3,600.0 | 3,200.0 | 71,009.0 | 281,781.8 |
| 2013/14 | 28,212 | 1,115 | 18,875 | 48,202 | 4,314.0 | 3,272.9 | 3,074.6 | 48,202.0 | 183,708.9 |
| 2014/15 | 26,335 | 810 | 18,788 | 45,933 | 5,848.0 | 4,515.0 | 3,848.5 | - | - |
| 2015/16 | 21,517 | 460 | 17,526 | 39,503 | 7,249.6 | 5,943.4 | 4,092.9 | 39,503.0 | 105,760.8 |
| 2016/17 | 27,023 | 681 | 19,989 | 47,693 | 7,636.0 | 6,164.0 | 4,347.0 | 47,693.0 | 129,428.7 |
| 2017/18 | 36,551 | 633 | 11,897 | 43,193 | 2,980.0 | 2,980.0 | 2,980.0 | 43,193.3 | 116,587.3 |
| 2018/19 | 30,664 | 2,068 | 27,927 | 66,546 | 2,210.0 | 2,210.0 | 2,210.0 | 66,546.2 | 123,185.6 |
| 2019/20 | 31,380 | 883 | 27,056 | 59,318 | 5,472.0 | 3,815.0 | 3,180.0 | 59,318.0 | 261,088.6 |
| 2020/21 | 28,783 | 2,576 | 41,668 | 73,027 | 6,665.0 | 3,749.0 | 3,065.0 | 73,027.0 | 329,205.8 |
| 2021/22 | 37,414 | 1,776 | 27,353 | 66,523 | 8,783.4 | 4,535.0 | 4,093.8 | 66,543.0 | 469,647.0 |
| 2022/23r | 28,422 | 878 | 31,109 | 60,409 | 5,978.0 | 4,234.0 | 2,965.0 | 60,409.3 | 393,329.3 |
| 2023/24 | 46,329 | 1,426 | 23,948 | 71,703 | 11803.3 | 7,981.54 | 10,191.41 | 71,703.5 | 801,946.67 |
| **Badiliko (Asilimia) 2022/23 - 2023/24** | **63.0** | **62.5** | **-23.0** | **18.7** | **97.4** | **88.5** | **243.7** | **18.7** | **103.9** |

**Chanzo:** Bodi ya Kahawa Tanzania
+Kahawa iliyosafishwa
1Msimu ni kati ya Julai na Juni
-Takwimu hazikupatikana

## Jedwali Na. 42: ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

| Msimu[1] | Eneo (Hekta) | | | Katani iliyopatikana | | Mauzo nchini+ | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (Tani) | Bei kwa Mkulima (shilingi/tani) | Kiasi (tani) | Thamani (Shilingi milioni) |
| 2009/10 | 30,556 | 11,849 | 42,405 | 24,092 | 1,200,000 | 12,761 | 10,375 |
| 2010/11 | 31,117 | 12,169 | 43,286 | 25,090 | 1,300,000 | 11,617 | 13,154 |
| 2011/12 | 32,601 | 14,302 | 46,903 | 36,600 | 1,500,000 | 11,511 | 14,390 |
| 2012/13 | 33,649 | 11,994 | 45,643 | 34,874 | 1,600,000 | 11,466 | 16,823 |
| 2013/14 | 35,266 | 11,044 | 46,310 | 37,805 | 1,724,864 | 9,160 | – |
| 2014/15 | 35,946 | 12,494 | 48,440 | 38,872 | 2,071,446 | 8,972 | 17,513 |
| 2015/16 | 34,723 | 13,231 | 47,954 | 41,795 | 2,700,000 | 9,075 | 20,342 |
| 2016/17 | 41,661 | 12,850 | 54,511 | 36,533 | 2,700,000 | 9,559 | 21,541 |
| 2017/18 | 40,635 | 14,389 | 55,024 | 43,280 | 3,000,000 | 12,111 | 30,803 |
| 2018/19 | 43,406 | 18,031 | 61,437 | 33,271 | 3,300,000 | 14,646 | 43,907 |
| 2019/20 | 41,757 | 17,044 | 58,801 | 35,341 | 3,500,000 | 12,646 | 38,323 |
| 2020/21 | 41,685 | 16,898 | 58,583 | 39,343 | 3,500,000 | 13,440 | 39,545 |
| 2021/22 | 45,505 | 21,687 | 67,192 | 48,359 | 3,626,139 | 12,428 | 45,065 |
| 2022/23r | 47,774 | 24,575 | 72,349 | 56,773 | 3,482,613 | 14,289 | 49,710 |
| 2023/24 | 73,687 | 25,689 | 99,376 | 61,216 | 3,566,226 | 15,120 | 53,921 |
| **Badiliko (Asilimia) 2022/23 - 2023/24** | **54.2** | **4.5** | **37.4** | **7.8** | **2.4** | **5.8** | **8.5** |

**Chanzo:** Bodi ya Katani

Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

## Jedwali Na. 43: MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

| Msimu [1] | Maua yaliyonunuliwa (Tani) | | | | Mauzo Nchini: Kiasi (Tani) | | | Mauzo Nchini: Thamani (Shilingi '000) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kaskazini | Kusini | Jumla | Bei[2] (Shilingi/ Kilogramu) | Utomvu | Poda | Dawa | Utomvu | Poda | Dawa |
| 2009/10 | - | 1,780.0 | 1,780.0 | 1,500.0 | 57.0 | 69.0 | 1,035.0 | 37,361.0 | 1,473.0 | 248.0 |
| 2010/11 | - | 1,786.8 | 1,786.8 | 1,500.0 | 57.2 | 69.3 | 69.3 | 37,503.7 | 1,478.6 | 246.9 |
| 2011/12 | 0.0 | 5,700.0 | 5,700.0 | 1,700.0 | 82.0 | - | 750.0 | - | 204.0 | 360,919.0 |
| 2012/13 | 0.0 | 6,100.0 | 6,100.0 | 2,400.0 | 84.0 | - | 2,000.0 | - | - | 462,000.0 |
| 2013/14 | 34.0 | 2,691.8 | 2,726.2 | 2,000.0 | 90.0 | 60.0 | 830.0 | 6,900,000.0 | 160,500.0 | 233,000.0 |
| 2014/15 | 31.0 | 2,255.0 | 2,286.0 | 2,500.0 | 76.0 | 30.0 | 430.0 | 133.6 | 116,048.0 | 235,612.7 |
| 2015/16 | 25.0 | 1,987.0 | 2,012.4 | 2,100.0 | 59.9 | 6.0 | 480.0 | 9,450,000.0 | 30,240.0 | 282,240.0 |
| 2016/17 | 39.0 | 2,111.8 | 2,151.0 | 2,050.0 | 53.2 | 162.0 | 727.0 | 6,782,016.0 | 651,810.0 | 436,232.0 |
| 2017/18 | 43.0 | 2,355.9 | 2,400.0 | 2,500.0 | 16.0 | 204.0 | 700.0 | 13,932,947.0 | 869,418.1 | 390,864.0 |
| 2018/19 | 68.0 | 2,050.0 | 2,118.0 | 3,200.0 | - | - | - | 144,487.0 | 844,213.9 | 409,299.4 |
| 2019/20 | 69.0 | 2,441.0 | 2,510.0 | 2,500.0 | 60.0 | 83.0 | 137.8 | 13,600,000.0 | 420,000.0 | 353,000.0 |
| 2020/21r | 33.0 | 2,379.0 | 2,412.0 | 2,500.0 | 75.0 | 109.0 | 945.0 | 16,097,877.0 | 488,807.0 | 523,494.0 |
| 2021/22 | 50.0 | 2,644.0 | 2,694.0 | 3,200.0 | 67.0 | 156.0 | 810.0 | 12,419,041.0 | 701,605.0 | 514,409.0 |
| 2022/23r | 48.0 | 4,191.0 | 4,239.0 | 3,500.0 | 87.0 | 762.0 | 144.0 | 16,239,000.0 | 4,191,000.0 | 237,000.0 |
| 2023/24 | 75.5 | 2,790.1 | 2,865.6 | 3,700.0 | 15.0 | 865.5 | 72.0 | 3,249,278.5 | 18518.7 | 89,100.0 |
| **Badiliko (Asilimia) 2022/23 - 2023/24** | **57.2** | **-33.4** | **-32.4** | **5.7** | **-82.8** | **13.6** | **-50.0** | **-80.0** | **-99.6** | **-62.4** |

**Chanzo:** Bodi ya Pareto Tanzania
1 Msimu ni kati ya Julai na Juni
2 Bei ni kwa maua ya daraja la tano
-Takwimu hazikupatikana
*Takwimu hizi hadi December 30 2002, Msimu bado unaendelea
r Takwimu zimeboreshwa

## Jedwali Na. 44: UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI

| Mwaka | Maji Baridi | | | | Maji Chumvi | | | | Jumla Kuu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya wavuvi | Idadi ya vyombo | Uzito (tani) | Thamani "000" (Shilingi) | Idadi ya wavuvi | Idadi ya Vyombo | Uzito (tani) | Thamani "000" (Shilingi) | Idadi ya wavuvi | Idadi ya vyombo | Uzito (tani) | Thamani "000" (Shilling) |
| 2010 | 141,206 | 47,635 | 294,474.00 | 684,844,020.0 | 36,321 | 7,664 | 52,683.40 | 89,639,934.0 | 177,527 | 55,299 | 347,157.40 | 774,483,954.0 |
| 2011 | 141,206 | 47,635 | 290,473.60 | 1,031,883,680.9 | 36,321 | 7,664 | 50,592.40 | 166,954,953.0 | 177,527 | 55,299 | 341,066.00 | 1,198,838,633.9 |
| 2012 | 146,420 | 49,321 | 314,944.00 | 1,129,349,924.7 | 36,321 | 7,664 | 50,079.40 | 177,781,799.0 | 182,741 | 56,985 | 365,023.40 | 1,307,131,723.7 |
| 2013 | 147,020 | 49,721 | 315,008.00 | 1,248,903,393.0 | 36,321 | 7,664 | 52,846.00 | 195,529,127.0 | 183,341 | 57,385 | 367,854.00 | 1,444,432,520.0 |
| 2014 | 147,479 | 49,627 | 314,061.54 | 1,287,248,813.0 | 36,321 | 7,664 | 51,912.40 | 207,649,600.0 | 183,800 | 57,291 | 365,973.94 | 1,503,574,790.0 |
| 2015 | 147,479 | 49,627 | 309,922.00 | 1,270,856,679.9 | 36,321 | 7,664 | 52,723.00 | 210,892,897.1 | 183,800 | 57,291 | 362,645.00 | 1,481,749,577.0 |
| 2016 | 149,018 | 49,688 | 308,771.59 | 1,274,485,403.6 | 54,511 | 9,650 | 53,823.30 | 211,891,899.2 | 203,529 | 59,338 | 362,594.89 | 1,486,377,302.7 |
| 2017 | 149,018 | 49,688 | 309,922.08 | 1,270,856,679.8 | 54,511 | 9,650 | 52,723.22 | 210,892,897.1 | 203,529 | 59,338 | 362,645.30 | 1,481,749,577.0 |
| 2018 | 149,018 | 49,688 | 323,120.77 | 1,495,678,680.0 | 53,035 | 9,242 | 53,231.94 | 248,262,840.0 | 202,053 | 58,930 | 376,352.71 | 1,743,941,520.0 |
| 2019 | 149,018 | 49,688 | 365,104.02 | 1,715,988,902.7 | 53,035 | 9,242 | 105,205.21 | 494,464,497.7 | 202,053 | 58,930 | 470,309.23 | 2,210,453,400.4 |
| 2020 | 149,504 | 50,116 | 409,828.31 | 2,049,141,547.2 | 53,035 | 9,242 | 63,763.93 | 318,819,664.2 | 202,539 | 59,358 | 473,592.24 | 2,367,961,211.4 |
| 2021 | 141,769 | 48,749 | 414,104.81 | 2,418,489,585.3 | 53,035 | 9,242 | 62,914.03 | 357,308,946.0 | 194,804 | 57,991 | 477,018.84 | 2,775,798,531.3 |
| 2022 | 144,728 | 49,206 | 404,639.12 | 2,711,082,104.0 | 53,035 | 9,242 | 66,873.42 | 448,051,914.0 | 197,763 | 58,448 | 471,512.54 | 3,159,134,018.0 |
| 2023 | 144,728 | 49,206 | 415,879.60 | 2,911,157,221.9 | 53,035 | 9,242 | 64,097.01 | 448,679,086.3 | 197,763 | 58,448 | 479,976.62 | 3,359,836,308.2 |
| 2024 | 148,626 | 50,024 | 458,799.57 | 3,850,702,150.5 | 53,035 | 9,242 | 63,988.76 | 502,033,490.1 | 201,661 | 59,266 | 522,788.33 | 4,352,735,640.5 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 45: MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI**

| Mwaka | Uzito (Tani) | Samaki wa mapambo | Thamani (dola za Marekani) | Thamani (Shilingi) | Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 37,996 | 61,215 | 152,973,357 | 233,714,590,011 | 6,153,278,023 |
| 2012 | 41,394 | 45,550 | 163,299,366 | 254,901,017,111 | 6,819,926,007 |
| 2013 | 38,574 | 44,260 | 147,659,779 | 234,884,628,956 | 6,117,769,194 |
| 2014 | 43,354 | 42,100 | 188,101,262 | 314,489,903,877 | 7,490,632,355 |
| 2015 | 41,060 | 87,630 | 259,286,762 | 547,228,222,096 | 13,097,411,199 |
| 2016 | 39,692 | 65,841 | 257,257,101 | 526,985,019,569 | 14,302,761,907 |
| 2017 | 36,063 | 101,110 | 182,450,278 | 406,568,122,272 | 10,446,850,539 |
| 2018 | 44,940 | 63,978 | 239,680,015 | 546,993,779,393 | 13,520,367,822 |
| 2019 | 45,775 | 136,915 | 158,657,946 | 376,763,802,643 | 25,567,600,873 |
| 2020 | 40,478 | 128,316 | 169,111,837 | 386,369,197,733 | 21,678,640,820 |
| 2021 | 42,302 | 181,268 | 176,083,787 | 414,232,629,494 | 18,436,276,859 |
| 2022 | 37,236 | 208,744 | 199,810,554 | 457,047,515,491 | 16,557,211,745 |
| 2023 | 42,371 | 166,024 | 213,383,805 | 509,909,916,965 | 16,214,093,692 |
| 2024 | 59,746 | 173,377 | 259,603,653 | 677,552,034,741 | 19,921,220,485 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 46: MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI**

| Mwaka | Kiasi (Tani) | Thamani (USD) | Thamani (Shilingi) | Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| 2010 | 27,229 | 139,666,995 | 194,012,069,314 | 4,509,670,994 |
| 2011 | 25,426 | 127,601,694 | 197,899,741,508 | 4,299,987,312 |
| 2012 | 28,951 | 141,189,162 | 220,149,518,646 | 4,967,311,025 |
| 2013 | 33,733 | 124,551,585 | 197,578,220,799 | 5,085,642,906 |
| 2014 | 24,473 | 665,856,773 | 1,131,575,531,076 | 4,569,314,170 |
| 2015 | 23,001 | 250,279,107 | 528,534,413,019 | 11,251,591,352 |
| 2016 | 26,045 | 177,338,054 | 345,417,803,263 | 6,964,514,349 |
| 2017 | 26,680 | 168,554,019 | 376,572,501,425 | 7,057,407,121 |
| 2018 | 32,167 | 179,522,959 | 409,654,290,065 | 9,689,153,198 |
| 2019 | 32,609 | 176,894,903 | 400,195,293,574 | 17,622,314,163 |
| 2020 | 24,173 | 132,369,802 | 302,303,225,916 | 13,627,647,551 |
| 2021 | 21,846 | 143,135,053 | 337,103,408,189 | 9,704,591,513 |
| 2022 | 21,647 | 162,165,160 | 375,439,047,154 | 8,917,297,123 |
| 2023 | 20,192 | 132,207,272 | 316,336,648,585 | 7,783,579,857 |
| 2024 | 24,433 | 174,810,125 | 455,716,058,504 | 9,647,995,399 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

## SURA YA 8

## MISITU, WANYAMAPORI NA UTALII

### Misitu na Nyuki

210. Mwaka 2024, tani 33,861 za asali na tani 1,918 za nta zilizalishwa ikilinganishwa na tani 33,276 za asali na tani 1,913 nta zilizozalishwa mwaka 2023. Kati ya kiasi hicho, tani 951.6 za asali zenye thamani ya shilingi milioni 11,419.5 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 1,199.8 zenye thamani ya shilingi milioni 11,998.2 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023, sawa na upungufu wa thamani wa asilimia 4.8. Kupungua kwa mauzo ya asali nje kulitokana na kuongezeka kwa ushindani katika masoko ya nje. Kwa upande mwingine, tani 458.14 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 6,675.4 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 479.23 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 4,792.3 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 39.3. Kuongezeka kwa mapato ya nta kulitokana na kupanda kwa bei ya nta kwenye masoko ya nje. Aidha, asali na nta iliyozalishwa nchini iliuzwa zaidi katika nchi za Marekani, Ujerumani, Japan, Poland, Ireland na New Zealand.

**Jedwali Na. 8.1: Mauzo ya Mazao ya Nyuki Nje ya Nchi, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|
| | Uzito (Tani) | Thamani (Shilingi) | Uzito (Tani) | Thamani (Shilingi) |
| 2020 | 2,032.4 | 13,413,721,200 | 251.0 | 3,865,400,000 |
| 2021 | 1,988.0 | 19,878,220,000 | 393.0 | 6,489,999,500 |
| 2022 | 1,562.9 | 15,629,295,500 | 793.5 | 11,903,470,950 |
| 2023 | 1,199.8 | 11,998,150,000 | 479.2 | 4,792,300,000 |
| 2024 | 951.6 | 11,419,488,000 | 458.14 | 6,675,405,000 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

### Upandaji wa Miti

211. Mwaka 2024, miche ya miti 34,126,916 ilioteshwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS ikilinganishwa na miche 33,068,643 iliyooteshwa mwaka 2023. Miche hiyo ilipandwa katika maeneo yaliyovunwa yenye hekta 4,930, maeneo yaliyorudishiwa miti (hekta 2,296) na maeneo ambayo miti haikuota vizuri (hekta 2,308) ikilinganishwa na hekta 4,508.2, hekta 2,071.1 na hekta 2,384.3 mtawalia mwaka 2023.

**Jedwali Na. 8.2: Uendelezaji wa Mashamba ya Miti, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Idadi ya Miche Iliyooteshwa | Eneo la Mashamba Mapya | Maeneo Yaliyorudishiwa Miti | Eneo Lililopandwa Miche baada ya Miti Kuvunwa | Eneo Lililorudishiwa Miche katika Maeneo Yasiyoota Vizuri | Eneo la Mashamba ya Miti Lililosafishwa | Eneo la Mashamba ya Miti Lililopogolewa | Eneo la Mashamba ya Miti ambalo Miti Ilipunguziwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Hekta | | | | |
| 2020 | 20,689,369 | 56,500 | 4,543 | 3,583 | 3,303 | 37,469 | 9,647 | 3,317 |
| 2021 | 31,295,703 | 30,000 | 4,498 | 3,328 | 2,076 | 41,527 | 10,860 | 4,685 |
| 2022 | 30,705,653 | 0 | 5,538 | 3,219 | 3,496 | 38,357 | 9,869 | 3,197 |
| 2023 | 33,068,643 | 0 | 2,071.10 | 4,508.20 | 2,384.30 | 27,681.30 | 7,155.50 | 2,690.60 |
| 2024 | 34,126,916 | 0 | 2,296 | 4,930 | 2,308 | 30,205 | 12,654 | 2,816 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

212. Mwaka 2024, miche 14,820,189 ilipandwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo misitu ya asili, vyanzo vya maji, makazi na maeneo yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za binadamu ikilinganishwa na miche 14,089,944 iliyopandwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Hii ilitokana na kuendelea kwa uhamasishaji na programu za upandaji miti zilizofanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, mipango 30 ya usimamizi wa hifadhi za misitu iliandaliwa na mipaka ya hifadhi ya misitu yenye urefu wa kilometa 2,194 ilisafishwa na kuwekwa vigingi 769 na mabango 177 mwaka 2024 ikilinganishwa na mipango 57, mipaka yenye urefu wa kilometa 1,713.2, vigingi 870 na mabango 973 yaliyowekwa mwaka 2023.

213. Mwaka 2024, Wakala wa Huduma za Misitu ulikamata na kutaifisha magunia 41,863 ya mkaa, nguzo 2,329, mbao zenye mita za ujazo 2,123.3, kuni zenye mita za ujazo 606, na magogo yenye mita za ujazo 791.8. Aidha, pikipiki 2,932, baiskeli 5,208, magari 300, majahazi 23 na pikipiki 35 za miguu mitatu za kubebea mizigo zilishikiliwa na kutozwa faini.

### Mauzo ya Bidhaa za Misitu Nje ya Nchi

214. Mwaka 2024, bidhaa za misitu zenye thamani ya shilingi bilioni 427.2 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na bidhaa za misitu zenye thamani ya shilingi bilioni 194.13 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023. Hii ilitokana na kuondolewa kwa zuio la baadhi ya miti kusafirishwa nje; kuongezeka kwa masoko mapya yanayohitaji bidhaa za miti kutoka Tanzania, ikiwemo soko la India; na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji taarifa za bidhaa za misitu zinazouzwa nje.

### Wanyamapori

215. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa kufanya doria 279,956 ikilinganishwa na doria 433,572 zilizofanyika mwaka 2023. Kati ya doria hizo, Shirika la Hifadhi za Taifa lilifanya doria 51,400,

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro doria 76,738, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori doria 151,068 na Kikosi cha Taifa cha Kupambana na Ujangili kilifanya doria 750. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 6,295 wa makosa ya ujangili wa wanyamapori na misitu ikilinganishwa na watuhumiwa 5,421 waliokamatwa mwaka 2023. Aidha, katika doria zilizofanyika, nyara mbalimbali zilikamatwa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8.3.**

**Jedwali Na 8.3: Nyara Zilizokamatwa katika Doria, Mwaka 2023 - 2024**

| Aina za Nyara | 2023 | 2024 |
|---|---|---|
| Meno ya tembo | 208 | 105 |
| Vipande vya meno ya tembo | 390 | 93 |
| Nyamapori (kilogramu) | 1,986 | 411 |
| Nyama kavu (vipande) | 299 | 346 |
| Kobe hai | 63 | 10 |
| Ngozi (vipande) | 9 | 5 |
| Magamba ya kakakuona | 123 | 734 |
| Chatu | 3 | 2 |
| Silaha | 408 | 127 |
| Risasi | 2,807 | 424 |
| Mitego | 17,211 | 2,367 |
| Magari | 34 | 4 |
| Pikipiki | 81 | 217 |
| Mifugo | 40,752 | 62,568 |
| Meno ya kiboko | 6 | 4 |
| Kucha za simba | 11 | 8 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

216. Mwaka 2024, mapato yatokanayo na sekta ndogo ya wanyamapori yalikuwa shilingi bilioni 819.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 634.3 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 29.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza utekelezaji wa mikataba sita (6) ya uwekezaji mahiri kwenye maeneo ya wanyamapori; juhudi mbalimbali za utangazaji wa vivutio vya utalii, ikiwemo Programu Maalum ya Tanzania - The Royal Tour na Amazing Tanzania; na uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya hifadhi. Kati ya mapato yaliyokusanywa, Shirika la Hifadhi za Taifa - TANAPA lilichangia asilimia 58.6, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro - NCAA asilimia 31.0 na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori - TAWA asilimia 10.4.

**Jedwali Na. 8.4: Mapato ya Sekta Ndogo ya Wanyamapori, Mwaka2020 - 2024**

| Mwaka | Shirika la Hifadhi za Taifa | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2020 | 85,614,710,442.0 | 47,862,177,819.0 | 20,913,213,013.0 | 154,390,101,274.0 |
| 2021 | 127,028,556,252.0 | 63,852,180,870.0 | 60,651,257,787.0 | 251,531,994,909.0 |
| 2022 | 293,079,503,086.0 | 144,354,627,647.0 | 63,030,304,315.3 | 500,464,435,048.3 |
| 2023 | 379,790,063,492.1 | 195,748,756,367.0 | 58,730,532,598.2 | 634,269,352,457.3 |
| 2024 | 480,223,465,704.4 | 254,396,987,140.3 | 85,228,986,090.1 | 819,849,438,934.8 |
| Ukuaji (Asilimia) | 26.4 | 30.0 | 45.1 | 29.3 |
| Mchango (Asilimia) | 58.6 | 31.0 | 10.4 | 100 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Uwindaji wa Kitalii na Utalii wa Picha**

217. Mwaka 2024, watalii 232,424 wa nje walitembelea maeneo ya uwindaji ikilinganishwa na watalii 191,475 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 21.4. Aidha, mapato yalitokana na uwindaji wa kitalii na utalii wa picha yalikuwa shilingi bilioni 85.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 58.7 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 45.1. Kati ya hayo, mapato yaliyotokana na uwindaji wa kitalii yalikuwa shilingi bilioni 61.08 ikilinganishwa na shilingi bilioni 40.43 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 51.1. Mapato yaliyotokana na utalii wa picha yalikuwa shilingi bilioni 24.15 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18.31 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 31.9. Ongezeko la mapato lilitokana na kuendelea kushamiri kwa utalii wa picha, wawindaji wa kitalii na watazamaji.

**Jedwali Na. 8.5: Idadi ya Wawindaji wa Kitalii na Mapato, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | | Mapato (Shilingi Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wawindaji | Watazamaji | Watalii wa picha | Jumla | |
| 2020 | 251 | 185 | 34,981 | 35,417 | 15,590.6 |
| 2021 | 548 | 101,382 | 66,648 | 168,578 | 35,726.0 |
| 2022 | 687 | 503 | 139,967 | 141,157 | 63,030.3 |
| 2023 | 599 | 498 | 190,378 | 191,475 | 58,730.5 |
| 2024 | 671 | 718 | 231,035 | 232,424 | 85,229.0 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Utalii**

218. Mwaka 2024, watalii 2,141,895 waliingia nchini ikilinganishwa na watalii 1,808,205 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutangaza utalii kupitia: programu maalum (The Royal Tour na Amazing Tanzania); balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali; mazao mapya ya utalii, ikiwemo

utalii wa faru weusi; na matamasha, mikutano na matukio mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wa utalii. Kati ya hao, watalii 1,041,473 walitembelea Hifadhi za Taifa na watalii 1,100,422 walitembelea maeneo mengine ya vivutio vya utalii nchini. Kwa upande mwingine, watalii wa ndani walikuwa 3,218,352 mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii 1,985,707 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 62.1. Kati ya hao, watalii 968,766 walitembelea Hifadhi za Taifa mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii 902,176 mwaka 2023. Idadi hiyo iliwezesha Tanzania kufikisha jumla ya watalii 5,360,247 wa nje na wa ndani mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii 3,793,912 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 41.3. Idadi hii pia ni zaidi ya lengo la nchi la kufikisha watalii milioni 5 ifikapo mwaka 2025.

219. Mwaka 2024, watalii 1,204,811 walitembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ikilinganishwa na watalii 843,473 waliotembelea eneo hilo mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 42.8. Kati ya hao, watalii 728,111 walitoka nje ya nchi na watalii 476,700 walikuwa wa ndani.

**Jedwali Na. 8.6: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini, Mwaka 2020 - 2024**

| **Mwezi** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---:|---:|---:|---:|---:|
| Januari | 132,684 | 79,116 | 94,441 | 146,877 | 180,422 |
| Februari | 137,204 | 79,730 | 101,042 | 144,019 | 184,092 |
| Machi | 66,581 | 72,285 | 93,889 | 118,186 | 155,810 |
| Aprili | 7,105 | 43,966 | 79,405 | 96,852 | 116,280 |
| Mei | 5,529 | 42,173 | 89,271 | 106,497 | 129,492 |
| Juni | 9,671 | 57,689 | 117,349 | 146,892 | 179,264 |
| Julai | 17,136 | 81,307 | 166,736 | 185,929 | 218,065 |
| Agosti | 24,863 | 87,397 | 158,049 | 186,030 | 211,056 |
| Septemba | 29,566 | 80,733 | 134,231 | 168,708 | 186,160 |
| Oktoba | 41,740 | 92,345 | 141,517 | 171,573 | 189,557 |
| Novemba | 61,183 | 92,939 | 123,351 | 154,012 | 174,042 |
| Desemba | 87,605 | 113,012 | 155,639 | 182,630 | 217,655 |
| **Jumla** | **620,867** | **922,692** | **1,454,920** | **1,808,205** | **2,141,895** |

**Chanzo:** Idara ya Uhamiaji na Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 8.7: Mwenendo wa Utalii katika Hifadhi za Taifa, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | Jumla | Mapato (Shilingi milioni) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | | |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614.7 |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028.6 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079.5 |
| 2023 | 888,506 | 902,176 | 1,790,682 | 379, 790.1 |
| 2024 | 1,041,473 | 968,766 | 2,010,239 | 480,223.4 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

220. Mwaka 2024, watalii 298,893 walitembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia ikilinganishwa na watalii 250,808 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Kati ya hao, watalii wa ndani walikuwa 260,992 na watalii wa nje walikuwa 37,901 mwaka 2024 ikilinganishwa na watalii wa ndani 219,727 na watalii wa nje 31,081 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na watalii waliotembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia yalikuwa shilingi milioni 2,123.05 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 1,984.21 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.0. Ongezeko hilo lilitokana na utangazaji wa utalii, hususan kupitia Programu za The Royal Tour na Amazing Tanzania, kuongezeka kwa doria katika misitu, kuzuia ukataji wa miti na kuboreshwa kwa miundombinu katika maeneo ya Hifadhi za Misitu.

**Jedwali Na. 8.8: Mwenendo wa Watalii Waliotembelea Vivutio vilivyopo katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na Mashamba ya Miti Mwaka 2024**

| Mwezi | Idadi ya Watali | | | Mapato | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndani | Nje | Jumla | Ndani | Nje | Jumla |
| Januari | 13,797 | 3,604 | 17,401 | 49,148,500 | 97,786,500 | 146,935,000 |
| Februari | 13,158 | 3,222 | 16,380 | 46,904,644 | 74,740,000 | 121,644,644 |
| Machi | 11,738 | 2,044 | 13,782 | 41,513,860 | 46,698,450 | 88,212,310 |
| Aprili | 10,063 | 1,184 | 11,247 | 34,905,615 | 28,371,290 | 63,276,905 |
| Mei | 16,904 | 1,252 | 18,156 | 40,643,125 | 28,230,090 | 68,873,215 |
| Juni | 25,141 | 3,055 | 28,196 | 95,895,990 | 82,901,590 | 178,797,580 |
| Julai | 24,500 | 4,941 | 29,441 | 129,262,405 | 151,394,895 | 280,657,300 |
| Agosti | 34,953 | 5,122 | 40,075 | 158,830,345 | 157,238,770 | 316,069,115 |
| Septemba | 31,149 | 4,429 | 35,578 | 154,621,055 | 142,088,220 | 296,709,275 |
| Oktoba | 25,871 | 3,960 | 29,831 | 114,872,600 | 115,255,870 | 230,128,470 |
| Novemba | 20,966 | 2,032 | 22,998 | 68,231,985 | 52,289,245 | 120,521,230 |
| Desemba | 32,752 | 3,056 | 35,808 | 125,272,896 | 85,954,080 | 211,226,976 |
| **Jumla** | **260,992** | **37,901** | **298,893** | **1,060,103,020** | **1,062,949,000** | **2,123,052,020** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Malikale**

221. Mwaka 2024, wageni 262,216 walitembelea vivutio vya malikale ikilinganishwa na wageni 147,275 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 78.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu katika vivutio vya Malikale. Aidha, mapato yaliyotokana na wageni waliotembelea vivutio vya malikale yalikuwa shilingi milioni 3,301.35 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi milioni 2,229.60 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 48.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa miundombinu ya uhifadhi, utalii wa malikale pamoja na utangazaji wa vivutio vya asili.

**Jedwali Na. 8.9: Wageni Waliotembelea Vivutio vya Malikale na Mapato Mwaka 2022 - 2024**

| Kituo | 2022 | | 2023 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wageni | Mapato | Wageni | Mapato | Wageni | Mapato |
| Magomeni | 531 | 1,601,668 | 688 | 1,069,522 | 4,912 | 282,234,640 |
| Kaole | 33,805 | 64,370,196 | 39,481 | 75,895,283 | 53,355 | 101,392,300 |
| Isimila | 10,104 | 29,627,384 | 3,890 | 3,845,142 | 26,416 | 102,418,740 |
| Mji Mkongwe Bagamoyo | 17,920 | 51,056,832 | 21,940 | 37,489,242 | 25,470 | 81,719,596.65 |
| Kalenga | 4,972 | 8,154,194 | 4,494 | 6,527,284 | 29,836 | 52,084,000 |
| Kilwa | 5,729 | 48,862,750 | 6,902 | 12,649,553 | 6,525 | 87,138,540 |
| Olduvai | 17,969 | 1,283,114,008.67 | 27,535 | 2,010,926,123.49 | 30,176 | 2,430,203,754.24 |
| Mbozi | 4,800 | 11,697,726 | 3,953 | 6,686,300 | 2,649 | 4,358,000 |
| Amboni | 17,044 | 34,148,326 | 15,522 | 25,368,567 | 22,192 | 36,810,000 |
| Tongoni | 193 | 464,164 | 657 | 1,003,257 | 717 | 1,410,500 |
| Ujiji | 4,664 | 14,338,354 | 4,531 | 10,437,353 | 21,668 | 30,632,000 |
| Kwihara | 271 | 300,000 | 1,013 | 1,343,103 | 987 | 3,108,135 |
| Kolo | 5,191 | 23,223,430 | 6,900 | 21,677,337 | 8,195 | 36,266,944.33 |
| CaravanSerai | 5,554 | 10,388,796 | 5,738 | 9,702,250 | 25,136 | 45,980,000 |
| Kunduchi | 4,297 | 5,008,416 | 4031 | 4,981,032 | 3,982 | 5,593,000 |
| **Jumla** | **133,044** | **1,586,356,244.67** | **147,275** | **2,229,601,348.49** | **262,216** | **3,301,350,150.22** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

**Makumbusho ya Taifa**

222. Mwaka 2024, wageni 475,175 walitembelea Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni 490,526 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 3.1. Upungufu huo ulitokana na kutokufanyika kwa matamasha, matukio na programu za kimakumbusho. Katika kipindi hicho, wageni wa ndani walikuwa 452,540 na wageni wa nje walikuwa 22,635. Aidha, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni katika vituo vya Makumbusho ya Taifa yalikuwa shilingi milioni 892.69 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi milioni 696.6 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa watafiti kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kufanya tafiti za kitaaluma katika maeneo ya makumbusho.

**Jedwali Na. 8.10: Idadi ya Watalii na Mapato katika Vivutio vya Makumbusho ya Taifa Mwaka 2022 - 2023**

| Na. | Kituo | 2023 | | | | 2024 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
| | | Nje | Ndani | Jumla | | Nje | Ndani | Jumla | |
| 1 | Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni | 8,802 | 202,040 | 210,842 | 271,096,910 | 11,338 | 182,557 | 193,895 | 372,133,504 |
| 2 | Kijiji cha Makumbusho | 4,489 | 148,209 | 152,698 | 208,770,300 | 6,464 | 188,152 | 194,616 | 341,048,688 |
| 3 | Makumbusho ya Azimio la Arusha | 400 | 23,233 | 23,633 | 22,932,000 | 495 | 17,786 | 18,281 | 32,507,267 |
| 4 | Makumbusho ya Elimu Viumbe | 2,875 | 45,139 | 48,014 | 87,433,275 | 4,039 | 37,090 | 41,129 | 110,913,381 |
| 5 | Makumbusho ya Mwl. Nyerere | 91 | 18,485 | 18,576 | 67,058,800 | 68 | 12,192 | 12,260 | 18,406,461 |
| 6 | Makumbusho ya Vita ya Majimaji | 78 | 27,714 | 27,792 | 30,847,300 | 107 | 12,071 | 12,178 | 14,159,739 |
| 7 | Makumbusho ya Dkt. Rashid Kawawa | 14 | 3,693 | 3,707 | 3,432,800 | 4 | 834 | 838 | 872,500 |
| 8 | Mji wa Kihistoria Mikindani | 16 | 5,248 | 5,264 | 4,997,000 | 120 | 1,858 | 1,978 | 2,650,884 |
| | **Jumla** | **16,765** | **473,761** | **490,526** | **696,568,385** | **22,635** | **452,540** | **475,175** | **892,692,423.84** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 47: WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA KATIKA MWAKA 2010 - 2024**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | Jumla | |
| 2010 | 540,440 | 333,294 | 873,734 | 113,856,861,145 |
| 2011 | 586,869 | 360,928 | 947,797 | 119,549,704,203 |
| 2012 | 537,675 | 364,217 | 901,892 | 137,545,109,618 |
| 2013 | 530,142 | 427,208 | 957,350 | 150,861,426,031 |
| 2014 | 535,140 | 417,220 | 952,360 | 152,977,487,000 |
| 2015 | 432,124 | 526,110 | 958,234 | 149,957,485,000 |
| 2016 | 439,119 | 518,457 | 957,576 | 175,089,696,000 |
| 2017 | 386,529 | 595,811 | 982,340 | 207,587,218,000 |
| 2018 | 726,003 | 442,543 | 1,168,546 | 214,486,751,736 |
| 2019 | 763,276 | 494,676 | 1,257,952 | 292,539,502,030 |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614,710,442 |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028,556,252 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079,503,086 |
| 2023 | 888,506 | 902,176 | 1,790,682 | 379,790,063,492 |
| 2024 | 1,041,505 | 968,766 | 2,010,239 | 480,223,465,704 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 48: MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU NJE YA NCHI MWAKA 2024**

| Na. | Bidhaa | Kiasi | Thamani (Dola za Marekani ) | Thamani (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sawn wood (m3) | 235,013 | 30,512,202 | 78,202,773,726 |
| 2 | Veneer (m3) | 188,231 | 107,329,358 | 275,085,144,554 |
| 3 | Wood-based panels (plywood, marine boards, MDF, particle boards) (kg) | 62,322 | 17,429,837 | 44,672,672,231 |
| 4 | Carvings (kg) | 15,159 | 780,616 | 2,000,718,808 |
| 5 | Wild ornamental plants (kg) | 26,962 | 131,498 | 337,029,374 |
| 6 | Resin (kg) | 3,307,625 | 2,531,294 | 6,487,706,522 |
| 7 | Poles (m3) | 3,419 | 945,385 | 2,423,021,755 |
| 8 | Herbal medicines (e.g. Leaves, barks) (kg) | 958 | 35,769 | 91,675,947 |
| 9 | Wattle extracts (kg) | 1,531,620 | 2,633,246 | 6,749,009,498 |
| 10 | Biomass briquettes (kg) | 1,899,000 | 736,879 | 1,888,620,877 |
| 11 | Wooden small items (kg) | 70,507 | 206,487 | 529,226,181 |
| 12 | Furniture, frames, and shutters (kg) | 23,396 | 71,070 | 182,152,410 |
| 13 | Essential oils (e.g. Sandalwood & baobab oils) (kg) | 26,002 | 2,121,235 | 5,436,725,305 |
| 14 | Woven products (e.g. Baskets, mats) (kg) | 5,461 | 64,866 | 166,251,558 |
| 15 | Gum Arabic (kg) | 271,300 | 304,670 | 780,869,210 |
| 16 | Clarinets (m3) | 65 | 630,514 | 1,616,007,382 |
| 17 | Wild fruits (e.g., tamarind, baobab & palm fruits) (kg) | 59,190 | 20,164 | 51,680,332 |
| 18 | Logs (special permit) (m3) | 168 | 25,261 | 64,743,943 |
| 19 | Withies (kg) | 70,950 | 69,250 | 177,487,750 |
| 20 | Wood bi-products (egg Sawdust, wood shaves, offcuts) (kg) | 26,961 | 61,248 | 156,978,624 |
| 21 | Pallet Wood (m3) | 151 | 18,154 | 46,528,702 |
| 22 | Fibre and Raffia (kg) | 1,501 | 18,800 | 48,184,400 |
| 23 | Firewood (m3) | 1 | 360 | 922,680 |
| 24 | Grasses (kg) | 1,500 | 2,250 | 5,766,750 |
| 25 | Tree seeds & seedlings (kg) | 11 | 35 | 89,705 |
| 26 | Barks (kg) | 2 | 5 | 12,815 |
| **Jumla** | | **7,827,475** | **166,680,451** | **427,202,001,039** |

**Jedwali Na. 49: MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII NCHINI 2016 - 2024**

| Maelezo | Kipimo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Watalii wa Kimataifa | Idadi | 1,505,702 | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,141,895 |
| Watalii wa hotelini | Idadi | 1,404,672 | 1,353,279 | 563,779 | 848,936 | 1,365,861 | 1,710,333 | 1,990,697 |
| Mapato | Dola za Marekani Milioni | 2,433 | 2,604 | 715 | 1,248 | 2,528 | 3,374 | 3,903 |
| Wastani wa siku za Mtalii kukaa hotelini | Siku | 10 | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (Dola za Marekani) | Safari za Vifurushi | 331 | 379 | 312 | 364 | 377 | 419 | 416 |
| | Safari zisizo za Vifurushi | 135 | 216 | 115 | 141 | 166 | 178 | 172 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 50: WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO**

| Mwaka | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Jumla |
|---|---:|---:|---:|
| 2010 | 281,513 | 242,133 | 523,646 |
| 2011 | 281,513 | 307,086 | 588,599 |
| 2012 | 310,537 | 254,730 | 565,267 |
| 2013 | 350,970 | 296,763 | 647,733 |
| 2014 | 332,469 | 278,221 | 610,690 |
| 2015 | 289,061 | 278,922 | 567,983 |
| 2016 | 284,794 | 265,845 | 550,639 |
| 2017 | 391,030 | 249,428 | 640,458 |
| 2018 | 410,574 | 268,880 | 679,454 |
| 2019 | 445,283 | 279,255 | 724,538 |
| 2020 | 122,228 | 125,953 | 248,181 |
| 2021 | 160,877 | 165,235 | 326,112 |
| 2022 | 388,853 | 256,422 | 645,275 |
| 2023 | 515,961 | 327, 512 | 843,473 |
| 2024 | 728,111 | 476,700 | 1,204,811 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

## SURA YA 9

## MADINI

**Leseni za Shughuli za Madini**

223. Mwaka 2024, leseni 12,009 za utafutaji wa madini, uchimbaji wa madini, uchenjuaji, usafishaji na biashara ya madini zilitolewa ikilinganishwa na leseni 11,251 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Hii ilitokana na juhudi za Serikali kuongeza vitendea kazi, kuboresha mfumo wa utoaji leseni wa *FlexiCadastre* na mafunzo yaliyotolewa kwa watumiaji wa mfumo. Kati ya leseni zilizotolewa, leseni 501 zilikuwa za utafutaji wa madini, leseni moja (1) ya uchimbaji mkubwa, leseni 26 za uchimbaji wa kati, leseni 9,497 za uchimbaji mdogo, leseni 18 za uchenjuaji wa madini, leseni moja (1) ya usafishaji wa madini, leseni 577 za biashara ya madini na leseni 1,388 za biashara ndogo ya madini.

**Vibali vya Uuzaji wa Madini**

224. Mwaka 2024, vibali 12,073 vya kuuza madini nje ya nchi vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,176.18 vilitolewa ikilinganishwa na vibali 11,258 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,478.42 vilivyotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 20.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya madini ya dhahabu, makaa ya mawe na vito katika masoko ya nje ya nchi.

**Dhahabu**

225. Mwaka 2024, uzalishaji wa dhahabu ulikuwa kilogramu 61,680.81 ikilinganishwa na kilogramu 54,760.32 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini zilizochochewa na ongezeko la bei ya dhahabu kwenye soko la dunia. Wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia ilifikia dola za Marekani 2,384.8 kwa wakia mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,940.5 kwa wakia mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 22.9.

226. Mwaka 2024, kilogramu 59,471 za dhahabu zilipata vibali vya kusafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na kilogramu 62,781.75 zilizopata vibali mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 5.3. Upungufu huo ulichangiwa na Benki Kuu ya Tanzania kununua kilogramu 1,987.34 za dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo, wa kati, wakubwa na wafanyabiashara wa madini baada ya kuchakatwa katika hatua za awali (fire assaying). Aidha, thamani ya dhahabu iliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 13.6 na kufikia dola za Marekani milioni 3,431.08 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,021.62 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

**Almasi**

227. Mwaka 2024, uzalishaji wa madini ya almasi ulikuwa karati 373,252.76 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 59.24 ikilinganishwa na karati 132,636.40 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 18.5 zilizozalishwa mwaka 2023. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na Mgodi wa Wiliamson Diamond Limited kuendelea na shughuli za uzalishaji baada ya kutatua changamoto za uzalishaji zilizojitokeza mgodini kuanzia Novemba 2022 hadi Julai 2023.

**Vito vya Thamani**

228. Mwaka 2024, madini ya vito ghafi (isipokuwa tanzanite na almasi) yenye kilogramu 46,299,069 yalizalishwa ikilinganishwa na kilogramu 55,954,779.72 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 17.3. Kupungua kwa uzalishaji kulichangiwa na kushuka kwa bei za madini ya vito kwenye masoko ya kimataifa.

**Tanzanite**

229. Mwaka 2024, madini ya tanzanite ghafi na magonga yaliyozalishwa yalikuwa kilogramu 83,014.66 ikilinganishwa na kilogramu 122,664.95 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 32.3. Aidha, karati 17,470 za madini ya tanzanite zenye thamani ya dola za Marekani milioni 2.43 zilikatwa na kusanifiwa mwaka 2024 ikilinganishwa na karati 34,904.33 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.52 zilizokatwa na kusanifiwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 49.9. Hii ilitokana na Serikali kuzuia tanzanite ghafi kutolewa nje ya eneo la Mirerani hali iliyosababisha wakataji kukosa malighafi. Wastani wa bei ya tanzanite ghafi kwa kilogramu katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 3,596.45 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,376.58 kwa kilogramu mwaka 2023.

**Makaa ya Mawe**

230. Mwaka 2024, tani 3,904,542.69 za makaa ya mawe zilizalishwa ikilinganishwa na tani 3,256,481.06 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya makaa ya mawe yanayotumika kama nishati kwenye uzalishaji wa saruji ndani na nje ya nchi, hususan kwa nchi za Burundi, Rwanda, Kenya na Uganda. Aidha, thamani ya makaa ya mawe yaliyozalishwa ilikuwa shilingi bilioni 1,035.93 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 878.86 mwaka 2023.

**Madini ya Jasi**

231. Mwaka 2024, tani 821,221.08 za madini ya jasi zilizalishwa ikilinganishwa na tani 549,835.74 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 49.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya madini ya jasi ambayo ni malighafi katika uzalishaji wa saruji. Katika kipindi hicho, tani 22,575 za madini ya jasi zenye thamani ya dola za Marekani

milioni 3.9 zilipata vibali vya kuuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 10,485.56 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.8 zilizopata vibali mwaka 2023. Kuongezeka kwa madini ya jasi yaliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi kulitokana na ongezeko la masoko ya madini ya jasi katika nchi za Malawi, Burundi, Uganda, Kenya na Kongo.

**Madini ya ujenzi**

232. Mwaka 2024, madini ya ujenzi yaliyozalishwa yalikuwa tani milioni 33.30 zenye thamani ya shilingi bilioni 586.48 ikilinganishwa na tani milioni 33.81 zenye thamani ya shilingi bilioni 543.99 mwaka 2023, sawa na upungufu wa uzalishaji kwa asilimia 1.5. Upungufu huu ulitokana na miradi mingi ya kimkakati iliyokuwa inatumia madini ujenzi kukamilika ikiwemo ujenzi wa bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere, ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa kwa kipande cha kati ya Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma, na ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi. Madini ujenzi yaliyozalishwa kwa wingi ni pamoja na kokoto, mchanga, moramu, changarawe na mawe ambayo hutumika kwa wingi katika shughuli za ujenzi.

**Madini Mengine**

233. Mwaka 2024, uzalishaji wa madini ya fedha ulikuwa kilogramu 3,129 ikilinganishwa na kilogramu 14,481.35 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 78.4. Aidha, madini ya fedha yaliyopata vibali vya mauzo nje ya nchi yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1.14 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 0.89 mwaka 2023. Ongezeko la thamani lilitokana na kuimarika kwa bei ya madini hayo kulikotokana na shughuli za uongezaji thamani katika viwanda vya kusafisha dhahabu ambapo madini ya fedha huvunwa kama madini ambata katika uongezaji thamani huo.

234. Mwaka 2024, uzalishaji wa madini ya lithium ulikuwa tani 52.00 ikilinganishwa na tani 2,060.72 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 97.5. Upungufu huo ulitokana na Serikali kusimamisha utoaji wa leseni za uchimbaji pamoja na kuzuia usafirishaji wa madini ya lithium ghafi nje ya nchi ili kuwezesha uongezaji thamani kufanyika nchini. Aidha, kibali kimoja cha mauzo ya madini ya lithium nje ya nchi chenye thamani ya shilingi milioni 48.98 kilitolewa ikilinganishwa na vibali 18 vyenye thamani ya shilingi milioni 2,656.13 vilivyotolewa mwaka 2023.

235. Mwaka 2024, uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 338.01 ikilinganishwa na tani 420.81 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 19.7. Katika kipindi hicho, vibali 18 vya mauzo ya madini ya bati nje ya nchi vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 6.9 vilitolewa ikilinganishwa na vibali 24 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 7.1 vilivyotolewa mwaka 2023.

**Masoko ya Madini**

236. Mwaka 2024 kulikuwa na masoko 43 ya madini na vituo 108 vya ununuzi ikilinganishwa na masoko 42 na vituo 98 vya ununuzi vilivyokuwepo mwaka 2023. Kwa upande mwingine, ukusanyaji wa maduhuli katika masoko ulikua shilingi bilioni 217.92 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 176.57 zilizokusanywa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Kati ya kiasi kilichokusanywa, shilingi bilioni 179.15 zilitokana na mrabaha, shilingi bilioni 29.48 zilitokana na ada ya ukaguzi na shilingi bilioni 9.29 zilitokana na tozo ya huduma. Kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli kulitokana na Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi, ukaguzi na udhibiti wa utoroshaji wa madini kwenye masoko na vituo vya ununuzi wa madini.

237. Mwaka 2024, tani 16.49 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.99 ziliuzwa katika masoko ya madini nchini ikilinganishwa na tani 17.25 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.34 zilizouzwa mwaka 2023. Aidha, karati 6,934.16 za madini ya almasi zenye thamani ya shilingi bilioni 3.2 ziliuzwa katika masoko ya madini mwaka 2024 ikilinganishwa na karati 13,311.73 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.96 zilizouzwa mwaka 2023.

**Jedwali Na. 51: UCHIMBAJI WA MADINI - KIASI KILICHOPATIKANA**

| MADINI | Kipimo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Almasi | Karati | 416,749.51 | 147,190.95 | 62,545.00 | 442,016.26 | 132,636.40 | 373,252.76 |
| Dhahabu | Kg | 48,408.09 | 55,805.33 | 59,638.00 | 56,942.98 | 54,760.32 | 61,680.81 |
| Tanzanite (ghafi) | Kg | - | 51,542.47 | 177,145.50 | 14,487.48 | 32,870.63 | 28,822.99 |
| Tanzanite magonga | Kg | - | 47,412.00 | 165,968.00 | 75,699.00 | 89,794.00 | 54,191.67 |
| Tanzanite (iliyokatwa na kusanifiwa) | Karati | - | 118,772.95 | 120,175.00 | 57,864.28 | 34,904.33 | 17,469.66 |
| Madini mengine ya Vito (ghafi) | Kg | 1,929,714.44 | 23,564,524.64 | 7,197,217.00 | 12,752,079.67 | 55,954,779.72 | 46,299,069.32 |
| Chumvi | Tani | 99,510.11 | 83,974.32 | 112,995.00 | 181,818.07 | 159,020.49 | 82,953.22 |
| Phosphate | Tani | - | 28,376.22 | 24,493.00 | 26,596.79 | 31,745.08 | 29,833.70 |
| Mawe ya Chokaa | 000 Tani | 5,526.59 | 6,788.35 | 8,506.00 | 7,741.00 | 10,128.67 | 9,731.18 |
| Bati | Tani | 24.32 | 47.00 | 211.00 | 538.17 | 420.81 | 338.01 |
| Jasi | Tani | 256,529.11 | 443,926.34 | 598,053.00 | 604,407.91 | 549,835.74 | 821,221.08 |
| Makaa ya Mawe | Tani | 712,136.37 | 689,959.96 | 976,319.00 | 2,511,419.40 | 3,256,481.06 | 3,904,542.69 |
| Pozolana | Tani | 263,063.59 | 160,077.81 | 216,934.00 | 226,038.26 | 351,988.16 | 287,136.94 |
| Kaolin | Tani | 15,342.55 | 98,453.67 | 100,950.00 | 46,973.44 | 75,246.95 | 86,054.98 |
| Madini ya Fedha | Kg | 12,607.07 | 13,186.58 | 9,324.00 | 13,602.43 | 14,481.35 | 3,129.06 |
| Shaba | Pound | - | 3,761,086.16 | 3,352,630.00 | 6,827,930.74 | 5,285,443.13 | 1,654,151.00 |
| chuma | Tani | - | 28,431.17 | 78,190.00 | 51,071.14 | 67,626.44 | 66,497.87 |
| Bauxite | Tani | - | 25,995.00 | 38,142.00 | 40,920.98 | 61,353.23 | 79,147.89 |
| Kinywe | Tani | - | - | - | - | - | 41,431.27 |
| $CO_2$ (ToL) | Kg | - | - | - | - | - | 17,780,132.68 |
| Madini ya Ujenzi | 000 Tani | 20,188.47 | 31,891.75 | 32,304.00 | 37,498.03 | 33,807.05 | 33,302.72 |
| Madini mengine ya viwandani | 000 Tani | - | 2,160.57 | 1,037.00 | 1,458.38 | 1,745.02 | 1,662.69 |
| Madini mengine ya metali | 000 Tani | - | - | - | 93.41 | 63.55 | 33.96 |
| Makinikia ya Shaba | Tani | - | 33,377.08 | - | 2,013.26 | 5,926.27 | 30,164.91 |
| Mbale za shaba (Copper ore) | Tani | - | 1,204.84 | - | 6,623.58 | 6,307.01 | 17,615.66 |

**Chanzo:** Wizara ya Madini

Carat = 0.205 gm

**Jedwali Na. 52: MADINI YALIYOPATA KIBALI CHA KUUZWA NJE YA NCHI**

| Aina ya Madini | Kipimo | Kiasi | | | | Thamani ('000 "USD) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Almasi (Rough) | 000 Karati | 47,337 | 326 | 194 | 373.17 | 8,473 | 65,903 | 31,474 | 59,243 |
| Dhahabu | 000 Gramu | 42,902 | 62,512 | 62,781 | 59,471 | 2,831,840 | 2,850,345 | 3,021,627 | 3,431,080 |
| Vito - Ghafi | 000 Gramu | 4,463,669 | 15,017,635 | 98,891,510 | 207,735,738 | 16,501 | 19,415 | 28,456 | 21,199 |
| Vito - Vilivyochongwa na kusanifiwa | Karati | 166,728 | 93,351 | 101,153 | 64,493 | 7,425 | 2,480 | 2,622 | 1,916 |
| Chumvi | Tani | 21,095 | 22,225 | 34,350 | 27,298 | 2,360 | 2,375 | 3,509 | 3,237 |
| Phosphate | Tani | 15,632 | 40,710 | 9,934 | 10,953 | 3,442 | 6,944 | 3,646 | 2,997 |
| Bati | Tani | 155 | 564 | 440 | 408 | 4,603 | 12,505 | 7,061 | 6,941 |
| Jasi | Tani | 9,129 | 8,300 | 10,486 | 22,575 | 936 | 941 | 1,802 | 3,895 |
| Kinywe | Tani | 2,887 | 7,271 | 13,475 | 38,140 | 1,264 | 2,909 | 5,394 | 22,693 |
| Fedha | 000 Gramu | 10,532 | 802 | 1,214 | 1,067 | 9,284 | 629 | 886 | 1,141 |
| Shaba | 000 Lb | 4,081 | 6,993 | 4,156 | 3 | 4,293 | 3,879 | 2,273 | 0.012 |
| Makinikia ya shaba | Tani | 16,679 | 26,591 | 25,688 | 35,098 | 121,871 | 189,648 | 179,044 | 245,198 |
| Makinikia ya dhahabu | Tani | - | 2,730 | 2,554 | 3,917 | - | 8,993 | - | 10,886 |
| Bauxite | Tani | 12,570 | 14,790 | 14,430 | 4,520 | 630 | 758 | 795 | 660 |
| makaa ya mawe | Tani | 346,779 | 848,434 | 1,601,850 | 995,646 | 11,838 | 43,806 | 158,575 | 70,284 |
| Madini ujenzi | Tani | 57,469 | 66,667 | 46,544 | 44,119 | 1,070 | 2,410 | 3,105 | 3,604 |
| Mawe ya chokaa | Tani | - | 194,980 | 249,396 | 217,072 | 1,944 | 1,806 | 6,344 | 2,281 |
| Madini ya metali | Tani | 6,965 | 32,113 | 34,462 | 18,438 | 6,411 | 21,500 | 30,948 | 21,817 |
| Madini ya Viwandani* | Tani | 16,715 | 34,042 | 28,636 | 27,846 | 9,108 | 6,961 | 3,266 | 6,597 |
| **Jumla** | | | | | | **3,043,293** | **3,244,207** | **3,490,827** | **3,915,669** |

**Chanzo:** Wizara ya Madini
* Takwimu zimeboreshwa

## SURA YA 10

## VIWANDA NA BIASHARA

**Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani**

238. Mwaka 2024, thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani iliongezeka kwa asilimia 4.9 na kufikia shilingi bilioni 27,725.7 kutoka shilingi bilioni 26,438.5 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea na jitihada za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa uliongezeka ikiwemo, konyagi kwa asilimia 35.1, bia (asilimia 29.7), tabaka za mbao (asilimia 27.5), chuma (asilimia 13.8), bati (asilimia 5.7), rangi (asilimia 2.6) na unga wa ngano (asilimia 2.2). Kwa upande mwingine, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani zilikuwa shilingi bilioni 12,039.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11,790.7 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Hii ilitokana na ongezeko la bei za baadhi ya malighafi zilizotumika katika uzalishaji viwandani ambazo ziliagizwa kutoka nje ya nchi.

**Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

239. Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo - SIDO lilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 24,197 mwaka 2024 ikilinganishwa na wajasiriamali 22,139 waliopata mafunzo mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Hii ilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali ambao ulichangia kuongezeka kwa mwitikio wa wananchi kujishughulisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu: usindikaji wa mafuta ya kula na vyakula vya mifugo; utengenezaji wa bidhaa za ngozi, chaki na vibuyu; ubanguaji korosho na uhifadhi na usindikaji vyakula; mbinu za uzalishaji mali na biashara; utunzaji wa vitabu vya hesabu; na uongozi wa vikundi/vyama vya wajasiriamali.

240. Mwaka 2024, Vituo vya Uendelezaji Teknolojia - TDCs vilivyopo chini ya SIDO vilitengeneza na kusambaza mashine 917 ikilinganishwa na mashine 878 zilizotengenezwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mashine za uchakataji wa mazao ya kilimo, mifugo, madini, misitu na uvuvi. Aidha, katika kuwaendeleza wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya, wajasiriamali saba (7) walipata mafunzo ya kukuza vipaji vyao mwaka 2024 ikilinganishwa na wajasiriamali nane (8) waliopata mafunzo mwaka 2023. Vilevile, wajasiriamali 32,198 walipatiwa ushauri wa kiufundi na biashara mwaka 2024 ikilinganishwa na wajasiriamali 29,640 waliopatiwa ushauri mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Hii ilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali ambao ulichangia kuongezeka kwa mwitikio wa wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujasiriamali kwa lengo la kujiongezea kipato na kukabiliana na changamoto za ajira.

241. Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali - NEDF ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8 kwa wajasiriamali 1,811 mwaka 2024

ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.4 zilizotolewa kwa wajasiriamali 2,038 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 11.1 wa mikopo iliyotolewa. Upungufu huo ulitokana na uelewa mdogo wa matumizi ya mfumo mpya wa kielektroniki wa maombi ya mikopo. Aidha, hali ya marejesho ya mikopo iliendelea kuimarika na kufikia asilimia 92.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 92.1 mwaka 2023. Kwa upande mwingine, mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 3,727 mwaka 2024 ikilinganishwa na fursa za ajira 4,532 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 17.8.

242. Mwaka 2024, Chuo cha Elimu ya Biashara - CBE kilitoa mafunzo ya kozi 35 za muda mfupi zinazohusu elimu ya biashara katika fani mbalimbali kwa washiriki 1,511 ikilinganishwa na kozi 33 za muda mfupi kwa washiriki 305 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kozi za muda mfupi katika nyanja za biashara kulikochangiwa na ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini.

243. Mwaka 2024, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO lilifanya tafiti tano (5) ikilinganishwa na tafiti saba (7) zilizofanyika mwaka 2023. Tafiti hizo ni: uibuaji wa fursa za uwekezaji kupitia *industrial mapping*; matumizi ya malighafi bioanuwai kutengeneza mkaa mbadala; matumizi ya vumbi la makaa ya mawe kutengeneza mkaa mbadala; matumizi bora ya nishati; na usanifu na utengenezaji wa jiko sanifu (Eco-carbonizer) kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa mbadala. Kwa upande mwingine, TIRDO ilifanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika viwanda 17 mwaka 2024 ikilinganishwa na viwanda 18 mwaka 2023. Aidha, TIRDO ilipima sampuli 549 za maabara mwaka 2024 ikilinganishwa na sampuli 188 mwaka 2023. Ongezeko la sampuli zilizopimwa lilitokana na kuboreshwa kwa huduma za maabara na utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

244. Mwaka 2024, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC kiliboresha, kuzalisha na kununua aina 83 za zana za kilimo na teknolojia vijijini ikilinganishwa na aina 338 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, CAMARTEC ilifanya ukaguzi na majaribio ya modeli 87 za zana za kilimo zilizozalishwa nje ya nchi ikilinganishwa na ukaguzi na majaribio ya modeli 82 mwaka 2023. Aidha, CAMARTEC ilitoa mafunzo kuhusu ubanguaji korosho na matumizi ya teknolojia na mashine mbalimbali kwa vijana 204 ikilinganishwa na vijana 63 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilichangiwa na utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwenye Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (KITEKI) katika kijiji cha Mwandete kilichopo Wilaya ya Maswa.

245. Mwaka 2024, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania - TEMDO ilisanifu teknolojia 12 zilizowezesha uzalishaji wa mashine tano (5) kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikilinganishwa na teknolojia tisa (9) zilizosanifiwa na kutengeneza mashine nne (4) mwaka 2023. Aidha, TEMDO iliunda na kusimika mtambo mkubwa wa kusafisha

mafuta ya alizeti na majokofu nane (8) kwa ajili ya kuhifadhia maiti katika hospitali mbalimbali. Vilevile, TEMDO ilitoa huduma za kihandisi kwa viwanda vitano (5) na kampuni tano (5) za uchimbaji madini Mkoani Geita.

**Usajili wa Biashara na Viwanda**

246. Mwaka 2024, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA ilisajili kampuni 16,748 ikilinganishwa na kampuni 15,397 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Katika kipindi hicho, majina ya biashara 30,753 yalisajiliwa ikilinganishwa na majina ya biashara 29,448 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.4. Aidha, leseni 20,364 za biashara daraja "A" zilitolewa mwaka 2024 ikilinganishwa na leseni 18,448 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Vilevile, BRELA ilitoa leseni 371 za viwanda mwaka 2024 ikilinganishwa na leseni 253 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 46.6. Ongezeko la usajili na utoaji wa leseni lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo: uwepo wa huduma ya kliniki ya biashara; matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa leseni; na utoaji wa mafunzo kwa maafisa biashara na elimu kwa umma.

247. Mwaka 2024, BRELA ilisajili alama 3,662 za biashara na huduma ikilinganishwa na alama 3,829 za biashara na huduma zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 4.4. Aidha, BRELA ilipokea na kufanyia kazi maombi 597 ya kuwekea ulinzi uvumbuzi wa sayansi na teknolojia mwaka 2024 ikilinganishwa na maombi 538 yaliyopokelewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 11.0. Kati ya hayo, maombi 108 yalikuwa ya ndani na maombi 489 yalipitia Shirika la Kanda la Afrika linalosimamia Haki Miliki za Kitaaluma - ARIPO.

**Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa**

248. Mwaka 2024, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - TanTrade iliratibu Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo kampuni 3,954 zilishiriki katika maonesho hayo ikilinganishwa na kampuni 3,500 zilizoshiriki mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Kati ya hizo, kampuni 3,503 zilikuwa za ndani na kampuni 451 kutoka nje ya nchi. Aidha, nchi 28 zilishiriki katika maonesho ya mwaka 2024 ikilinganishwa na nchi 19 mwaka 2023. Mauzo katika maonesho hayo yalikuwa shilingi bilioni 3.6 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 2.8 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Vilevile, kampuni za ndani zilipata fursa ya kuuza tani 20,000 za katani na tani 20,000 za mihogo zenye thamani ya shilingi bilioni 6.0 kwenye soko la China. Ajira za muda mfupi takribani 21,518 zilipatikana katika maonesho ya mwaka 2024 ikilinganishwa na ajira 11,869 mwaka 2023.

249. Mwaka 2024, TanTrade iliratibu ushiriki wa kampuni na taasisi 464 za Tanzania katika majukwaa 14 ya kimataifa ya kibiashara yaliyoandaliwa nje ya nchi kwa lengo la

kutangaza bidhaa, kuongeza masoko, na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara katika nchi mbalimbali. Kupitia maonesho hayo, Tanzania ilipata mauzo ya papo kwa papo ya shilingi bilioni 2.17 na miadi ya biashara ya shilingi bilioni 1.93. Aidha, mikataba ya biashara yenye thamani ya shilingi bilioni 17.0 inayojumuisha makubaliano ya kuuza asali na bidhaa za kilimo na viwanda katika masoko ya nje ilisainiwa. Kwa upande mwingine, TanTrade ilitekeleza programu 13 za mafunzo kwa wafanyabiashara 3,050, ikilinganishwa na programu 17 kwa wafanyabiashara 2,150 mwaka 2023.

250. Mwaka 2024, TanTrade kwa kushirikiana na taasisi wezeshi za biashara iliendelea kuratibu kliniki ya biashara kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara kutatua changamoto na kuboresha biashara zao. Kupitia kliniki hiyo, wafanyabiashara 986 walihudumiwa, ambapo changamoto 191 zilitatuliwa, kampuni 137 zilisajiliwa na kampuni 79 zilielimishwa kuhusu taratibu za kodi. Aidha, kampuni 148 zilipata mafunzo kuhusu mbinu bora za uzalishaji, alama za ubora, ufungashaji, pamoja na ushauri wa kitaalamu kuhusu mashine za uzalishaji, vifungashio, mikopo, na masoko. Vilevile, wafanyabiashara 45 waliunganishwa na masoko ya kitaifa na kimataifa. Kadhalika, kampuni tano (5) za Tanzania ziliunganishwa na kampuni kutoka Pakistani kwa ajili ya kuuza tani 300 za maharage.

251. Mwaka 2024, TanTrade iliendelea kukusanya na kusambaza taarifa za biashara kwa wafanyabiashara 146,888 kupitia TanTrade Biashara App, tovuti ya mamlaka, na mitandao ya kijamii ikilinganishwa na wafanyabiashara 107,943 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 36.1. Katika kipindi hicho, kanzidata ya wafanyabiashara iliboreshwa ambapo kampuni mpya 483 zilisajiliwa ikilinganishwa na kampuni 137 zilizosajiliwa mwaka 2023.

**Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo**

252. Mwaka 2024, Shirika la Viwango Tanzania - TBS liliandaa viwango 571 vya ubora ikilinganishwa na viwango 627 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Katika kipindi hicho, sampuli 38,724 zilipimwa ikilinganishwa na sampuli 28,791 zilizopimwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 34.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mwitikio wa wazalishaji na watumiaji wa bidhaa katika kuzingatia ubora na usalama wa bidhaa. Aidha, vifaa 9,653 vilifanyiwa uhakiki/ugezi mwaka 2024 ikilinganishwa na vifaa 10,564 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 8.6. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa muda wa kufanya ugezi kutoka mwaka mmoja hadi miaka miwili kulingana na matumizi ya kifaa husika.

253. Mwaka 2024, Shirika lilitoa leseni 534 za ubora ikilinganishwa na leseni 733 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 27.1. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya wajasiriamali kutokamilisha mchakato wa upatikanaji wa leseni ya nembo ya ubora pamoja na mwitikio mdogo wa ukaguzi wa awali kwa ajili ya kupatiwa leseni. Kati ya

leseni hizo, leseni 315 zilitolewa kwa wazalishaji wakubwa na wa kati, na leseni 219 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo. Aidha, mafunzo ya aina 81 ya udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 3,052 mwaka 2024 ikilinganishwa na mafunzo ya aina 73 yaliyotolewa kwa washiriki 2,194 mwaka 2023. Ongezeko la washiriki lilitokana na mwitikio mkubwa wa wadau kupata mafunzo ya viwango, ubora na usalama, upimaji na ugezi.

254. Mwaka 2024, Shirika lilisajili bidhaa 1,748 za chakula na vipodozi ikilinganishwa na bidhaa 1,623 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Hii ilitokana na utayari wa wafanyabiashara wa bidhaa za chakula na vipodozi kusajili bidhaa zao. Kati ya bidhaa hizo, bidhaa za chakula zilikuwa 1,370 na bidhaa za vipodozi zilikuwa 378. Aidha, Shirika lilisajili na kutoa vibali 9,963 vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji, na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi ikilinganishwa na vibali 9,775 vilivyotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Kati ya hivyo, vibali 7,900 vilikuwa vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vibali 2,063 kwa ajili ya bidhaa za vipodozi.

255. Mwaka 2024, Shirika lilikagua magari 45,697 yaliyotumika ikilinganishwa na magari 48,075 yaliyokaguliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Kati ya hayo, magari 904, sawa na asilimia 2.0 hayakukidhi viwango vya ubora na hivyo kufanyiwa maboresho. Aidha, bidhaa 78,073 zilikaguliwa kupitia mfumo wa ukaguzi bidhaa baada ya kuwasili nchini ikilinganishwa na bidhaa 62,796 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 24.3. Kati ya hizo, bidhaa 3,066, sawa na asilimia 3.9 hazikukidhi matakwa ya viwango vya ubora ambapo wamiliki wa bidhaa hizo walielekezwa kuziharibu au kuzirudisha kwenye nchi zilipotoka. Vilevile, bidhaa 34,589 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa kupitia mawakala wa Shirika kabla ya kuingizwa nchini mwaka 2024 ikilinganishwa na bidhaa 37,826 zilizokaguliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 9.4. Kati ya hizo, bidhaa 338 hazikukidhi matakwa ya viwango vya ubora na hivyo kuzuiwa kuingia nchini.

256. Mwaka 2024, Wakala wa Vipimo - WMA ilihakiki vipimo 981,397 ikilinganishwa na vipimo 971,541 vilivyohakikiwa mwaka 2023. Aidha, Wakala ilifanya kaguzi za kushtukiza 4,229 za vipimo vinavyotumika kwenye biashara, afya, usalama na mazingira ikilinganishwa na kaguzi 5,445 zilizofanyika mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 22.3. Vilevile, Wakala ilipima aina mpya 236 za vipimo kutoka ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na vipimo 214 vilivyopimwa mwaka 2023. Kati ya hivyo, vipimo 173 sawa na asilimia 73.3 viliidhinishwa na vipimo 63 havikuidhinishwa.

257. Mwaka 2024, Wakala ulitoa leseni na vibali 533 kwa mafundi wanaojihusisha na uundaji, usimikaji na urekebishaji wa vipimo ikilinganishwa na leseni na vibali 447 vilivyotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Hii ilitokana na kuendelea

kutolewa kwa elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na vibali na leseni. Katika kipindi hicho, meli 174 zenye ujazo wa lita milioni 9,302.90 za mafuta ya kupikia, petroli na dizeli zilihakikiwa ikilinganishwa na meli 147 zenye ujazo wa lita milioni 8,547.52 zilizohakikwa mwaka 2023. Kati ya hizo, lita milioni 176.12 zilikuwa za mafuta ya kupikia na lita milioni 9,126.78 za mafuta ya dizeli na petroli.

**Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia**

258. Mwaka 2024, Tume ya Ushindani - FCC iliidhinisha maombi ya muungano wa kampuni 56 ikilinganishwa na maombi ya kampuni 54 mwaka 2023. Maombi hayo yalitoka katika sekta za kilimo, uzalishaji viwandani, fedha, afya, mawasiliano, madini, biashara na nishati. Aidha, Tume ilisajili mikataba 68 ya walaji iliyoandaliwa na upande mmoja mwaka 2024 ikilinganishwa na mikataba 48 iliyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 41.7. Hii ilitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu kuhusu umuhimu wa kusajili mikataba kwa ajili ya kumlinda mlaji.

259. Mwaka 2024, Tume ilikagua makasha 6,357 ya kusafirishia mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na bandari kavu ikilinganishwa na makasha 6,909 yaliyokaguliwa mwaka 2023. Kati ya hayo, makasha 452 yenye thamani ya shilingi bilioni 17.9 yalibainika kuwa na bidhaa bandia ambazo ziliteketezwa. Bidhaa bandia zilizobainika zilikuwa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, vipuri vya pikipiki na magari, shajala pamoja na vifaa vya kielektroniki.

260. Mwaka 2024, Baraza la Ushindani - FCT lilipokea mashauri 14 ikilinganishwa na mashauri 56 yaliyopokelewa mwaka 2023. Kati ya hayo, mashauri 10 yaliamuliwa ikilinganishwa na mashauri 37 yaliyoamuliwa mwaka 2023. Mashauri hayo yalitoka kwa wazalishaji, wasambazaji na walaji katika sekta za nishati, maji, mawasiliano, usafirishaji wa anga na nchi kavu.

**Shirika la Maendeleo la Taifa**

261. Mwaka 2024, Shirika la Maendeleo la Taifa - NDC kupitia mradi wa mashamba ya mpira ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) lilizalisha tani 63.2 za zao la mpira ikilinganishwa na tani 95.3 za mpira zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 33.7. Upungufu huo ulitokana na mvua nyingi zilizoathiri uzalishaji wa zao la mpira. Katika kipindi hicho, Kiwanda cha Kuzalisha Dawa za Kibaiolojia kilizalisha lita 269,673 za viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya aina mbalimbali za mbu, hususan wanaoeneza malaria ikilinganishwa na lita 65,202 zilizozalishwa mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuanza ununuzi wa viuadudu kwa ajili ya kusambaza kwa halmashauri 57 nchini zenye maambukizi makubwa ya ugonjwa wa malaria. Aidha, uzalishaji huo uliwezesha mauzo ya viuadudu ya shilingi bilioni 4.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi milioni 771.9 mwaka 2023.

262. Mwaka 2024, Shirika la Maendeleo la Taifa - NDC kupitia kiwanda cha kuzalisha mashine na vipuri - KMTC lilizalisha mashine 12 na vipuri 37 ikilinganishwa na mashine 6 na vipuri 25 vilivyozalishwa mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho yaliyofanywa na Serikali katika kiwanda hicho na hivyo kuwezesha kuongeza uzalishaji. Aidha, jumla ya shilingi milioni 157.2 zilipatikana kutokana na mauzo ya mashine na vipuri mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi milioni 62.0 mwaka 2023.

**Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala**

263. Mwaka 2024, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ilitoa leseni 195 ikilinganishwa na leseni 176 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Kati ya hizo, leseni 190 zilikuwa za waendesha ghala na leseni tano (5) za meneja dhamana. Aidha, leseni zilizotolewa zilihusisha mazao ya muhogo mkavu, maharage, karanga, mahindi, mpunga, mchele, mtama, kahawa, kakao, mbaazi, soya, ufuta na korosho. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji kuhusu matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala na kuimarishwa kwa sheria, kanuni na taratibu kuhusu mfumo wa stakabadhi ghalani. Vilevile, tani 696,756.0 za mazao mbalimbali zilihifadhiwa kwenye ghala zilizopewa leseni mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 457,195.3 zilizohifadhiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 52.4. Hii ilitokana na uhamasishaji wa matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa wadau na hivyo kuongeza mwitikio wa wananchi kuhifadhi mazao.

**Jedwali Na. 53: MATUMIZI YA SARUJI NCHINI (Tani)**

| Mwaka | Kutoka Nje | Uuzaji nje | Uzalishaji wa ndani | Matumizi | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2007 | 101,827 | 52,170 | 1,629,890 | 1,679,547 | 10.9 |
| 2008 | 356,468 | 99,688 | 1,755,862 | 2,012,642 | 19.8 |
| 2009 | 516,182 | 57,569 | 1,940,845 | 2,399,458 | 19.2 |
| 2010 | 566,828 | 189,321 | 2,312,055 | 2,689,562 | 12.1 |
| 2011 | 768,343 | 217,944 | 2,408,765 | 2,959,164 | 10.0 |
| 2012 | 1,013,986 | 145,793 | 2,557,798 | 3,425,991 | 15.8 |
| 2013 | 1,218,453 | 154,481 | 2,369,819 | 3,433,791 | 0.2 |
| 2014 | 1,428,995 | 142,001 | 2,795,687 | 4,082,681 | 18.9 |
| 2015 | 896,872 | 129,083 | 3,140,160 | 4,404,187 | 7.9 |
| 2016 | 513,307 | 253,506 | 4,047,712 | 4,307,513 | (2.2) |
| 2017 | 188,599 | 226,588 | 4,397,684 | 4,359,695 | 1.2 |
| 2018 | 341,179 | 196,449 | 4,540,309 | 4,685,039 | 7.5 |
| 2019 | 448,579 | 410,607 | 5,290,878 | 5,328,850 | 13.7 |
| 2020 | 716,929 | 493,867 | 5,605,626 | 5,828,688 | 9.4 |
| 2021 | 690,474 | 441,828 | 6,614,359 | 6,863,005 | 17.7 |
| 2022 | 566,826 | 632,726 | 7,598,073 | 7,532,173 | 9.8 |
| 2023 | 809,199 | 531,699 | 7,673,016 | 7,950,515 | 5.6 |
| 2024 | 398,039 | 391,961 | 7,699,840 | 7,705,918 | (3.1) |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mapato Tanzania

## Jedwali Na. 54: UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti & tambi | Tani | 19,204 | 15,890 | 16,451 | 16,911 | 18,113 | 22,430 | 30,154 | 29,653 | 27,509 | 26,612 |
| Unga wa ngano | Tani | 533,257 | 498,940 | 606,432 | 662,967 | 680,393 | 767,476 | 737,652 | 684,708 | 839,266 | 858,021 |
| Konyagi | 000 Lita | 29,491 | 28,754 | 25,555 | 29,335 | 32,366 | 33,287 | 22,066 | 22,489 | 31,024 | 41,903 |
| Bia | 000 Lita | 386,310 | 383,251 | 396,864 | 412,555 | 391,299 | 385,851 | 380,464 | 456,035 | 498,611 | 646,552 |
| Chibuku | 000 Lita | 23,028 | 26,513 | 22,624 | 20,819 | 20,350 | 21,712 | 22,256 | 24,366 | 23,757 | 23,288 |
| Sigara | Milioni | 7,837 | 8,091 | 7,412 | 7,921 | 8,369 | 7,320 | 7,021 | 12,201 | 11,868 | 9,928 |
| Nguo | 000 $M^2$ | 100,496 | 76,436 | 52,052 | 52,613 | 45,415 | 53,067 | 65,365 | 48,504 | 39,774 | 31,712 |
| Kamba za katani | Tani | 8,851 | 9,216 | 8,188 | 8,148 | 9,287 | 8,187 | 8,583 | 6,171 | 5,093 | 4,846 |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 311 | 312 | 196 | 228 | 254 | 261 | 273 | 461 | 604 | 411 |
| Tabaka za mbao | $M^3$ | 36,317 | 34,983 | 37,302 | 37,849 | 42,563 | 34,237 | 29,867 | 25,305 | 17,788 | 22,688 |
| Dawa za pareto | Tani | 118 | 126 | 134 | 139 | 145 | 154 | 152 | 173 | 325 | 239 |
| Rangi | 000 Lita | 38,372 | 35,096 | 40,146 | 47,928 | 58,024 | 48,261 | 62,785 | 64,028 | 75,423 | 77,364 |
| Saruji | 000 Tani | 3,135 | 4,572 | 4,398 | 4,766 | 6,514 | 6,496 | 6,531 | 7,598 | 7,673 | 7,700 |
| Chuma | Tani | 205,575 | 219,765 | 231,591 | 275,267 | 272,531 | 277,785 | 293,797 | 311,781 | 343,575 | 391,100 |
| Bati | Tani | 91,385 | 91,421 | 84,541 | 84,132 | 100,963 | 107,836 | 119,844 | 129,038 | 118,767 | 125,555 |
| Betri | Milioni | 87 | 69 | 122 | 115 | 120 | 132 | - | - | - | - |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara
- Hakuna uzalishaji

## Jedwali Na. 55: VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Walioajiriwa | | | | Wengine | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021* | 2022* | 2023* | 2024* | 2021* | 2022* | 2023* | 2024* | 2021* | 2022* | 2023* | 2024* |
| 10 | Vyakula | 110,456 | 113,772 | 128,606 | 131,873 | 17,154 | 17,128 | 25,189 | 25,813 | 127,610 | 130,900 | 153,795 | 157,686 |
| 11 | Vinywaji | 10,406 | 10,718 | 37,026 | 38,399 | 68 | 68 | 7,758 | 7,950 | 10,474 | 10,786 | 44,784 | 46,349 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 7,637 | 7,866 | 7,501 | 7,470 | 5 | 5 | 2,104 | 2,156 | 7,642 | 7,871 | 9,605 | 9,626 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 55,262 | 56,921 | 43,938 | 45,670 | 16,902 | 16,876 | 2,455 | 2,516 | 72,164 | 73,797 | 46,393 | 48,186 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 2,331 | 2,401 | 7,116 | 6,696 | 253 | 301 | 782 | 559 | 2,584 | 2,702 | 7,898 | 7,255 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 12,319 | 12,689 | 8,474 | 9,838 | 1,765 | 1,762 | 1,555 | 1,602 | 14,084 | 14,451 | 10,029 | 11,440 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 8,202 | 8,448 | 10,752 | 9,032 | 161 | 161 | 468 | 754 | 8,363 | 8,609 | 11,220 | 9,786 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 10,940 | 11,268 | 19,982 | 20,661 | 181 | 221 | 3,317 | 2,538 | 11,121 | 11,489 | 23,299 | 23,199 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 6,449 | 6,643 | 11,279 | 11,201 | 45 | 63 | 1,149 | 1,086 | 6,494 | 6,706 | 12,428 | 12,287 |
| 23 | Bidhaa Nyingine za Madini zisizo za metali | 13,004 | 13,394 | 14,407 | 13,528 | 1,032 | 1,030 | 2,852 | 3,614 | 14,036 | 14,424 | 17,259 | 17,142 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 57,297 | 59,017 | 35,548 | 45,509 | 13,746 | 13,725 | 2,290 | 2,810 | 71,043 | 72,742 | 37,838 | 48,319 |
| | Jumla | 294,303 | 303,137 | 324,629 | 339,877 | 51,312 | 51,340 | 49,919 | 51,398 | 345,615 | 354,477 | 374,548 | 391,275 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 56: VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Mishahara (Shilingi Milioni) | | | Malipo Mengine (Shilingi Milioni) | | | Jumla (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* |
| 10 | Vyakula | 638,276 | 708,073 | 729,315 | 116,855 | 107,197 | 108,269 | 755,131 | 815,270 | 837,584 |
| 11 | Vinywaji | 391,173 | 433,949 | 464,325 | 166,249 | 152,508 | 153,118 | 557,422 | 586,457 | 617,443 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 174,246 | 193,300 | 192,267 | 48,731 | 44,703 | 43,771 | 222,977 | 238,003 | 236,038 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 194,154 | 215,385 | 239,385 | 102,478 | 94,008 | 98,196 | 296,632 | 309,393 | 337,581 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 11,033 | 12,239 | 11,751 | 1,115 | 1,022 | 973 | 12,148 | 13,261 | 12,724 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 51,360 | 56,976 | 58,400 | 7,272 | 6,672 | 7,912 | 58,632 | 63,648 | 66,312 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 93,328 | 103,534 | 99,022 | 20,693 | 18,983 | 17,902 | 114,021 | 122,517 | 116,924 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 126,700 | 140,556 | 141,779 | 19,800 | 18,164 | 18,340 | 146,500 | 158,720 | 160,119 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 65,110 | 72,230 | 71,247 | 9,574 | 8,782 | 8,579 | 74,684 | 81,012 | 79,826 |
| 23 | Bidhaa Nyingine za Madini zisizo za metali | 171,514 | 190,269 | 189,752 | 51,985 | 47,688 | 46,551 | 223,499 | 237,957 | 236,303 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 282,944 | 313,884 | 316,615 | 58,882 | 54,015 | 56,371 | 341,826 | 367,899 | 372,986 |
| | **Jumla** | **2,199,838** | **2,440,395** | **2,513,858** | **603,634** | **553,742** | **559,982** | **2,803,472** | **2,994,137** | **3,073,840** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 57: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO

| ISIC Rev.4 | Shughuli | PATO (Shilingi Milioni) | | | GHARAMA (Shilingi Milioni) | | | Thamani iliyoongezeka (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* |
| 10 | Vyakula | 9,685,138 | 10,228,274 | 10,793,951 | 4,451,126 | 4,534,228 | 4,754,349 | 5,234,012 | 5,694,046 | 6,039,602 |
| 11 | Vinywaji | 3,994,134 | 4,218,122 | 4,883,542 | 1,195,985 | 1,218,315 | 1,325,629 | 2,798,149 | 2,999,807 | 3,557,913 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 1,500,925 | 1,585,095 | 1,669,632 | 376,689 | 383,722 | 581,421 | 1,124,236 | 1,201,373 | 1,088,211 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 1,172,020 | 1,237,746 | 1,347,879 | 536,538 | 546,555 | 686,180 | 635,482 | 691,191 | 661,699 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 131,543 | 138,920 | 157,123 | 89,298 | 90,965 | 72,211 | 42,245 | 47,955 | 84,912 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 356,088 | 376,057 | 417,660 | 118,120 | 120,325 | 101,906 | 237,968 | 255,732 | 315,754 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 643,736 | 679,837 | 717,855 | 398,603 | 406,045 | 404,498 | 245,133 | 273,792 | 313,357 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 1,409,976 | 1,489,048 | 1,496,829 | 882,297 | 898,770 | 994,008 | 527,679 | 590,278 | 502,821 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 1,448,313 | 1,529,533 | 1,455,808 | 936,479 | 953,963 | 988,276 | 511,834 | 575,570 | 467,532 |
| 23 | Bidhaa Nyingine za Madini zisizo za metali | 1,849,354 | 1,953,064 | 1,779,275 | 938,535 | 956,057 | 902,970 | 910,819 | 997,007 | 876,305 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 2,843,313 | 3,002,764 | 3,006,193 | 1,650,951 | 1,681,774 | 1,227,743 | 1,192,361 | 1,320,990 | 1,778,450 |
| | **Jumla** | **25,034,540** | **26,438,460** | **27,725,747** | **11,574,622** | **11,790,719** | **12,039,191** | **13,459,918** | **14,647,741** | **15,686,556** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

## Jedwali Na. 58: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA

| Jina la Mkoa | Idadi ya Wafanyakazi | | | Idadi ya waajiriwa | | | Mishahara (Shilingi Milioni) | | | Thamani Iliyoongezeka (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* | 2022* | 2023* | 2024* |
| Dodoma | 3,836 | 4,053 | 5,851 | 3,280 | 3,512 | 5,060 | 27,527 | 30,537 | 43,440 | 168,432 | 183,296 | 272,330 |
| Arusha | 30,085 | 31,789 | 32,262 | 25,728 | 27,552 | 28,281 | 93,464 | 103,684 | 108,870 | 571,877 | 622,345 | 669,528 |
| Kilimanjaro | 22,590 | 23,870 | 24,297 | 19,319 | 20,689 | 20,968 | 118,386 | 131,332 | 131,440 | 724,363 | 788,285 | 823,995 |
| Tanga | 17,053 | 18,019 | 18,851 | 14,584 | 15,618 | 16,516 | 147,525 | 163,657 | 177,039 | 902,652 | 982,310 | 1,088,740 |
| Morogoro | 53,440 | 56,466 | 56,833 | 45,699 | 48,939 | 49,811 | 62,588 | 69,432 | 69,785 | 382,941 | 416,735 | 437,465 |
| Pwani | 16,634 | 17,576 | 18,673 | 14,226 | 15,235 | 16,147 | 88,796 | 98,507 | 106,800 | 543,307 | 591,254 | 656,779 |
| Dar es Salaam | 114,376 | 120,853 | 121,564 | 97,809 | 104,744 | 105,110 | 1,263,154 | 1,401,282 | 1,388,597 | 7,728,724 | 8,410,776 | 8,705,004 |
| Lindi | 1,706 | 1,802 | 2,482 | 1,461 | 1,565 | 2,174 | 561 | 622 | 884 | 3,439 | 3,741 | 5,448 |
| Mtwara | 4,946 | 5,225 | 6,044 | 4,229 | 4,529 | 5,228 | 20,947 | 23,238 | 26,490 | 128,162 | 139,472 | 166,058 |
| Ruvuma | 3,191 | 3,372 | 3,464 | 2,729 | 2,923 | 2,996 | 4,223 | 4,684 | 4,911 | 25,848 | 28,129 | 30,217 |
| Iringa | 8,505 | 8,987 | 9,421 | 7,273 | 7,788 | 8,148 | 49,967 | 55,431 | 57,263 | 305,725 | 332,705 | 358,974 |
| Mbeya | 10,186 | 10,763 | 11,356 | 8,710 | 9,327 | 9,953 | 101,656 | 112,773 | 123,104 | 621,992 | 676,882 | 757,044 |
| Singida | 3,941 | 4,164 | 4,898 | 3,371 | 3,610 | 4,292 | 3,656 | 4,056 | 4,762 | 22,365 | 24,339 | 29,847 |
| Tabora | 1,256 | 1,327 | 2,045 | 1,072 | 1,148 | 1,793 | 20,163 | 22,368 | 35,737 | 123,369 | 134,256 | 219,769 |
| Rukwa | 2,626 | 2,774 | 3,063 | 2,244 | 2,403 | 2,649 | 11,647 | 12,922 | 14,065 | 71,259 | 77,548 | 88,167 |
| Kigoma | 3,195 | 3,376 | 4,335 | 2,733 | 2,927 | 3,748 | 1,962 | 2,176 | 2,850 | 12,011 | 13,071 | 17,541 |
| Shinyanga | 4,698 | 4,964 | 5,951 | 4,019 | 4,304 | 5,143 | 20,028 | 22,218 | 26,217 | 122,537 | 133,351 | 164,344 |
| Kagera | 6,122 | 6,469 | 6,859 | 5,236 | 5,607 | 5,925 | 9,326 | 10,344 | 11,182 | 57,055 | 62,091 | 68,770 |
| Mwanza | 18,748 | 19,810 | 20,703 | 16,032 | 17,168 | 17,888 | 117,093 | 129,898 | 133,647 | 716,445 | 779,671 | 837,823 |
| Mara | 6,006 | 6,345 | 6,806 | 5,137 | 5,501 | 5,886 | 10,232 | 11,351 | 12,424 | 62,597 | 68,121 | 76,392 |
| Manyara | 8,736 | 9,230 | 9,561 | 7,471 | 8,000 | 8,267 | 4,871 | 5,404 | 5,514 | 29,809 | 32,440 | 34,573 |
| Njombe | 4,676 | 4,940 | 5,879 | 4,000 | 4,284 | 5,084 | 9,297 | 10,314 | 12,521 | 56,889 | 61,909 | 77,003 |
| Katavi | 2,423 | 2,560 | 3,401 | 2,072 | 2,219 | 2,980 | 2,000 | 2,219 | 2,942 | 12,235 | 13,315 | 18,440 |
| Simiyu | 2,978 | 3,147 | 3,317 | 2,546 | 2,725 | 2,907 | 7,466 | 8,283 | 9,040 | 45,690 | 49,722 | 55,599 |
| Geita | 1,023 | 1,081 | 1,574 | 874 | 938 | 1,380 | 369 | 409 | 596 | 2,247 | 2,445 | 3,718 |
| Songwe | 1,501 | 1,586 | 1,785 | 1,283 | 1,374 | 1,543 | 2,934 | 3,254 | 3,738 | 17,948 | 19,532 | 22,988 |
| **Total** | **354,477** | **374,548** | **391,275** | **303,137** | **324,629** | **339,877** | **2,199,838** | **2,440,395** | **2,513,858** | **13,459,918** | **14,647,741** | **15,686,556** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

# SURA YA 11

# UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

## UJENZI

### Mtandao wa Barabara Nchini

264. Mwaka 2024, mtandao wa barabara nchini ulifikia kilometa 181,864.81 ikilinganishwa na kilometa 181,655.49 mwaka 2023. Kati ya hizo, kilometa 37,435.04 zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania - TANROADS na kilometa 144,429.77 zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini - TARURA.

265. Mwaka 2024, mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TANROADS uliongezeka na kufikia kilometa 37,435.04 kutoka kilometa 37,225.72 mwaka 2023. Ongezeko la mtandao wa barabara lilitokana na kukasimishwa, kupandishwa hadhi na kufunguliwa kwa barabara mpya za wilaya. Kati ya mtandao huo, kilometa 12,527.44 ni barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani na kilometa 24,907.6 ni barabara za mikoa zinazounganisha miji mikuu ya mikoa na wilaya.

266. Mwaka 2024, barabara kuu na za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa kilometa 35,415.75 ikilinganishwa na kilometa 34,150.76 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya barabara za wilaya kukasimishwa kuwa barabara za mikoa. Kati ya barabara hizo, kilometa 5,136.55 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 20,182.79 zilikuwa katika hali ya wastani na kilometa 10,096.41 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 3,219.43, kilometa 17,945.45 na kilometa 12,985.88 mtawalia mwaka 2023. Kupungua kwa barabara zenye hali nzuri kulichangiwa na mvua kubwa zilizoharibu miundombinu ya barabara.

267. Hadi Desemba 2024, barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometa 11,612.15 ikilinganishwa na kilometa 10,750.72 mwaka 2023. Kati ya hizo, kilometa 1,739.89 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 3,914.34 katika hali ya wastani na kilometa 5,957.92 katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 1,345.44, kilometa 3,377.99 na kilometa 6,027.29 mtawalia mwaka 2023.

268. Mwaka 2024, kilometa 23,803.60 za barabara za mikoa na zinazounganisha mikoa na wilaya zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilifanyiwa tathmini ikilinganishwa na kilometa 23,400.04 zilizofanyiwa tathmini mwaka 2023. Kati ya barabara hizo, kilometa 3,396.66 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 16,268.45 katika hali ya wastani na kilometa 4,138.49 katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 1,873.99, kilometa 14,567.46 na kilometa 6,958.59 mtawalia mwaka 2023.

**Jedwali Na. 11.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Zilizofanyiwa Tathmini Mwaka 2024**

| Aina ya Barabara | Nzuri | | Wastani | | Mbaya | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kilometa | % | Kilometa | % | Kilometa | % | Kilometa |
| Barabara kuu lami | 5,672.17 | 59.3 | 2,436.89 | 25.5 | 1,457.44 | 15.2 | 9,566.50 |
| Barabara kuu changarawe/udongo | 285.75 | 14.0 | 1,477.45 | 72.2 | 282.45 | 13.8 | 2,045.65 |
| **Jumla Ndogo** | **5,957.92** | 51.3 | **3,914.34** | 33.7 | **1,739.89** | 15.0 | **11,612.15** |
| Barabara za mikoa lami | 921.17 | 35.2 | 1,172.31 | 44.8 | 520.39 | 19.9 | 2,613.87 |
| Barabara za mikoa changarawe/udongo | 3,217.32 | 15.2 | 15,096.14 | 71.3 | 2,876.27 | 13.6 | 21,189.73 |
| **Jumla Ndogo** | **4,138.49** | 17.4 | **16,268.45** | 68.3 | **3,396.66** | 14.3 | **23,803.60** |
| **Jumla Kuu** | **10,096.41** | **28.5** | **20,182.79** | **57.0** | **5,136.55** | **14.5** | **35,415.75** |

**Chanzo:** Wizara ya Ujenzi

269. Mwaka 2024, mtandao wa barabara unaosimamiwa na TARURA ulikuwa na kilometa 144,429.77 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Kati ya hizo, kilometa 41,731.29 zilikuwa katika hali nzuri, kilometa 53,762.00 katika hali ya wastani na kilometa 48,936.48 katika hali mbaya. Hadi Desemba 2024, mtandao wa barabara za wilaya zenye kiwango cha lami ulifikia kilometa 3,467.30, changarawe kilometa 44,372.21 na udongo kilometa 96,590.27 ikilinganishwa na kilometa 3,224.12 za lami, kilometa 41,107.52 za changarawe na kilometa 100,098.13 za udongo mwaka 2023.

**Jedwali Na. 11.2: Hali ya Mtandao wa Barabara za Vijijini na Mijini Mwaka 2024**

| Aina ya Barabara | Hali ya Barabara (Kilometa) | | | Jumla (Kilometa) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | Nzuri | Wastani | Mbaya | | |
| Barabara za lami | 2,783.20 | 577.54 | 106.55 | 3,467.29 | 2.4 |
| Barabara za changarawe | 22,337.24 | 17,094.74 | 4,940.22 | 44,372.21 | 30.7 |
| Barabara za udongo | 16,610.85 | 36,089.72 | 43,889.71 | 96,590.27 | 66.9 |
| **Jumla** | **41,731.29** | **53,762.00** | **48,936.48** | **144,429.77** | **100** |
| Asilimia | 28.9 | 37.2 | 33.9 | 100 | |

**Chanzo:** Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini

270. Mwaka 2024, TARURA ilijenga, ilikarabati na kutengeneza barabara za wilaya zenye urefu wa kilometa 30,209.86 ikilinganishwa na kilometa 42,153.35 zilizojengwa na kukarabatiwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 28.3. Upungufu huo ulitokana na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi na matengenezo ya barabara iliyokuwa inaendelea kutekelezwa mwaka 2023 katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hizo, barabara zenye urefu wa kilometa 243.18 zilijengwa kwa kiwango cha lami, kilometa 3,264.69 kwa kiwango cha changarawe na kilometa 26,701.99 zilifanyiwa ukarabati maalum, ukarabati wa kawaida na matengenezo ya maeneo korofi. Aidha, Wakala ilijenga madaraja 83,

makalavati 485, mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye mita za mraba 100,646.46 na kukarabati madaraja 37 mwaka 2024 ikilinganishwa na madaraja 2,741 makalavati 3,308, mitaro ya maji yenye urefu wa kilometa 102,891.69 na madaraja 31 yaliokarabatiwa mwaka 2023.

**Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari**

271. Mwaka 2024, TANROADS ilifanya matengenezo ya barabara kuu za mikoa zenye urefu wa kilometa 885.87 ikilinganishwa na kilometa 5,990.87 zilizofanyiwa matengenezo mwaka 2023. Kupungua kwa barabara kuu za mikoa zilizofanyiwa matengenezo kulitokana na Wakala kuelekeza nguvu zaidi kwenye ujenzi unaoendelea wa barabara zenye hali mbaya zilizohamishwa kutoka TARURA. Aidha, madaraja 1,039.16 yalifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na madaraja 3,271 yaliyofanyiwa matengenezo mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 68.2. Upungufu huo ulitokana na kuimarika kwa miundombinu ya barabara na madaraja kufuatia ujenzi na matengenezo ya miundombinu hiyo inayoendelea nchini.

272. Mwaka 2024, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania - TEMESA uliendelea kusimamia vivuko 32 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Katika kipindi hicho, abiria 26,240,229, magari 403,265 na mizigo tani 207.21 ilivushwa kupitia vivuko hivyo ikilinganishwa na abiria 29,775,113, magari 794,514 na mizigo tani 307.18 iliyovushwa mwaka 2023. Kupungua kwa abiria, magari na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na baadhi ya vivuko kuwa kwenye matengenezo, ikiwemo MV Magogoni, MV Nyerere, MV Chato I, MV Ukara I, MV Kigamboni, MV. Ruhuhu, MV Old Ruvuvu, MV Sabasaba, MV Kilambo na MV Pangani. Kwa upande mwingine, TEMESA ilitengeneza magari 25,095 mwaka 2024 ikilinganishwa na magari 27,964 yaliyotengenezwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 10.3. Hii ilitokana na kuanza kutumika kwa mfumo wa malipo kabla ya matengenezo ya gari kufanyika ili kuepuka malimbikizo ya madai ambapo badhi ya magari yalishindwa kuendana na utaratibu huu wa kufanya malipo ya kabla.

**Mfuko wa Barabara**

273. Mwaka 2024, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya shilingi bilioni 1,186.94 ikilinganishwa na shilingi bilioni 906.8 zilizokusanywa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 30.9. Hii ilichangiwa na ongezeko la magari ya mizigo ya kigeni yanayotumia barabara za Tanzania na hivyo kuongeza makusanyo ya ushuru (transit charges) kutokana na maboresho katika bandari ya Dar es Salaam na bandari ya Tanga.

**Nyumba na Majengo ya Serikali**

274. Mwaka 2024, Wakala wa Majengo Tanzania - TBA uliendelea kusanifu na kusimamia miradi 135 ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali ikilinganishwa na miradi 110 mwaka 2023. Kuongezeka kwa miradi ya ujenzi kulitokana na mahitaji

makubwa ya majengo ya ofisi na nyumba kwa washitiri. Aidha, Wakala ulikarabati nyumba na majengo 108 mwaka 2024 ikilinganishwa na nyumba na majengo 132 yaliyokarabatiwa mwaka 2023.

275. Mwaka 2024, nyumba 6,493 zilipangishwa kwa wapangaji wa kibiashara na watumishi wa umma kama ilivyokuwa mwaka 2023. Katika kipindi hicho, TBA ilikusanya kodi ya pango jumla ya shilingi bilioni 8.8. Kati ya nyumba ilizopangishwa, nyumba 2,382 zilipangishwa kwa watumishi wa umma kwa ajili ya makazi na nyumba 4,111 zilipangishwa kwa shughuli za kibiashara.

**Usajili wa Makandarasi**

276. Mwaka 2024, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilisajili makandarasi 1,812 ikilinganishwa na makandarasi 1,807 waliosajiliwa mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Bodi kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Usajili wa Makandarasi. Usajili huo uliwezesha makandarasi waliosajiliwa kufikia 17,293 mwaka 2024 kutoka makandarasi 15,841 mwaka 2023. Aidha, Bodi ilisajili miradi 4,691 ya ujenzi mwaka 2024 ikilinganishwa na miradi 4,539 iliyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa shughuli za ujenzi nchini.

277. Mwaka 2024, miradi 3,581 ilikaguliwa na Bodi ikilinganishwa na miradi 3,354 iliyokaguliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendea kazi. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 2,092 ilikidhi vigezo na miradi 1,489 haikukidhi vigezo. Aidha, hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa kwa miradi ambayo haikukidhi vigezo, ikiwemo kutozwa faini kwa makandarasi na kusimamisha ujenzi wa baadhi ya miradi. Vilevile, Bodi ilipeleka mahakamani mashauri 68 ya makosa mbalimbali mwaka 2024 ikilinganishwa na mashauri 64 mwaka 2023. Makosa hayo ni pamoja na kutekeleza miradi kwa kutumia kampuni au wataalam wasio makandarasi kinyume cha sheria.

**Usajili wa Wahandisi**

278. Mwaka 2024, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 3,636 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 2,981 waliosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 22.0. Kati ya hao, wahandisi 3,441, sawa na asilimia 94.6 walikuwa watanzania na wahandisi 195 (asilimia 5.4) walitoka nje ya nchi. Kutokana na usajili huo, wahandishi waliosajiliwa walifikia 40,981 mwaka 2024 kutoka wahandisi 37,345 waliosajiliwa mwaka 2023. Hii ilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa usajili kwa wataalam wa kada ya uhandisi. Aidha, Bodi ilisajili mafundi sanifu 480 mwaka 2024 ikilinganishwa na mafundi sanifu 348 waliosajiliwa mwaka 2023.

279. Hadi Desemba 2024, kampuni za ushauri zilizosajiliwa na Bodi zilifikia 443 kutoka kampuni 421 zilizosajiliwa mwaka 2023. Aidha, Bodi ilisajili wahandisi washauri 18 mwaka 2024 ikilinganishwa na wahandisi washauri 31 waliosajiliwa mwaka 2023. Upungufu wa wahandisi waliosajiliwa ulitokana na baadhi ya wahandisi kukosa sifa kwa mujibu wa sheria. Kati ya hao, wahandisi washauri 14 walikuwa watanzania na wahandisi washauri wanne (4) walikuwa wa kigeni. Kutokana na usajili huo, wahandisi washauri waliosajiliwa walifikia 677 mwaka 2024 kutoka wahandisi washauri 659 mwaka 2023.

280. Mwaka 2024, Bodi ilisajili maabara mbili (2) za vifaa vya ujenzi na uhandisi ikilinganishwa na maabara 11 zilizosajiliwa mwaka 2023. Upungufu huo ulitokana na mwamko mdogo wa taasisi na watu binafsi kusajili maabara zao. Hadi Desemba 2024, maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi zilizosajiliwa zilifikia 53.

281. Mwaka 2024, wahandisi 1,722 walipata mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 1,704 waliopata mafunzo mwaka 2023. Kati ya hao, wahandisi 158 walihitimu na kusajiliwa kama wahandisi wataalamu mwaka 2024 ikilinganishwa na wahandisi 364 waliosajiliwa mwaka 2023. Kwa upande mwingine, Bodi ilisajili miradi 1,509 ya ujenzi mwaka 2024 ikilinganishwa na miradi 795 iliyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 89.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuendelea kutumia mfumo wa kielektroniki katika usajili wa miradi ya ujenzi. Aidha, Bodi ilikagua miradi 330 mwaka 2024 ikilinganishwa na miradi 185 iliyokaguliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 78.4. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 139 ilibainika kuwa na mapungufu ambapo miradi 74 haikusajiliwa na miradi 65 haikuhusisha huduma ya Wahandisi washauri kwa upande wa umeme na mitambo.

**Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

282. Mwaka 2024, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili wataalamu 174 ikilinganishwa na wataalamu 140 waliosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 24.3. Ongezeko hilo, lilitokana na uhamasishaji kwa wataalamu kuhusu umuhimu wa kujisajili kupitia mfumo wa kielektroniki wa Bodi.

283. Hadi Desemba 2024, wataalamu wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi waliosajiliwa walifikia 1,616 kutoka wataalamu 1,442 waliokuwa wamesajiliwa mwaka 2023. Kati ya hao, wataalamu 1,583 ni watanzania na wataalamu 33 ni wageni. Aidha, wahitimu 245 walishiriki mafunzo kwa vitendo katika fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi mwaka 2024 ikilinganishwa na wahitimu 230 walioshiriki mafunzo mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Hii ilitokana na ongezeko la miradi ya ujenzi lililowezesha upatikanaji wa nafasi za kazi pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu katika sekta ya ujenzi.

284. Mwaka 2024, Bodi ilisajili kampuni 36 za ushauri wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ikilinganishwa na kampuni 32 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Hii ilitokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika usajili wa kampuni za ushauri elekezi pamoja na ongezeko la miradi ya ujenzi nchini. Hadi Desemba 2024, kampuni zilizosajiliwa zilifikia 475 kutoka kampuni 439 zilizokuwa zimesajiliwa mwaka 2023. Kati ya hizo, kampuni 470 zilikuwa za watanzania na kampuni tano (5) za wageni.

285. Mwaka 2024, Bodi ilisajili miradi 1,617 ya ujenzi wa majengo ikilinganishwa na miradi 1,396 iliyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.8. Ongezeko hilo lilitokana na ukaguzi wa miradi pamoja na udhibiti wa waendelezaji wa majengo kwa kuzingatia matakwa ya sheria. Aidha, Bodi ilikagua miradi 5,153 ya ujenzi wa majengo mwaka 2024 ikilinganishwa na miradi 4,885 iliyokaguliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wakaguzi katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kati ya miradi hiyo, miradi 4,310 ilikidhi vigezo, sawa na asilimia 83.6 na miradi 843 (asilimia 16.4) haikukidhi vigezo. Miradi ambayo haikukidhi vigezo waendelezaji wake walichukuliwa hatua mbalimbali ikiwemo: kufanya maboresho kwa miradi yenye mapungufu kwa mujibu wa mkataba wa awali; kukatwa fedha za malipo ya madai ya mradi na kutopewa kandarasi yoyote hapa nchini.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

286. Mwaka 2024, Baraza la Taifa la Ujenzi lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau sita (6) wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau nane (8) waliopewa ushauri wa kiufundi mwaka 2023. Aidha, Baraza lilisuluhisha migogoro 277 ikilinganishwa na migogoro 247 iliyosuluhishwa mwaka 2023. Kati ya hiyo, migogoro 15 ilifungwa mwaka 2024 ikilinganishwa na migogoro nane (8) iliyofungwa mwaka 2023 baada ya kupata usuluhishi.

287. Mwaka 2024, Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania - TBS liliandaa mapitio ya viwango vitatu (3) vya ubora wa vifaa vya ujenzi ikilinganishwa na viwango 83 mwaka 2023. Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya mapitio ya viwango vya ubora vilivyowasilishwa katika Baraza hilo. Vilevile, Baraza liliendesha kozi tatu (3) kwa wadau wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na kozi tano (5) zilizoendeshwa mwaka 2023.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

288. Mwaka 2024, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ilitoa mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 271 ikilinganishwa na wanafunzi 208 waliopatiwa mafunzo mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 30.3. Aidha, Taasisi ilitoa mafunzo kwa wanafunzi 432 wa Elimu ya Ufundi Stadi - VETA mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 424 waliopata mafunzo mwaka 2023.

289. Mwaka 2024, Taasisi ilihamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa wadau 270 ikilinganishwa na wadau 177 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 52.5. Ongezeko hilo lilichangiwa na uhitaji wa teknolojia stahiki ya nguvukazi katika halmashauri mbalimbali. Katika kipindi hicho, Taasisi ilitoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa mafundi sanifu sita (6) ikilinganishwa na mafundi sanifu 12 wa mwaka 2023. Aidha, Taasisi ilitoa mafunzo kwa washiriki 24 kutoka katika vikundi vya wanawake na vijana ikilinganishwa na washiriki 290 waliopewa mafunzo mwaka 2023.

**MAENDELEO YA ARDHI**

**Utayarishaji wa Hatimiliki, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Utatuzi wa Migogoro**

290. Mwaka 2024, hatimiliki za viwanja na mashamba zilizoandaliwa kwa ajili ya usajili zilikuwa 111,450 ikilinganishwa na hatimiliki 133,944 zilizoandaliwa mwaka 2023. Aidha, hakimiliki za kimila 87,110 zilitolewa kwa wananchi mwaka 2024 ikilinganishwa na hatimiliki 74,830 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwanja na mashamba yaliyopimwa kufuatia kuendelea kwa utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi.

291. Mwaka 2024, vyeti 232 vya ardhi za vijiji vilitolewa ikilinganishwa na vyeti 149 vilivyotolewa mwaka 2023. Usajili huo ulifikia vijiji 12,201 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, migogoro ya ardhi 5,464 ilitatuliwa kiutawala mwaka 2024 ikilinganishwa na migogoro 2,503 iliyotatuliwa mwaka 2023. Ongezeko la migogoro iliyotatuliwa lilitokana na kuimarika kwa utaratibu wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi kupitia Dawati la Huduma kwa Wateja, Kliniki za Ardhi na mikutano ya wadau uwandani.

**Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria**

292. Mwaka 2024, hatimiliki na nyaraka za kisheria 224,691 zilisajiliwa ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka 200,318 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Hii ilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuimarika kwa kliniki za ardhi; na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria zilizosajiliwa.

**Jedwali Na 11.3: Usajili wa Hatimilki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria, Mwaka 2019 - 2024**

| Hati na Nyaraka Zilizosajiliwa | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: Hati Zilizosajiliwa** | | | | | | |
| Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura 334 | 47,948 | 57,180 | 61,527 | 83,195 | 90,408 | 101,262 |
| Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemu ya Jengo (Unit Title Act No.17/2008). | 321 | 924 | 232 | 380 | 294 | 351 |
| **Jumla Hatimiliki** | **48,269** | **58,104** | **61,759** | **83,575** | **90,702** | **101,613** |
| **B: Miamala na Nyaraka za Kisheria Zilizosajiliwa** | | | | | | |
| Miamala iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura 334 | 15,018 | 35,477 | 39,252 | 51,413 | 57,395 | 64,624 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura 117 | 26,096 | 33,938 | 36,354 | 42,112 | 44,655 | 55,954 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika, Sura 210 | 3,129 | 5,698 | 4,265 | 5,972 | 7,566 | 2,500 |
| **Jumla Nyaraka za Kisheria** | **44,243** | **75,113** | **79,871** | **99,497** | **109,616** | **123,078** |
| **Jumla Kuu: Hatimilki na Nyaraka za Kisheria** | **92,512** | **133,217** | **141,630** | **183,072** | **200,318** | **224,691** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Uthamini wa Mali na Upimaji wa Mashamba na Viwanja**

293. Mwaka 2024, Serikali iliidhinisha taarifa 60,449 za uthamini wa kawaida na fidia ikilinganishwa na taarifa 94,551 mwaka 2023. Taarifa zilizoidhinishwa zilipungua kutokana na kupungua kwa mahitaji ya fidia katika miradi ya kimkakati na miamala ya ardhi, hususan katika maeneo ya uhamisho wa milki, uhuishaji wa milki, mikopo na uthamini kwa ajili ya mizania ya kimahesabu.

294. Mwaka 2024, ramani za upimaji zenye viwanja 194,209 na mashamba 7,170 ziliidhinishwa ikilinganishwa na ramani zenye viwanja 314,977 na mashamba 2,564 zilizoidhinishwa mwaka 2023. Upungufu wa viwanja vilivyopimwa ulitokana na baadhi ya kampuni za upangaji na upimaji zilizokasimiwa jukumu hilo kutokamilisha kazi kwa wakati.

**Jedwali Na 11.4: Viwanja na Mashamba Yaliyoidhinishwa, Mwaka 2023 - 2024**

| Na. | Mikoa | 2023 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Viwanja** | **Mashamba** | **Viwanja** | **Mashamba** |
| 1 | Arusha | 5,836 | 1,541 | 2,113 | 21 |
| 2 | Dar es Salaam | 25,765 | - | 27,289 | - |
| 3 | Dodoma | 21,461 | 520 | 29,434 | 162 |
| 4 | Geita | 4,631 | - | 6,105 | - |
| 5 | Iringa | 10,670 | 16 | 12,114 | 26 |
| 6 | Kagera | 2,225 | 20 | - | - |
| 7 | Katavi | 5,963 | - | 4,927 | 13 |
| 8 | Kigoma | 5,794 | 129 | 13,661 | 105 |
| 9 | Kilimanjaro | 1,617 | 27 | 7,688 | 21 |
| 10 | Lindi | 5,731 | 15 | 6,213 | 18 |
| 11 | Manyara | 17,870 | 44 | 5,377 | 53 |
| 12 | Mara | 17,001 | 1 | 5,946 | 10 |
| 13 | Mbeya | 55,558 | 3 | 8,486 | 25 |
| 14 | Morogoro | 23,652 | 157 | 10,252 | 40 |
| 15 | Mtwara | 7,129 | 9 | 2,200 | 6 |
| 16 | Mwanza | 8,010 | 9 | 14,428 | - |
| 17 | Njombe | 7,359 | 23 | - | - |
| 18 | Pwani | 19,580 | - | - | - |
| 19 | Rukwa | 2,472 | 12 | - | - |
| 20 | Ruvuma | 8,449 | 2 | 5,615 | 13 |
| 21 | Shinyanga | 7,579 | - | 3,445 | - |
| 22 | Simiyu | 4,664 | - | 3,301 | 2 |
| 23 | Singida | 9,938 | 20 | 11,328 | 57 |
| 24 | Songwe | 4,148 | 3 | 4,281 | 4 |
| 25 | Tabora | 13,340 | 9 | - | - |
| 26 | Tanga | 18,535 | 4 | 10,006 | 6,594 |
| | **Jumla** | **314,977** | **2,564** | **194,209** | **7,170** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

295. Mwaka 2024, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 562 iliandaliwa katika wilaya 27 ikilinganishwa na mipango 734 iliyoandaliwa katika wilaya 47 mwaka 2023. Idadi hiyo ilifikisha vijiji 4,274 vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi hadi mwaka 2024.

**Jedwali Na 11.5: Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Mwaka 2024**

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Vijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ruvuma | Nyasa | Ng'ombo, Chimate Kwambe, Ngindo, Tumbi, Kihagara, Ndonga, Liweta, Mkili, Konganywita, Mipotopoto, Uhuru, Mkalawa na Mitomoni. | 14 |
| | | Mbinga | Mkaranga, Ndembo, Silo, Liyombo, Mapipili, Lukiti, Ulolela, Kitura, Mzuzu, Mahilo, Lituru, Mahenge, Mitambotambo, Mhagawa Asili, Langandondo, Linda, Mbuji, Kilanga juu, Mahilo Asili, Mawono, Myau, Kibanga, Likwela, Kihulila, Mpapa, Buruma, Mitawa, Mitanga, Maguu, Kibandai "A", Kibandai Asili, Langiro Asili, Mkuwani, Mkuka, Kipapa, Matuta, Mhilo, Kitumbi, Langiro, Lingomba, Mkoha, Mkoha Asili, Kihongo, Mkinga, Mikalanga, Ilela, Kikuli, Makonga, Ugogo, Ugano, Malindindo, Matekela, Mkeyeto na Kitesa. | 54 |
| 2 | Kigoma | Buhigwe | Biharu, Kigege, Migongo, Nyamugali, Kibande, Kalege, Nyanga, Nyamihanga, Mubanga, Chagwe, Nyankoronko, Muhinda, Nyakimwe na Nyaruboza. | 14 |
| | | Kibondo | Kisogwe na Busunzu. | 2 |
| 3 | Dodoma | Kondoa | Kalamba Chini na Kalamba Juu. | 2 |
| 4 | Geita | Mbogwe | Nyang'holongo, Bunigonzi, Mwabukwalule, Ushetu, Shibutwe, Kisumo, Nyang'wale, Iboya, Bwendaseko, Nambubi, Mubamba, Msendamila, Buzigula, Bulilila, Nyikonga, Ikunguigazi, Mwigilo, Ibambula, Bugalagala, Isebya, Mgaya, Isungambula na Kasaka. | 23 |
| | | Nyang'wale | Nyang'wale, Bujula Miyenze, Idetemya, Nyabulanda, Nyashilanga, Nyakaswi, Ibambila, Kaseme A, Shabaka, Ihushi, Wavu, Nyamgongwa, Lubando, na Mhama. | 14 |
| 5 | Tabora | Nzega | Upina, Ubinga, Ibushi, Nkiniziwa, Usag Luhumbo ali, Inagana, Ugembe, Gulumbai, Usongwanhala, Ilole, Mwino, Malolo na Mahene. | 14 |
| | | Uyui | Izugawima, Matanda, Mbuyuni, Kagera, Ikonola, Ilundo, Gilimba, Katunda, Ulimakafu, Tulieni, Nzubuka, Kikungu, Itundaukulu, Nsimbo, Kinyamwe, Shitage, Bukili, Ndolo, Ilolangulu Kusini, Ilolangulu, Imalampaka, Isenegezya, Nzigala, Mputi, Itobela, Nhumbo, Nkutu, Maswanya, Ideka, Chali, Magiri, Mayombo, Ibelamilundi, Mhulidede, Busenda, Ngokolo, Utura, Mbiti, Kigwa B, Hiari Ya Moyo, Kalemela, Saw Mill, Mwitikila, Kinamagi, Mtakuja, Ishihimulwa, Bukala, Mbeya, Mabama naTumaini. | 50 |
| | | Kaliua | Ukumbisiganga, Kangeme, Mwahalaja, Mwendakulima, Nsimbo, Chemkeni, Mwanduti, Ntwigu, Nhwande, Imagi, King'wangoko, Ilege, Busondi, Busubi, Busanda, Kabanga, Nyasa, Mwenakulima-Seleli, Mpagasha, Kagera, Iyombo, Seleli, Mwongozo, Ibambo, Ibapa, Ichemba, Sasu, Mgelela, Bulela, Mkiligi, Nsungwa, Ulanga, Usonga, Utantamke, Mwamashimba, Tupendane, Makingi, Usigala, Silambo, Kanoge, Ndorobo, Imalaupina, Kazaroho, Usimba-Zugimlole, Magele, Igombe, Usimba, Imalamihayo, Usangi na Zugimlole. | 50 |
| | | Sikonge | Tumaini, Ifuta | 2 |
| | | Urambo | Matagata, Zugimlole, Nyahua, Makibo | 4 |

**Jedwali Na 11.5 Linaendelea**

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Vijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Morogoro | Morogoro | Visaraka, Lubumu, Seregete A, Seregete B, Kisemo, Magera, Pulambili, Chanyumbu, Kidugalo, Kwaba, Mkulazi, Kiwege, Muhungamkola na Lubungo A. | 14 |
| | | Mvomero | Mgudeni, Matale, Lungo, Mlumbilo, Kunke, Dihinda, Kaole, Difinga, Manza, Homboza, Kinyenze, Mkuyuni, Tangeni, Lukuyu, Chohelo, Mnyanza, Yowe, Dasi, Kibigiri, Lusungi, Kipangilo, Dibago, Bwage, Mndela, Kisimagulu, Semwali, Mlaguzi, Maskati, Komtonga, Kikeo, Chohero, Kododo, Luale, Kibuko, Ndugutu, Ng'owo, Lukunguni, Masalawe, Digalama, Mwarazi, Londo, Mhale, Pinde, Kibaoni, Kidudwe, Ng'ungulu, Vitonga na Mongwe. | 48 |
| 7 | Kilimanjaro | Rombo | Ikuini, Shimbi Mashariki, Msaranga, Kiraeni, Mahorosha, Ngareni, Aleni chini, Leto, Kitowo, Kiwanda, Ngaseni, Kirongo chini, Marangu na Usongo. | 14 |
| 8 | Mbeya | Busokelo | Isange, Bujingijila, Isale, Mpunguti, Kikuba, Bumbigi, Ipepo, Matamba, Lusungo, Ipuguso, Mwela, Ikubo, Kilasi na Luteba. | 14 |
| | | Rungwe | Nditu na Suma. | 2 |
| | | Chunya | Mlimanjiwa, Soweto, Mawelo, Lupamarket, Mtande, Lola, Upendo, Nkwangu, Ifumbo, Godima, Isewe, Mapinduzi, Majengo, Mamba, Magunga, Mwiji, Nkung'ungu, Igundu, Igangwe, Kalangali na Isangawana. | 21 |
| 9 | Katavi | Mlele | Wachawaseme, Kaulolo, Nsenkwa, Mgombe, Kanoge na Mtakuja. | 6 |
| 10 | Rukwa | Sumbawanga | Jangwani, Mkima, Memya, Kapoka, Mpwapwa na Malolwa. | 6 |
| | | Nkasi | Kasu B, Kasu A, Kipande, Kantawa, Katani, Nchenje, Kitosi, Chonga, Mpasa, Myula, Ntalamila, Sintali, Kilambo, Nkana, Kalundi, Ifundwa, Tundu, Makupa, Kala, Ntuchi Kaskazini, Milundikwa, Ntuchi Kusini, Komanchindo, Chalatila, Mlambo, Chala A, Chala B, Chala C, Katongolo, Kacheche, Londokazi, Kate, Mwenge, Majengo Mapya, Mkinga, Kalungu, Chima, King'ombe na Masolo. | 39 |
| 11 | Shinyanga | Shinyanga | Shabuluba, Nduguti, Nzagaluba, Bukumbi, Masengwa, Mwajada, Bubale, Singita, Igembya, Mwamalulu, Kitwangi na Ilobashi. | 12 |
| 12 | Simiyu | Bariadi | Chungu cha Bawawa, Salaliya Nyamikoma, Damidami, Mwamalula, Mwantimba, Matombo, Mwauchumu, Mwashagata, Gibishi, Chungu, Halawa, Mwasilimbi, Ihusi, Senta, Igabanhilo, Mawaumatondo na Mwasinasi. | 18 |

**Jedwali Na 11.5 Linaendelea**

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Vijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 13 | Lindi | Kilwa | Miguruwe, Nakingombe, Kandawale, Mtembei Mpopera, Kipindimbi, Njinjo, Likawage, Kisima Mkika, Nanjirinji A, Nanjirinji B, Nakiu, Kiswere, Rushungi, Ruyaya, Kisongo, Lihimalyao Kusini, Lihimalyao Kaskazini, Namakongoro, Mikoma, Namwedo, Malalani, Pande Plot, Hoteli Tatu, Nang'oo Kiwala, Mtitimila, Mtandango, Tingi, Miteja, Mtu Kwao, Nangambi Naipuli, Kililima, Mingumbi, Mtoni, Tilawandu, Nampunga, Nambondo, Chapita, Namayuni, Lyomanga, Ngorongoro, Namakolo, Nahama, Ingirito, Chumo, Hongwe, Kijumbi, Miumbu na Njia nne. | 48 |
| | | Ruangwa | Namienje, Muhuru, Chibula, Nachikalala, Chikundi, Mandawa Chini, Namichiga A, Namichiga B, Mkutingome, Namilema, Chinongwe A, Chinongwe B, Juhudi A, Juhudi B, Ipingo, Nangumbu A, Nangumbu B, Michenga A, Michenga B, Mtakuja, Chimbila A, Chimbila B, Nandagala A, Nandagala B, Manokwe, Chienjele, Njawale, Namakuku, Namahema A, Namahema B, Mpara, Mpumbe, Mitope, Mmawa na Likunja. | 35 |
| | Njombe | Ludewa | Igalu, Kipingu, Kiyogo, Lipangala, Lugarawa, Luilo, Mdilidili, Nsungu, Shaurimoyo, Ugera, Madunda, Ludewa Mjini, Ligumbilo, Utilili, Madindo, Mbugani, Madilu, Ludewa Kijijini, Mawengi, Milo, Nkanda, Lumbila, Chanjale, Nsele, Kilondo, Ndowa, Makonde, Lifuma, Nsisi, Nkwimbili, Kimata na Lupingu. | 32 |
| | Singida | Iramba | Kyalosangi, Uwanza, Maluga, Galangala, Kisharita, Kisiriri, Ulemo, Kinalilya, Kisimba na Kisana. | 10 |
| | **Jumla** | | | **562** |

**Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

### Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa

296. Mwaka 2024, Serikali iliandaa na kuidhinisha michoro ya mipangomiji 2,985 ikilinganishwa na michoro 492 iliyoandaliwa na kuidhinishwa mwaka 2023. Katika kipindi hicho, makazi 297,550 yasiyopangwa yalirasimishwa ikilinganishwa na makazi 196,146 yaliyorasimishwa mwaka 2023. Idadi ya makazi yaliyorasimishwa iliongezeka kutokana na ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi shirikishi ya urasimishaji makazi.

### Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

297. Mwaka 2024, mashauri 30,545 (mashauri mapya 15,949 na mashauri 14,596 yanayoendelea kusikilizwa) yalikua kwenye Mabaraza 112 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ikilinganishwa na mashauri 35,635 yaliyokuwepo katika Mabaraza 96 mwaka 2023. Kupungua kwa mashauri hayo kulitokana na kuongezeka kwa idadi ya Mabaraza ya Ardhi

na Nyumba ya Wilaya. Kati ya hayo, mashauri 16,969 yaliamuliwa na mashauri 13,576 yanaendelea kusikilizwa.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara**

298. Mwaka 2024, Shirika la Nyumba la Taifa (National Housing Corporation - NHC) lilikamilisha ujenzi wa nyumba 147 na kuendelea na ujenzi wa nyumba 1,549 katika maeneo mbalimbali nchini ikilinganishwa na nyumba 524 zilizokamilika na nyumba 588 zilizoendelea na ujenzi mwaka 2023. Kati ya nyumba zilizokamilika, nyumba 10 zilikuwa za gharama nafuu na nyumba 137 za bei ya kati na juu ikilinganishwa na nyumba 303 za bei nafuu, nyumba 221 za bei ya kati na juu mwaka 2023. Katika kipindi hicho, Kampuni ya Nyumba kwa Watumishi (Watumishi Housing Investment - WHI) ilikamilisha ujenzi wa nyumba 30 zilizopo Njedengwa Dodoma mwaka 2024 ikilinganishwa na nyumba 45 zilizokamilika mwaka 2023.

## SURA YA 12

## UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO

### Usafiri wa Barabara

299. Mwaka 2024, leseni 329,112 za usafirishaji kwa vyombo vya moto vilivyosajiliwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara zilitolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini - LATRA ikilinganishwa na leseni 298,270 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Hii ilitokana na kuendelea kuhuishwa kwa leseni zilizoisha muda wake, kuongezeka kwa wawekezaji katika usafirishaji wa abiria na mizigo pamoja na elimu iliyoendelea kutolewa kwa umma kuhusu umuhimu wa kupata leseni kupitia vipindi vya elimu kwa umma, mitandao ya kijamii, maonesho mbalimbali, mikutano ya wadau na kituo cha huduma kwa wateja.

**Jedwali Na. 12.1: Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa, Mwaka 2020 - 2024**

| Kundi la Leseni | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya abiria | 52,081 | 53,451 | 50,452 | 50,316 | 64,635 | 28.5 |
| Magari ya mizigo | 142,559 | 133,428 | 142,154 | 183,392 | 201,388 | 9.8 |
| Bajaji/Pikipiki | 20,400 | 36,984 | 52,812 | 64,562 | 63,089 | -2.3 |
| **Jumla** | **215,040** | **223,863** | **245,418** | **298,270** | **329,112** | 10.3 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

300. Mwaka 2024, ajali zilizotokana na vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara zilikuwa 940 ikilinganishwa na ajali 1,009 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 6.8. Hii ilitokana na kaguzi za mara kwa mara barabarani, matumizi ya mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu pamoja na elimu iliyotolewa kwa wadau wa vyombo vya usafiri barabarani. Hata hivyo, ajali za barabarani zilizosababishwa na bajaji/pikipiki ziliongezeka kwa asilimia 2.4 na kufikia ajali 383 mwaka 2024 kutoka ajali 374 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na uzembe wa madereva, hususan uendeshaji usiozingatia sheria za barabarani.

**Jedwani Na. 12.2: Ajali za Barabarani Mwaka, 2020 - 2024**

| Aina ya Vyombo | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya abiria | 330 | 365 | 357 | 335 | 303 | -9.6 |
| Magari ya Mizigo | 407 | 224 | 268 | 300 | 254 | -15.3 |
| Bajaji/Pikipiki | 415 | 463 | 780 | 374 | 383 | 2.4 |
| **Jumla** | **1,152** | **1,052** | **1,405** | **1,009** | **940** | -6.8 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

**Usafiri wa Reli**

301. Mwaka 2024, Shirika la Reli Tanzania - TRC lilisafirisha shehena ya mizigo tani 249,197 kwa umbali wa kilometa 251,316,724 ikilinganishwa na tani 382,289 kwa umbali wa kilometa 360,780,885 zilizosafirishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa mizigo iliyosafirishwa kwa asilimia 34.8. Upungufu huo ulitokana na uhaba wa vitendea kazi ikiwemo vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo pamoja na kufungwa kwa njia ya reli katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha miezi mitatu kutokana na mvua iliyosababisha uharibifu wa miundombinu ya reli.

302. Mwaka 2024, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania ilianza kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria kupitia Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa - SGR kati ya Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma kwa lengo la kurahisisha usafirishaji wa abiria na kuchochea shughuli za kiuchumi. Katika kipindi cha Juni hadi Desemba 2024, abiria 1,395,119 walisafirishwa kupitia treni ya SGR. Aidha, Shirika lilisafirisha abiria 414,754 wa masafa marefu kwa umbali wa kilometa 302,105,666 kupitia treni ya MGR mwaka 2024 ikilinganishwa na abiria 489,560 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 370,748,514 mwaka 2023, sawa na upungufu wa abiria kwa asilimia 15.3. Hii ilitokana na kufungwa kwa njia katika baadhi ya maeneo kutokana na mvua zilizoharibu miundombinu ya reli, kuanza kwa uendeshaji wa treni ya SGR na ukarabati wa njia ya reli kutoka Kaliua hadi Mpanda. Vilevile, Shirika lilisafirisha abiria 3,068,057 kwa umbali wa kilomita 86,648,052 mwaka 2024 katika jiji la Dar es Salaam ikilinganishwa na abiria 2,560,891 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 71,704,948 mwaka 2023, sawa na ongezeko la abiria kwa asilimia 19.8. Ongezeko hilo lilitokana na Shirika kuongeza safari za treni mjini ili kupunguza foleni za magari barabarani zilizosababishwa na ujenzi wa barabara ya mwendokasi kipande cha Posta hadi Gongolamboto.

**Jedwali Na. 12.3: Abiria na Mzigo Iliyosafirishwa na TRC, Mwaka 2020 - 2024 (MGR)**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mizigo** | | | | | | |
| Shehena za mizigo | 281,037 | 370,906 | 418,905 | 382,289 | 249,197 | -34.8 |
| Umbali Km | 295,525,346 | 366,560,583 | 485,141,823 | 360,780,885 | 251,316,724 | -30.3 |
| **Abiria** | | | | | | |
| Masafa Marefu | 449,422 | 417,096 | 466,262 | 489,560 | 414,754 | -15.3 |
| Umbali Km | 343,787,534 | 316,205,354 | 343,076,014 | 370,748,514 | 302,105,666 | -18.5 |
| Abiria wa Mjini | 3,069,168 | 2,876,199 | 2,668,294 | 2,560,891 | 3,068,057 | 19.8 |
| Umbali Km | 98,213,376 | 80,533,572 | 72,712,232 | 71,704,948 | 86,648,052 | 20.8 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

**Jedwali Na. 12.4: Idadi ya Abiria waliosafirishwa kupitia treni ya SGR Mwaka 2024**

| Miezi | Juni | Julai | Agosti | Septemba | Oktoba | Novemba | Desemba | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SGR | 46,591 | 126,918 | 264,123 | 210,917 | 221,351 | 258,851 | 293,415 | **1,422,166** |

**Chanzo***:* Shirika la Reli Tanzania

303. Mwaka 2024, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia - TAZARA ilisafirisha tani 235,746 za mizigo ikilinganishwa na tani 301,040 zilizosafirishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 21.7. Hii ilitokana na kufungwa kwa njia ya reli kwa takribani miezi miwili kutokana na mvua za El-nino pamoja na uchakavu wa injini na mabehewa.

**Jedwali Na. 12.5: Shehena ya Mzigo Iliyosafirishwa na TAZARA, Mwaka 2020 - 2024**

| **Aina ya Mzigo** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda nje ya nchi | 71,249 | 75,140 | 17,863 | 28,064 | 29,249 | 4.2 |
| Kutoka nje ya nchi | 75,271 | 73,843 | 59,155 | 63,936 | 32,946 | -48.5 |
| Ndani ya TAZARA | 19,901 | 50,146 | 88,891 | 73,973 | 26,012 | -64.8 |
| **Jumla Ndogo** | **166,421** | **199,129** | **165,909** | **165,973** | **88,207** | -46.9 |
| Kampuni binafsi | 166,676 | 192,952 | 22,873 | 135,067 | 147,539 | 9.2 |
| **Jumla Kuu** | **333,097** | **392,081** | **188,782** | **301,040** | **235,746** | -21.7 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

304. Mwaka 2024, Mamlaka ilisafirisha abiria 1,950,953 ikilinganishwa na abiria 2,710,104 waliosafirishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 28.0. Kati ya hao, abiria 367,027 walikuwa wa safari ndefu (Dar es Salaam - Mbeya - Zambia), abiria 211,445 wa treni ya Udzungwa na abiria 1,372,481 wa treni ya jijini Dar es Salaam.

**Jedwali Na. 12.6: Abiria Waliosafirishwa na TAZARA, Mwaka 2020 - 2024**

| **Aina ya Abiria** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Njia ndefu | 493,799 | 432,981 | 514,382 | 534,603 | 367,027 | -31.3 |
| Udzungwa | 420,945 | 406,762 | 375,575 | 359,564 | 211,445 | -41.2 |
| Dar es salaam | 1,813,108 | 1,872,930 | 1,903,631 | 1,815,937 | 1,372,481 | -24.4 |
| **Jumla** | **2,727,852** | **2,712,673** | **2,793,588** | **2,710,104** | **1,950,953** | **-28.0** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia


**Usafiri wa Anga**

305. Mwaka 2024, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania - TCAA ilisajili ndege 21 ikilinganishwa na ndege 31 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 32.2. Hii ilitokana na kupungua kwa wateja waliohitaji kuingiza ndege nchini kwa mwaka husika kulikochangiwa na hali ya soko la usafiri wa anga duniani pamoja na taratibu za ununuzi wa ndege kuchukua muda mrefu. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilikagua na kutoa vyeti vya ubora kwa ndege 155 ikilinganishwa na ndege 120 mwaka 2023, sawa na ongezeko la

asilimia 29.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ndege mpya pamoja na ndege ambazo zilisitisha kuruka hapo awali zilizohitaji kuhuisha safari zake. Hadi Desemba 2024, mashirika 30 ya ndege za kimataifa yalitoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine - *Bilateral Air Services Agreement* (BASA) ikilinganishwa na mashirika 25 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ongezeko la ndege za kimataifa lilichangiwa na kuendelea kukua kwa soko la usafiri wa anga nchini na hivyo kuvutia mashirika mapya.

306. Mwaka 2024, abiria waliosafiri kwa njia ya anga walikuwa 7,375,522 ikilinganishwa na abiria 6,820,541 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Kati ya hao, abiria 4,014,552 walisafiri ndani ya nchi na abiria 3,360,970 walisafiri nje ya nchi. Ongezeko la abiria lilitokana na kuendelea kuimarika kwa miundombinu ya usafiri wa anga nchini.


**Kielelezo Na.12.1: Idadi ya Abiria Waliotumia Usafiri wa Anga, Mwaka 2020 - 2024**




| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 943,422 | 1,489,721 | 2,405,076 | 3,019,289 | 3,360,970 |
| Ndani ya nchi | 1,830,117 | 2,338,236 | 3,313,319 | 3,801,252 | 4,014,552 |
| Jumla | 2,773,539 | 3,827,957 | 5,718,395 | 6,820,541 | 7,375,522 |

307. Mwaka 2024, safari za ndege zilikuwa 277,022 ikilinganishwa na safari 199,711 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 38.7. Aidha, tani 42,747.4 za mizigo zilisafirishwa mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 36,265.0 zilizosafirishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 17.9. Kuongezeka kwa safari za ndege na mizigo kulitokana na kuendelea kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga pamoja na ongezeko la idadi ya watalii nchini.

**Kielelezo Na. 12.2: Safari za Ndege, Mwaka 2020 - 2024**




| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 17,885 | 26,414 | 195,619 | 41,090 | 46,447 |
| Ndani ya nchi | 103,370 | 126,908 | 156,060 | 158,621 | 230,575 |
| Jumla | 121,255 | 153,322 | 195,619 | 199,711 | 277,022 |

308. Mwaka 2024, Shirika la ndege Tanzania - ATCL liliendelea kutoa huduma katika vituo vya ndani 13 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Aidha, Shirika lilitoa huduma katika vituo 12 nje ya nchi ikilinganishwa na vituo 10 mwaka 2023 ambapo vituo vilivyoongezeka vilikuwa vya Dubai na Johannesburg. Katika kipindi hicho, Shirika lilisafirisha abiria 1,164,210 ikilinganishwa na abiria 1,070,347 waliosafirishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na kufunguliwa kwa vituo vya nje vya Dubai na Johannesburg. Aidha, Shirika lilisafirisha tani 9,364 za mizigo ndani na nje ya nchi mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 4,065 mwaka 2023. Ongezeko la usafirishaji wa mizigo lilitokana na Shirika kupata kibali cha kusafirisha mizigo kutokea Kenya, pamoja na kuongezeka kwa safari za nje zinazovutia usafirishaji wa mizigo kupitia ndege za abiria.

**Usafiri na Usafirishaji kwa Njia ya Maji**

309. Mwaka 2024, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania - TASAC lilitoa leseni 12 za waendeshaji wa shughuli za bandari ikilinganishwa na leseni 11 zilizotolewa mwaka 2023. Hii ilitokana na muda wa uhai wa leseni kuwa wa kipindi cha miaka mitatu, mitano na 10 kulingana na ukubwa na aina ya shughuli za bandari. Katika kipindi hicho, mawakala 1,188 wa ugomboaji shehena inayopita katika maeneo ya kiforodha walipewa leseni ikilinganishwa na mawakala 1,143 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Aidha, leseni za wakusanyaji/watawanyaji wa mizigo zilikuwa 46 ikilinganishwa na leseni 54 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 14.8. Upungufu huo ulitokana na kuchelewa kuhuisha leseni hizo kwa baadhi ya watoa huduma katika sekta ya usafirishaji majini.

310. Mwaka 2024, Shirika lilitoa leseni 58 za wapimaji uzito wa makasha ikilinganishwa na leseni 48 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.8. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa unaosimamiwa na Shirika la Bahari Duniani - IMO kuhusu Usalama wa Maisha Majini unaolenga kuimarisha usalama wa huduma za meli na bandari. Aidha, leseni za bandari kavu zilizotolewa zilifikia 96 mwaka 2024 kutoka leseni 77 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 24.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa kwa leseni za bandari kavu za magari kulikosababishwa na kuongezeka kwa magari yanayoingia nchini na bandari kutokuhifadhi magari katika eneo la bandari. Vilevile, leseni za uwakala wa meli zilifikia 56 mwaka 2024 kutoka leseni 41 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 36.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa fursa za biashara ya uwakala wa meli pamoja na utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Uwakala wa Meli, Sura 415 yaliyopunguza mawanda ya shughuli za TASAC na kuhamisha baadhi ya shughuli kwa sekta binafsi.

**Jedwali Na. 12.7: Leseni Zilizotolewa kwa Watoa Huduma, Mwaka 2020 - 2024**

| Na. | Aina ya leseni | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ugomboaji wa shehena | 903 | 947 | 1,129 | 1,143 | 1,188 | 3.9 |
| 2 | Uwakala wa meli | 24 | 24 | 34 | 41 | 56 | 36.6 |
| 3 | Ukusanyaji wa mizigo | 31 | 32 | 33 | 54 | 46 | -14.8 |
| 4 | Upimaji wa makasha | 47 | 54 | 47 | 48 | 58 | 20.8 |
| 5 | Bandari Kavu | 42 | 46 | 69 | 77 | 96 | 24.7 |

**Chanzo:** Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania

311. Mwaka 2024, TASAC ilitoa leseni kwa vyombo vidogo 10,675 vya usafiri majini vyenye urefu usiozidi mita 24 ikilinganishwa na vyombo vidogo 10,170 vilivyopata leseni mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na leseni. Aidha, Shirika lilisajili vyombo vikubwa 85 vya usafiri majini vyenye urefu wa zaidi ya mita 24 mwaka 2024 ikilinganishwa na vyombo vikubwa 94 vilivyosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 9.6. Hii ilitokana na kuchelewa kwa wamiliki wa vyombo kuhuisha usajili wa vyombo vyao.

312. Mwaka 2024, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA ilihudumia tani 29,050,200 za shehena ikilinganishwa na tani 26,358,900 zilizohudumiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.2. Ongezeko hilo lilitokana na: Mamlaka kuendelea kuboresha miundombinu na huduma katika bandari; kuendelea kujitangaza katika nchi za jirani ambazo ziliendelea kutumia Bandari ya Dar es Salaam; na kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi uliotokana na uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam.

**Jedwali Na. 12.8: Shehena Zilizohudumiwa na TPA, Mwaka 2020 - 2024 (Tani '000)**

| Bandari | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bandari Kuu za Mwambao** | | | | | | |
| Dar es Salaam | 15,875.9 | 17,025.0 | 19,870.2 | 22,916.2 | 24,509.4 | 7.0 |
| Tanga | 475 | 844 | 968.6 | 976.1 | 1,260.1 | 29.1 |
| Mtwara | 189 | 213 | 1,222.00 | 1,671.1 | 2,379.9 | 42.4 |
| **Jumla ndogo** | **16,539.9** | **18,082.0** | **22,060.8** | **25,563.4** | **28,149.3** | **10.1** |
| **Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu** | | | | | | |
| Kilwa, Lindi, Mafia, Bagamoyo na Pwani | 107 | 191 | 207.8 | 229.8 | 377.0 | 64.1 |
| Mwanza | 142 | 234 | 283.5 | 267.9 | 194.6 | -27.4 |
| Kigoma | 250 | 265 | 313.4 | 286.2 | 318.8 | 11.4 |
| Kyela | 17 | 11 | 13.7 | 11.6 | 10.4 | -10.3 |
| **Jumla ndogo** | **516** | **701** | **818.4** | **795.5** | **900.8** | **13.2** |
| **Jumla Kuu** | **17,055.9** | **18,783.0** | **22,879.2** | **26,358.9** | **29,050.2** | **10.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

313. Mwaka 2024, Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zilihudumia makasha 1,075,555 yenye urefu wa futi 20 ikilinganishwa na makasha 993,899 yaliyohudumiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Kati ya hayo, makasha 1,010,430 yalihudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam, Tanga (makasha 8,735) na Mtwara (makasha 47,548). Ongezeko la makasha lilitokana na uboreshaji wa miundombinu na vifaa uliofanyika katika bandari za Tanga na Mtwara pamoja na uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam.

**Jedwali Na. 12.9: Shehena ya Makasha Yenye Urefu wa Futi 20 Yaliyohudumiwa, Mwaka 2020 - 2024**

| Bandari | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | | | | | | |
| *Terminal 1* | 108,227 | 110,732 | 169,771 | 814,695 | 212,268 | -74.0 |
| *Terminal 2* | 601,654 | 606,169 | 715,707 | 163,954 | 798,162 | * |
| **Jumla ndogo** | 709,881 | 716,901 | 885,478 | 978,649 | 1,010,430 | 3.3 |
| Tanga | 7,401 | 5,817 | 7,712 | 7,299 | 8,735 | 19.7 |
| Mtwara | 19 | 90 | 0 | 7,951 | 56,390 | * |
| **Jumla ndogo** | 7,420 | 5,907 | 7,712 | 15,250 | 65,125 | * |
| **Jumla Kuu** | **717,301** | **722,808** | **893,190** | **993,899** | **1,075,555** | **7.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
* Badiliko ni zaidi ya asimilia 100

314. Mwaka 2024, Mamlaka ilihudumia abiria 3,907,224 ikilinganishwa na abiria 3,864,140 waliohudumiwa mwaka 2023. Ongezeko la abiria lilichangiwa na meli nyingine

kuanza kutoa huduma katika Bandari ya Tanga ikiwa ni mbadala wa meli iliyositisha kutoa huduma kipindi cha nyuma.

**Jedwali Na. 12.10: Abiria Waliohudumiwa, Mwaka 2020 - 2024**

| Bandari | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 1,639,683 | 2,303,471 | 2,300,228 | 2,302,998 | 2,420,905 | 5.1 |
| Tanga | 55,403 | 49,246 | 98,374 | 26,599 | 62,904 | * |
| Mwanza | 1,176,918 | 1,461,900 | 1,394,654 | 1,257,947 | 1,211,112 | -3.7 |
| Kigoma | 1,781 | 43,364 | 168,836 | 206,423 | 197,109 | -4.5 |
| Kyela | 5,670 | 17,209 | 37,565 | 70,173 | 15,194 | -78.4 |
| **Jumla** | **2,879,455** | **3,875,190** | **3,999,657** | **3,864,140** | **3,907,224** | **1.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
* Badiliko ni zaidi ya asimilia 100

**Muda wa Meli Kukaa Bandarini**

315. Mwaka 2024, muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa wastani wa siku 12.3 ikilinganishwa na wastani wa siku 10.6 mwaka 2023. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini kwa meli za makasha na shehena ya kawaida ulikuwa siku 12.7 na siku 13.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na siku 9.0 na siku 8.0, mtawalia mwaka 2023. Kuongezeka kwa muda wa meli kukaa bandarini kulitokana na miundombinu isiyotosheleza katika bandari ya Dar es Salaam iliyosababisha kasi ndogo ya upakuaji na upakiaji wa shehena kwenye meli. Kwa upande mwingine, muda wa meli za mafuta kukaa bandarini ulipungua na kufikia wastani wa siku 10.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na siku 14.7 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 12.11: Muda wa Meli Kukaa Bandarini, Mwaka 2020 - 2024 (Siku)**

| Kitengo/Meli | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Makasha | 3.3 | 3.8 | 10.4 | 9.0 | 12.7 |
| Shehena ya kawaida | 3.1 | 3.7 | 7.4 | 8.0 | 13.7 |
| Mafuta | 5.6 | 6.5 | 14.3 | 14.7 | 10.4 |
| **Wastani** | **4.0** | **4.7** | **10.7** | **10.6** | **12.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

316. Katika kuongeza ufanisi wa bandari, Serikali imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari nchini kwa kuingia ubia na Kampuni za DP World na Tanzania East Africa Gateway Terminal Limited (TEAGTL) katika kuendeleza na kuendesha baadhi ya maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam. Lengo la kushirikisha sekta binafsi ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari nchini ili ziweze kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Aidha, wawekezaji hao wamewezesha upatikanaji wa vifaa na mitambo ya kisasa na mifumo ya TEHAMA inayoendelea kuleta ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za bandari.

317. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari 2025, maboresho na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika Bandari ya Dar es Salaam umeleta mafanikio mbalimbali ikiwemo: kupungua kwa muda wa meli kusubiri nangani kutoka wastani wa siku 46 hadi wastani wa siku saba (7) kwa meli za mizigo mchanganyiko (General cargo) na kichele (bulk cargo); kupungua kwa muda wa kuhudumia meli za makasha gatini kutoka wastani wa siku 10 hadi siku tatu (3); kuongezeka kwa wastani wa shehena ya makasha inayohudumiwa kwa mwezi kutoka makasha (TEUs) 17,000 hadi makasha (TEUs) 25,000 ambalo ni ongezeko la asilimia 47.1; na kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yasiyo ya kikodi yanayokusanywa na taasisi mbalimbali za umma zinazotoa huduma bandarini.

**Shehena za Nchi Jirani**

318. Mwaka 2024, Bandari ya Dar es Salaam ilipitisha shehena za nchi jirani za tani 9,187,061 ikilinganishwa na tani 8,871,438 zilizopitishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kuendelea kutangaza fursa za bandari kupitia ofisi za masoko katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Rwanda, na Burundi.

**Jedwali Na. 12.12: Shehena za Nchi Jirani, Mwaka 2020 - 2024 (Tani)**

| Nchi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zambia | 1,159,013 | 1,507,746 | 1,975,793 | 2,311,278 | 2,248,505 | -2.7 |
| D.R. Congo | 1,840,657 | 2,357,867 | 3,379,124 | 3,726,938 | 4,180,902 | 12.2 |
| Burundi | 476,807 | 507,017 | 520,714 | 385,975 | 349,591 | -9.4 |
| Rwanda | 1,239,238 | 1,366,290 | 1,483,175 | 1,677,505 | 1,672,431 | -0.3 |
| Malawi | 407,472 | 471,385 | 557,826 | 581,981 | 594,281 | 2.1 |
| Uganda | 153,995 | 138,805 | 192,912 | 113,630 | 60,682 | -46.6 |
| Nyinginezo* | 63,104 | 72,488 | 127,546 | 74,131 | 80,669 | 8.8 |
| **Jumla** | **5,340,287** | **6,421,598** | **8,237,090** | **8,871,438** | **9,187,061** | **3.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
*Msumbiji, Sudani, Kenya, Comoro, Angola na Zimbabwe

**Uchukuzi Kwenye Maziwa**

319. Mwaka 2024, Kampuni ya Huduma za Meli - MSCL ilisafirisha abiria 432,309 ikilinganishwa na abiria 279,566 waliosafirishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 54.6. Katika kipindi hicho, Kampuni ilisafirisha tani 100,845 za mizigo ikilinganishwa na tani 44,598.70 zilizosafirishwa mwaka 2023. Ongezeko la mizigo na abiria waliosafirishwa lilitokana na kuendelea kuimarika kwa huduma za usafirishaji.

**Kampuni ya Meli ya China na Tanzania**

320. Mwaka 2024, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania - SINOTASHIP ilisafirisha tani 615,375 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani 619,870 zilizosafirishwa mwaka 2023. Kupungua kwa shehena ya mizigo kilitokana na meli kusimamisha safari kwa muda

ili kufanyiwa matengenezo. Aidha, Kampuni ilihudumia makasha 81,993 katika Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara ikilinganishwa na makasha 73,599 yaliyohudumiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 11.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa biashara ya uwakala na meli zinazoleta na kuondosha mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na Mtwara pamoja na kuimarisha mikakati ya kutafuta mizigo inayosafirishwa nje ya nchi ikiwemo kutumia bei shindani.

**Huduma za Hali ya Hewa**

321. Mwaka 2024, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania - TMA ilihudumia ndege 54,357 ikilinganishwa na ndege 48,516 zilizohudumiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.0. Aidha, jumla ya meli/boti 127,143 zilihudumiwa mwaka 2024 ikilinganishwa na meli/boti 131,749 zilizohudumiwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 3.5. Hii ilitokana na baadhi ya vyombo kusimamisha shughuli kutokana na taarifa za tahadhari kuhusu kuwepo kwa vimbunga ("Hidaya" na "Ialy") katika eneo la pwani ya nchi hususan pwani ya kusini pamoja na vipindi vya mvua kubwa na upepo mkali katika maeneo ya maziwa makuu (Ziwa Victoria na Tanganyika). Vilevile, Mamlaka ilitoa huduma mahsusi kwa wateja 1,642 mwaka 2024 ikilinganishwa na wateja 1,420 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.6.

322. Mwaka 2024, kiwango cha usahihi wa utabiri kilifikia asilimia 88.2 ikilinganishwa na asilimia 86.4 mwaka 2023. Kiwango hicho ni zaidi ya kiwango cha asilimia 70 kinachokubalika Kimataifa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani. Ongezeko la kiwango cha usahihi wa utabiri wa hali ya hewa lilichangiwa na Serikali kuendelea kuwekeza katika mitambo na vifaa vya kisasa vya utabiri wa hali ya hewa.

**Jedwali Na. 12.13: Viashiria vya ufanisi wa huduma za hali ya hewa, Mwaka 2020 - 2024**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya ndege zilizohudumiwa | 27,348 | 35,511 | 45,891 | 48,516 | 54,357 | 12 |
| Idadi ya Meli/boti zilizohudumiwa | 8,835 | 31,736 | 66,002 | 131,749 | 127,143 | -3.5 |
| Huduma mahsusi kwa sekta za kiuchumi na miradi ya kielelezo | - | 623 | 674 | 1,420 | 1,642 | 15.6 |
| Usahihi wa utabiri | 87.9 | 88.3 | 88.5 | 86.4 | 88.2 | 1.8 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

**Jedwali Na. 59: SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+**

| Maelezo | Kipimo | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani-Kilometa: | | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 3,937 | 863,107 | 32,095 | 32,927 | 65,968 | 68,806 | 71,872 | 133,124 | 204,221 |
| Zilizotumika | 000 | 1,756 | 89,092 | 17,526 | 18,944 | 33,655 | 38,930 | 48,464 | 81,137 | 127,320 |
| Matumizi | % | 47 | 10 | 55 | 58 | 51 | 57 | 67 | 61 | 62 |
| **Viti - kilometa:** | | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 37,877 | 225,259 | 231,943 | 321,771 | 557,216 | 552,682 | 690,408 | 1,227,755 | 1,766,296 |
| Vilivyotumika | 000 | 20,692 | 122,532 | 158,203 | 220,433 | 347,101 | 417,706 | 552,968 | 788,162 | 1,171,348 |
| Matumizi | % | 54.6 | 54.4 | 68.2 | 68.5 | 62.3 | 75.6 | 80.1 | 64.2 | 66.3 |
| Abiria ++ | 000 | 28 | 129 | 279 | 627 | 434 | 657 | 929 | 1,066 | 940,653 |
| Mizigo ya ziada | Ton | 1 | 41 | 55 | 96 | 86 | 75 | 54 | 0 | 0 |
| Mizigo mingine | Ton | 7 | 50 | 220 | 696 | 438 | 526 | 3,030 | 2,992 | 4,054 |
| Mizigo ya Posta | Ton | - | 32 | 119 | 295 | 61 | 21 | 72 | 91 | 158 |

**Chanzo:** Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

# SURA YA 13

# MAWASILIANO, HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

## MAWASILIANO

### Huduma za Posta

323. Mwaka 2024, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 789,299 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 1,146,627 zilizosafirishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 31.2. Upungufu huo ulitokana na kukua kwa matumizi ya njia za kidigitali katika mawasiliano pamoja na ushindani mkubwa kutoka kwa wasafirishaji binafsi. Aidha, barua 150,090 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2024 ikilinganishwa na barua 296,657 zilizosafirishwa nje ya nchi mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 49.4. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya mashirika ya ndege kusitisha baadhi ya safari katika nchi zenye vifurushi vingi, ikiwemo Australia.

324. Mwaka 2024, vifurushi 18,542 vilisafirishwa ndani ya nchi ikilinganishwa na vifurushi 18,760 vilivyosafirishwa mwaka 2023. Upungufu huo ulitokana na ushindani mkubwa kutoka katika sekta binafsi. Aidha, vifurushi vilivyosafirishwa nje ya nchi vilipungua kwa asilimia 4.5 na kufikia 2,340 mwaka 2024 ikilinganishwa na vifurushi 2,450 mwaka 2023.

325. Mwaka 2024, rejesta 89,381 zilisafirishwa nchini na Shirika ikilinganishwa na rejesta 86,014 zilizosafirishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Kwa upande mwingine, rejesta 2,915 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2024 ikilinganishwa na rejesta 7,751 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 62.4. Upungufu huo ulitokana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokana na ongezeko la matumizi ya barua pepe katika mawasiliano.

326. Mwaka 2024, Shirika lilituma nyaraka na vipeto 499,430 kwa njia ya haraka nchini ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 519,607 vilivyotumwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Upungufu huo ulitokana na ushindani mkubwa wa kibiashara kutoka sekta binafsi pamoja na uchakavu wa vitendea kazi. Aidha, nyaraka na vipeto vilivyotumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka vilifikia 15,506 mwaka 2024 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 7,923 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 95.7. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya wateja wakubwa kutuma nyaraka na vipeto vingi kwenda nje ya nchi pamoja na kuingia mikataba na mashirika ya ndege ya kimataifa ili kupanua wigo wa kibiashara. Vilevile, barua na nyaraka zilizopokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji ziliongezeka kwa asilimia 42.6 na kufikia 46,586 mwaka 2024 ikilinganishwa na barua na nyaraka 32,665 zilizopokelewa na

kusambazwa mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa viwango vya usambazaji barua na uingizaji wa taarifa kwenye mifumo.

327. Mwaka 2024, miamala ya fedha 14,161 ilifanyika kupitia njia ya Western Union ikilinganishwa na miamala 24,197 iliyofanyika mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 41.5. Upungufu huo ulitokana na kuimarika kwa mifumo mbadala ya kutuma fedha, ikiwemo benki na mitandao ya simu. Aidha, miamala 964 ya fedha ilifanyika kupitia njia ya Money Gram mwaka 2024 ikilinganishwa na miamala 1,121 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 14.0. Upungufu huo ulitokana na mabadiliko ya utaratibu wa uendeshaji wa biashara za Money Gram uliosababisha baadhi ya ofisi kufungwa.

**Huduma za Simu**

328. Mwaka 2024, kadi za simu za kiganjani ziliongezeka kwa asilimia 23.6 na kufikia 86,769,161 kutoka kadi 70,215,144 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya mawasiliano pamoja na matumizi ya simu za kiganjani katika utoaji wa huduma mbalimbali ikiwemo za fedha. Aidha, kadi za simu za mezani ziliongezeka na kufikia 78,299 mwaka 2024 kutoka kadi za simu za mezani 75,732 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya simu za mezani majumbani, ofisini na hotelini kwa kuwa simu hizi kwasasa hutumia laini kama simu za kiganjani badala ya miundombinu ya waya pamoja na kuimarika kwa miundombinu ya mawasiliano.

329. Mwaka 2024, wastani wa gharama za kupiga simu ndani ya mtandao ziliendelea kuwa shilingi 26 kwa dakika na nje ya mtandao shilingi 28 kwa dakika kama ilivyokuwa mwaka 2023. Hii ilitokana na uwepo wa ushindani katika soko la mawasiliano. Aidha, wastani wa bei za kupiga simu kwenye vifurushi ilikuwa shilingi 4.79 kwa dakika ndani ya mtandao na shilingi 6.27 kwa dakika nje ya mtandao. Vilevile, gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki zilikuwa shilingi 597.40 kwa dakika mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi 754 kwa dakika mwaka 2023. Kupungua kwa gharama za kupiga simu kwenye vifurushi na ndani ya Afrika Mashariki kulitokana na kuongezeka kwa ushindani kwa watoa huduma za mawasiliano wa kimataifa. Katika kipindi hicho, gharama za kupiga simu kwenda mataifa mengine zilikuwa shilingi 2,016.70 kwa dakika ikilinganishwa na shilingi 1,960 mwaka 2023.

**Huduma za Intaneti**

330. Mwaka 2024, kadi za simu zinazotumia intaneti ziliongezeka kwa asilimia 33.7 na kufikia milioni 48.0 ikilinganishwa na kadi za simu milioni 35.9 mwaka 2023. Aidha, matumizi ya intaneti nchini yaliongezeka kwa asilimia 91.1 na kufikia Gigabaiti (GB) milioni 1,961 mwaka 2024 ikilinganishwa na Gigabaiti milioni 1,026 mwaka 2023.

Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa huduma mbalimbali zinazotolewa kwa njia ya mtandao wa intaneti kwa sekta ya umma na binafsi.

**Jedwali Na. 13.1: Watumiaji wa Intaneti Nchini, Mwaka 2020 - 2024**

| Aina ya Huduma | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *Fixed wireless* | 510,683 | 1,034,958 | 6,003 | 8,315 | 83,201 | * |
| *Mobile wireless* | 27,371,350 | 25,176,367 | 31,100,860 | 35,815,632 | 47,859,272 | 34 |
| *Fixed wired* | 588,472 | 3,647,434 | 65,681 | 61,645 | 85,754 | 39 |
| **Jumla** | **28,470,505** | **29,858,759** | **31,172,544** | **35,885,592** | **48,028,227** | 34 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
***Badiliko zaidi ya asilimia 100**

**Utoaji wa Leseni za Mawasiliano**

331. Mwaka 2024, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni 316 za huduma mbalimbali za mawasiliano ikilinganishwa na leseni 352 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 10.2. Upungufu huo ulitokana na mabadiliko ya masharti ya utoaji leseni yaliyotolewa kupitia mwongozo wa utoaji leseni wa mwaka 2024.

**Jedwali Na. 13.2: Leseni Zilizotolewa, Mwaka 2020 - 2024**

| Na. | Aina ya Leseni | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Huduma za mawasiliano daraja B | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2. | Maudhui ya redio | 15 | 13 | 15 | 29 | 29 |
| 3. | Maudhui ya luninga | 7 | 9 | 9 | 5 | 1 |
| 4. | Ufungaji na utengenezaji wa vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki | 33 | 50 | 20 | 65 | 84 |
| 5. | Kuingiza nchini vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki | 30 | 44 | 45 | 42 | 49 |
| 6. | Kusambaza nchini vifaa vya mawasiliano | 12 | 16 | 20 | 25 | 8 |
| 7. | Kuuza vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki | 606 | 201 | 29 | 0 | 0 |
| 8. | Huduma za kusafirisha vifurushi na vipeto | 39 | 20 | 22 | 61 | 36 |
| 9. | V-sat | 57 | 21 | 69 | 11 | 7 |
| 10. | Maudhui ya mtandaoni | 305 | 151 | 0 | 109 | 91 |
| 11. | Maudhui kutokana na matumizi | 15 | 21 | 17 | 5 | 11 |
| **Jumla** | | 1,125 | 546 | 246 | 352 | 316 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

332. Hadi Desemba 2024, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulifikia urefu wa kilometa 14,795 zilizounganishwa kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara kutoka kilometa 11,436 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 29.4. Ongezeko hilo lilitokana na upanuzi wa

Mkongo wa Taifa ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mawasiliano ya simu na intaneti ndani ya nchi na nchi jirani kwa lengo la kufikia mapinduzi ya kidigitali. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano yalikuwa shilingi milioni 51,355 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 56,966 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 9.8. Upungufu huo ulitokana na kusitishwa kwa huduma kwenye baadhi ya maeneo ili kuwezesha ujenzi wa Mkongo kwenye maeneo mapya.

**Huduma za Mawasiliano**

333. Hadi Desemba 2024, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano ulifikisha huduma za mawasiliano katika kata 1,705 zenye vijiji 4,982 na wakazi 23,582,852 ikilinganishwa na kata 1,219 zilizokuwa na vijiji 3,648 na wakazi 14,926,860 mwaka 2023. Kuongezeka kwa kata, vijiji na wakazi waliofikiwa na huduma za mawasiliano kulitokana na utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano Vijijini. Katika kipindi hicho, minara 358 ilikamilika na kuanza kutoa huduma ya mawasiliano ya simu ikilinganishwa na minara 122 mwaka 2023. Kati ya hiyo, Halotel ilikuwa na minara 28, TTCL minara 30, Airtel minara 109, Yas minara 93 na Vodacom minara 98.

**HABARI**

334. Hadi Desemba 2024, kulikuwa na magazeti 354, vituo vya redio 250 na vituo vya runinga 67 vilivyosajiliwa na kupewa leseni kutoka magazeti 328, vituo vya redio 221 na vituo vya runinga 52[3] mwaka 2023. Ongezeko la vituo vya redio lilitokana na kukua kwa hitaji la kupashana habari na kupungua kwa gharama ya leseni kwa baadhi ya huduma kufuatia mabadiliko ya kanuni. Katika kipindi hicho, magazeti na majarida 26 yalisajiliwa ikilinganishwa na magazeti na majarida 32 yaliyosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 28. Aidha, vituo vipya vya redio 29 vilisajiliwa mwaka 2024 ikilinganishwa na vituo 18 vilivyosajiliwa mwaka 2023. Vilevile, vituo vipya 15 vya runinga vilisajiliwa mwaka 2024 ikilinganishwa na vituo 18 vilivyosajiliwa mwaka 2023. Kwa upande mwingine, blogu sita (6) zilisajiliwa mwaka 2024 ikilinganishwa na blogu 22 zilizosajiliwa mwaka 2023 na kufikisha jumla ya blogu 66 zilizosajiliwa nchini.

[3] Takwimu za vituo vya runinga na radio za mwaka 2023 zimefanyiwa marejeo.

**Jedwali 13.3: Usajili wa Vyombo vya Habari, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Idadi ya Magazeti/Majarida | Idadi ya Vituo vya Redio | Idadi ya Vituo vya Runinga | Idadi ya Blogu |
|---|---|---|---|---|
| 2020 | 24 | 15 | 1 | 40 |
| 2021 | 26 | 9 | 10 | 15 |
| 2022 | 46 | 15 | 9 | 6 |
| 2023 | 32 | 18 | 18 | 22 |
| 2024 | 26 | 29 | 15 | 6 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

335. Mwaka 2023/24, Shirika la Utangazaji Tanzania - TBC liliendelea kuongeza usikivu wa redio kwa kufunga mitambo ya redio masafa ya FM katika wilaya 14 ikilinganishwa na wilaya 20 mwaka 2022/23.

**Huduma za Utangazaji**

336. Mwaka 2024, watumiaji wa huduma za utangazaji (kwa kutumia idadi ya ving'amuzi vilivyolipiwa angalau mara moja ndani ya miezi mitatu) walikuwa 2,148,690 ikilinganishwa na watumiaji 3,678,199 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 41.6. Kati ya hao, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia satelaiti walifikia 1,568,241 kutoka watumiaji 1,880,636 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 16.6. Aidha, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini walikuwa 563,682 ikilinganishwa na watumiaji 1,781,340 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 68.4. Upungufu huo ulitokana na takwimu za mwaka 2024 kujumuisha visimbuzi vinavyotoa huduma za kutazama chaneli za kulipia pekee (vilivyolipiwa angalau mara moja) wakati takwimu za mwaka 2023 zilijumuisha visimbuzi vyote vilivyopo sokoni. Vilevile, watumiaji wa *cable television* waliongezeka na kufikia 16,767 mwaka 2024 kutoka watumiaji 16,223 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.4.

**Jedwali 13.4: Huduma za Utangazaji Zilizotolewa Nchini, Mwaka 2020 - 2024**

| Aina ya Huduma | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Visimbuzi vinavyotumia Mitambo iliyosimikwa ardhini - DTT | 1,472,317 | 1,613,031 | 1,667,465 | 1,781,340 | 563,682 | -68.4 |
| Visimbuzi vinavyotumia Satelaiti - DTH | 1,341,686 | 1,577,315 | 1,702,056 | 1,880,636 | 1,568,241 | -16.6 |
| Cable Television | 158,224 | 29,403 | 85,802 | 16,223 | 16,767 | 3.4 |
| **Jumla** | **2,769,841** | **3,219,749** | **3,455,323** | **3,678,199** | **2,148,690** | **-41.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## MAENDELEO YA UTAMADUNI

### Maendeleo ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa

337. Mwaka 2024, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliandaa na kurusha hewani vipindi 2,311 kuhusu sarufi na fasihi ya kiswahili kupitia redio na runinga ikilinganishwa na vipindi 1,187 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 94.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya lugha ya kiswahili ndani na nje ya nchi. Aidha, miswada ya vitabu vilivyopata ithibati ya lugha vilivyokusudiwa kutumika shuleni vilikuwa 62 mwaka 2024 ikilinganishwa na miswada ya vitabu 30 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na BAKITA kutangaza huduma za ithibati zinazotolewa kwa mujibu wa sheria pamoja na kuhamasisha vitabu vyote vinavyoandikwa kwa lugha ya kiswahili kupatiwa ithibati ya lugha.

338. Mwaka 2024, BAKITA ilisajili katika kanzidata wataalamu 78 wa Kiswahili ikilinganishwa na wataalamu 328 waliosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 76.2. Hii ilitokana na kupungua kwa mwitikio wa wadau kujisajili katika kanzidata. Hadi Desemba 2024, watanzania wanaofundisha Kiswahili nje ya nchi walifikia 498 kutoka watanzania 203 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ubidhaishaji Kiswahili wa Mwaka 2022 - 2032.

339. Mwaka 2024, BAKITA lilisajili vituo saba (7) vya kufundisha kiswahili kwa raia wa kigeni ikilinganishwa na vituo 15 vilivyosajiliwa mwaka 2023. Idadi hiyo inafikisha vituo vya kufundisha kiswahili kwa wageni vilivyosajiliwa kuwa 51 kutoka vituo 44 kwa mwaka 2023.

### Uhariri na Tafsiri ya Nyaraka

340. Mwaka 2024, BAKITA ilitafsiri nyaraka 6,234 ikilinganishwa na nyaraka 1,380 zilizotafsiriwa mwaka 2023. Kuongezeka kwa nyaraka zilizotafsiriwa kulitokana na jitihada za kutangaza huduma za tafsiri kwa wadau mbalimbali. Kati ya hizo, nyaraka 584 zilitafsiriwa kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya kiswahili; nyaraka 95 kutoka lugha ya kiswahili kwenda lugha ya kiingereza; nyaraka 533 kutoka lugha ya kifaransa kwenda lugha ya kiingereza; na nyaraka 924 kutoka lugha ya kiarabu kwenda lugha ya kiingereza. Aidha, nyaraka 3,038 zilitafsiriwa kutoka lugha ya kichina kwenda lugha za kiingereza na kiswahili na nyaraka 1,060 zilitafsiriwa kutoka lugha mbalimbali kwenda lugha ya kiingereza na kiswahili. Vilevile, Baraza liliratibu huduma ya ukalimani katika mikutano 14 ya kitaifa na kimataifa mwaka 2024 ikilinganishwa na mikutano 11 mwaka 2023.

341. Mwaka 2024, Baraza lilihariri miswada mitano (5) ikilinganishwa na miswada 10 iliyohaririwa mwaka 2023. Kupungua kwa miswada iliyohaririwa kulitokana na baadhi ya kampuni za uchapishaji wa vitabu kutumia wahariri binafsi. Kwa upande mwingine,

BAKITA ilibaini makosa 102 ya matumizi ya lugha ya kiswahili kupitia vyombo vya habari mwaka 2024 ikilinganishwa na makosa 192 yaliyobainika mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 46.9. Upungufu huo ulitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu kwa waandishi na watangazaji kuhusu matumizi sahihi ya lugha yanayozingatia ufasaha na usanifu.

**Jedwali Na. 13.5: Huduma Zilizotolewa na BAKITA, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Vipindi vya Redio na Runinga | Huduma ya Ithibati | Huduma ya Tafsiri | Huduma ya Ukalimani | Huduma ya Uhariri | Makosa ya Matumizi ya Lugha Vyombo vya Habari |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | 1,020 | 213 | 869 | 0 | 41 | 1,380 |
| 2021 | 1,008 | 203 | 1,148 | 0 | 23 | 1,205 |
| 2022 | 1,064 | 110 | 1,375 | 12 | 20 | 1,005 |
| 2023 | 1,187 | 30 | 1,380 | 11 | 10 | 192 |
| 2024 | 2,311 | 62 | 6,324 | 14 | 5 | 102 |

**Chanzo:** Baraza la Kiswahili la Taifa

## MAENDELEO YA SANAA

### Vibali vya Utayarishaji wa Filamu

342. Mwaka 2024, vibali 247 vya utayarishaji wa filamu vilitolewa na Bodi ya Filamu Tanzania ikilinganishwa na vibali 276 vilivyotolewa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 10.5. Upungufu huo ulitokana na kukua kwa teknolojia inayotumia vifaa vidogo kama simu janja kutumika kurekodi filamu zenye ubora.

### Usajili wa Kazi za Sanaa

343. Mwaka 2024, Taasisi ya Hakimiliki Tanzania - COSOTA ilisajili wabunifu wa kazi za sanaa 428 ikilinganishwa na wabunifu 518 waliosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 17.4. Aidha, kazi za sanaa zilizosajiliwa na COSOTA zilikuwa 1,409 mwaka 2024 ikilinganishwa na kazi 2,379 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 40.8. Upungufu wa usajili wa wabunifu na kazi za sanaa ulitokana na mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya Mwaka 2022 yaliyosababisha usajili wa wabunifu kufanywa na Chama cha Haki za Muziki Tanzania - TAMRISO.

344. Mwaka 2024, COSOTA ilitoa vyeti vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki 2,074 ikilinganishwa na vyeti 1,357 vilivyotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 52.8. Hii ilitokana na wabunifu wengi kutambua haki zao na kufahamu umuhimu wa kuwa na nyaraka ili kupunguza migogoro.

**Jedwali Na. 13.6: Huduma Zilizotolewa na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania, Mwaka 2020 - 2024**

| Na. | Huduma | Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| 1 | Usajili wa wabunifu wa kazi za sanaa | 1,436 | 2,066 | 424 | 518 | 428 |
| 2 | Usajili wa kazi za ubunifu | 1,431 | 3,827 | 3,904 | 2,379 | 1,409 |
| 3 | Vyeti vya umiliki | 1,431 | 3,835 | 1,430 | 1,357 | 2,074 |
| 4 | Leseni | 354 | 370 | 621 | 360 | 0 |

**Chanzo**: Taasisi ya Hakimiliki Tanzania

### Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo

345. Mwaka 2024, vikundi vya sanaa na utamaduni vilivyoshiriki katika Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo viliongezeka kwa asilimia 81.4 na kufikia vikundi 78 ikilinganishwa na vikundi 43 vilivyoshiriki mwaka 2023. Kati ya hivyo, vikundi 67 vilitoka ndani ya nchi na vikundi 11 vilitoka nje ya nchi. Ongezeko la vikundi vya sanaa lilitokana na matangazo yaliyotolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, ikiwemo mitandao ya kijamii.

### Usajili wa Wasanii katika Fani za Sanaa

346. Mwaka 2024, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) liliendelea kurasimisha kazi za sanaa nchini ambapo wasanii binafsi 992 walisajiliwa ikilinganishwa na wasanii 1,089 waliosajiliwa mwaka 2023. Kati ya usajili uliofanyika, wasanii wa muziki walikuwa 563 sawa na asilimia 56.8 ya wasanii wote, maonesho 260 (asilimia 26.2), na ufundi 169 (asilimia 17.0).

**Jedwali Na. 13.7: Wasanii wa Sanaa Waliosajiliwa, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Ufundi | Maonesho | Muziki | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2020 | 34 | 172 | 171 | 377 |
| 2021 | 68 | 197 | 201 | 466 |
| 2022 | 87 | 178 | 207 | 472 |
| 2023 | 225 | 179 | 685 | 1,089 |
| 2024 | 169 | 260 | 563 | 992 |

**Chanzo:** Baraza la Sanaa la Taifa

### Utoaji wa Tuzo za Kazi za Sanaa

347. Mwaka 2023/24, tuzo 47 zilitolewa kwa wasanii wa muziki wa kitanzania ikilinganishwa na tuzo 54 zilizotolewa mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 13.0. Kati ya hizo, tuzo 37 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 10 zilikuwa za nje ya nchi. Kupungua kwa idadi ya tuzo zilizotolewa kulitokana na maboresho ya kuondoa vipengele vilivyokosa ushindani mwaka 2022/23.

**Jedwali Na. 13.8: Tuzo za Muziki kwa Wasanii wa Kitanzania, Mwaka 2019/20 - 2023/24**

| Mwaka | Idadi ya Tuzo za Ndani | Idadi ya Tuzo za Nje | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2019/20 | 8 | 2 | 10 |
| 2020/21 | 15 | 13 | 28 |
| 2021/22 | 47 | 14 | 61 |
| 2022/23 | 44 | 10 | 54 |
| 2023/24 | 37 | 10 | 47 |

**Chanzo:** Baraza la Sanaa la Taifa

348. Mwaka 2024, tuzo za filamu 86 zilitolewa kwa wadau ikilinganishwa na tuzo 56 zilizotolewa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 53.6. Ongezeko hilo lilitokana na hamasa ya wadau kufanya matamasha katika kanda na mikoa. Kati ya tuzo zilizotolewa, tuzo 67 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 19 zilikuwa za nje ya nchi.

**Jedwali Na. 13.9: Tuzo za Filamu Zilizotolewa kwa Wasanii, Mwaka 2020 - 2024**

| Tuzo | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Tuzo za ndani | 2 | 33 | 50 | 41 | 67 |
| Tuzo za nje | 2 | 3 | 13 | 15 | 19 |
| **Jumla** | **4** | **36** | **63** | **56** | **86** |

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania

**Urasimishaji wa Kazi za Utamaduni na Sanaa**

349. Mwaka 2024, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliwezesha urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa 4,533 ikilinganishwa na kazi 2,386 zilizorasimishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 90.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wasanii kuhusu umuhimu wa kubadilisha sanaa kuwa biashara.

350. Mwaka 2024, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ulitoa mikopo kwa miradi 152 ya utamaduni na sanaa yenye thamani ya shilingi milioni 3,128.9 ikilinganishwa na miradi 97 yenye thamani ya shilingi milioni 2,148.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 45.6. Ongezeko hilo lilitokana na wasanii kufanya marejesho kwa wakati. Aidha, marejesho ya mikopo yalikuwa asilimia 95.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 91.6 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, ajira 449,531 zilizalishwa kupitia mikopo iliyotolewa ikilinganishwa na ajira 286,985 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 56.6.

**Jedwali Na. 13.10: Mikopo Iliyotolewa na Ajira Zilizozalishwa, Mwaka 2022 - 2024**

| Mwaka | Miradi | Ajira Zilizozalishwa | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 2022 | 5 | 14,732 | 185,000,000 |
| 2023 | 97 | 286,985 | 2,148,450,000 |
| 2024 | 152 | 449,531 | 3,128,900,000 |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

351. Mwaka 2024, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliwezesha mafunzo ya urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa kwa wasanii 5,841 ikilinganisha na wasanii 3,296 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 77.2. Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio wa wasanii kupata taarifa za umuhimu wa mafunzo kupitia vyombo vya habari.

## MAENDELEO YA MICHEZO

352. Mwaka 2024, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lilisajili vilabu vya michezo 152 ikilinganishwa na vilabu 154 vilivyosajiliwa mwaka 2023. Katika kipindi hicho, vyama vya michezo vilivyosajiliwa vilikuwa 45 ikilinganishwa na vyama 34 vilivyosajiliwa mwaka 2023. Kwa upande mwingine, vituo/shule za michezo zilizosajiliwa zilikuwa 49 mwaka 2024 ikilinganishwa na vituo/shule za michezo 28 zilizosajiliwa mwaka 2023. Aidha, wakuzaji/mawakala waliosajiliwa walikuwa 66 mwaka 2024 ikilinganishwa na wakuzaji/mawakala 59 waliosajiliwa mwaka 2023.

**Jedwali Na. 13.11: Usajili wa Wadau wa Michezo, Mwaka 2020 - 2024**

| Mwaka | Vilabu vya Michezo | Vyama vya Michezo | Vituo/shule za Michezo | Wakuzaji/ Mawakala wa Michezo | Taasisi za Michezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | 110 | 12 | 5 | 26 | 10 |
| 2021 | 216 | 15 | 22 | 60 | 9 |
| 2022 | 178 | 15 | 33 | 40 | 10 |
| 2023 | 154 | 34 | 28 | 59 | 0 |
| 2024 | 152 | 45 | 49 | 66 | 0 |

**Chanzo:** Baraza la Michezo la Taifa

## Jedwali Na. 60: HUDUMA ZA POSTA

| **Maelezo** | **Kipimo** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi Ndogo Posta | Namba | 66 | 57 | 46 | 40 | 29 | 29 | 29 | 31 |
| Franchised Post Offices | Namba | 87 | 87 | 79 | 72 | 70 | 70 | 70 | 63 |
| Ofisi Kubwa | Namba | 154 | 157 | 139 | 132 | 144 | 144 | 144 | 150 |
| **Jumla** | Namba | 307 | 301 | 264 | 244 | 243 | 243 | 243 | 244 |
| Masanduku Binafsi | 000 | 161 | 161 | 145 | 126 | 126 | 126 | 152 | 158 |
| Masanduku Yaliokodishwa | 000 | 143 | 157 | 126 | 125 | 125 | 125 | 119 | 150 |
| Maombi Yasiotimizwa | 000 | 1 | 3 | 1 | 1 | 2 | - | - | 8 |
| Mifuko Pekee Iliyokodishwa | Namba | 342 | 675 | 442 | 291 | 240 | 180 | 60 | 47 |
| Barua Zilizotumwa bila Vifurushi | Milioni | 5 | 9 | 11 | 6 | 4 | 2 | 2 | 1 |
| Regista na Barua za Amana | 000 | 269 | 280 | 186 | 65 | 45 | 50 | 25 | 92 |
| Vifurushi Nchini | 000 | 51 | 63 | 32 | 4 | 6 | 10 | 7 | 19 |
| Vifurushi Nje | 000 | 3 | 4 | 3 | 2 | 2 | 1 | 6 | 2 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | 4,635 | 6,027 | 5,570 | 2,803 | 1,726 | 1,374 | 463 | 231 |
| **Huduma za Haraka, barua na vifurushi** | | | | | | | | | |
| Ndani ya Nchi | Namba | 560,710 | 655,927 | 511,274 | 466,029 | 627,822 | 481,588 | 354,746 | 499,430 |
| Nje ya Nchi | Namba | 9,534 | 14,346 | 13,742 | 7,080 | 11,642 | 5,150 | 6,254 | 15,506 |
| EMS Money Fax | Namba | 18 | - | - | 52 | - | - | - | |
| EMS Fax (Fax message received) | Namba | 129 | - | - | - | - | - | - | - |
| **Overnight Mail Services** | Namba | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | Namba | 24,966 | 14,553 | 19,598 | 46,093 | 30,339 | 24,889 | 26,171 | 16,279 |
| Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa | Namba | 2,120 | 5,346 | 7,800 | - | - | - | - | - |
| **Huduma za gari ndogo** | Namba | | | | | | | | |
| Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | Namba | - | 2,919 | 2,518 | 5,651 | 3,293 | 6,377 | 5,178 | 427 |
| Amna za Haraka Zilizotolewa | Namba | 127 | 104 | 109 | 52 | - | - | - | - |
| Amana za Haraka Zilizolipwa | | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Amana za Haraka za Nje ya Nchi** | | | | | | | | - | - |
| Zilizotumwa | Namba | 8 | 11 | 26 | - | - | - | - | |
| Zilizopokelewa | Namba | 43 | 37 | - | - | - | - | - | - |
| Amana za Posta zilizouzwa | Namba | 45 | 2 | - | - | - | - | - | - |
| Amana za Posta Zilizolipwa | Namba | 8 | - | - | - | - | - | - | - |
| **Benki ya Akiba (Transaction)** | | | | | | | | | - |
| Uwekaji Amana (Deposit) | Namba | 59,249 | 108,972 | 91,567 | 56,064 | 94,689 | 96,959 | 70,110 | 56,253 |
| Uchukuaji Amana (Withdrawal) | Namba | 76,926 | 133,531 | 103,958 | 75,065 | 69,203 | 94,374 | 106,845 | 234,055 |

**Chanzo:** Shirika la Posta Tanzania

**Jedwali Na. 61: IDADI YA KADI ZA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI**

| **Kampuni** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. Simu za Kiganjani** | | | | | | | | |
| Tigo/Yas | 12,583,640 | 12,572,826 | 13,032,073 | 13,369,276 | 15,940,373 | 19,698,263 | 25,419,851 | 29.0 |
| Vodacom | 14,143,657 | 15,672,390 | 15,621,457 | 15,913,553 | 18,180,904 | 21,272,484 | 26,327,611 | 23.8 |
| Airtel | 10,954,621 | 12,722,224 | 13,823,756 | 14,700,426 | 16,616,488 | 19,146,016 | 20,061,071 | 4.8 |
| TTCL Mobile | 587,191 | 981,072 | 963,384 | 1,813,719 | 1,495,577 | 1,644,194 | 1,655,861 | 0.7 |
| Hallotel | 3,942,237 | 4,641,701 | 6,818,228 | 7,200,140 | 8,028,138 | 8,529,919 | 12,371,713 | 45.0 |
| **Jumla** | **42,211,346** | **46,590,213** | **51,292,702** | **52,997,114** | **60,261,480** | **70,290,876** | **85,836,107** | 22.1 |
| **B. Simu za Mezani** | | | | | | | | |
| Mobile Network | 43,497,261 | 47,685,232 | 51,220,233 | 54,044,384 | 60,192,331 | 70,215,144 | 86,769,161 | 23.6 |
| Fixed Network | 124,298 | 76,288 | 72,834 | 71,834 | 84,696 | 75,732 | 78,299 | 3.4 |
| **Jumla** | **43,621,559** | **47,761,520** | **51,293,067** | **54,116,218** | **60,277,027** | **70,290,876** | 86,847,460 | 23.6 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## SURA YA 14

## NISHATI

### Ufuaji wa Umeme

353. Mwaka 2024, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulikuwa megawati 3,052.46 ikilinganishwa na megawati 1,887.50 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 61.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kufanya kazi kwa mitambo mitano kati ya tisa katika Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP yenye uwezo wa kuzalisha megawati 1,175. Hadi Desemba 2024, ujenzi wa JNHPP ulikuwa umefikia asilimia 99.5 na utakapokamilika wote utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.


354. Mwaka 2024, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 11,958.84 ikilinganishwa na saa za gigawati 10,379.56 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.2. Kati ya umeme uliozalishwa, saa za gigawati 11,628.82 zilizalishwa katika Gridi ya Taifa, saa za gigawati 90.87 zilizalishwa katika vituo nje ya Gridi ya Taifa na saa za gigawati 239.15 zilinunuliwa kutoka nchi jirani. Umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa ulitokana na vyanzo vifuatavyo: mitambo ya nguvu za maji gigawati 6,034.03, sawa na asilimia 51.9; gesi asilia saa za gigawati 5,552.19 (asilimia 47.7); mafuta saa za gigawati 26.95 (asilimia 0.2); na tungamotaka saa za gigawati 15.65 (asilimia 0.1). Aidha, umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ulikuwa saa za gigawati 10,776.49 mwaka 2024 ikilinganishwa na saa za gigawati 8,651.32 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 24.6.

355. Mwaka 2024, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 9,114.7 ikilinganishwa na saa za gigawati 8,232 zilizouzwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Kati ya umeme uliouzwa, saa za gigawati 4,150.1 zilikuwa za matumizi ya nyumbani, saa za gigawati 4,187.5 wateja wakubwa na saa za gigawati 777.1 ziliuzwa Zanzibar. Kwa upande mwingine, umeme uliopotea ulikuwa asilimia 14.48 ya umeme uliozalishwa mwaka 2024 ikilinganishwa na upotevu wa asilimia 14.63 mwaka 2023. Upotevu huo ulitokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme, urefu wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuzidiwa kwa mashineumba. Hadi Desemba 2024, Serikali kupitia Mradi wa Usambazaji wa Nishati Vijijini iliunganisha umeme katika vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara ikilinganishwa na vijiji 11,720 mwaka 2023.

356. Mwaka 2024, miundombinu ya kusafirisha umeme nchini ilifikia urefu wa kilometa 8,025.38 kutoka kilometa 7,745.38 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Aidha, miundombinu ya kusambaza umeme ilifikia kilometa 197,597.34 kutoka kilometa 176,750.88 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Vilevile, wateja waliounganishwa na umeme nchini walifikia 5,225,193 kutoka wateja 4,714,129 mwaka

2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuendelea kutumika kwa mfumo wa maombi ya umeme wa NIKONEKT pamoja na utekelezaji wa miradi ya ujazilizi na ya miji ya pembezoni mwa miji.

**Kielelezo Na. 1: Umeme kutoka Vyanzo Mbalimbali Mwaka 2024**




**Gesi Asilia**

357. Mwaka 2024, gesi asilia iliyozalishwa ilikuwa futi za ujazo milioni 69,538.3 ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 85,173.2 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 18.4. Kati ya hizo, futi za ujazo milioni 42,610.75 zilizalishwa na viwanda vinavyomilikiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania - TPDC na futi za ujazo milioni 26,927.55 zilizalishwa katika viwanda vya SONGAS Plant na Maurel & Prom. Upungufu wa uzalishaji ulitokana na kupungua kwa mahitaji ya gesi asilia kwa ajili ya kuzalisha umeme. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia katika vitalu vya Songosongo na Mnazi Bay kwa upande wa TPDC yalikuwa dola za Marekani milioni 144.10 ikilinganishwa na mapato ya dola za Marekani milioni 124.53 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa asilimia ya ushiriki wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania katika mradi wa Mnazi Bay kutoka asilimia 20 hadi asilimia 40 baada ya kununua asilimia 20 ya hisa za Kampuni ya Wentworth.

358. Mwaka 2024, mtandao wa usambazaji wa gesi asilia ulifikia kilometa 177.82 kutoka kilometa 170.72 mwaka 2023. Hadi Desemba 2024, nyumba 1,514, viwanda 57, taasisi 14 na vituo sita (6) vya kujaza gesi asilia kwenye magari viliunganishwa kwenye miundombinu

ya gesi asilia. Katika kipindi hicho, takriban magari 5,000 na pikipiki 5,000 za magurudumu matatu za kusafirisha abiria ziliunganishwa na mfumo wa gesi asilia.

**Jedwali Na. 14.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia, Mwaka 2020 – 2024 (Futi za Ujazo Milioni)**

| Mwaka | Songosongo | Mnazi Bay | Jumla | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2020 | 33,149.94 | 23,934.21 | 57,084.15 | -10.6 |
| 2021 | 35,095.18 | 29,828.96 | 64,924.14 | 13.7 |
| 2022 | 46,116.99 | 32,942.96 | 79,059.95 | 21.8 |
| 2023 | 45,976.38 | 39,196.81 | 85,173.19 | 7.7 |
| 2024 | 33,695.42 | 35,842.88 | 69,538.30 | -18.4 |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na. 14.2: Mapato ya Mauzo ya Gesi Asilia, Mwaka 2020 - 2024 (Dola za Marekani)**

| Mwaka | Songosongo | Mnazi Bay | Jumla | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2020 | 20,995,963 | 34,122,450 | 55,118,413 | -13.9 |
| 2021 | 16,018,066 | 42,886,054 | 58,904,120 | 6.9 |
| 2022 | 26,933,872 | 44,355,811 | 71,289,683 | 21.0 |
| 2023 | 45,264,440 | 79,265,141 | 124,529,581 | 75.0 |
| 2024 | 33,054,000 | 111,041,488 | 144,095,489 | 15.7 |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

### Uagizaji Mafuta

359. Mwaka 2024, mafuta yaliyoingizwa nchini yalikuwa lita za ujazo milioni 4,249.2 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 4,010.3 zilizoingizwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.0. Hii ilitokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi nchini hususan, katika sekta za viwanda, ujenzi, biashara na utalii. Kati ya kiasi kilichoingizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 2,364.6, petroli lita za ujazo milioni 1,632.4, mafuta ya taa lita za ujazo milioni 7.19, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 217.18 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 27.78. Katika kipindi hicho, akiba ya mafuta nchini ilikuwa siku 14 kwa mafuta ya petroli, dizeli siku 12, mafuta ya ndege siku 27 na mafuta ya taa siku 75.

**Jedwali Na. 14.3: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini kwa Matumizi ya Ndani, Mwaka 2024 (Lita za Ujazo)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Ndege | Mafuta ya Taa | Mafuta Mazito | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 166,613,385 | 158,377,846 | 17,838,772 | 924,417 | - | 343,754,421 |
| Februari | 199,199,680 | 114,947,502 | 20,658,448 | 660,062 | - | 335,465,691 |
| Machi | 155,263,807 | 96,702,904 | 14,656,930 | - | 6,325,386 | 272,949,027 |
| Aprili | 112,646,767 | 100,468,126 | 18,037,444 | - | 6,325,386 | 237,477,723 |
| Mei | 229,546,809 | 129,762,481 | 30,824,289 | - | - | 390,133,578 |
| Juni | 179,222,497 | 110,534,039 | 15,524,723 | - | - | 305,281,259 |
| Julai | 165,099,370 | 117,332,764 | - | - | - | 282,432,134 |
| Agosti | 186,474,186 | 121,451,980 | 20,235,866 | 672,197 | 5,782,773 | 334,617,001 |
| Septemba | 214,787,315 | 165,028,645 | 24,255,194 | 665,297 | - | 404,736,452 |
| Oktoba | 217,744,005 | 165,298,775 | 36,749,060 | 1,322,792 | - | 421,114,633 |
| Novemba | 167,685,451 | 103,498,506 | - | - | 7,452,387 | 278,636,344 |
| Desemba | 209,243,253 | 137,103,218 | 16,261,725 | 658,742 | - | 363,266,938 |
| Yaliyobadilishwa Matumizi | 161,094,797 | 111,934,072 | 2,137,793 | 2,285,047 | 1,895,261 | 279,346,971 |
| **Jumla 2024** | **2,364,621,322** | **1,632,440,858** | **217,180,244** | **7,188,555** | **27,781,193** | **4,249,212,172** |
| **Jumla 2023** | **2,216,780,181** | **1,557,545,600** | **213,766,743** | **4,260,353** | **17,973,859** | **4,010,326,735** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **6.7** | **4.8** | **1.6** | **68.7** | **54.6** | **6.0** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani**

360. Mwaka 2024, lita za ujazo milioni 5,304 za mafuta ziliingia nchini kwenda nchi jirani ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 4,721.6 zilizoingizwa nchini mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuimarika kwa huduma za bandari. Kati ya kiasi kilichoagizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 3,642.5, petroli lita za ujazo milioni 1,414.8, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 241.1, mafuta ya taa lita za ujazo milioni 0.65, na mafuta mazito lita za ujazo milioni 5.1.

**Jedwali Na. 14.4: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani Mwaka 2024 (Lita za Ujazo)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Ndege | Mafuta ya Taa | Mafuta Mazito | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 147,656,029 | 143,570,113 | 17,838,772 | - | - | 309,064,915 |
| Februari | 255,491,001 | 112,892,478 | 11,969,341 | - | - | 380,352,820 |
| Machi | 235,545,214 | 82,634,067 | 10,871,594 | - | - | 329,050,875 |
| Aprili | 289,705,681 | 119,935,545 | 24,289,756 | - | 4,809,492 | 438,740,474 |
| Mei | 447,367,999 | 141,936,163 | 38,598,062 | - | - | 627,902,225 |
| Juni | 336,876,977 | 88,376,821 | 30,735,924 | 650,058 | - | 456,639,780 |
| Julai | 306,766,058 | 108,107,302 | - | - | - | 414,873,360 |
| Agosti | 254,002,514 | 177,243,334 | 20,578,273 | - | - | 451,824,122 |
| Septemba | 192,052,523 | 153,061,095 | 18,744,295 | - | - | 363,857,912 |
| Oktoba | 407,518,379 | 106,985,820 | 34,125,152 | - | - | 548,629,351 |
| Novemba | 464,479,540 | 168,617,495 | 7,980,750 | - | - | 641,077,785 |
| Desemba | 466,137,109 | 123,362,014 | 27,517,840 | - | - | 617,016,963 |
| Yaliyobadilishwa Matumizi | 161,094,797 | 111,934,072 | 2,137,793 | - | 1,895,261 | 277,061,924 |
| **Jumla 2024** | **3,642,504,229** | **1,414,788,174** | **241,111,967** | **650,058** | **5,064,827** | **5,304,119,255** |
| **Jumla 2023** | **3,241,437,112** | **1,256,438,949** | **219,727,447** | **3,967,029** | **-** | **4,721,570,538** |
| Badiliko (Asilimia) | **12.4** | **12.6** | **9.7** | **-83.6** | | **12.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

### Mwenendo wa Bei za Mafuta

361. Mwaka 2024, wastani wa bei ya mafuta katika soko la dunia kwa tani ulikuwa dola za Marekani 729 kwa petroli, dola za Marekani 694 kwa dizeli na dola za Marekani 728 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na dola za Marekani 777, dola za Marekani 770 na dola za Marekani 805, mtawalia mwaka 2023. Bei hizo zilipungua kwa asilimia 6.3 kwa mafuta ya petroli, mafuta ya dizeli (asilimia 9.8) na mafuta ya taa (asilimia 9.5). Kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta ghafi ikilinganishwa na mahitaji kufuatia nchi zisizo wanachama wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta - OPEC kama Marekani na Canada kuongeza uzalishaji na hivyo kuzidi punguzo la uzalishaji lililokuwa linatekelezwa na wanachama wa OPEC. Aidha, matumizi ya mafuta duniani yalipungua hasa kutokana na nchi ya China kupunguza matumizi ya dizeli na petroli kufuatia ongezeko la matumizi ya magari ya umeme (Electric Vehicles) na magari makubwa yanayotumia gesi asilia (LNG powered trucks)

362. Mwaka 2024, wastani wa bei za ukomo za mafuta kwa lita katika soko la ndani uliongezeka hadi shilingi 3,130 kwa mafuta ya petroli na shilingi 3,041 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na shilingi 2,999 mafuta ya petroli na shilingi 3,015 kwa mafuta ya taa mwaka 2023. Wastani wa bei ya mafuta ya petroli uliongezeka kwa asilimia 4.4 na mafuta

ya taa asilimia 0.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za uagizaji na usafirishaji wa mafuta. Hata hivyo, wastani wa bei za mafuta ya dizeli ulipungua kwa asilimia 0.6 mwaka 2024 kutokana na kuongezeka kwa uagizaji sambamba na matumizi ya nishati mbadala ambayo yalipunguza uhitaji wa bidhaa hiyo sokoni.

**Jedwali Na. 14.5: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Dunia Mwaka 2024 (Dola za Marekani kwa Tani)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa |
|---|---:|---:|---:|
| Januari | 733 | 746 | 770 |
| Februari | 760 | 782 | 784 |
| Machi | 741 | 794 | 779 |
| Aprili | 752 | 842 | 783 |
| Mei | 693 | 743 | 721 |
| Juni | 702 | 718 | 739 |
| Julai | 718 | 763 | 754 |
| Agosti | 673 | 704 | 707 |
| Septemba | 612 | 652 | 649 |
| Oktoba | 642 | 662 | 679 |
| Novemba | 656 | 660 | 695 |
| Desemba | 651 | 678 | 681 |
| **Wastani kwa 2024** | **694** | **729** | **728** |
| **Wastani kwa 2023** | **770** | **777** | **805** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-9.8** | **-6.2** | **-9.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 14.6: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Ndani Mwaka 2024 (Shilingi/Lita)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa |
|---|---:|---:|---:|
| Januari | 3,078 | 3,084 | 3,510 |
| Februari | 3,029 | 3,051 | 2,840 |
| Machi | 3,126 | 3,163 | 2,840 |
| Aprili | 3,210 | 3,257 | 2,840 |
| Mei | 3,196 | 3,314 | 2,840 |
| Juni | 3,112 | 3,261 | 3,261 |
| Julai | 3,115 | 3,210 | 3,261 |
| Agosti | 3,131 | 3,231 | 3,257 |
| Septemba | 3,011 | 3,140 | 3,121 |
| Oktoba | 2,846 | 3,011 | 2,943 |
| Novemba | 2,844 | 2,943 | 2,943 |
| Desemba | 2,779 | 2,898 | 2,831 |
| **Wastani Mwaka 2024** | **3,040** | **3,130** | **3,041** |
| **Wastani Mwaka 2023** | **3,058** | **2,999** | **3,015** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-0.6** | **4.4** | **0.9** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Gesi Inayotokana na Petroli**

363. Mwaka 2024, gesi inayotokana na petroli (Liquefied Petroleum Gas - LPG) iliyoagizwa nchini ilikuwa tani za ujazo 344,374 ikilinganishwa na tani za ujazo 364,982 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 5.6. Hii ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa LPG kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani hasa nchini Kenya baada ya waagizaji wa LPG nchini humo kuongeza uagizaji wa bidhaa hiyo kupitia bandari ya Mombasa.

364. Mwaka 2024, utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia uliendelea kwa kutoa elimu kwa watanzania, kusambaza mitungi ya gesi 452,455 yenye ruzuku pamoja na kuhamasisha suala la ubunifu katika teknolojia za nishati safi ya kupikia. Aidha, mifumo ya nishati safi ya kupikia iliendelea kupelekwa katika taasisi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha sekta binafisi kuingia zaidi katika mnyororo mzima wa thamani wa nishati safi ya kupikia. Matumizi ya nishati safi ya kupikia yanasaidia kulinda afya, kutunza mazingira na kuimarisha ustawi wa jamii nzima, lengo likiwa ni kufikia asilimia 80 ya watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034 kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 9.2.

**Jedwali Na. 14.7: LPG iliyoingizwa Nchini Mwaka 2023 - 2024 (Tani)**

| **Mwezi** | **2023** | **2024** |
|---|---:|---:|
| Januari | 25,165 | 28,921 |
| Februari | 23,229 | 33,344 |
| Machi | 23,951 | 29,622 |
| Aprili | 26,793 | 42,961 |
| Mei | 37,670 | 40,634 |
| Juni | 25,414 | 25,397 |
| Julai | 36,129 | 22,894 |
| Agosti | 29,310 | 33,511 |
| Septemba | 33,258 | 24,486 |
| Oktoba | 30,556 | 21,649 |
| Novemba | 38,375 | 26,161 |
| Desemba | 35,132 | 14,793 |
| **Jumla** | **364,982** | **344,374** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 62: UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NCHINI NA UPATIKANAJI WA UMEME MWAKA 2024**

| Kituo | Uwezo wa Mashine (MW) | Uzalishaji (GWh) |
|---|---|---|
| **Umeme Kutokana na Maji** | | |
| JNHPP | 1,117.00 | 3,339.40 |
| Kidatu | 204 | 943.22 |
| Kihansi | 180 | 826.69 |
| Mtera | 80 | 337.6 |
| New Pangani Falls | 68 | 357.06 |
| Rusumo | 26.67 | 94.29 |
| Hale | 21 | 12 |
| Nyumba ya Mungu | 8 | 62.52 |
| Uwemba | 0.84 | 1.93 |
| Mwenga | 4 | 26.77 |
| Yovi | 0.95 | 3.32 |
| Matembwe | 0.59 | - |
| Darakuta | 0.32 | 1.77 |
| Luponde | 0.9 | 1.97 |
| Andoya | 1 | 0.69 |
| Tulila | 5 | 24.79 |
| **Jumla Ndogo Maji** | **1,718.27** | **6,034.03** |
| **Umeme Kutokana na Gesi Asilia** | | |
| Kinyerezi II | 248.22 | 1,562.50 |
| Ubungo Gas Plant II | 129 | 903.29 |
| Ubungo Gas Plant I | 102 | 390.37 |
| Songas | 189 | 866.73 |
| Ubungo Gas Plant III | 92.5 | 465.88 |
| Tegeta Gas Plant | 45 | 210.05 |
| Kinyerezi I | 335 | 976.13 |
| Mtwara I | 30.6 | 92.78 |
| Mtwara II (TM 16) | 20 | 74.59 |
| Somanga | 7.5 | 9.85 |
| **Jumla Ndogo Gesi Asilia** | **1,198.82** | **5,552.19** |
| **Umeme Kutokana na Mafuta** | | |
| Zuzu | 7.44 | 2.48 |
| Nyakato | 63 | 21.33 |
| Biharamulo | 2.72 | - |
| Songea | 5.74 | - |
| Liwale | 0.85 | - |
| Tunduru | 1.05 | - |
| Ludewa | 1.27 | - |
| Mbinga | 1.0 | - |

**Jedwali Na. 62: Linaendelea**

| Kituo | Uwezo wa Mashine (MW) | Uzalishaji (GWh) |
|---|---|---|
| Loliondo | 1.0 | - |
| Ngara | 1.25 | - |
| Kasulu | 4.55 | 3.14 |
| Kibondo | 2.5 | - |
| **Jumla Ndogo Mafuta** | **92.37** | **26.95** |
| **Umeme Kutokana na Tungamotaka** | | |
| TANWAT | 1.5 | 1.92 |
| TPC | 9.0 | 13.73 |
| **Jumla Ndogo Tungamotaka** | **10.5** | **15.65** |
| **Jumla ya Gridi ya Taifa** | **3,019.96** | **11,628.82** |
| **Umeme Nje ya Gridi ya Taifa (Off-Grid)** | | |
| Bukoba | 2.6 | 0.03 |
| Inyonga | 1.6 | 3.26 |
| Kigoma | 8.8 | 40.73 |
| Mafia | 3.2 | 8.26 |
| Mpanda | 6.3 | 35.38 |
| Sumbawanga | 5.0 | 1.72 |
| Solowazi | 5.0 | 1.49 |
| **Jumla Nje ya Gridi ya Taifa** | **32.5** | **90.87** |
| **Umeme Kutoka Nchi Jirani** | | |
| Uganda (Masaka) | | 136.16 |
| Uganda (Kikagati) | | 38.35 |
| Zambia | | 64.64 |
| **Jumla Umeme Kutoka Nchi Jirani** | | **239.15** |
| **Jumla Kuu** | **3,052.46** | **11,958.84** |

**Chanzo:** Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

**Jedwali Na. 63: MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI (Saa za Gigawati)**

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Zanzibar | Jumla | Umeme Uliozalishwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wateja wadogo (D1) | Wateja wa Kati (T1) | Wateja Wakubwa (T2, T3 & T8) | T5+T7 | | |
| 2013 | 280.6 | 1,747.0 | 2,560.4 | 218.7 | 4,806.70 | 5,946.20 |
| 2014 | 217 | 1,891.0 | 2,595.0 | 348.5 | 5,051.50 | 6,186.80 |
| 2015 | 148.8 | 2,082.7 | 2,721.1 | 344.6 | 5,297.10 | 6,416.90 |
| 2016 | 345.3 | 2,263.4 | 2,887.2 | 375.6 | 5,871.50 | 7,092.20 |
| 2017 | 301.5 | 2,371.0 | 2,893.3 | 390.4 | 5,956.20 | 7,115.30 |
| 2018 | 319.8 | 2,481.9 | 3,075.0 | 414.0 | 6,290.70 | 7,354.80 |
| 2019 | 307.2 | 2,655.9 | 3,198.1 | 481.5 | 6,642.80 | 7,804.90 |
| 2020 | 325.8 | 2,668.6 | 3,205.1 | 474.9 | 6,674.30 | 7,862.90 |
| 2021 | 339.9 | 2,900.0 | 3,527.0 | 546.3 | 7,313.20 | 8,580.80 |
| 2022 | 351 | 3,063.1 | 3,730.6 | 584.9 | 7,729.60 | 9,064.90 |
| 2023 | 393.6 | 3,313.2 | 3,864.2 | 661.0 | 8,232.00 | 10,379.60 |
| 2024 | 430.5 | 3,719.6 | 4,187.5 | 777.1 | 9,114.70 | 11,958.90 |

**Chanzo:** Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

**Jedwali Na. 64: MAUZO YA UMEME KWA MIKOA (GWh)**

| Mkoa | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 161.0 | 179.7 | 177.7 | 228.7 | 249.3 | 297.2 | 336.7 |
| Arusha | 383.3 | 406.3 | 385.6 | 395.6 | 413.9 | 452.1 | 496.6 |
| Manyara | 32.4 | 34.8 | 35.2 | 53.5 | 59.0 | 67.3 | 52.5 |
| Kilimanjaro | 181.7 | 185.2 | 183.9 | 195.2 | 206.3 | 218.7 | 260.9 |
| Tanga | 353.9 | 351.3 | 342.2 | 375.5 | 408.7 | 391.5 | 433.1 |
| Morogoro | 274.9 | 268.0 | 266.8 | 298.5 | 307.3 | 329.7 | 327.3 |
| Pwani | 393.1 | 450.7 | 517.9 | 597.9 | 635.7 | 714.8 | 826.7 |
| Dar-es-Salaam | 2,481.6 | 2,596.5 | 2,534.0 | 2,652.0 | 2,805.9 | 2,932.0 | 3,188.5 |
| Lindi | 25.8 | 29.7 | 30.5 | 33.8 | 36.2 | 41.5 | 44.8 |
| Mtwara | 52.8 | 55.9 | 55.9 | 58.6 | 60.9 | 66.5 | 69.0 |
| Ruvuma | 41.9 | 50.3 | 53.7 | 56.9 | 59.4 | 66.5 | 76.5 |
| Iringa | 103.7 | 108.9 | 109.1 | 117.3 | 123.8 | 133.6 | 147.3 |
| Mbeya | 186.9 | 201.6 | 209.9 | 226.9 | 231.5 | 231.8 | 244.3 |
| Singida | 45.7 | 49.5 | 53.1 | 58.1 | 65.1 | 69.5 | 88.7 |
| Tabora | 60.7 | 68.4 | 69.7 | 76.4 | 77.9 | 80.9 | 89.0 |
| Rukwa | 25.9 | 27.3 | 28.6 | 31.1 | 32.5 | 39.0 | 45.1 |
| Kigoma | 40.2 | 40.3 | 41.0 | 47.5 | 52.3 | 59.6 | 69.6 |
| Shinyanga | 339.5 | 354.1 | 352.2 | 421.7 | 411.2 | 395.3 | 440.3 |
| Kagera | 90.6 | 80.3 | 79.2 | 96.8 | 108.1 | 119.2 | 154.9 |
| Mwanza | 287.7 | 295.2 | 300.9 | 325.6 | 344.5 | 348.4 | 371.6 |
| Mara | 165.8 | 163.9 | 188.1 | 195.5 | 215.1 | 241.2 | 246.1 |
| Njombe | 35.4 | 39.1 | 42.0 | 45.7 | 47.8 | 53.0 | 59.7 |
| Katavi | 11.2 | 13.6 | 16.3 | 21.8 | 24.0 | 27.8 | 36.3 |
| Geita | 49.2 | 53.0 | 60.8 | 77.7 | 83.0 | 96.9 | 123.3 |
| Simiyu | 22.4 | 24.2 | 24.8 | 28.6 | 31.0 | 34.3 | 39.8 |
| Songwe | 29.3 | 33.2 | 40.4 | 50.2 | 54.4 | 62.8 | 68.9 |
| **Jumla Tanzania Bara** | **5,876.6** | **6,161.0** | **6,199.5** | **6,767.1** | **7,144.8** | **7,571.1** | **8,337.6** |
| **Zanzibar** | 414.0 | 481.5 | 474.9 | 546.3 | 584.9 | 661.0 | 777.1 |
| **Jumla kuu** | **6,290.6** | **6,642.5** | **6,674.4** | **7,313.4** | **7,729.7** | **8,232.1** | **9,114.7** |

Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

## SURA YA 15

## MAJI

### Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

365. Mwaka 2024, kiwango cha rasilimali za maji kinachofaa kwa matumizi kilikuwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2023. Kati ya kiwango hicho, mita za ujazo bilioni 105 zilikuwa juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 zilikuwa chini ya ardhi. Aidha, kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 64.2 Tanzania Bara ya mwaka 2024 kwa Mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka kilikuwa takribani wastani wa mita za ujazo 1,961. Kiwango hicho zaidi ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

366. Mwaka 2024, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yalikadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 68 kwa mwaka ikilinganishwa na mita za ujazo bilioni 66 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii zikichagizwa zaidi na ongezeko la idadi ya watu. Aidha, vyanzo 74 vya maji vilitambuliwa na kufikia vyanzo 3,339 mwaka 2024 kutoka vyanzo 3,265 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, vyanzo vilivyowekewa mipaka ili visiharibiwe na shughuli za kibinadamu vilifikia 350 kutoka vyanzo 316 mwaka 2023. Ongezeko la vyanzo vilivyotambuliwa na vilivyowekewa mipaka lilitokana na uwekezaji wa Serikali katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

367. Mwaka 2024, vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi vilipungua hadi 1,181 kutoka vituo 1,205 mwaka 2023. Hii ilitokana na mafuriko yaliyoharibu vituo katika maeneo mbalimbali nchini. Vituo hivyo vinajumuisha: vituo 341 vya hali ya hewa; vituo 358 vya kufuatilia maji katika mito, maziwa na mabwawa; vituo 95 vya maji chini ya ardhi; vituo 33 vya kufuatilia mchanga kwenye mito; na vituo 354 vya ubora wa maji.

### Ubora wa Maji

368. Mwaka 2024, sampuli 9,187 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora ikilinganishwa na sampuli 6,490 zilizokusanywa na kuhakikiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 41.6. Hii ilitokana na ununuzi wa vifaa vya uchunguzi wa ubora wa maji katika maabara za Singida, Mwanza na Iringa pamoja na elimu iliyotolewa kwa jamii kuhusu masuala ya ubora wa maji. Kati ya sampuli zilizokusanywa na kuhakikiwa: sampuli 8,457 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani; sampuli 335 za ufuatiliaji wa mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji; sampuli 70 utafiti; sampuli 85

matumizi ya viwandani; sampuli 21 umwagiliaji; sampuli 69 ujenzi; sampuli 109 za viwanda vya samaki na sampuli 41 za kupima uwezo wa utendaji kazi wa maabara.

369. Mwaka 2024, Serikali ilihakiki ubora wa maji katika sampuli 8,457 za matumizi ya majumbani ikilinganishwa na sampuli 5,764 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 46.7. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli za maji 6,223 (asilimia 73.6) zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika kimataifa na sampuli 2,234 hazikukidhi viwango. Kutokidhi viwango kwa sampuli kulitokana na uwepo wa kiasi kikubwa cha rangi, tope, ugumu wa maji, madini ya chumvi, nitrate, fluoride, manganese na chuma katika maeneo mbalimbali nchini.

370. Mwaka 2024, sampuli 395 za maji kwa ajili ya shughuli za viwandani, umwagiliaji, ujenzi, utafiti na upimaji wa uwezo wa utendaji kazi wa maabara zilifanyiwa uhakiki na kukidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kwa matumizi ikilinganishwa na sampuli 315 mwaka 2023. Uchunguzi wa ubora wa maji ulibaini hali ya ubora wa maji wa vyanzo vya maji ni ya kuridhisha na vinafaa kuendelezwa kwa matumizi yaliyokusudiwa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

371. Mwaka 2024, sampuli 281 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilikusanywa na kuhakikiwa ubora ikilinganishwa na sampuli 377 zilizohakikiwa ubora mwaka 2023. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli 142, sawa na asilimia 50.5 hazikukidhi viwango vya ubora kutokana na kuwepo kwa Chemical Oxygen Demand (COD), Biological Oxygen Demand (BOD), Nitrate na Phosphate kuliko kiwango kinachohitajika kwa ajili ya maji hayo kurudishwa kwenye mazingira.


**Huduma ya Maji Vijijini**

372. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya majisafi vijijini kwa kukamilisha vituo 6,832 vya kuchotea maji vya jamii vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 4,976,352 ikilinganishwa na vituo 8,751 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 4,178,368 mwaka 2023. Kutokana na kukamilika kwa vituo hivyo, idadi ya vituo vinavyotoa huduma ilifikia 158,475 mwaka 2024 kutoka vituo 151,643 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya maji vijijini. Aidha, kaya zilizounganishwa na huduma ya maji zilikuwa 276,464 ikilinganishwa na kaya 207,498 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 33.2. Hadi Desemba 2024, wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulifikia asilimia 83.0 kutoka asilimia 79.6 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa miradi na miundombinu ya kutolea huduma ya maji vijijini na kuimarishwa kwa vyombo vya utoaji huduma ya maji ngazi ya jamii vyenye jukumu la kusimamia na kuendesha miradi ya maji vijijini.

**Huduma ya Maji Mijini**

373. Mwaka 2024, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ilifikia wastani wa asilimia 91.6 ikilinganishwa na asilimia 90 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa miradi ya maji inayohudumia wakazi wa maeneo ya mijini. Katika kipindi hicho, jumla ya miradi ya maji mijini iliyokamilika ilikuwa 68 ikilinganishwa na miradi 70 mwaka 2023. Kwa upande mwingine, wateja 2,334,950 waliunganishwa na huduma ya majisafi mwaka 2024 ikilinganishwa na wateja 1,990,206 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 17.3. Hii ilitokana na kuendelea kwa ukarabati wa miundombinu ya maji na kuunganisha wateja kwenye miradi iliyokamilika katika miji mikuu ya mikoa na wilaya.

**Kielelezo Na. 15.1: Mwenendo wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini, Mwaka 2019 - 2024**




374. Mwaka 2024, uzalishaji wa maji unaojumuisha miji mikuu ya mikoa, mamlaka za maji za miradi ya kitaifa na miji mikuu na midogo ya wilaya ulikuwa mita za ujazo milioni 399.9 ikilinganishwa na mita za ujazo milioni 395.9 mwaka 2023. Mapato yaliyotokana na mauzo ya majisafi na salama yalikuwa shilingi bilioni 409.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 383.9 mwaka 2023.

**Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa**

375. Mwaka 2024, visima 2,034 vilichimbwa katika maeneo mbalimbali nchini ikilinganishwa na visima 1,188 mwaka 2023. Kati ya hivyo, visima 816 vilichimbwa na Serikali na visima 1,218 vilichimbwa na sekta binafsi. Kuongezeka kwa idadi ya visima vilivyochimbwa kulitokana na uwekezaji wa sekta binafsi na juhudi za Serikali katika kuwapatia wananchi huduma ya maji. Visima hivyo vilichimbwa katika mabonde

yafuatayo: Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika visima 85; Bonde la Maji la Ziwa Rukwa (200); Bonde la Maji la Ziwa Nyasa (32); Bonde la Maji la Pangani (133); Bonde la Kati (561); Bonde la Maji la Rufiji (67); Bonde la Maji la Ruvuma na Pwani ya Kusini (333); Bonde la Maji la Wami/Ruvu (429); na Bonde la Maji la Ziwa Victoria visima 194.

376. Mwaka 2024, Serikali iliendelea na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya mabwawa nane (8) yenye matumizi mbalimbali ikiwemo kuvuna maji ya mvua yalijengwa katika maeneo yafuatayo: Misigiri (Iramba); Lalago na Ipililo (Maswa); Igombe (Tabora); Mputa (Mkinga); Kwa Mjembe (Bagamoyo); Mihingo (Bunda) na Nsekwa (Mlele).

**Uondoaji wa Majitaka**

377. Mwaka 2024, mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa kilomita 1,514.6 ikilinganishwa na kilomita 1,503.4 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, wateja waliounganishwa katika mtandao wa majitaka waliongezeka na kufikia 118,114 ikilinganishwa na wateja 115,269 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa miradi ya usafi wa mazingira katika miji ya Nzega na Tunduma. Hadi Desemba 2024, miradi minne (4) ya uondoshaji wa majitaka isiyotumia mfumo wa mabomba ilikamilika katika miji ya Nzega, Tunduma, Muheza na Pangani na kufikisha miji 16 inayotumia mfumo huo.

**Jedwali Na. 65: UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI**

| A. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIJI MIKUU YA MIKOA (RWSSA) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Maji | 2023 | | 2024 | |
| | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) |
| Arusha | 29,033,530 | 22,414,906,277 | 29,910,310 | 24,853,605,909.80 |
| Babati | 4,111,770 | 4,299,991,437 | 4,046,479 | 5,176,143,778.60 |
| Bukoba | 2,876,972 | 3,126,973,721 | 3,821,822.55 | 4,948,455,950.59 |
| Dodoma | 21,998,770 | 21,013,601,786 | 22,074,907 | 26,939,287,694.42 |
| DAWASA | 141,097,720 | 142,034,738,371 | 128,430,974 | 142,457,866,444.50 |
| Geita | 1,900,004 | 1,873,449,388 | 1,903,596.50 | 1,779,321,430 |
| Iringa | 6,365,079 | 8,904,401,229 | 6,842,191 | 9,357,492,342.35 |
| Kigoma | 1,906,628 | 955,509,319 | 4,302,722 | 4,264,177,966.83 |
| Lindi | 3,586,158 | 2,779,730,026 | 825,297.09 | 1,047,789,152.28 |
| Mpanda | 894,474 | 1,028,659,374 | 1,690,351.28 | 1,057,504,344.50 |
| Mbeya | 14,037,363 | 14,465,894,142 | 16,983,394 | 14,877,554,873.70 |
| Morogoro | 11,081,500 | 13,052,443,221 | 13,204,380 | 13,017,394,443.97 |
| Moshi | 14,513,727 | 11,564,651,416 | 15,133,589 | 12,077,739,739.30 |
| Mtwara | 4,585,970 | 4,456,114,662 | 4,571,368 | 4,681,361,139 |
| Musoma | 6,588,171 | 4,694,349,536 | 7,166,728.75 | 4,820,954,561.95 |
| Mwanza | 30,808,692 | 31,296,954,665 | 32,506,489 | 28,817,580,006.74 |
| Njombe | 1,167,132 | 1,247,612,800 | 1,192,753 | 1,235,981,614.30 |
| Bariadi | 587,861 | 281,000,789 | 792,598.65 | 573,693,695.80 |
| Kahama | 5,489,976 | 8,163,134,057 | 5,296,706 | 9,351,795,738.25 |
| Singida | 5,171,242 | 8,993,680,073 | 3,860,851 | 4,368,522,065 |
| Songea | 3,572,570 | 3,714,319,686 | 3,054,507 | 4,148,976,894 |
| Sumbawanga | 3,168,035 | 3,625,873,850 | 2,080,663 | 2,299,933,211.65 |
| Tabora | 2,626,954 | 1,605,691,901 | 5,662,197 | 8,742,194,182.47 |
| Shinyanga | 6,043,371 | 7,731,582,765 | 5,439,369 | 9,334,937,296.92 |
| Tanga | 12,427,071 | 15,238,912,081 | 12,817,591 | 15,692,481,071.81 |
| Vwawa-Mlowo | 465,324 | 179,390,823 | 460,265 | 212,112,523 |
| **JUMLA - RWSSA** | **336,106,064** | **338,743,567,395** | **334,072,100** | **356,134,858,072** |


| B. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIRADI YA KITAIFA (NWP) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Maji | 2023 | | 2024 | |
| | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) |
| Wanging'ombe | 769,160 | 478,777,525 | 594,936 | 516,850,512.65 |
| Kahama Shinyanga | 21,320,537 | 15,907,526,430 | 22,946,316 | 19,215,386,395 |
| Mugango Kiabakari | 797,070.00 | 87,931,281.50 | 113,416 | 124,152,040.98 |
| Masasi Nachingwea | 304,971 | 3,066,700,000 | 2,448,638 | 2,844,822,240 |
| Makonde | 1,110,799 | 577,101,267 | 794,252 | 865,643,748.96 |
| Maswa | 1,674,963 | 720,559,301 | 1,030,434.60 | 757,912,360 |
| HTM | 1,301,273 | 774,307,500 | 2,684,825.20 | 1,185,581,857 |
| **JUMLA - NWP** | **27,278,773** | **21,612,903,304.5** | **30,612,818** | **25,510,349,155** |

**Jedwali Na. 65: Linaendelea**

| C. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIJI MIKUU NA MIDOGO YA WILAYA (DTWSSA) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Maji** | **2023** | | **2024** | |
| | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** |
| Karatu | 1,542,730 | 1,033,678,521 | 1,362,240 | 1,064,503,558 |
| Kondoa | 1,026,791 | 438,234,820 | 517,567 | 463,785,280 |
| Mpwapwa | 781,334 | 376,061,939 | 753,813 | 523,603,796 |
| Ludewa | 399,330 | 56,283,412 | 405,485 | 75,037,660 |
| Makete | 327,840 | 155,575,654 | 366,938 | 200,079,129 |
| Mafinga | 992,558 | 494,079,542 | 868,160 | 582,908,223 |
| Makambako | 774,438 | 663,048,409 | 861,974 | 767,776,200 |
| Biharamulo | 380,372 | 332,382,119 | 531,812 | 337,551,807 |
| Ngara | 633,585 | 382,372,406 | 653,467 | 353,053,709 |
| Kasulu | 924,620 | 239,296,172 | 2,605,092.70 | 360,802,781 |
| Same-Mwanga | 835,149 | 453,965,789 | 848,493 | 504,193,937 |
| Kilwa Masoko | 537,592 | 330,774,544 | 543,294.68 | 320,429,341 |
| Loliondo | 142,816 | 193,029,014 | 127,089 | 190,486,645 |
| Kiteto Kibaya | 121,592 | 87,583,788 | 184,252 | 210,565,786.70 |
| Mbulu | 622,042 | 288,966,069 | 847,790 | 558,118,048.22 |
| Bunda | 1,068,510 | 1,124,825,262 | 1,109,148 | 1,482,506,024.25 |
| Orkesumet | 245,742 | 396,208,712 | 178,095 | 337,823,000 |
| Sengerema | 1,753,457 | 1,486,271,589 | 1,504,470 | 1,271,169,906 |
| Chunya | 105,711 | 93,317,128 | 108,257 | 88,844,720 |
| Itumba Isongele | 319,442 | 60,516,128 | 610,396 | 66,990,185.67 |
| Kyela-Kasumulu | 1,797,684 | 95,151,875 | 1,674,713 | 136,372,174.85 |
| Mbarali Rujewa | 722,880 | 124,993,361 | 663,442 | 135,971,594 |
| Rungwe Tukuyu | 2,183,067 | 285,691,030 | 3,709,395 | 373,582,485 |
| Ifakara | 234,002 | 101,438,817 | 479,185 | 109,805,527.26 |
| Kilosa | 498,482 | 312,097,280 | 498,482 | 312,097,280 |
| Mahenge | 13,133 | 121,621,229 | 13,133 | 121,621,229 |
| Morogoro Mikumi | 234,547 | 265,759,895 | 234,547 | 265,759,895 |
| Rufiji Utete | 179,552 | 148,630,131 | 130,315 | 96,016,354.36 |
| Namtumbo | 352,755 | 99,558,414 | 358,612.56 | 164,978,569 |
| Kahama | 5,171,242 | 8,993,680,073 | 5,296,706 | 9,351,795,738.25 |
| Kishapu | 160,435 | 251,289,017 | 201,240 | 283,146,284 |
| Maganzo | 230,265 | 130,447,372 | 98,670 | 165,793,728 |
| Mwanhuzi | 105,852 | 172,259,845 | 276,401 | 263,376,171.20 |
| Maswa | 252,115 | 225,647,984 | 1,030,434.60 | 757,912,360 |
| Manyoni | 480,205 | 601,229,730 | 616,783 | 561,690,983.90 |
| Korogwe | 480,205 | 433,949,873 | 480,205 | 433,949,873 |
| Lushoto | 691,876 | 253,726,203 | 489,596.40 | 294,718,993 |
| Korogwe Mombo | 579,254 | 148,250,389 | 579,254 | 148,250,389 |
| Songe | 258,420 | 47,095,986 | 71,369 | 64,872,979 |
| Igunga | 1,530,809 | 1,831,6 86,105 | 1,391,465 | 1,836,015,647.88 |
| Nzega | 1,598,960 | 1,705,317,300 | 1,202,285 | 1,737,630,749.60 |
| Turiani | 1,243,590 | 1,806,130,380 | 749,413.33 | 420,371,639.60 |
| **JUMLA - DTWSSA** | **32,534,981** | **25,010,437,201** | **35,233,480** | **27,795,960,382** |
| **JUMLA KUU (A+B+C)** | **395,919,818** | **383,880,636,311** | **399,918,398** | **409,441,167,609** |

**Chanzo:** Wizara ya Maji

**Kielelezo Na. 11.1: Mchanganuo Wa Mapato ya Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa Mwaka 2024**



**Jedwali Na. 66: KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MIKUU YA MIKOA MWAKA 2024**

| Mkoa | Mji | Makadario ya Idadi ya watu | Idadi ya Watu Waliofikiwa na Huduma | Watu Wanaoishi kwenye Maeneo yaliyofikiwa na Miundombinu ya maji (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Arusha | Arusha Jiji | 631,369 | 631,369 | 100.0 |
| Dar es Salaam | Dar es Salaam Jiji | 5,614,660 | 5,221,634 | 93.0 |
| Pwani | Kibaha Manispaa | 295,615 | 283,415 | 95.9 |
| Dodoma | Dodoma Jiji | 784,260 | 721,519 | 92.0 |
| Geita | Geita Mjini | 402,918 | 308,833 | 76.6 |
| Iringa | Iringa Manispaa | 216,306 | 216,306 | 100.0 |
| Kagera | Bukoba Manispaa | 156,697 | 138,328 | 88.3 |
| Katavi | Mpanda Manispaa | 273,792 | 213,938 | 78.1 |
| Kigoma | Kigoma Manispaa | 246,509 | 242,147 | 98.2 |
| Kilimanjaro | Moshi Manispaa | 226,665 | 226,665 | 100.0 |
| Lindi | Lindi Manispaa | 177,999 | 133,156 | 74.8 |
| Manyara | Babati Mjini | 136,930 | 133,608 | 97.6 |
| Mara | Musoma Manispaa | 174,672 | 174,523 | 99.9 |
| Mbeya | Mbeya Jiji | 575,094 | 530,722 | 92.3 |
| Morogoro | Morogoro Manispaa | 481,895 | 349,374 | 72.5 |
| Mtwara | Mtwara Manispaa | 156,824 | 140,350 | 89.5 |
| Mwanza | Mwanza Jiji | 1,237,237 | 1,237,237 | 100.0 |
| Njombe | Njombe Mjini | 96,584 | 81,039 | 83.9 |
| Rukwa | Sumbawanga Manispaa | 222,775 | 211,955 | 95.1 |
| Ruvuma | Songea Manispaa | 303,989 | 286,024 | 94.1 |
| Shinyanga | Shinyanga Manispaa | 231,701 | 183,857 | 79.4 |
| Simiyu | Bariadi Mjini | 340,441 | 254,637 | 74.8 |
| Singida | Singida Manispaa | 263,676 | 226,038 | 85.7 |
| Songwe | Vwawa-Mlowo | 141,821 | 71,684 | 50.5 |
| Tabora | Tabora Manispaa | 345,331 | 314,047 | 90.9 |
| Tanga | Tanga Jiji | 402,180 | 402,180 | 100.0 |
| | | **14,137,940** | **12,934,585** | **91.5** |

## SURA YA 16

## ELIMU MAFUNZO NA TEKNOLOJIA

**Elimu ya Awali**

378. Mwaka 2024, idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika elimu ya awali ilikuwa 1,676,559 (wasichana 824,648 na wavulana 851,911) ikilinganishwa na wanafunzi 1,679,542 walioandikishwa mwaka 2023. Kati ya walioandikishwa, wanafunzi 7,323 (wasichana 3,100 na wavulana 4,223) walikuwa na mahitaji maalum ikilinganishwa na wanafunzi 6,919 waliokuwa na mahitaji maalum mwaka 2023. Katika kipindi hicho, wanafunzi walioandikishwa katika shule za Serikali walikuwa 1,558,549 (wasichana 767,029 na wavulana 791,520) ikilinganishwa na wanafunzi 1,562,286 walioandikishwa mwaka 2023. Aidha, wanafunzi walioandikishwa katika shule zisizo za Serikali waliongezeka na kufikia 118,010 mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 117,256 walioandikishwa mwaka 2023.

379. Mwaka 2024, idadi ya walimu katika shule za awali za Serikali iliongezeka kwa asilimia 35.7 na kufikia 13,042 (wanawake 8,890 na wanaume 4,152) kutoka walimu 9,608 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuajiri walimu ili kukabiliana na upungufu wa walimu katika shule za awali za Serikali. Kati ya hao, walimu wenye sifa za kufundisha elimu ya awali walikuwa 10,348 ikilinganishwa na walimu 7,958 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 30.0. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa elimu ya awali ulifikia 1:120 mwaka 2024 ikilinganishwa na uwiano wa 1:163 mwaka 2023. Uwiano huo ulizidi kiwango cha uwiano wa 1:25 unaokubalika kitaifa.

**Elimu ya Msingi**

380. Mwaka 2024, idadi ya shule za msingi ilifikia 20,533 kutoka shule 19,733 mwaka 2023. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 18,055 ikilinganishwa na shule 17,463 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi. Katika kipindi hicho, shule zisizo za Serikali zilifikia 2,478 kutoka shule 2,270 mwaka 2023.

381. Mwaka 2024, idadi ya wanafunzi katika shule za elimu ya msingi ilifikia 11,391,185 (wasichana 5,808,963 na wavulana 5,582,222) kutoka wanafunzi 11,425,482 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za elimu ya msingi walikuwa 78,106 (wasichana 34,031 na wavulana 44,075) ikilinganishwa na wanafunzi 74,295 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za msingi za Serikali ilikuwa 10,739,975 (wasichana 5,482,061 na wavulana 5,257,914) ikilinganishwa na wanafunzi 10,824,374 mwaka 2023. Vilevile, idadi ya wanafunzi katika shule za msingi zisizo za Serikali ilikuwa 651,210 (wasichana 326,902 na wavulana 324,308) mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 601,108 mwaka 2023. Katika

kipindi hicho, wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na vifo, utovu wa nidhamu na utoro walikuwa 158,555 (wasichana 67,394 na wavulana 91,161) ikilinganishwa na wanafunzi 193,605 mwaka 2023.

382. Mwaka 2024, watahiniwa 1,204,899 (wasichana 656,160 na wavulana 548,739) walifanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi ikilinganishwa na watahiniwa 1,356,392 mwaka 2023. Aidha, watahiniwa 195 walifutiwa matokeo ya darasa la saba mwaka 2024 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo udanganyifu na utovu wa nidhamu. Kati ya watahiniwa 1,204,704 waliobaki, watahiniwa 974,229 (wasichana 525,172 na wavulana 449,057) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 80.9 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 80.6 mwaka 2023.

383. Mwaka 2024, idadi ya walimu katika shule za elimu ya msingi za Serikali ilifikia 194,367 (wanawake 94,648 na wanaume 99,719) kutoka walimu 176,540 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.1. Hii ilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kuajiri walimu katika shule za elimu ya msingi. Katika kipindi hicho, idadi ya walimu katika shule za elimu ya msingi zisizo za Serikali ilifikia 35,473 (wanawake 15,206 na wanaume 20,267) kutoka walimu 30,783 mwaka 2023. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa shule za elimu ya msingi za Serikali na zisizo za Serikali ulikuwa 1:50 mwaka 2024 ikilinganishwa na uwiano wa 1:55 mwaka 2023. Uwiano huo umendelea kuimarika licha ya kuwa bado ulizidi kiwango halisi cha uwiano wa 1:45 unaokubalika kitaifa .

**Elimu ya Sekondari**

384. Idadi ya shule za sekondari iliongezeka na kufikia 6,269 mwaka 2024 kutoka shule 5,926 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Kati ya hizo, shule 4,905 zilikuwa za Serikali na shule 1,364 zisizo za Serikali. Ongezeko la idadi ya shule lilitokana na jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya madarasa na shule mpya za sekondari pamoja na uwekezaji wa sekta binafsi.

385. Mwaka 2024, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita ilikuwa 3,314,198 ikilinganishwa na wanafunzi 3,077,355 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Kati ya hao, wasichana walikuwa 1,753,013 na wavulana 1,561,185. Katika kipindi hicho, wanafunzi wenye mahitaji maalum katika elimu ya sekondari walikuwa 15,179 (wasichana 7,825 na wavulana 7,354) ikilinganishwa na wanafunzi 14,651 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali ilikuwa 2,999,530 (wasichana 1,588,885 na wavulana 1,410,645) mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 2,774,947 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Vilevile, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne ilikuwa 3,087,870 ikilinganishwa na wanafunzi 2,881,335 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Kati ya hao, wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa

2,811,848 ikilinganishwa na wanafunzi 2,618,325 katika shule za Serikali mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Hii ilitokana na idadi kubwa ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza kufuatia utekelezaji wa programu ya elimu msingi bila ada. Kwa upande mwingine, idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na vifo, utovu wa nidhamu na utoro ilikuwa 148,337 (wasichana 72,212 na wavulana 76,125) ikilinganishwa na wanafunzi 136,318 mwaka 2023.

386. Mwaka 2024, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne walikuwa 517,460 (wasichana 271,918 na wavulana 245,542) ikilinganishwa na watahiniwa 529,596 waliofanya mtihani mwaka 2023. Aidha, watahiniwa 765 wa kidato cha nne waliofanya mtihani mwaka 2024 walifutiwa matokeo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo udanganyifu na utovu wa nidhamu. Kati ya watahiniwa 516,695 waliobaki, watahiniwa 477,262 (wasichana 249,078 na wavulana 228,184) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 92.4 ikilinganishwa na asilimia 89.4 mwaka 2023. Kwa upande mwingine, watahiniwa 103,812 (wasichana 46,793 na wavulana 57,019) walifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha sita mwaka 2024 ikilinganishwa na watahiniwa 96,319 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Kati ya hao, watahiniwa 476 walifutiwa matokeo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo udanganyifu na utovu wa nidhamu. Kati ya watahiniwa 103,336 waliobaki, watahiniwa 103,252 (wasichana 46,615 na wavulana 56,637) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.92 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.90 mwaka 2023.

387. Mwaka 2024, idadi ya walimu katika shule za sekondari za Serikali ilifikia 106,631 (wanawake 35,637 na wanaume 70,994) kutoka walimu 96,130 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Hii ilitokana na Serikali kuendelea kuajiri walimu katika shule za sekondari. Aidha, idadi ya walimu katika shule za sekondari zisizo za Serikali ilifikia 22,055 (wanawake 5,185 na wanaume 16,870) mwaka 2024 kutoka walimu 21,779 mwaka 2023. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa shule za elimu ya sekondari za Serikali na zisizo za Serikali uliendelea kuwa kiwango cha 1:26 mwaka 2024 kama ilivyokuwa mwaka 2023 ukilinganishwa na uwiano wa 1:40 unaokubalika kitaifa.

**Elimu katika Vyuo vya Ualimu**

388. Mwaka 2024, wanachuo katika vyuo vya ualimu walikuwa 20,261 (wanawake 10,073 na wanaume 10,188) ikilinganishwa na wanachuo 23,162 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 12.5. Upungufu huo ulitokana na mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023 inayoelekeza wanafunzi wa masomo ya ualimu waliomaliza kidato cha sita kupata stashahada ya kwanza kwenye vyuo vikuu badala ya kujiunga na vyuo vya uwalimu. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2023/24 wanachuo waliodahiliwa walikuwa 10,828 ikilinganishwa na wanachuo 13,051 mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 17.0. Wanachuo waliofanya mtihani wa kuhitimu mafunzo ya

ualimu katika ngazi ya stashahada na astashahada walikuwa 7,918 mwaka 2024 ikilinganishwa na wanachuo 7,901 mwaka 2023. Kati ya hao, wanachuo 7,905 walifaulu na kuhitimu mafunzo ya ualimu mwaka 2024, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.8 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 97.4 mwaka 2023. Kiwango cha ufaulu kiliongezeka kutokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ualimu.

**Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

389. Mwaka 2023/24, taasisi 10,026 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na taasisi 6,649 zilizokaguliwa mwaka 2022/23. Kuongezeka kwa taasisi zilizokaguliwa kulitokana na Serikali kuimarisha mazingira ya utendaji kazi katika ofisi za uthibiti ubora wa shule za kanda na wilaya.

**Jedwali Na. 16.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu, Mwaka 2022/23 - 2023/24**

| Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---:|---:|
| Shule za Awali na Msingi | 5,623 | 7,837 |
| Shule za Sekondari | 986 | 2,137 |
| Vyuo vya Ualimu | 40 | 44 |
| FDCs | | 7 |
| **Jumla** | **6,649** | **10,026** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

390. Mwaka 2023/24, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 206,617 (wanawake 99,730 na wanaume 106,887) ikilinganishwa na wanafunzi 193,343 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo hadi 490 mwaka 2023/24 kutoka vyuo 474 mwaka 2022/23.

**Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi**

391. Mwaka 2023/24, idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA ilikuwa 30,728 (wanawake 9,627 na wanaume 21,101) ikilinganishwa na wanafunzi 39,764 mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 22.7. Hii ilitokana na wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi kuhamasika kuendelea na masomo katika ngazi ya elimu ya sekondari. Vilevile, wanafunzi 15,228 (wanawake 5,086 na wanaume 10,142) walihitimu mafunzo ya ufundi stadi kwa kozi za muda mrefu katika vyuo vya VETA mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wanafunzi 39,551 mwaka 2022/23.

392. Mwaka 2023/24, idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - (Folk Development College - FDCs) ilikuwa 18,001 (wanawake 7,606 na wanaume 10,395) ikilinganishwa na wanafunzi 17,695 mwaka 2022/23. Katika kipindi hicho, wanafunzi

13,783 walihitimu mafunzo katika vyuo vya FDCs ikilinganishwa na wanafunzi 13,527 waliohitimu mwaka 2022/23. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kulitokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

393. Mwaka 2024, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ilidahili wanafunzi 148 (wanawake 49 na wanaume 99) ikilinganishwa na wanafunzi 168 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 11.9. Katika kipindi hicho, wanafunzi 92 (wanawake 28 na wanaume 64) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 131 waliohitimu mwaka 2023. Kwa upande mwingine, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 12,643 (wanawake 2,953 na wanaume 9,690) mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 9,664 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Aidha, wanafunzi 2,494 (wanawake 681 na wanaume 1,813) walihitimu mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 1,978 waliohitimu mwaka 2023.

394. Mwaka 2024, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 8,862 (wanawake 2,658 na wanaume 6,204) ikilinganishwa na wanafunzi 7,783 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 13.9. Kuongezeka kwa udahili kulitokana na uboreshaji wa mitaala, pamoja na miundombinu ya kujifunzia na kufundishia. Katika kipindi hicho, wanafunzi 1,522 (wanawake 372 na wanaume 1,150) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 1,185 waliohitimu mwaka 2023. Kwa upande mwingine, Chuo cha Ufundi Arusha kilidahili wanafunzi 2,877 (wanawake 749 na wanaume 2,128) mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 2,887 waliodahiliwa mwaka 2023. Aidha, wanafunzi 1,139 (wanawake 246 na wanaume 893) walihitimu katika Chuo cha Ufundi Arusha mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 830 waliohitimu mwaka 2023.

**Elimu ya Juu**

395. Hadi Desemba 2024, taasisi za elimu ya juu nchini zilikuwa 54 (Serikali 21 na zisizo za Serikali 33). Kati ya taasisi hizo, vyuo vikuu vilikuwa 33, vyuo vishiriki 16 na kampasi tano (5). Aidha, wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu nchini walikuwa 334,854 (wanawake 150,543 na wanaume 184,311) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wanafunzi 314,643 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanafunzi waliohitimu elimu ya sekondari na wanafunzi waliojiunga baada ya kupata sifa katika vyuo vya elimu ya kati, upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na kuongezeka kwa programu zilizotolewa. Vilevile, wanafunzi 56,520 (wanawake 28,946 na wanaume 27,574) walihitimu katika taasisi za elimu ya juu mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wanafunzi 57,742 waliohitimu mwaka 2022/23, sawa na upungufu wa asilimia 2.2. Kwa upande mwingine, idadi ya wanataaluma katika taasisi za elimu ya juu

ilikuwa 8,625 (wanawake 2,617 na wanaume 6,008) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wanataaluma 8,507 (wanawake 2,528 na wanaume 5,979) mwaka 2022/23.

396. Mwaka 2023/24, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 738.2 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 635.7 iliyotolewa mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 16.1. Katika kipindi hicho, wanafunzi 229,652 walinufaika na mikopo ikilinganishwa na wanafunzi 202,016 walionufaika mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 13.7. Ongezeko la wanufaika na mikopo iliyotolewa lilitokana na jitihada za Serikali za kuongeza fursa za elimu nchini. Vilevile, shilingi bilioni 7.2 zilitolewa kupitia ufadhili wa SAMIA ambapo wanafunzi 1,220 walinufaika mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.4 kwa wanafunzi 593 walionufaika mwaka 2022/23. Kwa upande mwingine, Serikali ilitoa mikopo kwa wanafunzi 2,299 wa ngazi ya stashahada katika fani za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati ambapo kiasi cha shilingi bilioni 7.4 kilitumika mwaka 2023/24.

**Udhibiti wa Mionzi**

397. Mwaka 2024, Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania ilipokea na kutathmini maombi 711 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi 842 ya leseni mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 15.6. Aidha, maombi 595 yalipata leseni baada ya kukidhi vigezo mwaka 2024 ikilinganishwa na maombi 767 mwaka 2023., Vituo vinavyomiliki na kutumia mionzi vilifikia 1,637 mwaka 2024 kutoka vituo 1,425 mwaka 2023. Vilevile, vituo 932 vilikaguliwa ili kudhibiti usalama wa wagonjwa na wafanyakazi mwaka 2023/24 ikilinganishwa na vituo 971 vilivyokaguliwa mwaka 2022/23.

398. Mwaka 2023/24, Tume ilipima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,627 katika vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na wafanyakazi 2,120 waliopimwa mwaka 2022/23. Matokeo ya vipimo yalibainisha kuwa viwango vya mionzi walivyopata wafanyakazi vipo katika viwango vinavyokubalika. Kwa upande mwingine, Tume ilipima viwango vya mionzi katika sampuli 39,233 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na sampuli 41,544 mwaka 2022/23. Kati ya hizo, sampuli 9,245 zilikuwa za vyakula kutoka nje, sampuli 29,161 za vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi na sampuli 827 zilikuwa za mbolea na tumbaku. Matokeo yalionesha kuwa sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na uchafuzi wa viasili vya mionzi.

**Jedwali Na. 67: SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2007 | 401,011 | 218,060 | 105,770 | 70,796 | 21,789 | 11,668 | 829,094 |
| 2008 | 395,930 | 332,393 | 175,353 | 95,214 | 25,240 | 11,743 | 1,035,873 |
| 2009 | 480,529 | 308,131 | 159,789 | 167,355 | 31,201 | 12,695 | 1,159,700 |
| 2010 | 382,207 | 398,870 | 293,519 | 279,995 | 26,065 | 20,674 | 1,401,330 |
| 2011 | 403,873 | 396,724 | 380,528 | 279,117 | 30,265 | 25,164 | 1,515,671 |
| 2012 | 457,321 | 386,250 | 355,740 | 343,376 | 31,206 | 28,859 | 1,602,752 |
| 2013 | 444,532 | 506,036 | 193,901 | 302,963 | 30,581 | 26,698 | 1,504,711 |
| 2014 | 479,089 | 506,170 | 356,787 | 178,246 | 33,619 | 26,899 | 1,580,810 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 467,982 | 366,396 | 263,981 | 278,690 | 45,533 | 47,007 | 1,469,589 |
| 2017 | 491,535 | 443,614 | 296,034 | 236,775 | 53,749 | 43,494 | 1,565,201 |
| 2018 | 587,186 | 480,327 | 358,960 | 278,239 | 57,287 | 52,687 | 1,814,686 |
| 2019 | 637,335 | 555,087 | 388,029 | 334,284 | 52,428 | 56,042 | 2,023,205 |
| 2020 | 659,661 | 588,561 | 454,139 | 360,356 | 58,402 | 51,138 | 2,172,257 |
| 2021 | 718,592 | 616,791 | 498,703 | 422,403 | 66,576 | 56,880 | 2,379,945 |
| 2022 | 784,061 | 648,525 | 499,958 | 454,981 | 77,873 | 64,301 | 2,529,699 |
| 2023 | 952,657 | 719,377 | 486,848 | 459,443 | 82,069 | 74,553 | 2,774,947 |
| 2024 | 981,013 | 845,297 | 538,667 | 446,871 | 108,451 | 79,231 | 2,999,530 |
| **Badiliko (Asilimia) 2023- 2024** | **3.0** | **17.5** | **10.6** | **-2.7** | **32.1** | **6.3** | **8.1** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 68: SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2007 | 47,437 | 46,927 | 41,340 | 35,746 | 11,299 | 8,667 | 191,416 |
| 2008 | 42,971 | 43,232 | 43,177 | 35,980 | 12,576 | 8,594 | 186,530 |
| 2009 | 44,255 | 36,384 | 37,064 | 34,061 | 11,851 | 9,096 | 172,711 |
| 2010 | 56,620 | 57,876 | 50,778 | 46,820 | 12,269 | 13,006 | 237,369 |
| 2011 | 63,282 | 67,205 | 65,859 | 54,521 | 11,083 | 11,926 | 273,876 |
| 2012 | 65,058 | 69,403 | 64,453 | 61,209 | 9,684 | 11,713 | 281,520 |
| 2013 | 70,060 | 77,407 | 67,998 | 65,637 | 8,592 | 9,651 | 299,345 |
| 2014 | 109,784 | 96,732 | 76,574 | 66,898 | 8,865 | 7,686 | 366,539 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | |
| 2016 | 70,844 | 81,499 | 72,970 | 73,231 | 21,091 | 17,731 | 337,366 |
| 2017 | 71,160 | 79,548 | 77,168 | 72,056 | 24,146 | 19,578 | 343,656 |
| 2018 | 64,844 | 71,685 | 74,932 | 74,848 | 24,030 | 23,441 | 333,780 |
| 2019 | 63,629 | 64,488 | 68,064 | 74,121 | 22,050 | 22,900 | 315,252 |
| 2020 | 63,232 | 64,727 | 64,328 | 67,255 | 20,032 | 21,675 | 301,249 |
| 2021 | 61,784 | 64,901 | 64,889 | 63,481 | 17,917 | 19,010 | 291,982 |
| 2022 | 66,052 | 62,741 | 65,172 | 63,625 | 18,989 | 17,310 | 293,889 |
| 2023 | 68,757 | 67,294 | 62,761 | 64,198 | 20,653 | 18,745 | 302,408 |
| 2024 | 75,776 | 70,365 | 67,192 | 62,689 | 18,557 | 20,089 | 314,668 |
| **Badiliko (Asilimia) 2023 - 2024** | **10.2** | **4.6** | **7.1** | **-2.4** | **-10.1** | **7.2** | **4.1** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 69: IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA**

| | 2023 | | | 2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** |
| **Elimu ya msingi** | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII | 5,616,919 | 5,808,563 | 11,425,482 | 5,582,222 | 5,808,963 | 11,391,185 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa la I-VII | 5,318,340 | 5,506,034 | 10,824,374 | 5,257,914 | 5,482,061 | 10,739,975 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII | 298,579 | 302,529 | 601,108 | 324,308 | 326,902 | 651,210 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 107,409 | 99,914 | 207,323 | 119,986 | 109,854 | 229,840 |
| Idadi ya walimu katika shule za msingi za Serikali | 89,367 | 87,173 | 176,540 | 99,719 | 94,648 | 194,367 |
| Idadi ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 18,042 | 12,741 | 30,783 | 20,267 | 15,206 | 35,473 |
| **Elimu ya Sekondari** | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 1,469,153 | 1,608,202 | 3,077,355 | 1,561,185 | 1,753,013 | 3,314,198 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI | 1,324,090 | 1,450,857 | 2,774,947 | 1,410,645 | 1,588,885 | 2,999,530 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 145,063 | 157,345 | 302,408 | 150,540 | 164,128 | 314,668 |
| Idadi ya walimu katika shule za Sekondari za Serikali | 62,723 | 33,407 | 96,130 | 70,994 | 35,637 | 106,631 |
| Idadi ya walimu katika shule za Sekondari za binafsi | 16,999 | 4,780 | 21,779 | 16,870 | 5,185 | 22,055 |
| Jumla ya walimu katika shule za Sekondari | 79,722 | 38,187 | 117,909 | 87,864 | 40,822 | 128,686 |

**Chanzo:** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Jedwali Na. 70: IDADI YA TAASISI ZA ELIMU**

| **Aina ya Taasisi** | **2023** | | | **2024** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** |
| Shule za Msingi | 17,463 | 2,270 | 19,733 | 18,055 | 2,478 | 20,533 |
| Shule za Sekondari | 4,578 | 1,348 | 5,926 | 4,905 | 1,364 | 6,269 |
| Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari) | 35 | 30 | 65 | 35 | 30 | 65 |
| Vyuo vya Ufundi Stadi | 124 | 563 | 687 | 162 | 698 | 860 |
| Vyuo vya Elimu ya Ufundi | 180 | 294 | 474 | 180 | 294 | 474 |
| **Jumla** | **22,380** | **4,505** | **26,885** | **23,337** | **4,864** | **28,201** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

## SURA YA 17

## AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

### AFYA

### Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

399. Mwaka 2024, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyokuwa vinafanya kazi iliongezeka kwa asilimia 8.8 na kufikia jumla ya vituo 12,846 ikilinganishwa na vituo 11,805 mwaka 2023. Kati ya hivyo, vituo 7,627 vilimilikiwa na Serikali, sekta binafsi ilikuwa na vituo 4,123, na mashirika ya dini yalikuwa na vituo 1,096. Ongezeko hilo lilitokana na ufunguzi na usajili wa vituo vipya, uboreshaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji taarifa pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya kutolea huduma za afya.

**Jedwali Na. 17.1: Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2023 - 2024**

| Aina ya Vituo | 2023 | | | | 2024 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Mashirika ya Dini | Watu Binafsi | Jumla | Serikali | Mashirika ya Dini | Watu Binafsi | Jumla |
| Hospitali | 228 | 121 | 87 | 436 | 250 | 123 | 89 | 462 |
| Vituo vya Afya | 831 | 163 | 132 | 1,126 | 958 | 163 | 133 | 1,254 |
| Zahanati | 6,010 | 714 | 1080 | 7,804 | 6,394 | 729 | 1,205 | 8,328 |
| **Jumla ndogo** | **7,069** | **998** | **1,299** | **9,366** | **7,602** | **1,015** | **1,427** | **10,044** |
| Polyclinic | - | 44 | 321 | 365 | - | 42 | 349 | 391 |
| *Nyinginezo | 21 | 34 | 1,935 | 1,990 | 25 | 37 | 2,258 | 2,320 |
| *Martenity/nursing homes* | 1 | - | 83 | 84 | - | 2 | 89 | 91 |
| **Jumla Kuu** | **7,091** | **1,076** | **3,638** | **11,805** | **7,627** | **1,096** | **4,123** | **12,846** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

* Inajumuisha kliniki, maabara na vituo vya uchangiaji wa damu

### Hali ya Utoaji Huduma

400. Mwaka 2024, jumla ya wagonjwa 47,495,667 walihudumiwa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati ikilinganishwa na wagonjwa 45,164,482 waliohudumiwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Hii ilitokana na uboreshwaji wa huduma za afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kusogezwa kwa vituo karibu na wananchi na hivyo kuongeza hamasa kwa wananchi kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya badala ya kutumia miti-shamba. Kati ya waliohudumiwa, wagonjwa wa nje walikuwa 45,629,561 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,866,106. Aidha, idadi ya vitanda vya wagonjwa iliongezeka kwa asilimia 15.8 na kufikia 145,374 mwaka 2024 kutoka vitanda 125,500 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya

na kukamilika kwa majengo ya vyumba vya wagonjwa mahututi pamoja na vyumba vya huduma za dharura.

**Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

401. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi katika vituo vya afya nchini. Wastani wa upatikanaji wa bidhaa muhimu za afya katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma ulifikia asilimia 86.0 ikilinganishwa na asilimia 75.6 mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

**Jedwali Na. 17.2: Upatikanaji wa Dawa katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Mwaka 2024**

| Ngazi ya Kituo | Idadi ya Aina za Dawa Zinazotakiwa | Upatikanaji wa Dawa (Asilimia) |
|---|---|---|
| Zahanati | 101 | 75 |
| Vituo vya Afya | 181 | 78 |
| Hospitali za Wilaya | 207 | 79 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa | 212 | 97 |
| Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda | 238 | 99 |
| **Wastani** | | **86** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

**Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

402. Mwaka 2024, wajawazito 2,712,948 walihudhuria kliniki ikilinganishwa na wajawazito 2,597,643 mwaka 2023. Kati ya hao, wajawazito 1,184,977 (asilimia 43.7) walifanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 ikilinganishwa na 1,053,738 (asilimia 40.6) mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa elimu ya afya kwa umma kupitia njia mbalimbali, ikiwemo redio na televisheni kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema.

403. Mwaka 2024, wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara nne (4) walikuwa asilimia 123 ya makadirio ikilinganishwa na asilimia 117 mwaka 2023. Aidha, wajawazito waliohudhuria kliniki na kupima Virusi vya Ukimwi (VVU) walikuwa asilimia 98.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 98.1 mwaka 2023. Kati ya hao, asilimia 0.58 ya wajawazito waligundulika kuwa na VVU ikilinganishwa na asilimia 0.77 mwaka 2023. Vilevile, asilimia 97.7 ya wajawazito waliogundulika kuwa na VVU walianzishiwa matibabu ya kufubaza VVU ikilinganishwa na asilimia 96.4 mwaka 2023.

404. Mwaka 2024, wanawake 733,927 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi ikilinganishwa na wanawake 601,922 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 21.9. Kati ya hao, wanawake 18,685 (asilimia 2.5) waligundulika kuwa na saratani ya

mlango wa kizazi na wanawake 20,392 (asilimia 2.8) waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani hiyo.

405. Mwaka 2024, huduma za dharura za afya ya uzazi na mtoto mchanga ziliendelea kuboreshwa kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya vinavyofanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni. Katika kipindi hicho, vituo hivyo vilifikia 577 ikilinganishwa na vituo 523 mwaka 2023. Aidha, wodi maalum za huduma kwa watoto wachanga wagonjwa - NCU zilifikia 362 kutoka wodi 189 mwaka 2023.

**Huduma za Chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja**

406. Mwaka 2024, idadi ya watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya iliongezeka kwa asilimia 5.4 na kufikia watoto 2,219,417 ikilinganishwa na watoto 2,105,713 waliozaliwa mwaka 2023. Aidha, watoto 3,113,112 wenye umri chini ya mwaka mmoja walitarajiwa kupata chanjo mbalimbali ambapo watoto waliopata chanjo ya PENTA - 3 walikuwa asilimia 96, Surua Rubella - 1 (asilimia 99), Surua Rubella - 2 (asilimia 93), OPV - 3 (asilimia 92), Rota - 2 (asilimia 93) na PCV - 3 (asilimia 95).

**Huduma za Matibabu ya Kibingwa**

407. Mwaka 2024, huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ziliendelea kutolewa katika hospitali maalum nchini. Wagonjwa waliopandikizwa figo walifikia 149 kutoka wagonjwa 124 mwaka 2023. Aidha, wagonjwa waliopata huduma ya upandikizaji wa uroto walifikia 20 mwaka 2024 kutoka wagonjwa 15 mwaka 2023. Wagonjwa waliowekewa puto ili kupunguza unene uliokithiri walifikia 186 mwaka 2024 kutoka wagonjwa 166 mwaka 2023. Wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum (Catheterization Laboratory) walifikia 2,695 kutoka wagonjwa 2,239 mwaka 2023. Vilevile, watoto waliopandikiziwa vifaa vya usikivu waliongezeka hadi 83 mwaka 2024 kutoka watoto 61 mwaka 2023.

408. Mwaka 2024, wagonjwa 34 walipata huduma ya upandikizaji wa nyonga bandia, na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopata huduma hiyo kufikia 237 ikilinganishwa na wagonjwa 203 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, wagonjwa 69 walifanyiwa upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu (arthroscopy) na hivyo kuongeza idadi ya wagonjwa waliofanyiwa upasuaji huo hadi 471 kutoka wagonjwa 402 mwaka 2023. Aidha, wagonjwa wawili (2) walipatiwa huduma ya upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kupitia tundu la pua, na hivyo kuongeza idadi ya wagonjwa waliohudumiwa na kufikia 33 mwaka 2024 kutoka wagonjwa 31 mwaka 2023. Ongezeko la wagonjwa waliopata huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi hapa nchini lilitokana na kuongezeka kwa teknolojia na upatikanaji wa vifaa tiba vyenye uwezo wa kutoa huduma hizo. Kwa upande mwingine, huduma mpya za kibingwa na ubingwa bobezi zilizotolewa mwaka 2024 ni pamoja na upandikizaji wa mimba kwa wanawake nane (8), upasuaji na uchunguzi wa

kichwa na ubongo bila kufungua fuvu kwa wagonjwa 12, na upandikizaji wa meno bandia kwa wagonjwa 64.

**Udhibiti wa Malaria**

409. Mwaka 2024, vipimo 9,644,925 vya malaria na vichupa 3,739,685 vya dawa ya sindano ya kutibu malaria kali vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya afya ikilinganishwa na vipimo 24,171,900 na vichupa 1,755,363 mwaka 2023. Upungufu wa vipimo na vichupa vilivyonunuliwa ulitokana na uwepo wa akiba ya vipimo katika Bohari ya Dawa ambayo ilitosheleza mahitaji ya miezi 8 ya mwanzo wa mwaka. Aidha visa vya malaria vilipungua kwa asilimia 5.3 na kufikia wagonjwa 3,357,685 mwaka 2024 ikilinganishwa na wagonjwa 3,536,947 mwaka 2023. Kupungua kwa maambukizi kulitokana na uzingatiaji wa kanuni za kujikinga, ikiwemo matumizi ya vyandarua na juhudi za Serikali katika kuangamiza viluilui wa mbu. Vilevile, vyandarua 8,078,158 vyenye dawa vilinunuliwa na kusambazwa mwaka 2024 ikilinganishwa na vyandarua 9,575,639 vilivyonunuliwa na kusambazwa mwaka 2023.

410. Mwaka 2024, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu - NIMR ilifanya uchambuzi wa mbu 14,720 waenezao malaria katika vituo 34 ikilinganishwa na mbu 8,772 waliofanyiwa uchambuzi katika vituo 32 mwaka 2023. Matokeo yalionesha kuwa mbu 8,807 walikuwa *Anopheles Gambiae* s.s, sawa na asilimia 59.8 na mbu 5,155 walikuwa *Anopheles Funestus* (asilimia 35). Aidha, uchambuzi huo ulionesha kuwa uwezo wa mbu kueneza vimelea vya malaria ulipungua hadi asilimia 0.05 ikilinganishwa na asilimia 0.10 mwaka 2023. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa afua mbalimbali ikiwemo upuliziaji wa viuadudu vya kibaiolojia katika mazalia ya mbu na uhamasishaji wa jamii kuhusu usafi wa mazingira ili kuondoa vyanzo vya mazalia ya mbu.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu**

411. Mwaka 2024, wagonjwa 76,684 wa kifua kikuu waligundulika na kuanzishiwa matibabu ikilinganishwa na wagonjwa 93,184 mwaka 2023. Aidha, wagonjwa 307 wa kifua kikuu sugu waligundulika ambapo wagonjwa 289, sawa na asilimia 94, walianzishiwa matibabu. Vilevile, idadi ya vituo vya uchunguzi na tiba ya kifua kikuu ilifikia 1,859 mwaka 2024 kutoka vituo 1,773 mwaka 2023. Vituo vinavyoweza kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sugu vilipungua hadi 305 mwaka 2024 kutoka vituo 314 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, idadi ya wagonjwa waliogundulika kwa kutumia vipimo vya maabara iliongezeka hadi asilimia 61 kutoka asilimia 49 mwaka 2023. Kwa upande mwingine, mashine za kupima kifua kikuu kwa njia ya vinasaba zilifikia 569 mwaka 2024 kutoka mashine 384 mwaka 2023.

**Lishe**

412. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe (2021/22 - 2025/26) ili kukabiliana na athari za lishe duni na kuimarisha ukuaji wa watoto. Katika kipindi hicho, jumla ya watoto 1,145,739 walinyonyeshwa maziwa ya mama ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, sawa na asilimia 93 ya lengo ikilinganishwa na watoto 1,133,419 (asilimia 89.) mwaka 2023. Aidha, asilimia 99.8 ya watoto 9,456,378 walio chini ya umri wa miaka mitano walipatiwa matone ya Vitamini A mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 87.0 ya watoto 9,421,026 mwaka 2023.

413. Mwaka 2024, watoto waliozaliwa na uzito pungufu walikuwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2023. Kupungua kwa watoto waliozaliwa na uzito pungufu kulitokana na utekelezaji wa afua za lishe kwa wajawazito, ikiwemo utoaji wa vidonge vya madini chuma, elimu ya lishe, kuhamasisha ulaji wa vyakula vilivyoongezwa virutubishi, ulaji wa vyakula mchanganyiko kutoka katika makundi yote sita ambayo ni vyakula vya nafaka, mizizi yenye wanga na ndizi mbichi; vyakula vya asili ya wanyama na mazao yake; vyakula vya jamii ya mikunde na mbegu za mafuta; mbogamboga; matunda; na mafuta yatokanayo na mimea, sambamba na kuhudhuria kliniki kwa wakati kujua maendeleo ya mama na mtoto. Mjumuisho wa afua zote hizi husaidia kujua ongezeko la uzito kwa watoto wadogo.

**Mafunzo katika Kada za Afya**

414. Mwaka 2024, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya katika ngazi ya stashahada walikuwa 24,823 (wanawake 13,688 na wanaume 11,135) ikilinganishwa na wanafunzi 24,463 waliodahiliwa mwaka 2023. Aidha, wanafunzi waliohitimu stashahada walikuwa 24,995 (wanawake 13,834 na wanaume 11,161) ikilinganishwa na wanafunzi 14,974 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 17.3: Wanafunzi Waliodahiliwa na Kuhitimu Mafunzo ya Afya Mwaka 2024**

| Kozi | Waliodahiliwa | | | Waliohitimu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | Jumla | Wanawake | Wanaume | Jumla |
| Utabibu wa Kinywa na Meno | 201 | 263 | 464 | 367 | 497 | 864 |
| Utabibu | 3,301 | 4,466 | 7,767 | 3,067 | 3,937 | 7,004 |
| Rediografia | 19 | 37 | 56 | 517 | 800 | 1317 |
| Sayansi ya Afya ya Mazingira | 46 | 55 | 101 | 44 | 94 | 138 |
| Sayansi ya Taarifa za Afya | 32 | 20 | 52 | 44 | 20 | 64 |
| Teknolojia ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Taarifa za Afya | 17 | 11 | 28 | 67 | 98 | 165 |
| Sayansi ya Maabara za Tiba | 531 | 688 | 1,219 | 724 | 864 | 1,588 |
| Uuguzi na Ukunga | 2,493 | 1,384 | 3,877 | 2,393 | 1,157 | 3,550 |
| Optometria | 61 | 67 | 128 | 85 | 121 | 206 |
| Sayansi ya Ufamasia | 6,900 | 4,054 | 10954 | 6,336 | 3,374 | 9,710 |
| Fisiotherapia | 79 | 81 | 160 | 178 | 189 | 367 |
| Mteknolojia Tiba kazi | 8 | 9 | 17 | 12 | 10 | 22 |
| **Jumla** | **13,688** | **11,135** | **24,823** | **13,834** | **11,161** | **24,995** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

## MAENDELEO YA JAMII

### Ustawi wa Jamii

415. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kutekeleza kampeni ya kuhamasisha jamii kujenga nyumba bora kwa kutumia gharama nafuu. Aidha, nyumba 8,201 zilijengwa ikilinganishwa na nyumba 6,151 zilizojengwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 33.3.

### Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

416. Mwaka 2024, wanafunzi 13,912 (wanawake 8,362 na wanaume 5,550) walidahiliwa katika taasisi na vyuo vya ustawi na maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanafunzi 11,574 waliodahiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.2. Aidha, wanafunzi 9,943 walifaulu mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 9,803 waliofaulu mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 1.43.

**Jedwali Na. 17.4: Udahili wa Wanafunzi katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

| Taasisi | Ngazi ya Elimu | 2023 | | | 2024 | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | |
| Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | Stashahada | 560 | 924 | 1,484 | 550 | 1,190 | 1,740 | 17.3 |
| | Astashahada | 1,419 | 2,613 | 4,032 | 1,197 | 2,229 | 3,426 | -15.0 |
| | **Jumla ndogo** | **1,979** | **3,537** | **5,516** | **1,747** | **3,419** | **5,166** | **-6.3** |
| Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | Astashahada | 446 | 915 | 1,361 | 856 | 659 | 1,515 | 11.3 |
| | Stashahada | 149 | 378 | 527 | 359 | 163 | 522 | -0.9 |
| | Shahada | 102 | 169 | 271 | 646 | 389 | 1,035 | 281.9 |
| | Stashahada ya Juu | 313 | 459 | 772 | 2 | 5 | 7 | -99.1 |
| | Shahada ya Uzamili | 42 | 46 | 88 | 73 | 77 | 150 | 70.5 |
| | **Jumla ndogo** | **1,052** | **1,967** | **3,019** | **1,936** | **1,293** | **3,229** | **7.0** |
| Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama | Astashahada | 318 | 840 | 1,158 | 691 | 1,159 | 1,850 | 59.8 |
| | Stashahada | 65 | 152 | 217 | 276 | 461 | 737 | 239.6 |
| | Shahada | 521 | 1,143 | 1,664 | 830 | 1,940 | 2,770 | 66.5 |
| | Stashahada ya Juu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | Stashahada ya Uzamili | 0 | 0 | 0 | 14 | 2 | 16 | |
| | Shahada ya Uzamili | 0 | 0 | 0 | 56 | 88 | 144 | |
| | **Jumla ndogo** | **904** | **2,135** | **3,039** | **1,867** | **3,650** | **5,517** | **81.5** |
| | **Jumla Kuu** | **3,935** | **7,639** | **11,574** | **5,550** | **8,362** | **13,912** | **20.2** |

**Chanzo:** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

417. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Uanagenzi kwa kuwaunganisha wanafunzi na wahitimu wa taaluma ya maendeleo ya jamii kwenye mashirika, taasisi, na kampuni ili kupata mafunzo kwa vitendo. Katika kipindi hicho, wahitimu 1,567 wa taaluma ya maendeleo ya jamii walipata mafunzo kwa vitendo ikilinganishwa na wahitimu 1,421 waliopata mafunzo kwa vitendo mwaka 2023.

**Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto**

418. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma za malezi, makuzi, na maendeleo ya awali kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Katika kipindi hicho, vituo 410 vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 340 vilivyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.6. Aidha, watoto 203,926 (wasichana 104,672 na wavulana 99,254) waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana mwaka 2024 ikilinganishwa na watoto 198,432 walioandikishwa mwaka 2023. Vituo hivyo vilikuwa na walezi 1,684 mwaka 2024 ikilinganishwa na walezi 1,589 mwaka 2023.

**Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto**

419. Mwaka 2024, watoto 36 (wasichana 15 na wavulana 21) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za malezi ya kambo ikilinganishwa na watoto 45 waliopata huduma mwaka 2023. Katika kipindi hicho, watoto walioasiliwa walikuwa 26 ikilinganishwa na watoto 40 walioasiliwa mwaka 2023. Aidha, watoto 586 (wasichana 307

na wavulana 279) waliwekwa kwa walezi wa kuaminika na watoto 1,310 (wasichana 608 na wavulana 702) waliopo katika makao ya watoto waliunganishwa na familia zao. Vilevile, Serikali ilifanya utambuzi wa watoto 5,353 (wasichana 2,528 na wavulana 2,825) wanaoishi na kufanya kazi mtaani na kuwapa huduma mbalimbali. Kati ya waliotambuliwa, watoto 812 waliunganishwa na familia zao, watoto 256 walipelekwa katika makao ya watoto, watoto 65 waliwekwa kwa walezi wa kuaminika, watoto 25 waliunganishwa na vyuo vya ufundi na watoto 17 walihitimu katika vyuo vya ufundi.

420. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika makao ya watoto ya Taifa Kurasini - Dar es Salaam na Kikombo - Dodoma. Katika kipindi hicho, watoto 252 (wasichana 99 na wavulana 153) walipatiwa huduma hizo ikilinganishwa na watoto 209 waliopatiwa huduma mwaka 2023. Aidha, watoto 13,381 (wanawake 6,688 na wanaume 6,693) walipatiwa huduma za msingi kupitia makao ya watoto ya binafsi mwaka 2024 ikilinganishwa na watoto 13,036 waliopatiwa huduma za msingi mwaka 2023.

421. Mwaka 2024, watoto 104 (wasichana wawili na wavulana 102) walio katika mkinzano na sheria waliwezeshwa kupata huduma za msingi, ikiwemo chakula, mavazi, malazi, matibabu, na elimu ikilinganishwa na watoto 325 waliopata huduma za msingi mwaka 2023. Katika kipindi hicho, watoto 46 (wasichana wawili na wavulana 44) waliokuwa katika mkinzano na sheria walichepushwa kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai (badala ya kuwapa hukumu) kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na watoto 48 mwaka 2023. Aidha, watoto 12 (msichana mmoja na wavulana 11) walihukumiwa na kupelekwa katika Shule ya Maadilisho Irambo mkoani Mbeya mwaka 2024 ikilinganishwa na wavulana tisa (9) waliohukumiwa mwaka 2023. Hadi Desemba 2024, watoto 34 waliendelea kupatiwa huduma za marekebisho ya tabia katika Shule ya Maadilisho Irambo.

**Ukatili wa Kijinsia**

422. Mwaka 2024, Serikali iliendelea na juhudi za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Katika kipindi hicho, matukio 19,717 ya ukatili wa kijinsia ikiwemo ubakaji, kujeruhi na shambulio la aibu yalitolewa taarifa ikilinganishwa matukio 38,314 yaliyotolewa taarifa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 48.5. Aidha, matukio 7,320 ya ukatili dhidi ya watoto yalitolewa taarifa mwaka 2024 ikilinganishwa na matukio 17,969 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 59.3. Matukio hayo ni pamoja na kutelekeza familia, ubakaji, ulawiti, kutupa watoto, shambulio la aibu na mimba za utotoni. Makosa ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliyotolewa taarifa yalipungua kutokana na juhudi za Serikali na wadau mbalimbali katika kuimarisha ulinzi wa watoto na wanawake na kutokomeza matukio ya ukatili. Aidha, mifumo ya utoaji wa taarifa za matukio ya ukatili katika ngazi mbalimbali iliimarishwa.

**Huduma za Ustawi kwa Wazee**

423. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuboresha huduma kwa wazee katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali na kufuatilia utoaji wa huduma hizo katika makazi 15 yanayomilikiwa na sekta binafsi. Katika kipindi hicho, wazee 245 (wanawake 147 na wanaume 98) walipatiwa huduma za msingi katika makazi ya wazee ya Serikali kama ilivyokuwa mwaka 2023. Aidha, wazee 279 (wanawake 161 na wanaume 118) walihudumiwa katika makazi ya wazee yanayomilikiwa na sekta binafsi mwaka 2024 ikilinganishwa na wazee 245 mwaka 2023.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

424. Mwaka 2024, Serikali ilisajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,438 ikilinganishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,484 yaliyosajiliwa mwaka 2023. Kati ya hayo, mashirika 56 yalikuwa ya kimataifa, mashirika 1,317 ya kitaifa, mashirika 39 ya kimkoa, na mashirika 26 katika ngazi ya wilaya. Mashirika yaliyosajiliwa yalijihusisha na utekelezaji wa afua mbalimbali, ikiwemo elimu, afya, uwezeshaji wa jamii, nishati, maji, utawala bora, masuala ya jinsia na kilimo. Baadhi ya miradi bunifu inayotekelezwa na mashirika hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba kwa kaya masikini, matumizi ya nishati safi, ujenzi wa karakana za ufundi stadi, huduma za maji safi na salama, na kuongeza thamani ya mazao kwa vikundi vya wakulima, na watu wenye ulemavu pamoja na kutoa mikopo kwa wakulima.

425. Mwaka 2024, mikataba ya fedha 232 ya Mashirika yasiyo ya Serikali ilikaguliwa na kuidhinishwa ikilinganishwa na mikataba 500 iliyokaguliwa na kuidhinishwa mwaka 2023. Aidha, shilingi bilioni 2,614.88 zilipokelewa na mashirika hayo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 671.44 zilizopokelewa mwaka 2023. Vilevile, utendaji kazi wa Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali 507 ulifuatiliwa katika mikoa 15 ikilinganishwa na mashirika 2,824 yaliyofuatiliwa mwaka 2023. Ufutialiaji huo ulilenga kuhakiki uzingatiaji wa sheria, mila na tamaduni za nchi pamoja na kubainisha manufaa ya miradi kwa jamii. Kupitia ufuatiliaji huo, Mashirika 211 yalibainika kutozingatia sheria, ikiwemo kutowasilisha taarifa za utekelezaji kwa wakati na kutokulipa ada za mwaka kulikosababisha mashirika hayo kupewa onyo na kuwekwa kwenye uangalizi maalum. Kwa upande mwingine, Mashirika yalijengewa uwezo kuhusu miongozo mbalimbali, ikiwemo Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo, Mwongozo wa Ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Bajeti ya Serikali, na Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, Toleo la pili la mwaka 2024.

**Jedwali Na. 71: IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA**

| Mwaka | Wagonjwa wa Nje | | | | Jumla ya Wagonjwa waliolazwa | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hospitali | Zahanati | Vituo vya Afya | Jumla Wagonjwa wa nje | | |
| 2007 | 1,842,671 | 28,328,093 | 4,520,026 | 34,690,790 | 2,979,115 | 37,669,905 |
| 2008 | 1,934,805 | 29,744,498 | 4,746,027 | 36,425,330 | 3,128,071 | 39,553,401 |
| 2009 | 2,128,286 | 32,718,948 | 5,220,630 | 40,067,864 | 3,440,870 | 43,508,734 |
| 2010 | 2,341,114 | 35,990,843 | 5,742,693 | 44,074,650 | 3,784,957 | 47,859,607 |
| 2011 | 2,622,048 | 39,917,117 | 6,431,816 | 48,970,981 | 4,239,152 | 53,210,133 |
| 2012 | 2,815,529 | 41,333,522 | 6,657,817 | 50,806,868 | 4,388,108 | 55,194,976 |
| 2013 | 2,903,275 | 42,682,479 | 6,873,056 | 52,458,810 | 4,529,971 | 56,988,781 |
| 2014 | 5,910,725 | 14,008,692 | 475,295 | 20,394,712 | 1,665,935 | 22,060,647 |
| 2015 | 4,480,781 | 25,072,487 | 6,006,466 | 35,559,734 | 1,858,956 | 37,418,690 |
| 2016 | 4,984,645 | 20,859,281 | 6,515,219 | 32,359,145 | 1,775,835 | 34,134,980 |
| 2017 | 5,266,252 | 21,115,639 | 7,050,725 | 33,432,616 | 1,650,224 | 35,082,840 |
| 2018 | 4,675,045 | 27,473,506 | 8,903,461 | 41,052,012 | 1,359,264 | 42,411,276 |
| 2019 | 9,821,148 | 26,500,182 | 10,153,322 | 46,474,652 | 1,852,720 | 48,327,372 |
| 2020 | 10,150,504 | 22,154,653 | 9,741,820 | 42,046,977 | 1,852,720 | 43,899,697 |
| 2021 | 11,348,037 | 19,705,594 | 9,219,985 | 40,273,616 | 1,651,001 | 41,924,617 |
| 2022 | 27,290,723 | 1,486,649 | 12,567,881 | 41,345,253 | 1,626,308 | 42,971,561 |
| 2023 | 14,047,587 | 9,399,664 | 19,959,991 | 43,407,242 | 1,757,240 | 45,164,482 |
| 2024 | 14,109,193 | 20,907,765 | 10,612,603 | 45,629,561 | 1,866,106 | 47,495,667 |

**Chanzo:** Wizara ya Afya

**Jedwali Na. 72: IDADI YA VITANDA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI**

| Aina ya Vituo | 2023 | | | | 2024 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Serikali** | **Shirika la kujitolea/ Dini** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Shirika la kujitolea/ Dini** | **Binafsi** | **Jumla** |
| Hospitali ya Taifa | 1,731 | - | - | 1,731 | 1,500 | 0 | 0 | 1,731 |
| Hospitali Maalum za Kibingwa | 1,305 | - | - | 1,305 | 611 | 0 | 0 | 1,305 |
| Hospitali za Rufaa za Kanda | 1,446 | - | - | 1,446 | 417 | 0 | 0 | 1,446 |
| Hospitali za Mikoa | 14,226 | - | - | 14,226 | 12,667 | 2083 | 375 | 14,226 |
| Hospitali za Wilaya | 16,541 | - | - | 16,541 | 12,607 | 6423 | 1256 | 16,541 |
| Hospitali nyingine | 680 | 17,396 | 5,001 | 23,077 | 0 | 2,248 | 545 | 23,077 |
| Vituo vya Afya | 23,066 | 5,380 | 2,334 | 30,780 | 17,085 | 3,682 | 1,670 | 30,780 |
| Zahanati | 27,750 | 4,896 | 3,748 | 36,394 | 19,110 | 2,920 | 2,191 | 36,394 |
| **Jumla** | **86,745** | **27,672** | **11,083** | **125,500** | **62,497** | **17,356** | **6,037** | **123,769** |

**Chanzo:** Wizara ya Afya



## Sehemu ya Tatu

# MAENDELEO KATIKA MAENEO MENGINE

## SURA YA 18

## MASUALA MTAMBUKA NA MAENDELEO YA WATU

### MASUALA MTAMBUKA

**Mazingira**

426. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Biashara ya Kaboni na kuhamasisha uwekezaji katika biashara hiyo ikiwa ni juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesijoto unaochangia katika mabadiliko ya tabianchi. Katika kipindi hicho, kampuni zilizowekeza kwenye miradi ya biashara ya kaboni zilifikia 66 kutoka kampuni 35 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 88.6. Miradi hiyo imeendelea kuchangia katika kupunguza uharibifu wa misitu pamoja na kuongeza upandaji miti kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 na marekebisho yake ya mwaka 2023. Hadi Desemba 2024, shilingi bilioni 45 zilipatikana kupitia biashara ya kaboni ambazo zilitolewa kwa Halmashauri za Tanganyika, Kiteto, Mbulu, Karatu, Kyerwa, Karagwe, Missenyi, Muleba Bukoba Vijijini na Ngara.

427. Mwaka 2024, miradi 1,764 ilipata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa ikilinganishwa na miradi 1,260 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 40.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu kwa umma kuhusu TAM pamoja na matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa TAM unaowezesha mwekezaji kufuatilia maombi ya kibali kwa urahisi. Aidha, miradi 234 ilisajiliwa kwa ajili ya Ukaguzi wa Mazingira mwaka 2024 ikilinganishwa na miradi 446 mwaka 2023. Kati ya hiyo, miradi 126 ilipata vyeti ikilinganishwa na miradi 281 iliyopata vyeti mwaka 2023. Miradi ambayo haikupata vyeti haikuruhusiwa kuendelea na utekelezaji wa shughuli zake hadi pale itakapotimiza masharti yote yanayohitajika kwa mujibu wa sheria na kanuni za mazingira nchini.

428. Mwaka 2024, maombi 10 ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati (TMK) yalipokelewa ikilinganishwa na maombi nane (8) yaliyopokelewa mwaka 2023. Kati ya maombi hayo, hati tatu (3) za TMK zilitolewa kama ilivyokuwa mwaka 2023.

**Jedwali Na. 18.1: Vyeti vya Tathmini na Ukaguzi wa Mazingira, Mwaka 2022-2024**

| Na. | Aina ya Vyeti | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati | 2 | 3 | 3 |
| 2. | Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira | 1,079 | 1,260 | 1,764 |
| 3. | Vyeti vya Ukaguzi wa Mazingira | 199 | 281 | 126 |
| | **Jumla** | **1,280** | **1,544** | **1,893** |

**Chanzo:** Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira

429. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuhamasisha urejelezaji wa taka nchini kwa kutoa elimu kwa wadau wakiwemo wamiliki wa viwanda na wafanyabiashara ili kupunguza taka zinazotupwa kwenye mazingira. Katika kipindi hicho, vibali 154 vya taka hatarishi vikijumuisha vibali vya kuhifadhi, kukusanya, kusafirisha ndani ya nchi, upitishaji nchini na usafirishaji nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 256 vilivyotolewa mwaka 2023.

430. Mwaka 2024, miti 286,657,203 ilipandwa ikilinganishwa na miti 266,970,203 iliyopandwa mwaka 2023. Kati ya hiyo, miti 223,716,211 ilistawi, sawa na asilimia 78.0 ya miti iliyopandwa ikilinganishwa na miti 211,805,184 iliyostawi mwaka 2023.

**Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

431. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kudhibiti matumizi ya kuni na mkaa kama nishati ya kupikia. Katika kipindi hicho, ufuatiliaji wa utekelezaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi za umma na binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku ulifanyika ambapo hadi Desemba 2024, taasisi 551 zilitumia nishati safi ya kupikia.

**Usalama wa Raia**

432. Mwaka 2024, makosa makubwa ya jinai 50,574 yalitolewa taarifa na wananchi ikilinganishwa na makosa 53,640 yaliyotolewa taarifa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 5.7. Makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa yalipungua kutokana na juhudi za Serikali na wadau mbalimbali katika kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao na kutokomeza matukio ya ukatili, hali iliyochangia kuwepo kwa matukio machache ya kutolea taarifa. Kati ya makosa yaliyotolewa taarifa, makosa 13,076 yalikuwa dhidi ya binadamu, makosa 20,946 ya kuwania mali, makosa 924 ya uhalifu wa kifedha na makosa 15,628 dhidi ya maadili ya jamii. Kwa upande mwingine, makosa madogo yaliyotolewa taarifa yalikuwa 564,477 mwaka 2024 ikilinganishwa na makosa 563,462 yaliyotolewa taarifa mwaka 2023.

433. Mwaka 2024, matukio ya ajali yaliyotolewa taarifa yalikuwa 1,735 (barabarani 1,700, majini 33 na angani 2) ikilinganishwa na matukio 1,759 yaliyotolewa taarifa mwaka 2023. Aidha, matukio ya ajali 1,170 yalisababisha vifo vya watu 1,715 na majeruhi 2,719 mwaka 2024 ikilinganishwa na matukio ya ajali 1,118 yaliyosababisha vifo vya watu 1,647 na majeruhi 2,716 mwaka 2023. Serikali iliendelea kufanya kaguzi rasmi na zisizo rasmi katika vituo vya mabasi na magari pamoja na operesheni endelevu ili kuimarisha usimamizi wa sheria.

434. Mwaka 2024, wafungwa na mahabusu katika magereza yote nchini walikuwa 26,755 (wafungwa 18,989 na mahabusu 7,766) ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu

26,994 mwaka 2023. Idadi hiyo inaendana na uwezo wa magereza wa kuhifadhi wafungwa 29,902. Aidha, wafungwa 2,630 walinufaika na msamaha wa Rais mwaka 2024. Kati ya hao, wafungwa 51 waliachiliwa huru na wafungwa 2,579 walipunguziwa adhabu ya vifungo ikilinganishwa na wafungwa 296 walioachiwa huru na wafungwa 1,948 walipunguziwa adhabu ya vifungo mwaka 2023. Katika kipindi hicho, wafungwa 1,527 walinufaika na adhabu ya vifungo vya nje (Extra Mural Labour 1,415 na Parole 112) ikilinganishwa na wafungwa 1,191 walionufaika na adhabu ya vifungo vya nje mwaka 2023.

435. Mwaka 2024, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipokea miito 2,634 ya matukio ya moto ikilinganishwa na miito 2,079 iliyopokelewa mwaka 2023. Ongezeko la matukio ya moto lilichangiwa na matumizi yasiyo sahihi ya nishati mbalimbali, ikiwemo umeme na gesi. Aidha, elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto ilitolewa kupitia vipindi 865 vya redio na vipindi 97 vya luninga mwaka 2024. Vilevile, miito ya maokozi ilikuwa 1,182 mwaka 2024 ikilinganishwa na miito 1,242 ya maokozi mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 4.8. Hii ilitokana na elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya namba ya simu 114 ya dharura. Kwa upande mwingine, Jeshi lilifanya kaguzi za kinga na tahadhari dhidi ya moto katika maeneo 63,763 mwaka 2024 ikilinganishwa na maeneo 60,482 yaliyokaguliwa mwaka 2023.

436. Mwaka 2024, wageni walioingia nchini kwa vibali halali walikuwa 2,009,183 ikilinganishwa na wageni 1,727,486 walioingia nchini mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii na uwekezaji. Aidha, wageni 1,824,938 walitoka nchini kwa vibali halali ikilinganishwa na wageni 1,564,277 waliotoka nchini mwaka 2023.

437. Mwaka 2024, hati za kusafiria 164,252 zilitolewa kwa watanzania ikilinganishwa na hati za kusafiria 151,774 zilizotolewa mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na uhitaji wa hati hizo kwa ajili ya safari za kibiashara, masomo, kikazi na matibabu nje ya nchi. Aidha, watanzania 507,032 walitoka nchini mwaka 2024 ikilinganishwa na watanzania 420,469 waliotoka nchini mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.6. Vilevile, watanzania 486,874 waliingia nchini ikilinganishwa na watanzania 398,421 walioingia nchini mwaka 2023. Kwa upande mwingine, vibali 22,500 vya ukaazi vilitolewa mwaka 2024 ikilinganishwa na vibali 20,191 vya ukaazi vilivyotolewa mwaka 2023. Ongezeko la utoaji wa vibali vya ukaazi lilichangiwa na kukua kwa uwekezaji nchini.

438. Mwaka 2024, waomba hifadhi 725 walipokelewa nchini ikilinganishwa na waomba hifadhi 12,391 waliopokelewa mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 94.1. Aidha, wakimbizi 13,856 walirejeshwa nchini kwao kwa hiari mwaka 2024 ikilinganishwa na wakimbizi 19,416 waliorejeshwa mwaka 2023. Vilevile, wakimbizi 6,453 walihamishiwa

nchi ya tatu ikilinganishwa na wakimbizi 7,890 waliohamishiwa nchi ya tatu mwaka 2023. Kwa upande mwingine, wahamiaji haramu 26,604 walikamatwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wahamiaji haramu 26,542 waliokamatwa mwaka 2023. Kati ya waliokamatwa, watuhumiwa 19,297 waliondoshwa nchini. Urejeshwaji wa watuhumiwa nchini kwao ulitokana na kuimarishwa kwa shughuli za udhibiti zilizofanywa na Serikali.

439. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kudhibiti vitendo vya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika kipindi hicho, waathirika 127 wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu waliokolewa na kupewa huduma muhimu ikiwemo hifadhi ya muda, chakula na matibabu ikilinganishwa na waathirika 133 waliookolewa mwaka 2023.

**Utambuzi na Usajili wa Watu**

440. Hadi Desemba 2024, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA ilisajili na kutambua watu 25,484,820 kutoka watu 24,376,028 waliotambuliwa na kusajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Aidha, Mamlaka ilitoa namba za utambulisho 21,354,858 hadi Desemba 2024 kutoka namba za utambulisho 20,608,213 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa kujisajili pamoja na kuongezeka kwa uhitaji wa Kitambulisho cha Taifa katika kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Vilevile, Mamlaka ilizalisha vitambulisho 21,115,671 hadi Desemba 2024 kutoka vitambulisho 18,982,537 vilivyozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka kuzalisha vitambulisho kwa wananchi wote waliosajiliwa mwaka 2024 na kuzalisha vitambulisho kwa wananchi wote waliosajiliwa miaka ya nyuma ambao hawakupata vitambulisho.

441. Hadi Desemba 2024, Mamlaka iliunganisha taasisi 124 (taasisi za umma 59 na taasisi binafsi 65) katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi ikilinganishwa na taasisi 93 zilizounganishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 33.3. Ongezeko hilo lilitokana na watoa huduma kuendelea kujiunga na Mfumo huo kwa lengo la kurahisisha uhakiki wa taarifa za watu ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma.

**Usajili wa Jumuiya**

442. Mwaka 2024, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iliendelea kusajili na kusimamia uendeshaji wa jumuiya kwa kuzingatia Sheria ya Jumuiya, Sura 337. Katika kipindi hicho, jumuiya 528 zilisajiliwa ikilinganishwa na jumuiya 412 zilizosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 28.2. Ongezeko hilo lilitokana na kampeni za kuhamasisha usajili wa jumuiya zilizofanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na Mbeya.

**Usajili, Ufilisi na Udhamini**

443. Mwaka 2024, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA ulisajili vizazi 1,682,214 ikilinganishwa na vizazi 1,441,795 vilivyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Ongezeko hilo lilitokana na ufuatiliaji wa usajili wa watoto walio na umri chini ya miaka mitano katika mikoa mbalimbali. Aidha, watoto 1,109,710 walisajiliwa kupitia Mpango wa Usajili kwa Watoto Walio Chini ya Umri wa Miaka Mitano ikilinganishwa na watoto 863,206 waliosajiliwa mwaka 2023. Vilevile, vizazi 572,504 vilisajiliwa kupitia usajili wa kawaida mwaka 2024 ikilinganishwa na vizazi 477,421 vilivyosajiliwa mwaka 2023. Kwa upande mwingine, Wakala ulisajili matukio ya vifo 39,071 mwaka 2024 ikilinganishwa na matukio ya vifo 35,663 yaliyosajiliwa mwaka 2023.

444. Mwaka 2024, Wakala ulisajili na kutoa hati za viapo vya ndoa 50,592 ikilinganishwa na hati za viapo vya ndoa 45,455 zilizosajiliwa mwaka 2023. Hii ilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kwa wafungisha ndoa wa madhehebu ya dini kuwasilisha mrejesho kwa ajili ya taarifa hizo kuingizwa kwenye daftari la Msajili Mkuu wa Ndoa. Aidha, hati za talaka 1,569 zilisajiliwa mwaka 2024 ikilinganishwa na hati za talaka 866 zilizosajiliwa mwaka 2023. Ongezeko la idadi ya talaka lilichangiwa na: kuwa na mahusiano mengine nje ya ndoa; ukatili wa kijinsia ndani ya ndoa; tofauti za mitazamo na matarajio kati ya wanandoa; wanandoa kushindwa kutimiza wajibu na majukumu yao; na uingiliaji wa wazazi au jamaa katika masuala ya wanandoa, hivyo kuongeza migogoro na kusababisha ndoa kuvunjika. Aidha, usajili wa talaka ulichagizwa na maboresho ya mfumo wa ndoa na talaka ikiwemo kufungamanisha mfumo huo na mfumo wa mahakama, pamoja na elimu iliyotolewa kuhusu umuhimu wa kusajili talaka. Kwa upande mwingine, Wakala ulisajili hati za watoto wa kuasili 39 baada ya kupokea amri ya mahakama mwaka 2024 ikilinganishwa na hati za watoto wa kuasili 32 zilizosajiliwa mwaka 2023.

445. Mwaka 2024, Wakala ulitoa hati 165 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na hati 84 za miunganisho ya wadhamini zilizotolewa mwaka 2023. Hadi Desemba 2024, bodi za wadhamini zilikuwa 4,954 kutoka bodi za wadhamini 5,987 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, bodi za wadhamini zilizosajiliwa mwaka 2024 zilikuwa 172. Upungufu wa bodi mwaka 2024 ulitokana na bodi za wadhamini 743 kufutwa kutokana na kushindwa kuwasilisha mrejesho wa wadhamini katika Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu na bodi za wadhamini 462 kuhamishiwa kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutokana na kupoteza vigezo vya kuwa chini ya Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini. Vilevile, wosia 181 ziliandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wosia 156 zilizoandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2023. Hii ilitokana na Wakala kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuandika na kutunza wosia kama sehemu ya kuepusha migogoro ya wanafamilia pindi mwenye mali anapofariki.

**Maendeleo ya Sheria na Mahakama**

446. Mwaka 2024, miswada 19 ya mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya iliandaliwa ikilinganishwa na miswada 26 iliyoandaliwa mwaka 2023. Kati ya hiyo, miswada 17 ilipitishwa kuwa sheria ikilinganishwa na miswada 14 iliyopitishwa mwaka 2023. Aidha, sheria ndogo 1,228 ziliandaliwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali ikilinganishwa na sheria ndogo 569 zilizoandaliwa na kuchapishwa mwaka 2023. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshwaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, kutafsiri sheria kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili pamoja na kufanya mapitio ya sheria zote kuu 446 ili kuwezesha watumiaji wa sheria hizo kupata sheria zinazoendana na wakati.

447. Mwaka 2024, mikataba 1,806 ya kitaifa na kimataifa ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na mikataba 1,812 iliyofanyiwa upekuzi mwaka 2023. Aidha, Hati za Makubaliano 515 zilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na Hati za Makubaliano 511 zilizofanyiwa upekuzi mwaka 2023. Mikataba hiyo ilihusisha ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo pamoja na utoaji wa huduma za jamii.

448. Mwaka 2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) iliendesha mashauri 8,981 ikilinganishwa na mashauri 7,849 yaliyoendeshwa mwaka 2023. Kati ya hayo, mashauri 8,293 yalikuwa madai ya kitaifa, mashauri 131 madai ya kimataifa na mashauri 557 madai ya kikatiba na haki za binadamu. Aidha, OWMS ilimaliza mashauri 1,486 ikilinganishwa na mashauri 1,386 yaliyomalizika mwaka 2023. Kati ya hayo, mashauri 1,272 yalikuwa ya kitaifa, mashauri 99 ya kimataifa na mashauri 115 ya kikatiba na haki za binadamu. Vilevile, OWMS ilibakiwa na mashauri 7,495 yaliyoendelea kusikilizwa katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi.

449. Mwaka 2024, OWMS ilishughulikia mashauri 229 ya usuluhishi ikilinganishwa na mashauri 177 yaliyoshughulikiwa mwaka 2023. Kati ya hayo, mashauri 200 yalihusu usuluhishi wa kitaifa na mashauri 29 yalihusu usuluhishi wa kimataifa. Aidha, mashauri 35 yalimalizwa mahakamani na kwenye mabaraza na mashauri 13 yalimalizwa kwa njia ya majadiliano. Kati ya mashauri yaliyomalizwa, mashauri 44 yalihusu usuluhishi wa kitaifa na mashauri 4 yalihusu usuluhishi wa kimataifa. Vilevile, mashauri 181 ya usuluhishi wa kitaifa na kimataifa yaliendelea katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi.

450. Mwaka 2024, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilizindua Kliniki ya Sheria katika mkoa wa Dodoma ili kufikisha huduma za kisheria kwa wananchi kwa ukaribu na bila malipo. Aidha, Kliniki hiyo ilihudumia wananchi 145 na kusikiliza migogoro 66 iliyohusu ardhi, ndoa, jinai, madai, ajira, ukatili, mirathi na matunzo ya watoto. Kwa upande mwingine, Mahakama ya Tanzania iliendelea kusogeza huduma za mahakama

karibu na wananchi kwa kuanzisha ujenzi wa vituo tisa (9) jumuishi vya utoaji haki katika mikoa mbalimbali nchini. Vilevile, Mahakama ya Tanzania iliongeza upatikanaji wa huduma ya mahakama inayotembea kwa kuwa na magari sita (6) yanayofanya kazi katika mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.


**Utawala Bora**

451. Mwaka 2024, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya chambuzi 635 za mifumo ya utendaji kazi na utoaji wa huduma ikilinganishwa na chambuzi 806 zilizofanyika mwaka 2023. Aidha, TAKUKURU ilifuatilia matumizi ya rasilimali za umma katika utekelezaji wa miradi 1,834 ya maendeleo ikilinganishwa na miradi 1,800 iliyofuatiliwa mwaka 2023. Miradi hiyo ilijumuisha sekta za utawala, nishati, ujenzi, maji, fedha, elimu, afya, kilimo, usafirishaji, na viwanda. Ukaguzi huo, ulibaini miradi 205 kuwa na kasoro kwenye utekelezaji na kuanzishiwa uchunguzi ikilinganishwa na miradi 171 iliyobainika mwaka 2023.

452. Mwaka 2024, TAKUKURU ilifungua kesi za rushwa 662 katika mahakama mbalimbali nchini ikilinganishwa na kesi 600 zilizofunguliwa mwaka 2023. Aidha, kesi 676 ziliamuliwa mahakamani mwaka 2024 ikilinganishwa na kesi 496 zilizoamuliwa mwaka 2023. Kati ya kesi zilizoamuliwa, Jamhuri ilishinda kesi 436 ikilinganishwa na kesi 336 ilizoshinda mwaka 2023.

453. Taarifa ya *Transparency International* (TI) ya mwaka 2024 inaonesha kuwa Tanzania ilipata alama 41 kati ya alama 100 ya Fahirisi ya Rushwa ikilinganishwa na alama 40 mwaka 2023. Aidha, kwa matokeo hayo Tanzania ilishika nafasi ya pili kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki nyuma ya Rwanda na nafasi ya 14 kwa nchi za Afrika. Vilevile, nafasi ya Tanzania katika kupambana na vitendo vya rushwa iliimarika na kufikia nafasi ya 82 kati ya nchi 180 mwaka 2024 ikilinganishwa na nafasi ya 87 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 18.1: Mwenendo wa Fahirisi ya Rushwa katika Sekta ya Umma, Mwaka 2015 - 2024**




**Jitihada za Kupunguza Umaskini**

454. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuboresha hali ya maisha ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali, ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF. Kaya zinazonufaika na Mpango wa TASAF katika kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya Mpango kuanzia Julai 2021 hadi Desemba 2024 zilikuwa 1,371,916 zenye wanufaika 6,983,665. Kati ya wanufaika wa Mpango, wanawake walikuwa 3,493,707 (asilimia 50.03) na wanaume 3,489,958 (asilimia 49.97). Aidha, watoto wenye umri wa hadi miaka mitano (5) waliotakiwa kuhudhuria kliniki walikuwa 768,186, sawa na asilimia 11.0 ya wanufaika wote wa TASAF. Vilevile, wanufaika waliokuwa na umri wa kwenda shule kati ya miaka 6 hadi 18 walikuwa 2,933,160 (asilimia 42.0) na wanufaika wenye umri kati ya miaka 19 hadi 60 wanaoweza kushiriki katika shughuli za uzalishaji walikuwa 2,583,971 (asilimia 37.0). Wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 walikuwa 698,348, sawa na asilimia 10.0 ya wanufaika wote. Tathmini ya hali ya uchumi wa kaya zilizonufaika na afua za mpango wa TASAF zinaonesha uwepo wa kaya 394,505 zilizoimarika kiuchumi na kwamba zinaweza kumudu mahitaji yao ya msingi bila kutegemea ruzuku ya Mpango. Hivyo, kaya hizo zilihitimu kutoka kwenye mpango na zinaendesha maisha yao kwa kujitegemea bila kutegemea ruzuku ya serikali kupitia TASAF.

**Jedwali Na. 18.2: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Mwaka 2023 - 2024**

| Jinsia | Idadi ya Wanufaika | | Idadi ya Wanufaika mwaka 2024 kwa Umri | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2023 | 2024 | 0 - 5 | 6 - 18 | 19 - 60 | Zaidi ya 60 |
| Wanaume | 3,338,214 | 3,489,958 | 409,419 | 1,616,881 | 1,200,993 | 262,665 |
| Wanawake | 3,600,267 | 3,493,707 | 358,767 | 1,316,279 | 1,382,978 | 435,683 |
| **Jumla** | **6,938,481** | **6,983,665** | **768,186** | **2,933,160** | **2,583,971** | **698,348** |
| **Asilimia ya wanufaika wote** | | | **11.0** | **42.0** | **37.0** | **10.0** |

**Chanzo:** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

455. Mwaka 2024, shilingi bilioni 2,035.58 zilitolewa kupitia uhawilishaji fedha kwa wanufaika wote ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,834.33 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 11.0. Aidha, vikundi 68,346 vyenye wanachama 906,958 (wanawake 773,931 na wanaume 133,027) viliundwa kutoka katika kaya maskini ikilinganishwa na vikundi 56,518 vyenye wanachama 778,940 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la vikundi kwa asilimia 20.9. Ongezeko hilo lilitokana na wanufaika kuhamasika kuunda vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Vilevile, shilingi bilioni 7.6 zilikopeshwa kwa wanachama wa vikundi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.8 zilizokopeshwa mwaka 2023.

456. Mwaka 2024, Serikali kwa kushirikiana na walengwa wa Mpango wa TASAF iliendelea kutekeleza miradi ya ajira za muda kwa lengo la kuongeza kipato cha kaya na kuchochea maendeleo ya jamii. Miradi hii hufanywa na walengwa wa Mpango wenye uwezo wa kufanya kazi na kulipwa ujira baada ya kukamilisha kazi waliyopangiwa. Mwaka 2024, miradi 27,863 ya kutoa ajira za muda ilitekelezwa na shilingi bilioni 123.6 zililipwa kwa walengwa walioshiriki katika utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na miradi 17,421 mwaka 2023. Aidha, miradi hiyo ilinufaisha kaya 662,374 na ililenga sekta za huduma za jamii kama afya, elimu na maji, pamoja na kutatua changamoto za mawasiliano, usafirishaji na utunzaji wa mazingira.

## SURA YA 19

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

### Usajili wa Miradi ya Uwekezaji

457. Mwaka 2024, Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC kilisajili miradi 901 ikilinganishwa na miradi 526 iliyosajiliwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 71.3. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi 321 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 404 ya wageni na miradi 176 ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni. Aidha, miradi iliyosajiliwa ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 9,312.69 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,720.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 62.8. Ongezeko hilo lilichangiwa na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kati ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2024, miradi 51 ilikuwa ya upanuzi na ukarabati ikilinganishwa na miradi 57 ya upanuzi na ukarabati iliyosajiliwa mwaka 2023. Miradi iliyosajiliwa mwaka 2024 ilikuwa na fursa za ajira 212,293 ikilinganishwa na fursa za ajira 137,010 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 54.9.

### Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta

458. Mwaka 2024, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kusajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,079.03 ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji mizigo dola za Marekani milioni 1,361.15 na sekta ya ujenzi wa majengo ya biashara dola za Marekani milioni 1,135.13. Katika kipindi hicho, sekta iliyosajili idadi kubwa ya miradi ilikuwa uzalishaji viwandani iliyosajili miradi 415, ikifuatiwa na usafirishaji mizigo miradi 149 na ujenzi wa majengo ya biashara miradi 105. Kuongezeka kwa usajili wa miradi kulitokana na kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji, utoaji wa huduma kwa njia ya kielektroniki pamoja na kupeleka huduma karibu na wawekezaji kupitia ofisi za kanda.

**Jedwali Na. 19.1: Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2024**

| Na. | Sekta | Miradi Iliyosajiliwa | | | | Fursa za ajira | Thamani (Dola za Marekani Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watanzania | Wageni | Ubia | Jumla | | |
| 1 | Kilimo | 28 | 38 | 13 | 79 | 125,760 | 687.2 |
| 2 | Mawasiliano | 1 | 2 | 2 | 5 | 836 | 809.74 |
| 3 | Utalii | 43 | 18 | 22 | 83 | 6,949 | 348.82 |
| 4 | Uzalishaji viwandani | 98 | 237 | 80 | 415 | 45,883 | 4,079.03 |
| 5 | Ujenzi majengo ya biashara | 32 | 57 | 16 | 105 | 7,475 | 1,135.13 |
| 6 | Usafirishaji mizigo | 92 | 29 | 28 | 149 | 18,622 | 1,361.15 |
| 7 | Huduma | 9 | 9 | 7 | 25 | 2,937 | 285.28 |
| 8 | Rasilimali watu | 9 | 4 | 1 | 14 | 2,181 | 142.67 |
| 9 | Madini | 2 | 1 | 4 | 7 | 135 | 7.35 |
| 10 | Nishati | 3 | 6 | 2 | 11 | 204 | 112.47 |
| 11 | Miundombinu ya kiuchumi | 4 | 3 | 0 | 7 | 1,283 | 298.75 |
| 12 | Huduma za fedha | 0 | 0 | 1 | 1 | 28 | 45.1 |
| | **Jumla** | **321** | **404** | **176** | **901** | **212,293** | **9,312.69** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

**Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa**

459. Mwaka 2024, mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa usajili wa miradi kwa asilimia 39.5 ukifuatiwa na mkoa wa Pwani asilimia 18.4 na Arusha asilimia 7.1. Hii ilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na uwepo wa Ofisi za Kanda za Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

**Jedwali Na. 19.2: Mgawanyiko wa Miradi Iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2024**

| Mkoa | Sekta | | | | | | | | | | | | Jumla ya Miradi Kimkoa | Mgawanyo Kimkoa (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kilimo | Ujenzi wa Majengo ya Biashara | Miundombinu ya Uchumi | Nishati | Taasisi za Fedha | Rasilimali Watu | Uzalishaji Viwandani | Madini na Petroli | Huduma | Mawasiliano ya Simu | Utalii | Usafirishaji Mizigo | | |
| Dar-es-salaam | 7 | 70 | 3 | 1 | 1 | 10 | 118 | 0 | 18 | 5 | 17 | 106 | 356 | 40 |
| Pwani | 18 | 16 | 2 | 0 | 0 | 0 | 116 | 0 | 2 | 0 | 3 | 9 | 166 | 18 |
| Ruvuma | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 10 | 1 |
| Mwanza | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 23 | 0 | 1 | 0 | 0 | 6 | 37 | 4 |
| Morogoro | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 22 | 2 |
| Shinyanga | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 14 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 2 |
| Arusha | 6 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 34 | 8 | 64 | 7 |
| Dodoma | 4 | 8 | 0 | 0 | 0 | 1 | 24 | 1 | 1 | 0 | 6 | 2 | 47 | 5 |
| Kigoma | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 8 | 1 |
| Tanga | 2 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 12 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 23 | 3 |
| Lindi | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 13 | 1 |
| Simiyu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 5 | 1 |
| Katavi | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 1 |
| Njombe | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 11 | 1 |
| Geita | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 14 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 18 | 2 |
| Kilimanjaro | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 18 | 2 |
| Mbeya | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 14 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 20 | 2 |
| Mtwara | 7 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 12 | 1 |
| Mara | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 5 | 0 | 8 | 1 |
| Manyara | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 9 | 1 |
| Iringa | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 11 | 1 |
| Kagera | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 1 |
| Songwe | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 1 |
| Singida | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 6 | 1 |
| Rukwa | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Tabora | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **79** | **105** | **7** | **11** | **1** | **14** | **415** | **7** | **25** | **5** | **83** | **149** | **901** | **100** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

### Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje

460. Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2024, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 3.9 na kufikia dola za Marekani milioni 23,042.5 mwaka 2023 kutoka dola za Marekani milioni 22,182.4[4] mwaka 2022. Kati ya uwekezaji huo, uwekezaji wa moja kwa moja ulikuwa dola za Marekani milioni 19,139.6, sawa na asilimia 83.1 ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani 204.3 (asilimia 0.9) na uwekezaji mwingine ulifikia dola za Marekani 3,698.6 (asilimia 16.1). Aidha, mitaji iliyowekezwa na sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa bei za miaka husika ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,694.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,745.8 zilizowekezwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 2.9.

**Jedwali Na. 19.3: Uwekezaji wa Sekta Binafsi kutoka Nje ya Nchi, Mwaka 2019 - 2023 (Dola za Marekani Milioni)**

| Aina ya uwekezaji | Kiasi kilichowekezwa | | | | | Limbikizo lililowekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka Nje | 1,217.2 | 943.8 | 1,190.5 | 1,437.6 | 1,648.9 | 14,762.9 | 15,612.6 | 15,741.1 | 18,095.8 | 19,139.6 |
| Uwekezaji wa Hisa | 5.5 | 1.8 | 4.9 | 0.2 | 1.4 | 104.6 | 124.8 | 126.8 | 195.8 | 204.3 |
| Uwekezaji mwingine | 17.3 | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 44.5 | 2,810.0 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,890.8 | 3,698.6 |
| **Jumla** | **1,240.0** | **860.1** | **1,186.8** | **1,745.8** | **1,694.8** | **17,677.5** | **18,461.9** | **18,924.3** | **22,182.4** | **23,042.5** |


**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

### Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje

461. Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,648.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,437.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato na muunganiko na ununuzi wa kampuni za kimataifa pamoja na kuimarika kwa ugharamiaji wa miradi ya kimataifa.

[4] Takwimu za uwekezaji kwa mwaka 2022 zimefanyiwa marekebisho

**Kielelezo Na. 19.1: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje, Mwaka 2017 - 2023**




462. Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliendelea kuongezeka ambapo nchi za OECD zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wa asilimia 42.4 ikilinganishwa na asilimia 42.7 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, mchango wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nchi za EAC na SADC ulikuwa asilimia 30.0 ikilinganishwa na asilimia 18.0 mwaka 2022. Aidha, nchi za Mauritius na Afrika Kusini zilichangia zaidi katika uwekezaji kwa upande wa nchi za SADC na Kenya ilichangia zaidi katika uwekezaji kutoka nchi za EAC.

**Jedwali Na. 19.4: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nchi za SADC na EAC, Mwaka 2019 - 2023 (Dola za Marekani Milioni)**


| **Kanda/Nchi** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|
| **SADC** | **503.7** | **44.2** | **126.5** | **208.6** | **430.9** |
| Botswana | -2.2 | -0.6 | -0.5 | 3.9 | 56.0 |
| Mauritius | 423.8 | 48.9 | 73.5 | 150.3 | 242.0 |
| Afrika ya Kusini | 77.4 | -6.2 | 51.4 | 54.4 | 121.8 |
| Nchi nyingine za SADC | 4.8 | 2.2 | 2.1 | -0.1 | 11.1 |
| **EAC** | **-34.4** | **24.7** | **30.0** | **49.9** | **64.8** |
| Kenya | -37.1 | 24.6 | 30.3 | 48.9 | 63.8 |
| Uganda | 0.2 | 0.1 | -0.2 | 1.0 | 1.1 |
| Nchi Nyingine za EAC | 2.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **Jumla Kuu** | **469.3** | **68.9** | **156.5** | **258.5** | **495.7** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi**

463. Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliendelea kujikita zaidi katika shughuli za uchimbaji madini na mawe, fedha na bima pamoja na uzalishaji viwandani. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 70.4 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za uchimbaji madini na mawe zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 532.5, sawa na asilimia 32.3 ya uwekezaji wote, ikifuatiwa na uzalishaji viwandani wenye thamani ya dola za Marekani milioni 361 (asilimia 21.9) na shughuli za fedha na bima zenye thamani ya dola za Marekani milioni 267.6 (asilimia 16.2) mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 19.2: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi, Mwaka 2019 - 2023**



**Jedwali Na. 19.5: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi, Mwaka 2019 - 2023 (Dola za Marekani Milioni)**

| Shughuli za kiuchumi | Kiasi kilichowekezwa | | | | | Limbikizo lililowekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Malazi na huduma za chakula | 6.3 | -7.5 | -0.3 | 36.3 | 15.2 | 380.9 | 372.2 | 356.9 | 545.7 | 492.1 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 8.0 | -12.0 | 2.0 | -3.7 | 4.4 | 70.2 | 61.2 | 78.1 | 123.2 | 122.3 |
| Kilimo | 30.3 | 15.5 | 20.8 | 14.3 | 57.8 | 1,582.4 | 1,596.4 | 579.5 | 660.4 | 679.1 |
| Sanaa na burudani | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.7 | 0.1 | 0.6 | 0.6 | 2.1 | 1.4 | 1.3 |
| Ujenzi | 81.2 | -2.3 | -15.4 | 15.5 | 19.6 | 290.7 | 286.1 | 305.8 | 292.0 | 401.1 |
| Elimu | 3.2 | 0.8 | -2.2 | -0.1 | -0.5 | 9.8 | 10.5 | 9.7 | 7.9 | 7.0 |
| Umeme na gesi | 8.9 | -22.8 | -2.3 | 1.5 | 8.0 | 59.7 | 36.7 | 13.9 | 48.6 | 47.3 |
| Fedha na bima | 162.9 | 85.4 | 132.8 | 238.4 | 267.6 | 1,274.9 | 1,321.7 | 1,463.7 | 1,565.8 | 1,692.9 |
| Afya na huduma za jamii | 1.3 | -1.2 | 11.3 | -4.4 | 4.1 | 61.6 | 60.0 | 92.7 | 16.5 | 19.0 |
| Habari na mawasiliano | 274.7 | 60.3 | 34.5 | 89.5 | 198.0 | 1,463.2 | 1,517.2 | 1,204.6 | 2,044.4 | 2,105.3 |
| Uzalishaji viwandani | 225.5 | 176.2 | 352.0 | 180.1 | 361.0 | 2,221.4 | 2,375.1 | 2,412.1 | 3,132.1 | 3,265.5 |
| Uchimbaji madini na mawe | 384.5 | 614.2 | 596.3 | 847.1 | 532.5 | 6,589.4 | 7,205.0 | 8,509.1 | 8,640.6 | 9,172.1 |
| Shughuli za kitaalamu na kisayansi | 1.2 | 1.0 | 0.6 | 0.0 | 0.4 | 19.1 | 20.1 | 0.2 | 20.1 | 19.0 |
| Upangishaji majengo | -3.3 | -4.0 | -1.2 | -0.2 | 6.4 | 66.8 | 58.3 | 83.5 | 71.2 | 72.3 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 13.0 | 26.6 | 18.1 | 12.1 | 18.0 | 191.2 | 213.6 | 129.5 | 278.4 | 297.3 |
| Biashara | 19.3 | 13.4 | 43.5 | 10.7 | 156.3 | 481.0 | 477.9 | 499.8 | 647.7 | 745.9 |
| **Jumla** | **1,217.2** | **943.8** | **1,190.5** | **1,437.6** | **1,648.9** | **14,762.9** | **15,612.6** | **15,741.1** | **18,095.8** | **19,139.6** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

464. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). Katika kipindi hicho, utekelezaji wa Mpango uliwezesha kufutwa au kupunguzwa kwa tozo na ada 37 ikilinganishwa na tozo na ada 66 zilizofutwa au kupunguzwa mwaka 2023. Aidha, Mfumo wa Government Enterprises Service Bus (GovESB) uliendelea kuwezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana kwa urahisi na kubadilishana taarifa. Hadi Desemba 2024, mifumo 202 ya taasisi 179 za umma iliunganishwa kupitia mfumo wa GovESB ikilinganishwa na mifumo 90 ya taasisi za umma 83 iliyounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

465. Mwaka 2024, Serikali iliendelea kuimarisha na kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini - GePG ili kurahisisha ulipaji ada na tozo mbalimbali Serikalini. Hadi kufikia Desemba 2024, jumla ya watoa huduma na taasisi waliounganishwa walifikia 1,007 kutoka watoa huduma 983 waliounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.4.

466. Mwaka 2024, Baraza la Taifa la Biashara - TNBC liliratibu Mkutano wa 15 wa Baraza kwa kuwakutanisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi. Mkutano huo ulioongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara. Pamoja na masuala mengine, Mkutano uliazimia kubainisha changamoto mpya zinazoikabili sekta binafsi na kuandaa Mpango wa Pili wa Maboresho ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II). Maazimio ya

Mkutano huo yaliwezesha kufanyika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23. Aidha, Taarifa ya tathmini hiyo ilikamilika na kuzinduliwa tarehe 11 Septemba, 2024.

467. Tathmini hiyo ilionesha matokeo chanya mbalimbali yakiwepo kupungua kwa: muda wa kushughulikia maombi ya vibali kutoka wastani wa siku 14 hadi siku tatu (3); muda wa usajili wa hospitali binafsi kutoka miezi 12 hadi miezi mitatu (3); muda wa usafiri kwa malori ya mizigo kutoka Dar es Salaam hadi mpakani mwa Zambia (Tunduma) na mpakani mwa Rwanda (Rusumo) kutoka siku nne (4) na saba (7) hadi siku mbili (2) na tatu (3), mtawalia; muda wa kupata cheti cha usajili wa sehemu za kazi (registration certificate) kutoka siku 14 hadi siku moja (1); muda wa kutoa leseni ya kukidhi matakwa ya sheria ya usalama na afya mahali pa kazi (compliance license) kutoka siku 28 hadi siku tatu (3); na muda wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka zaidi ya siku 14 zilizoko kisheria hadi wastani wa kati ya siku tatu (3) hadi saba (7). Aidha, michakato ya ushughulikiaji wa maombi (business processes) mfano taasisi ya OSHA, hatua zimepungua kutoka 33 hadi saba (7); kupungua au kutokuwa na foleni kabisa katika ofisi nyingi za mamlaka za udhibiti zikiwepo BRELA, GCLA, TCRA na TMDA kutokana na matumizi ya mifumo ya kielekroniki. Kwa ujumla, tathmini imebainisha kuwa mwekezaji/mfanyabiashara Tanzania anaweza kusajili kampuni chini ya masaa nane (8) na kupata leseni ya biashara chini ya saa moja (1).

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

468. Mwaka 2024, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi - NEEC liliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Katika kipindi hicho, mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ilitoa mikopo, dhamana na ruzuku zenye thamani ya shilingi bilioni 759.7 kwa wajasiriamali 6,183,835 (wanawake 3,062,174 na wanaume 3,121,661) ikilinganishwa na shilingi bilioni 743.7 zilizotolewa kwa wajasiriamali 6,064,957 mwaka 2023, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 2.1. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 408.04 zilikuwa mikopo ya moja kwa moja na dhamana iliyotolewa kwa wanufaika 746,157 na shilingi bilioni 351.6 ilikuwa ruzuku iliyotolewa kwa wanufaika 5,437,050. Aidha, mifuko na programu za uwezeshaji ilizalisha ajira 8,153,224 (wanawake 4,419,046 na wanaume 3,734,178) mwaka 2024 ikilinganishwa na ajira 7,764,975 zilizozalishwa mwaka 2023. Sekta zilizonufaika zaidi zilijumuisha kilimo, mifugo na uvuvi kwa asilimia 47.2 ikifuatiwa na sekta ya viwanda na biashara asilimia 12.9. Kwa upande wa mifuko inayotoa mikopo ya moja kwa moja na dhamana, kiasi cha shilingi bilioni 493.9 zinazotokana na mikopo ya miaka ya nyuma iliyoiva kilirejeshwa katika kipindi hicho. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa kiasi cha fedha kinachorejeshwa ni pungufu ya kiasi kinachostahili kurejeshwa katika kipindi husika cha kuiva kwa mkopo kutokana na mapungufu katika mfumo wa uwekaji wa

kumbukumbu za utoaji na urejeshaji wa mikopo. Mifuko inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha katika eneo hilo ili kuhakikisha ufanisi katika urejeshaji wa mikopo kwa wakati na hivyo kuwa na uendelevu wa mifuko.

**Jedwali Na. 19.6: Mikopo iliyotolewa kwa Shughuli za Kiuchumi, Mwaka 2023 - 2024**

| Na. | Sekta | 2023 | | 2024 | | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiasi Kilichotolewa | Marejesho | Kiasi Kilichotolewa | Marejesho | |
| 1 | Afya | 11,371,315,575.0 | 15,456,000,000.0 | 12,620,531,799.5 | 16,520,115,765.0 | 3.1 |
| 2 | Elimu | 50,856,718,840.0 | 70,125,500,000.0 | 49,986,771,028.5 | 64,219,843,200.0 | 12.3 |
| 3 | Madini | 31,647,381,000.0 | 47,650,000,000.0 | 32,986,272,576.9 | 39,125,564,356.0 | 8.1 |
| 4 | Kilimo, mifugo na uvuvi | 196,435,467,263.4 | 216,435,000,000.0 | 190,117,945,356.7 | 198,645,264,116.2 | 46.6 |
| 5 | Utalii | 38,962,628,100.0 | 58,210,000,000.0 | 37,709,174,814.6 | 63,195,254,370.6 | 9.2 |
| 6 | Viwanda na biashara | 65,082,586,480.1 | 104,301,000,000.0 | 57,415,570,446.9 | 74,673,297,106.1 | 14.1 |
| 7 | Nishati | 25,237,308,000.0 | 32,450,000,000.0 | 20,783,592,858.4 | 28,993,174,432.0 | 5.1 |
| 8 | Nyinginezo | 10,938,769,909.0 | 14,380,000,000.0 | 6,428,786,815.9 | 8,542,350,250.9 | 1.6 |
| **Jumla** | | **430,532,175,167.6** | **559,007,500,000.0** | **408,048,645,697.3** | **493,914,863,596.8** | **100** |

**Chanzo:** Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
*Angalizo: Marejesho yanahusiana na mikopo ya zamani iliyoiva na hayana uhusiana wa moja kwa moja na mikopo iliyotolewa kwa mwaka husika*

469. Mwaka 2024, Baraza liliratibu utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali 628,514 (wanawake 347,585 na wanaume 280,929) ikilinganishwa na wajasiriamali 490,199 waliopata mafunzo mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 28.2. Hii ilitokana na wajasiriamali kuhamasika kushiriki katika mafunzo.

470. Hadi Desemba 2024, vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi vilikuwa 27 ikilinganishwa na vituo 20 vilivyokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, vituo vilitoa huduma kwa wananchi 43,716 (wanawake 17,439 na wanaume 26,277) mwaka 2024 ikilinganishwa na wananchi 40,657 waliopatiwa huduma mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Ongezeko hilo lilitokana na wananchi kutembelea vituo vya uwekezaji ili kupata huduma za mafunzo, ushauri wa kibiashara, urasimishaji wa biashara, mikopo, ruzuku, na dhamana. Aidha, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.09 ilitolewa kupitia vituo vya uwezeshaji kwa wajasiriamali 341 (wanawake 164 na wanaume 177) mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.3 zilizotolewa kwa wajasiriamali 5,218 mwaka 2023. Kupungua kwa idadi ya wanufaika wa mikopo kulitokana na zoezi la maboresho ya mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambayo yalisababisha kusitishwa kwa shughuli hiyo kwa muda katika kipindi cha mwaka 2023 na 2024. Marejesho ya mikopo yalikuwa kiasi cha shilingi bilioni 6.73, sawa na asilimia 94.9 ya mikopo iliyotolewa ikilinganishwa na shilingi bilioni 10.6 (asilimia 93.9) mwaka 2023. Urejeshaji wa mikopo unaoridhisha ulitokana na jitihada za vituo kutembelea miradi ya wanufaika wa mikopo, fursa za mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa fedha na utunzaji wa kumbukumbu.

**Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati**

471. Mwaka 2024, miradi ya kimkakati na uwekezaji katika sekta mbalimbali ilizalisha ajira 217,808 za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 162,968 zilizozalishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 33.7. Kati ya ajira zilizozalishwa, ajira 208,526 zilikuwa za watanzania na ajira 9,282 za wageni ikilinganishwa na ajira 156,661 za watanzania na ajira 6,307 za wageni mwaka 2023. Ongezeko la ajira kwa watanzania lilitokana na juhudi za Serikali kuhakikisha mikataba inayoingiwa inaweka vipengele vya ushiriki wa watanzania.

472. Mwaka 2024, makandarasi 4,691 walishiriki kwenye miradi ya ujenzi ikilinganishwa na makandarasi 3,360 walioshiriki kwenye miradi ya ujenzi mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 39.6. Aidha, idadi ya wakandarasi wa kitanzania waliosajiliwa ilikuwa 878 na wakandarasi walioingia ubia wa kutoa huduma katika miradi ya kimkakati walikuwa 37.

**Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

473. Mwaka 2024, Serikali ilipokea na kuchambua miradi 32 inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi - PPP ikilinganishwa na miradi 10 iliyopokelewa na kuchambuliwa mwaka 2023. Hadi Desemba 2024, miradi mitano (5) ilikuwa katika hatua za ununuzi wa mbia ikilinganishwa na miradi minne (4) mwaka 2023. Aidha, miradi minne (4) ilifikia hatua ya utekelezaji, ambapo miradi miwili (2) ni ya uendeshaji wa bandari inayosimamiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mradi wa Ubungo - East African Logistic na Mradi wa Jengo la biashara (commercial complex) wa Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam - DDC. Vilevile, maandiko 104 ya miradi yalikuwa katika hatua mbalimbali za uchambuzi ikilinganishwa na maandiko 72 mwaka 2023. Kwa upande mwingine, Serikali ilitoa mafunzo kwa wadau 1,577 mwaka 2024 ikilinganishwa na wadau 555 mwaka 2023. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wadau katika uibuaji, uandaaji, ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya PPP.

.

**Jedwali Na. 73: KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA MWAKA 2023 - 2024**

| Sekta | 2023 | | | | | | | | 2024 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | E | F | G | H | A | B | C | D | E | F | G | H |
| Kilimo | 48 | 43 | 5 | 14 | 21 | 13 | 30,718 | 793.1 | 79 | 73 | 6 | 28 | 38 | 13 | 125,760 | 687.2 |
| Mawasili bv ano | 2 | 2 | - | 0 | 1 | 1 | 43 | 28.5 | 5 | 4 | 1 | 1 | 2 | 2 | 836 | 809.7 |
| Utalii | 58 | 48 | 10 | 23 | 19 | 16 | 4,103 | 188.6 | 83 | 75 | 8 | 43 | 18 | 22 | 6,949 | 348.8 |
| Uzalishaji Viwandani | 208 | 193 | 15 | 49 | 111 | 48 | 26,563 | 1688.5 | 415 | 400 | 15 | 98 | 237 | 80 | 45,883 | 4,079.0 |
| Majengo ya biashara | 57 | 54 | 3 | 14 | 29 | 14 | 3,596 | 1054.2 | 105 | 103 | 2 | 32 | 57 | 16 | 7,475 | 1,135.1 |
| Usafirishaji Mizigo | 111 | 87 | 24 | 66 | 22 | 23 | 18,780 | 1322.5 | 149 | 132 | 17 | 92 | 29 | 28 | 18,622 | 1,361.2 |
| Huduma | 20 | 20 | - | 4 | 7 | 9 | 1,832 | 282.7 | 25 | 25 | 0 | 9 | 9 | 7 | 2,937 | 285.3 |
| Rasilimali Watu | 6 | 6 | - | 3 | 1 | 2 | 443 | 7.1 | 14 | 13 | 1 | 9 | 4 | 1 | 2,181 | 142.7 |
| Madini | 6 | 6 | 0 | 4 | 0 | 2 | 495 | 47.5 | 7 | 7 | 0 | 2 | 1 | 4 | 135 | 7.4 |
| Nishati | 3 | 3 | - | 1 | 1 | 1 | 118 | 58.2 | 11 | 10 | 1 | 3 | 6 | 2 | 204 | 112.5 |
| Miundombinu ya Kiuchumi | 7 | 7 | - | 4 | 2 | 1 | 50,319 | 249.4 | 7 | 7 | 0 | 4 | 3 | 0 | 1,283 | 298.8 |
| Huduma za kifedha | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **1** | **1** | **0** | **0** | **0** | **1** | **28** | **45.1** |
| **Jumla** | **526** | **469** | **57** | **182** | **214** | **130** | **137,010** | **5,720.4** | **901.0** | **850.0** | **51.0** | **321.0** | **404.0** | **176.0** | **212,293** | **9,312.7** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania
A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
B Miradi Mipya
C Miradi inayoendelea
D Miradi ya wazawa
E Miradi ya Wageni
F Miradi ya Ubia
G Jumla ya Ajira
H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD Milioni)
- Takwimu Hazikupatikana



Sehemu ya Nne

# SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

## SURA YA 20

## UENDELEZAJI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Utangulizi**

474. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Benki ya Dunia kuhusu nishati safi ya kupikia (World Bank Multi-Tier Framework - MTF) wa mwaka 2020, nishati safi ya kupikia hupimwa kwa kuzingatia ufanisi, urahisi wa kutumia, upatikanaji, usalama, unafuu na kiwango kidogo cha sumu. Aidha, Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani wa mwaka 2021 umeeleza kuwa nishati safi na teknolojia hupimwa kwa viwango vya chembechembe ndogo za vumbi zenye ukubwa usiozidi 2.5µm (PM2.5) na hewa ya kaboni monoksaidi inayotolewa.

475. Kwa muktadha wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034), nishati safi ya kupikia ni dhana inayotumika kuelezea na kubainisha nishati na teknolojia sahihi zinazotoa moshi wenye kiwango kidogo cha sumu pale zinapotumika kwa usahihi. Dhana ya nishati safi ya kupikia ina lengo la kuhakikisha uwepo wa usalama, uendelevu na urahisi wa upatikanaji wa nishati ya kupikia, kuokoa muda, kupunguza gharama za matumizi pamoja na athari za kimazingira na kiafya kwa watumiaji. Aidha, utumiaji wa nishati safi ya kupikia ni nyenzo muhimu katika kutekeleza makubaliano ya kitaifa na kimataifa yanayolenga kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa gesi joto (greenhouse gas) duniani.

**Sera na Mikakati ya Kitaifa Inayohusiana na Nishati Safi ya Kupikia**

476. Kwa kutambua umuhimu wa nishati safi ya kupikia, mwaka 2024 Serikali ilizindua rasmi Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) unaolenga kuwezesha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kila mwananchi ili kulinda afya, mazingira na kuboresha maisha. Lengo la Mkakati ni kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa sera mbalimbali zenye lengo la kuwezesha upatikanaji wa nishati safi, nafuu, endelevu na ya uhakika ya kupikia nchini. Miongoni mwa sera hizo ni:

i. Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 yenye lengo la kuboresha maisha ya wananchi kupitia matumizi ya nishati za kisasa za kupikia;

ii. Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 yenye lengo la kuimarisha uhifadhi wa misitu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira kupitia matumizi ya nishati mbadala zenye gharama nafuu na zinazopatikana kwa urahisi kama vyanzo vya nishati ya kupikia;

iii. Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kuhakikisha kuwa kuna eneo la misitu la kutosha chini ya usimamizi madhubuti;

iv. Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 inayolenga kuwa na utaratibu mzuri na endelevu wa kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira kwa faida ya afya ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo; na

v. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mwanamke na Jinsia ya Mwaka 2000 inayolenga kutunza mazingira kwa ajili ya kumpunguzia mwanamke mzigo wa kutafuta kuni na maji ili kuwezesha ushiriki wake katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

**Hali Ilivyo**


**Hali ya Uzalishaji wa Hewa Ukaa**

477. Mpango wa kuzuia uharibifu wa mazingira na kulinda afya za wananchi unaathiriwa kwa kiasi kikubwa na uzalishaji wa hewa ukaa duniani. Mataifa yote duniani yanapaswa kutekeleza makubaliano ya kitaifa na kimataifa yanayolenga kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa uzalishaji wa hewa ukaa unazidi kuongezeka duniani, hususan kwa nchi zilizoendelea kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani. Kulingana na Takwimu za Benki ya Dunia (World Bank Open Data), uzalishaji wa hewa ukaa (carbon dioxide emission) duniani ulifikia tani milioni 39,023.94 mwaka 2023 kutoka tani milioni 25,725.44 mwaka 2000.

478. Kwa mujibu wa Takwimu za Benki ya Dunia, uzalishaji wa hewa ukaa kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa tani milioni 825.51 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 571.77 mwaka 2000. Katika nchi za Afrika Magharibi na Kati, uzalishaji wa hewa ukaa ulifikia tani milioni 245.64 mwaka 2023 kutoka tani milioni 146.74 mwaka 2000. Katika nchi za Latin America na Caribbean, uzalishaji wa hewa ukaa ulifikia tani milioni 1,749.80 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 1,350.00 mwaka 2000. Katika nchi za Umoja wa Ulaya, uzalishaji wa hewa ukaa ulipungua na kufikia tani milioni 2,512.07 kutoka tani milioni 3,563.26 mwaka 2000. Uzalishaji wa hewa ukaa Amerika Kaskazini ulikuwa tani milioni 5,257.40 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 6,472.17 mwaka 2000. Katika nchi za Asia Mashariki na Pacific, uzalishaji wa hewa ukaa uliongezeka na kufikia tani milioni 17,247.09 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 6,713.22 mwaka 2000. Katika nchi za Asia Kusini, uzalishaji wa hewa ukaa ulifikia tani milioni 3,332.51 mwaka 2023 kutoka tani milioni 1,151.44 mwaka 2000. Kutokana na


uchambuzi wa Takwimu za Benki ya Dunia, nchi za Afrika ikiwemo zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara zinachangia kiwango kidogo sana katika uzalishaji wa hewa ukaa.

**Kielelezo Na. 20.1: Uzalishaji wa Hewa Ukaa Kikanda**




479. Kwa upande wa nchi, China, Marekani na India zinaongoza kwa uzalishaji wa hewa ukaa. Uzalishaji wa hewa ukaa nchini China ulifikia tani milioni 13,259.64 mwaka 2023 kutoka tani milioni 3,666.95 mwaka 2000. Marekani ilizalisha hewa ukaa tani milioni 4,682.04 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 5,928.97 mwaka 2000. Katika nchi ya India, uzalishaji wa hewa ukaa ulifikia tani milioni 2,955.18 mwaka 2023 kutoka tani milioni 995.65 mwaka 2000. Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kenya iliongoza kwa uzalishaji wa hewa ukaa ambapo tani milioni 21.73 zilizalishwa mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 8.91 mwaka 2000. Tanzania ni ya pili kwa uzalishaji wa hewa ukaa ambapo tani milioni 19.37 zilizalishwa mwaka 2023 ikilinganishwa na tani milioni 3.11 mwaka 2000. Licha ya Tanzania kuwa nchi ya pili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzalisha kiwango kikubwa cha hewa ukaa, uzalishaji wake upo chini ya wastani wa tani milioni 825.51 zilizozalishwa katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

**Kielelezo Na. 20.2: Uzalishaji wa Hewa Ukaa kwa baadhi ya Nchi**





480. Uzalishaji wa hewa ukaa hutofautiana kulingana na nishati, ambapo makaa ya mawe huzalisha kiwango cha juu zaidi cha hewa ukaa ikilinganishwa na gesi asilia ambayo huzalisha kiwango cha chini zaidi. Aidha, gesi asilia huzalisha hewa ukaa takriban asilimia 45 pungufu ya kiwango kinachozalishwa na makaa ya mawe ikilinganishwa na bidhaa za mafuta ambazo huzalisha hewa ukaa kwa takriban asilimia 25 pungufu.

**Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Duniani**

481. Upatikanaji wa nishati safi ya kupikia unatofautiana katika maeneo mbalimbali duniani. Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara zina kiwango kidogo cha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ambacho hakiendani na ongezeko la idadi ya watu. Kiwango cha ongezeko la idadi ya watu katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kilikuwa wastani wa watu milioni 26 kwa mwaka kati ya mwaka 2010 na 2019 ikilinganishwa na ongezeko la upatikanaji wa huduma ya nishati safi, ambalo lilikuwa wastani wa watu milioni 8 kwa mwaka. Kulingana na Takwimu za Benki ya Dunia, kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kiliongezeka na kufikia asilimia 22.24 ya idadi ya watu mwaka 2022 kutoka asilimia 8.85 mwaka 2000. Katika nchi za *Latin America na Caribbean,* kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia kiliongezeka na kufikia asilimia 89.16 ya idadi ya watu mwaka 2022 kutoka asilimia 80.22 mwaka 2000. Katika nchi za Asia Mashariki na Pacific, kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za

kupikia kiliongezeka na kufikia asilimia 85.33 ya idadi ya watu mwaka 2022 kutoka asilimia 41.69 mwaka 2000. Katika nchi za Umoja wa Ulaya pamoja na Amerika Kaskazini, kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia kilibaki kuwa asilimia 100 tangu mwaka 2000 hadi mwaka 2022. Aidha, upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia duniani uliongezeka na kufikia asilimia 73.74 mwaka 2022 kutoka asilimia 49.17 mwaka 2000.

**Kielelezo Na. 20.3: Upatikanaji wa Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia Kikanda (Asilimia)**




482. Uzoefu wa nchi mbalimbali duniani kulingana na takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2023 unaonesha kuwa nchi za Asia, hususan Asia Mashariki na Kusini pamoja na nchi za Latini Amerika na Caribbean zina mwenendo mzuri wa upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia. Kiwango cha upatikanaji nchini China kiliongezeka kutoka asilimia 41.3 mwaka 2000 hadi asilimia 87.8 mwaka 2022. Nchini India, kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia kiliongezeka kutoka asilimia 22.6 mwaka 2000 na kufikia asilimia 74.5 mwaka 2022. Aidha, kiwango cha upatikanaji katika nchi ya Brazil kiliongezeka kutoka asilimia 89.05 mwaka 2000 na kufikia asilimia 96.5 mwaka 2022. Nchini Afrika Kusini, kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia kiliongezeka kutoka asilimia 56.0 mwaka 2000 hadi asilimia 89.4 mwaka 2022. Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kiwango cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia nchini Kenya kiliongezeka kutoka asilimia 1.70 mwaka 2000 na kufikia asilimia 30.0 mwaka 2022. Nchini Tanzania, kiwango cha upatikanaji

kiliongezeka kutoka asilimia 0.7 mwaka 2000 hadi asilimia 9.2 mwaka 2022. Mwenendo wa upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia unaonesha kuwa Tanzania ina kiwango kisichoridhisha cha upatikanaji wa nishati safi na teknolojia za kupikia. Kutokana na hilo, Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) ili kuongeza kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

**Jedwali Na. 20.1: Upatikanaji wa Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia kwa Baadhi ya Nchi, Mwaka 2000 - 2023 (Asilimia ya Idadi ya Watu)**

| Mwaka | Tanzania | Kenya | Uganda | Rwanda | Burundi | Afrika Kusini | Botswana | Angola | Brazil | China | India |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2000 | 0.7 | 1.7 | 0.9 | 0.1 | 0.3 | 56.0 | 44.2 | 40.9 | 89.1 | 41.3 | 22.6 |
| 2001 | 0.7 | 2.2 | 0.9 | 0.1 | 0.3 | 58.0 | 46.2 | 41.4 | 89.8 | 41.8 | 23.9 |
| 2002 | 0.7 | 2.5 | 0.9 | 0.1 | 0.3 | 60.0 | 47.9 | 41.5 | 90.2 | 42.9 | 25.1 |
| 2003 | 0.7 | 3.0 | 0.8 | 0.1 | 0.3 | 62.3 | 49.3 | 42.1 | 90.7 | 44.1 | 26.0 |
| 2004 | 0.8 | 3.5 | 0.8 | 0.1 | 0.3 | 64.5 | 51.0 | 41.8 | 91.3 | 45.5 | 27.3 |
| 2005 | 0.8 | 4.1 | 0.8 | 0.1 | 0.3 | 66.7 | 52.1 | 42.7 | 91.6 | 46.7 | 28.1 |
| 2006 | 0.9 | 4.7 | 0.8 | 0.1 | 0.3 | 69.0 | 53.4 | 43.1 | 92.1 | 48.5 | 29.3 |
| 2007 | 1.0 | 5.2 | 0.8 | 0.2 | 0.2 | 71.2 | 54.8 | 43.1 | 92.5 | 50.3 | 30.7 |
| 2008 | 1.1 | 5.9 | 0.8 | 0.2 | 0.2 | 73.3 | 56.3 | 43.7 | 93.1 | 52.7 | 31.9 |
| 2009 | 1.2 | 6.5 | 0.8 | 0.2 | 0.2 | 75.3 | 57.3 | 44.0 | 93.4 | 55.2 | 33.4 |
| 2010 | 1.4 | 7.0 | 0.9 | 0.3 | 0.2 | 77.1 | 58.4 | 44.6 | 93.9 | 57.4 | 35.3 |
| 2011 | 1.6 | 7.6 | 0.9 | 0.3 | 0.2 | 78.7 | 59.4 | 44.8 | 94.3 | 60.1 | 37.2 |
| 2012 | 1.9 | 8.5 | 0.9 | 0.4 | 0.2 | 80.0 | 60.1 | 45.7 | 94.7 | 62.9 | 39.2 |
| 2013 | 2.2 | 9.5 | 0.9 | 0.5 | 0.2 | 81.4 | 60.5 | 46.0 | 95.1 | 65.8 | 42.0 |
| 2014 | 2.7 | 10.6 | 0.9 | 0.7 | 0.2 | 82.8 | 61.4 | 46.6 | 95.4 | 68.8 | 44.4 |
| 2015 | 3.2 | 11.9 | 0.9 | 0.9 | 0.2 | 83.8 | 61.8 | 47.3 | 95.7 | 71.5 | 47.4 |
| 2016 | 3.9 | 13.8 | 0.8 | 1.2 | 0.2 | 84.9 | 62.5 | 47.8 | 95.8 | 74.4 | 50.9 |
| 2017 | 4.5 | 15.8 | 0.8 | 1.7 | 0.1 | 85.8 | 63.0 | 48.3 | 96.1 | 77.1 | 54.3 |
| 2018 | 5.3 | 18.1 | 0.8 | 2.4 | 0.1 | 86.6 | 63.7 | 48.6 | 96.2 | 79.5 | 58.6 |
| 2019 | 6.2 | 20.7 | 0.8 | 3.3 | 0.1 | 87.4 | 64.4 | 49.0 | 96.4 | 82.0 | 62.2 |
| 2020 | 7.2 | 23.6 | 0.7 | 4.6 | 0.1 | 88.1 | 64.8 | 49.7 | 96.4 | 83.8 | 66.8 |
| 2021 | 8.1 | 26.4 | 0.7 | 6.2 | 0.1 | 88.7 | 65.4 | 49.8 | 96.5 | 85.9 | 70.5 |
| 2022 | 9.2 | 30.0 | 0.6 | 8.3 | 0.1 | 89.4 | 66.0 | 50.0 | 96.5 | 87.8 | 74.5 |

**Chanzo**: Benki ya Dunia

483. Kulingana na ripoti ya *Unlocking Clean Cooking Pathways* ya mwaka 2023 iliyotolewa na Benki ya Dunia, gharama za kiafya kwa mwaka zinazohusiana na uchafuzi wa hewa majumbani (Household Air Pollution - HAP) duniani kutokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia zilifikia dola za Marekani trilioni 1.4. Aidha, uchafuzi wa hewa majumbani unahusishwa na vifo vya mapema takriban milioni 4 kila mwaka, hususan kwa wanawake na watoto. Gharama ya kijinsia inayotokana na kuathirika kwa shughuli za uzalishaji mali kwa wanawake ni dola za Marekani trilioni 0.8 kwa mwaka. Takwimu hii inahusisha muda ambao wanawake hutumia kutafuta nishati ya kupikia, maandalizi ya chakula na upikaji, pamoja na usafishaji wa majiko. Muda unaotumika kutekeleza shughuli


hizo huchangia kwa kiasi kikubwa katika umaskini wa muda[5] kwa wanawake. Uchambuzi huu unaonesha kuwa gharama za utoaji wa gesi joto kutokana na matumizi ya kuni zinazopatikana kwa njia isiyo endelevu kwa ajili ya kupikia, pamoja na matumizi ya nishati isiyo safi majumbani kama mkaa zinakadiriwa kufikia dola za Marekani trilioni 0.2 kwa mwaka.

**Matumizi ya Nishati Safi Tanzania**

484. Kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, nishati na teknolojia zinazotambulika kuwa safi kwa matumizi kutokana na kuwa na kiwango kidogo cha sumu ni pamoja na umeme, bayogesi, gesi asilia, gesi ya mitungi au gesi oevu, bayoethano, nishati ya jua, majiko banifu na mkaa mbadala wenye viwango vilivyothibitishwa na mamlaka ya kudhibiti viwango. Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia za Mwaka 2023, idadi ya watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia iliongezeka kutoka asilimia 0.70 mwaka 2000 hadi asilimia 9.20 mwaka 2022. Kiwango hiki ni chini ya kiwango cha wastani cha dunia cha asilimia 73.74 na cha nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara cha asilimia 22.24 kwa mwaka 2022. Kiwango kidogo cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kinachangiwa na gharama za awali za matumizi ya nishati safi kuwa kubwa, uwekezaji mdogo katika nishati safi na teknolojia za kupikia, uwezo mdogo wa watanzania walio wengi kumudu gharama ya nishati safi na uhaba wa miundombinu ya kupokea na kuhifadhi baadhi ya nishati safi, hususan gesi ya mitungi au gesi oevu.


[5] **Umaskini wa muda** ni ukosefu wa muda wa ziada wa kutosha kwa ajili ya kupumzika, burudani, au maendeleo binafsi kutokana na muda mwingi kutumika katika kazi za kulipwa au zisizo na malipo. Umaskini huu unaathiri watu wanaolazimika kutumia sehemu kubwa ya siku yao katika shughuli za msingi kama vile ajira, kulea watoto, kuhudumia wagonjwa na kazi za nyumbani, hali inayosababisha wasiwe na muda au kuwa na muda mdogo sana kwa ajili yao binafsi. Aina hii ya umaskini inajitokeza sana kwa wanawake na watu wenye kipato cha chini. **Umaskini wa muda** unaweza kuongeza **umaskini wa kiuchumi**, hususan kwa wanawake, ambao mara nyingi hubeba mzigo mkubwa wa kazi zisizo na malipo.

**Kielelezo Na. 20.4: Mwenendo wa Matumizi ya Nishati Safi na Teknolojia ya Kupikia Tanzania Mwaka 2010 - 2022**




485. Nishati na teknolojia zinazotumika kupikia nchini ni pamoja na kinyesi cha wanyama na mabaki ya mimea, kuni, mkaa, mafuta ya taa, mkaa mbadala, bayoethano, gesi ya mitungi au gesi oevu, gesi asilia, bayogesi, umeme, majiko banifu na majiko ya nishati ya jua. Kwa mujibu wa Mpangokazi wa Nishati ya Kupikia wa Mwaka 2022, asilimia 82 ya nishati kuu inayotumika nchini inatokana na tungamotaka (biomass). Aidha, inakadiriwa kuwa takriban asilimia 63.5 ya kaya nchini zinatumia nishati ya kuni kupikia, ikifuatiwa na mkaa asilimia 26.2, gesi ya mitungi asilimia 5.1, umeme asilimia 3.0 na nishati nyingine asilimia 2.2.

**Kielelezo Na. 20.5: Matumizi ya Nishati ya Kupikia kwa Kaya Tanzania Bara Mwaka 2019/20**





**Hali ya Upatikanaji wa Nishati na Teknolojia za Kupikia Nchini**

486. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya upatikanaji wa nishati nchini, ikiwemo miradi ya kuzalisha na kusambaza umeme, miradi ya utafutaji, uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia, bayogesi, bayoethano pamoja na gesi ya mitungi. Kwa kuzingatia mchanganuo wa matumizi ya nishati ya kupikia katika Kielelezo Na. 20.5, sehemu hii inaonesha hali ya upatikanaji, gharama na usambazaji wa nishati hizo kama ifuatavyo:

**Kuni**

487. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18, matumizi ya nishati ya kuni yamekithiri, hususan maeneo ya vijijini ambapo asilimia 84.8 ya kaya hutumia nishati hiyo ikilinganishwa na asilimia 17.4 katika maeneo ya mijini. Mahitaji ya nishati ya kuni vijijini ni makubwa kwa kuwa ni nishati pekee inayopatikana kwa gharama nafuu kwa mtazamo wa watumiaji. Hata hivyo, matumizi ya kuni kama nishati ya kupikia yalipungua na kufikia asilimia 60.9 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 73.1 mwaka 2007. Upungufu huo unatokana na hatua za Serikali za kuhifadhi mazingira na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kwa upande wa mikoa, mkoa wa Kagera unaongoza kwa kuwa na kaya nyingi zinazotumia nishati ya kuni kupikia (asilimia 87.5), ikifuatiwa na Simiyu (asilimia 83.8), Singida (asilimia 80.1), Manyara (asilimia 80.0) na Kilimanjaro (asilimia 79.2). Aidha, mkoa wenye kiwango kidogo cha kaya zinazotumia kuni ni Dar es Salaam ambapo asilimia 5.9 ya kaya zinatumia nishati hiyo.


**Kielelezo Na. 20.6: Matumizi ya Kuni Kama Nishati ya Kupikia katika Ngazi ya Mkoa, Mwaka 2017/18 (Asilimia ya Kaya)**





**Mkaa**

488. Mkaa ni chanzo kikubwa zaidi cha nishati katika maeneo ya mijini kwa kuwa inaaminika kuwa nafuu na hupatikana kwa vipimo mbalimbali kulingana na kipato cha mtumiaji. Kulingana na tafiti za mapato na matumizi ya kaya binafsi, matumizi ya nishati ya mkaa kupikia yaliongezeka kutoka asilimia 22.7 mwaka 2007 hadi asilimia 28.8 mwaka 2017/18. Ongezeko hilo linatokana na urahisi wa kusafirisha, kusambaza na kuhifadhi mkaa. Kwa mujibu wa Mpangokazi wa Nishati ya Kupikia wa Mwaka 2022, inakadiriwa kuwa tani 10 hadi 12 za magogo huchomwa ili kuzalisha tani moja ya mkaa. Aidha, kwa mujibu wa ripoti ya *The Potential and* Optimal *Strategies for Charcoal Sub-Sector Development in Tanzania* ya Mwaka 2019, matumizi ya mkaa yamekithiri maeneo ya mjini ambapo zaidi ya asilimia 50 ya mkaa unaozalishwa nchini hutumika Jijini Dar-es-Salaam. Aidha, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18 unaonesha kuwa mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na kaya nyingi zaidi zinazotumia mkaa kupikia (asimia 58.9), ikifuatiwa na Morogoro (asilimia 43.9), Mwanza (asilimia 40.0), Kigoma (asilimia 35.7) na Rukwa (asilimia 35.7). Mkoa wenye kiwango kidogo zaidi cha kaya zinazotumia mkaa kupikia ni Kilimanjaro (asilimia 6.8), ikifuatiwa na Arusha (asilimia 10.5), Singida (asilimia 10.9) na Kagera (asilimia 11.0). Vilevile, Utafiti huo unaonesha kuwa asilimia 60.5 ya kaya katika maeneo ya mijini hutumia nishati ya mkaa ikilinganishwa na asilimia 11.5 katika maeneo ya vijijini.

**Kielelezo Na. 20.7: Matumizi ya Mkaa Kama Nishati ya Kupikia katika Ngazi ya Mkoa Mwaka 2017/18 (Asilimia ya Kaya)**




**Kielelezo Na. 20.8: Mwenendo wa Matumizi wa Nishati ya Kuni na Mkaa Mwaka 2007 - 2017/18**




489. Licha ya mkaa kuwa chanzo kikubwa cha nishati ya kupikia hasusan mijini, matumizi yake yamekuwa na athari za kiafya na kimazingira. Kwa mujibu wa ripoti ya *The Contribution of Forest Sector to the National Economy* ya mwaka 2021, sekta ya misitu nchini ilizalisha na kuuza mkaa tani milioni 1.9 mwaka 2020 ambazo zilichangia asilimia 44.2 ya pato la sekta hiyo, sawa na takriban shilingi trilioni mbili (2). Ongezeko la mahitaji ya nishati ya mkaa nchini linatokana na kuongezeka kwa idadi ya watu; ukuaji wa miji;

urahisi wa upatikanaji, usafirishaji, usambazaji na uhifadhi wa mkaa; na ongezeko la bei ya nishati mbadala. Aidha, uuzaji wa mkaa katika vipimo vidogo, pamoja na gharama ndogo ya majiko yanayotumia nishati ya mkaa ikilinganishwa na nishati nyingine huchangia kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya nishati ya mkaa. Gharama ya kununua kilogramu moja ya mkaa ni takriban shilingi 1,500 ambapo inakadiriwa kwa kaya ya wastani wa watu sita hutumia kilogramu mbili za mkaa kwa ajili ya kupika milo mitatu kwa siku.

**Gesi ya Mitungi**

490. Gesi ya mitungi - LPG ni gesi ya kupikia inayohifadhiwa katika mitungi ambayo uzalishaji wake unatokana na uchakataji wa mafuta ghafi na gesi asilia yenye kiwango cha propani na buteni kinachozidi asilimia 15. Tanzania imekuwa ikiagiza LPG kutoka nje ya nchi kwa kuwa utafutaji unaoendelea nchini bado haujagundua uwepo wa mafuta na hakuna kiwanda cha kuchakata mafuta ghafi. Aidha, gesi asilia iliyogunduliwa nchini ina kiwango kidogo cha propani (asilimia 0.3) na buteni (asilimia 0.06) ambacho hakitoshi kuzalisha gesi ya mitungi. LPG iliyoingizwa nchini mwaka 2022 ilikuwa tani za ujazo 250,200. Kati ya hizo, tani za ujazo 160,610 zilitumika nchini na tani za ujazo 89,590 zilipita kuelekea nchi jirani. Vilevile, matumizi ya LPG yaliongezeka nchini kutoka tani za ujazo 20,000 mwaka 2010 hadi tani za ujazo 160,610 mwaka 2022.

491. Miundombinu ya kupokea LPG nchini inapatikana katika bandari za Dar es Salaam na Tanga. Gati la kupokelea LPG lina uwezo wa kupokea meli zinazobeba shehena ya juu ya tani za ujazo 5,500. Aidha, uwezo wa gati la upokeaji wa LPG ni mdogo na hivyo, kupunguza faida za kiuchumi zinazotokana na uagizaji wa LPG. Hifadhi ya kupokea LPG kwa upande wa Dar es Salaam na Tanga ina uwezo wa kuhifadhi tani za ujazo 15,750 kwa wakati mmoja. Vilevile, hifadhi ya LPG katika mikoa iliyobaki ni tani za ujazo 2,055 na hifadhi zote zinamilikiwa na kampuni binafsi.

492. Gharama za awali za kununua mtungi wa kilogramu 15 ni takriban shilingi 110,000, jiko la LPG la sahani mbili ni takriban shilingi 50,000 na mtungi wa kilogramu 6 pamoja na jiko lake ni takriban shilingi 58,000. Gharama hizi za awali ni kubwa ikilinganishwa na gharama za awali za matumizi ya tungamotaka. Aidha, gharama za kujaza mitungi ya gesi ya kilogramu 6 inakadiriwa kuwa kati ya shilingi 17,000 hadi shilingi 25,000 na mitungi ya kilogramu 15 ni kati ya shilingi 44,000 hadi shilingi 59,000. Vilevile, kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18, maeneo ya mijini yana kiwango kikubwa cha kaya zinazotumia LPG (asilimia 8.1) ikilinganishwa na vijijini (asilimia 0.4). Hii inatokana na gharama kubwa za kununua na kujaza mitungi ya gesi kwa watumiaji, urahisi wa upatikanaji wa nishati hiyo na kuongezeka kwa uelewa kuhusu matumizi salama ya LPG majumbani husasan katika maeneo ya mijini.

**Umeme**

493. Kwa mujibu wa *Energy Access and Use Situation Survey II in Tanzania Mainland* ya mwaka 2020, kaya zilizounganishwa na huduma ya umeme maeneo ya mijini ni asilimia 73.2 na maeneo ya vijijini ni asilimia 24.5. Jiji la Dar-es-Salaam linaongoza kwa kaya zilizounganishwa na huduma ya umeme ambapo asilimia 85.7 ya kaya ziliunganishwa. Aidha, Serikali kupitia miradi mbalimbali inaendelea na jitihada za kuongeza upatikanaji wa huduma ya umeme katika maeneo mengine nchini.

494. Gharama za kuunganisha umeme majumbani hutofautiana mijini na vijijini ambapo mijini ni shilingi 320,960 na vijijini ni shilingi 27,000. Gharama ya kizio (unit) kimoja cha umeme kwa matumizi ya nyumbani ni shilingi 298 kwa wateja wa kati. Kwa wateja wa chini, matumizi yasiyozidi kizio cha 75 kwa mwezi ni shilingi 100. Endapo matumizi yatazidi kizio cha 75 kwa mwezi kwa wateja wa chini, gharama kwa kila kizio kinachozidi ni shilingi 350. Aidha, yapo majiko sanifu yanayotumia umeme na yana uwezo wa kupika mlo mmoja kwa wastani wa kizio kimoja. Hata hivyo, gharama za awali za kununua majiko hayo ambazo huanzia shilingi 50,000 ni kubwa kwa mwananchi wa kipato cha chini kumudu. Nishati ya umeme kwa ajili ya kupikia inatumika zaidi maeneo ya mijini kuliko vijijini kwa sababu ya uwezo wa wananchi wa mijini kumudu gharama za majiko ya umeme na gharama za ununuzi wa vizio vya umeme. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18, asilimia 5.5 ya kaya zilizopo mijini zinatumia nishati ya umeme kupikia ikilinganishwa na asilimia 0.4 ya kaya zilizopo vijijini.

**Kinyesi cha Wanyama na Mabaki ya Mimea**

495. Nishati ya kinyesi cha wanyama hutokana na kukausha kinyesi cha wanyama kama vile, kinyesi cha ng'ombe kisha kutumika kama nishati kwa kutumia majiko ya mkaa au kuni. Aina hii ya nishati hupatikana zaidi maeneo ya vijijini katika jamii za wafugaji. Nishati inayotokana na mabaki ya mimea kama vile, majani na taka za kilimo hutumika majumbani na viwandani ikiambatana na aina mbalimbali za teknolojia ya majiko. Aidha, nishati za kinyesi cha wanyama na mabaki ya mimea hazina gharama ya ununuaji kwa kuwa zinapatikana kwa kukusanywa kutoka katika mifugo na mashamba yaliyopo jirani.

**Mafuta ya Taa**

496. Mafuta ya taa yamekuwa yakitumiwa kwa miaka mingi kama chanzo cha nishati ya kupikia katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18, asilimia 1.3 ya kaya Tanzania Bara zinatumia mafuta ya taa kama chanzo cha nishati ya kupikia. Nishati ya mafuta ya taa inatumika sana mijini ambapo asilimia 2.8 ya kaya hutumia nishati hiyo kupikia ikilinganishwa na asilimia 0.5 ya kaya za vijijini. Aidha, Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na kiwango kikubwa cha asilimia 6.5 ya kaya zinazotumia mafuta ya taa kama nishati ya kupikia. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa matumizi ya mafuta ya taa kwa ajili ya kupikia yamekuwa na

changamoto mbalimbali, ikiwemo usalama mdogo kwa sababu yanaweza kusababisha moto au mlipuko. Aidha, mafuta ya taa yanatoa harufu na moshi yanapochomwa, hivyo kuathiri ubora wa hewa ndani ya nyumba au jikoni, na kusababisha athari za kiafya, hususan matatizo ya kupumua, magonjwa ya moyo na kansa ya mapafu.

**Mkaa Mbadala**

497. Utengenezaji mkaa mbadala ulianza miaka ya 1980 kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC, Arusha. Mkaa mbadala ni mkaa unaotengenezwa kutumia aina mbalimbali za masalia ya mimea na mabaki ya mazao ambayo hugundishwa kwa kifungio kama vile, udongo, wanga (ikiwemo unga wa muhogo na viazi vitamu), molasi na/au gundi. Masalia yanayotumika ni karatasi, vumbi la mbao, maranda ya mbao, majani makavu na pumba za mpunga. Matumizi ya masalia hayo husaidia katika hifadhi ya mazingira. Ubora na bei ya mkaa mbadala inategemea mchanganyiko unaotumika kutengeneza mkaa huo.

498. Vumbi la makaa ya mawe hutumika pia kutengeneza mkaa mbadala unaotoa nishati ya kupikia. Vumbi hilo huchanganywa na vumbi la mbao pamoja na molasi na kugandamizwa kutengeneza vitofali au gololi za mkaa. Changamoto iliyopo katika utengenezaji wa mkaa huu ni jinsi ya kupunguza kiwango cha sumu pale unapochomwa, uhaba wa mitambo ya kuzalisha kiasi cha mkaa unaohitajika, na uelewa wa kutosha wa kupata mchanganyiko sahihi ili kupunguza kiwango cha joto kinachozalishwa. Aidha, mnyororo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa mkaa mbadala bado haujawekwa rasmi ili kurahisisha upatikanaji wa mkaa huo.

499. Changamoto zinazokabili uendelezaji wa teknolojia ya mkaa mbadala ni pamoja na uelewa mdogo wa jamii kuhusu aina hii ya nishati na gharama za awali za uzalishaji mkaa mbadala, ikiwemo gharama kubwa za ununuzi wa mashine za kuzalisha na kukausha. Changamoto nyingine ni pamoja na uwezo wa nishati inayozalishwa na mkaa huo kutofautiana kutokana na aina ya malighafi iliyotumika na utengenezaji wa baadhi ya aina ya mkaa mbadala kuhitaji majiko maalum, hivyo kuongeza gharama kwa mtumiaji. Aidha, malighafi inayotumika kutengeneza aina mojawapo ya mkaa huo ni vumbi litokanalo na mkaa wa asili, hivyo utengenezaji wake unaweza kuendelea kuchochea uharibifu wa misitu. Vilevile, ukosefu wa masoko, gharama na upatikanaji wa malighafi ni miongoni mwa vikwazo vya uendelezaji wa teknolojia hii. Kwa kuzingatia changamoto hizo, gharama za mkaa mbadala zinaanzia shilingi 500 hadi shilingi 1,500 kwa kilogramu moja kulingana na malighafi iliyotumika.

**Bayoethano**

500. Bayoethano ni nishati itokanayo na uchachushaji wa mabaki ya mazao ya mimea, hususan mazao ya wanga kama vile, sukari na nafaka. Pamoja na matumizi mengine, nishati hii hutumika kwa ajili ya kupikia. Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa - UNIDO imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuhamasisha Matumizi ya Bayoethano kama nishati mbadala ya kupikia kuanzia mwaka 2018. Mradi huo ulilenga kunufaisha kaya 500,000 katika Jiji la Dar es Salaam, ambapo hadi mwaka 2024 kaya zaidi ya 10,000 zilinufaika. Kupitia Mradi huo, gharama za jiko la sahani moja zilikuwa ni takriban shilingi 38,000 na jiko la sahani mbili takriban shilingi 90,000. Bei hizo zilijumuisha ruzuku ambayo ni nusu ya bei halisi ya majiko hayo. Aidha, bei ya mafuta ya bayoethano ni shilingi 2,500 kwa lita ambapo lita moja inaweza kutumika kwa masaa manne.

501. Teknolojia ya bayoethano haijasambaa kwa kiwango kikubwa nchini kutokana na changamoto ya upatikanaji wa malighafi. Aidha, uelewa mdogo wa watumiaji na ukosefu wa miongozo ya kuhamasisha matumizi ya nishati na teknolojia hiyo vinachangia kupunguza kasi ya matumizi ya nishati ya bayoethano.

**Bayogesi**

502. Bayogesi ni mchanganyiko wa gesi mbalimbali, ikiwemo gesi ya methane inayotokana na uchakataji wa kinyesi cha wanyama na binadamu, mabaki ya vyakula au masalia ya mimea katika mazingira ya kutokuwepo kwa hewa ya oksijeni. Uzalishaji wa bayogesi unakadiriwa kutumia kiasi cha kilo 40 hadi 60 za malighafi kuzalisha gesi ya kutosha ya kupikia kwa muda wa saa sita (6) kwa matumizi ya nyumbani kwa kaya ya watu wanne.

503. Kwa mujibu wa Programu ya Uenezi wa Mitambo ya Bayogesi kwa Ngazi ya Kaya ya Mwaka 2017 iliyotekelezwa na CAMARTEC, inakadiriwa kuwa mifumo 12,000 ya uzalishaji bayogesi ilifungwa kwa ngazi ya kaya na mingine 100 ilifungwa kwa ngazi ya taasisi nje ya Programu. Matumizi ya bayogesi yamekuwepo nchini tangu miaka ya 70. Kutoenea kwa matumizi ya nishati hii kumetokana na gharama kubwa ya awali inayojumuisha utengenezaji wa mitambo ya bayogesi ambayo hutegemea upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, maji na malighafi za kuzalisha gesi hiyo. Gharama ya mitambo kwa ngazi ya kaya ni kuanzia shilingi 1,600,000 hadi shilingi 2,000,000 kwa ukubwa wa mita za ujazo sita (6), shilingi 2,400,000 hadi shilingi 3,000,000 kwa mita za ujazo tisa (9) na shilingi 3,200,000 hadi shilingi 3,600,000 kwa mita za ujazo 13. Gharama hizo ni kubwa ikilinganishwa na gharama ya awali ya matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kuwa kikwazo kwa mwananchi wa kipato cha chini kumudu.

504. Changamoto nyingine ya matumizi ya nishati hii ni upatikanaji hafifu wa malighafi za uhakika; uhaba wa maji kwa ajili ya kuendeleza teknolojia hii; na mitazamo hasi ya jamii kuhusu kinyesi kutumika kama malighafi. Aidha, hakuna tafiti za kutosha kuhusu uendelezaji wa teknolojia ya kupikia ya bayogesi. Licha ya changamoto hizo, mitambo ya bayogesi hudumu kwa angalau miaka 30 endapo itajengwa kwa kukidhi viwango na haihitaji usimamizi wa karibu na ukarabati wa mara kwa mara. Hivyo, matumizi ya bayogesi yanaweza kuwa mbadala wa matumizi ya nishati za kuni na mkaa endapo changamoto zilizobainishwa zitatatuliwa.

**Gesi Asilia**

505. Gesi asilia inatambulika kuwa nishati safi ikilinganishwa na nishati nyingine zitokanazo na mafuta ya petroli kwa sababu inatoa kiasi kidogo cha hewa ukaa. Tanzania ina hazina ya takriban futi za ujazo trilioni 57.54 za gesi asilia iliyothibitishwa, kiasi ambacho ni kikubwa kubadili uchumi na Pato la Taifa na kinaipa Tanzania nafasi ya kwanza katika nchi za Afrika Mashariki kwa wingi wa gesi asilia. Sehemu kubwa ya gesi hiyo, takriban futi za ujazo trilioni 49.5 zipo katika kina kirefu chini ya Bahari ya Hindi. Aidha, kati ya kiasi cha gesi asilia kilichogundulika nchini, ni takriban futi za ujazo trilioni 8.8 tu kinazalishwa kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo ya viwandani na majumbani.

506. Gesi asilia hutumika katika maeneo yaliyopitiwa na miundombinu ya usambazaji wa gesi hiyo. Aidha, imekuwa vigumu kwa maeneo mengi kufikiwa kwa haraka kutokana na uchache wa miundombinu inayohitajika. Vilevile, maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani ni maeneo yaliyopo katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam. Hadi mwaka 2024, taasisi 13 na nyumba 1,511 ziliunganishwa na gesi asilia ambapo Mtwara ziliunganishwa nyumba 425, Lindi nyumba 209 na Dar es Salaam nyumba 877.

507. Gharama ya kuunganisha miundombinu ya gesi asilia katika maeneo ambayo yamepitiwa na miundombinu ya usambazaji inategemea umbali uliopo kutoka katika miundombinu hiyo. Gharama za kununua jiko la gesi asilia ni takriban shilingi 50,000 na kizio kimoja cha gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani kinagharimu kiasi cha shilingi 1,000. Aidha, inakadiriwa kuwa wastani wa kizio kimoja cha gesi asilia kinatosheleza kaya ya wastani wa watu sita (6) kupika milo mitatu kwa siku na mtumiaji hulipia kadri anavyotumia.

**Majiko Banifu**

508. Majiko banifu ni aina ya majiko yanayotumia teknolojia zenye ufanisi unaopunguza kiasi cha moshi wenye kemikali zenye sumu na hutumia nishati za tungamotaka kwa usanifu. Aidha, majiko haya yanahitaji uwepo wa miundombinu ya karakana maalumu ya kutengeneza na kukarabati pindi yanapoharibika. Changamoto ya kutopatikana kwa urahisi

kwa majiko banifu katika maeneo mengi nchini hasa vijijini inasababisha matumizi madogo ya majiko hayo. Vilevile, ukosefu wa tafiti za kutosha katika eneo hili umesababisha kuwa na teknolojia ya utengenezaji wa majiko isiyokidhi viwango vya ubora.

**Majiko ya Nishati ya Jua**

509. Majiko ya nishati ya jua hutumia teknolojia ya kunasa mionzi ya jua na kuibadilisha kuwa joto ambalo hutunzwa na kutumika kupika chakula. Majiko hayo yanatumia nishati ya jua kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya kioo kinacholenga mionzi ya jua, paneli za jua au vifaa vingine vya kubadili mionzi ya jua kuwa nishati. Majiko yanayotumia nishati ya jua huweza kuwa na muundo wa kisasa au wa jadi na hutumiwa katika mazingira ya mijini na vijijini kwa ajili ya nishati mbadala na endelevu.

510. Changamoto zinazokabili majiko ya nishati ya jua ni pamoja na gharama kubwa ya ununuzi ikilinganishwa na majiko yanayotumia kuni na mkaa. Aidha, uzalishaji wa nishati ya jua unategemea hali ya hewa na mionzi ya jua hivyo kusababisha changamoto kwa watumiaji, kwa kuwa majiko hayo hayana uwezo wa kuhifadhi nishati kwa matumizi ya baadaye. Hii inamaanisha kuwa nishati inayozalishwa inapaswa kutumiwa moja kwa moja au kutumika kwa kuchaji betri kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Hata hivyo, utunzaji huo wa chaji ni changamoto katika maeneo yenye vipindi virefu vya ukosefu wa jua au wakati mahitaji ya nishati yanapozidi uzalishaji. Ni muhimu kuzingatia kuwa teknolojia za nishati ya jua zinaendelea kufanyiwa tafiti na kuzidi kuimarika. Hivyo, changamoto hizi zinaweza kupungua kadiri teknolojia inavyoendelea kukua na kusambaa zaidi.

**Athari za Matumizi ya Nishati Isiyo Safi ya Kupikia**

511. Nishati isiyo safi ya kupikia ina athari mbalimbali za kiafya, kimazingira, kiuchumi, kielimu pamoja na kijamii kama ifuatavyo:

i. **Athari za Kiafya:** Moshi unaotokana na matumizi ya nishati isiyo safi huwa na gesi zenye sumu pamoja na chembe chembe ndogo za vumbi zenye viambata vya sumu ambazo huweza kudhoofisha mfumo wa upumuaji na kusababisha magonjwa sugu kama kikohozi, homa ya mapafu, kifua kikuu, pumu na saratani ya mapafu. Aidha, sumu hizo huchangia kuharibika kwa ujauzito, kujifungua kabla ya wakati au kujifungua watoto wenye matatizo ya kiafya. Magonjwa mengine yanayohusishwa na sumu hizo ni pamoja na magonjwa ya moyo, macho, shinikizo la damu na kupooza. Vilevile, ubebaji wa mizigo mikubwa ya kuni migongoni au vichwani huathiri uti wa mgongo, kichwa na miguu kwa wahusika. Inakadiriwa kuwa takriban watu 33,024 nchini hufariki kwa mwaka kutokana na magonjwa ya mfumo wa upumuaji yanayosababishwa na uchafuzi wa hewa katika makazi;

ii. **Athari za Kimazingira:** Utaratibu wa upatikanaji wa nishati isiyo safi ya kupikia unahusishwa moja kwa moja na uharibifu wa mazingira. Aidha, hewa ukaa

inayozalishwa kutokana na matumizi ya nishati isiyo safi kama vile, mkaa na kuni ina athari hasi katika mazingira, ikiwemo mabadiliko ya tabianchi yanayosabisha mafuriko au ukame, ongezeko la joto duniani, ongezeko la kina cha maji baharini, kuyeyuka kwa barafu, kupotea kwa baadhi ya viumbehai na ongezeko la chumvi baharini;

iii. **Ukataji hovyo wa misitu:** Kwa mujibu wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 2021 - 2031, inakadiriwa kuwa kiasi cha hekta 469,420 za misitu hukatwa kwa mwaka kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, ikiwemo kukata miti kwa ajili ya kuni na kuchoma mkaa. Hali hii inachangia kuongezeka kwa ukame nchini pamoja na athari za kiikolojia. Kwa mujibu wa Mpangokazi wa Utekelezaji wa Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira (2021-2026), takriban asilimia 16 ya eneo la nchi tayari limegeuka kuwa jangwa kutokana na ukataji wa miti;

iv. **Athari za Kijamii**: Katika jitihada za kutafuta kuni, wanawake na watoto hukumbwa na matukio ya ukatili wa kijinsia, ikiwemo kubakwa kutokana na kwenda kutafuta kuni maeneo ya mbali na makazi ya watu ambayo ni hatarishi. Sambamba na hilo, wanawake wengi hukumbwa na kadhia ya kupigwa na waume zao kutokana na kutumia muda mrefu kutafuta kuni, hivyo kuchelewa kurudi nyumbani, jambo linalohatarisha maisha, ustawi wa ndoa na familia. Aidha, waokota kuni huwa katika hatari ya kudhuriwa na wanyamapori pamoja na kukosa fursa za kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Matumizi ya nishati isiyo safi na salama kwa muda mrefu husababisha macho kuwa mekundu na hivyo, jamii huusisha waathirika na imani za kishirikina; na

v. **Athari za Kiuchumi:** Utafutaji wa kuni, hususan vijijini kwa ajili ya kupikia majumbani hutumia wastani wa saa sita kila siku na hivyo, kupunguza muda ambao ungetumika katika shughuli za kiuchumi. Aidha, uhusishaji wa watoto katika kutafuta nishati ya kuni huathiri mahudhurio na ufaulu wao shuleni kutokana na kutumia muda wa masomo na nguvu zao katika shughuli hiyo. Vilevile, wanawake wanapokwenda kutafuta nishati hiyo hukosa muda wa kujiendeleza kielimu na kiuchumi.

**Changamoto Zinazoathiri Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

512. Changamoto zinazoathiri matumizi ya nishati safi ya kupikia zinajumuisha:

i. **Uelewa mdogo wa wananchi na taasisi:** Kuna uelewa mdogo kwa umma kuhusu athari za kiafya, kimazingira, kielimu, kiuchumi na kijamii zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia na hivyo kuathiri kasi ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia;

ii. **Upatikanaji mdogo wa nishati safi, nafuu, endelevu na ya uhakika ya kupikia:** Upatikanaji usioridhisha unakwamisha wananchi kuhamia kirahisi katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hali hii inasababisha upatikanaji usio na uhakika pamoja na kuongezeka kwa gharama za matumizi ya nishati safi;

iii. **Gharama za nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia:** Gharama kubwa za awali za vifaa na majiko sanifu ya kupikia pamoja na gharama za matumizi ya nishati safi ni changamoto inayosababisha wananchi wengi kushindwa kumudu kutumia nishati safi za kupikia nchini. Gharama hizo husababisha wananchi kutumia nishati zisizo safi na salama ambazo zinaaminika kuwa nafuu katika maeneo yao kuendana na uwezo wa kipato;

iv. **Kutowiana kwa baadhi ya sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu usimamizi, uendelezaji na matumizi ya nishati ya kupikia:** Kukinzana kwa sera, sheria, kanuni na miongozo ni kikwazo kwa wananchi kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Mathalan, Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 pamoja na Sheria ya Misitu, Sura ya 323 na Kanuni zake, zinatambua shughuli za uzalishaji wa kuni na mkaa. Hali hii inakinzana na malengo ya Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia yanayo hamasisha utunzaji wa mazingira kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa;

v. **Uwekezaji mdogo katika nishati safi ya kupikia:** Uendelezaji wa nishati safi ya kupikia unakabiliwa na changamoto ya uwekezaji usiotosheleza katika mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia ambao unazorotesha kasi ya upatikanaji wa nishati hiyo. Aidha, kuna uhamasishaji hafifu kwa wadau kujua fursa zilizopo katika uwekezaji nishati safi ya kupikia;

vi. **Uwezo mdogo wa watekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia**: Baadhi ya taasisi zinazotekeleza miradi inayohusu nishati safi ya kupikia zina uwezo mdogo wa kifedha, kiujuzi na rasilimali watu. Hali hii inachangia kupunguza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia; na

vii. **Uhaba wa tafiti, ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia katika nishati safi ya kupikia:** Uhaba wa tafiti, ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia za kutosha zinazohusu masuala ya nishati safi ya kupikia unasababisha uhaba wa takwimu, ufahamu mdogo kuhusu hali halisi ya mwenendo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na kushindwa kuandaa mikakati sahihi ya kuongeza matumizi ya nishati hizo nchini. Aidha, uhaba wa teknolojia za kutosha katika nishati, vifaa, majiko na mifumo ya kibiashara unasababisha kuongezeka kwa gharama za nishati safi ya kupikia.

**Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizopo Katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

513. Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) kwa lengo la kuhakikisha asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikiapo mwaka 2034 kutoka kiwango kilichopo cha asilimia 9.2 mwaka 2022. Katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa, Serikali imeainisha hatua mbalimbali zitakazotekelezwa ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika matumizi ya nishati safi, ikiwemo:

i. Kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia;

ii. Kuhamasisha wananchi na taasisi kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia;

iii. Kuboresha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uzalishaji, upokeaji, uhifadhi na usambazaji wa nishati safi ya kupikia, pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia;

iv. Kuhakikisha gharama za awali na matumizi ya nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia zinapungua pamoja na kuhamasisha taasisi za fedha kuwezesha wadau wa nishati safi ya kupikia kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa nishati safi na kupunguza gharama za upatikanaji wake;

v. Kupitia, kuandaa na kufanya maboresho ya sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu nishati ya kupikia na kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo hiyo;

vi. Kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa za biashara zilizopo katika mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia pamoja na kuhamasisha matumizi ya mifuko ya fedha na programu za kitaifa na kimataifa katika kukuza na kuendeleza uwekezaji katika nishati safi ya kupikia;

vii. Kuwezesha upimaji wa viwango vya ubora wa nishati, vifaa na majiko ya nishati ya kupikia; na kuhakikisha watekelezaji na wasimamizi wa miradi ya nishati safi ya kupikia wanajengewa uwezo; na

viii. Kuimarisha uwezo wa taasisi na vituo vinavyofanya tafiti, ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia pamoja na kuimarisha ushirikiano kati

ya wawekezaji wa nishati safi ya kupikia na taasisi za utafiti na maendeleo, vyuo vya elimu ya ufundi na ufundi stadi, na vyuo vya elimu ya juu.

**Hitimisho**

514. Kutokana na athari za kiafya, kimazingira na kiuchumi zinazosababishwa na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia kama mkaa na kuni, matumizi ya nishati safi ya kupikia yanatoa fursa nzuri ya kuboresha afya ya jamii, kupunguza uharibifu wa mazingira, na kuimarisha uchumi wa kaya na Taifa kwa ujumla. Kwa kuzingatia upungufu wa miundombinu, uelewa mdogo wa faida za nishati safi, na changamoto za kifedha kwa kaya maskini, kuna umuhimu wa Serikali, sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo kushirikiana katika kuongeza matumizi ya nishati safi. Hili linaweza kufanyika kupitia kampeni za uhamasishaji, upatikanaji wa mikopo nafuu, na uwekezaji katika teknolojia zinazofaa kwa mazingira ya Tanzania. Kwa kuzingatia hilo, Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) ambao unawahimiza wadau wote kushirikiana kwa pamoja kutatua changamoto za upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ili kuwanusuru watanzania hususan wanawake na athari hasi za matumizi ya nishati isiyo safi ambayo inaathiri afya zao na kuchangia katika uchafuzi wa mazingira.


- **Upatikanaji wa Maji Vijijini**
- **Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**
- **Usafirshaji wa Abiria kwa SGR**







## Mwenendo wa Mapato ya Ndani





Mji wa serikali-Mtumba
Mtaa wa hazina
S.L.P 2802
Dodoma
http://www.mof.go.tz